Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA NNE

**Kikao cha Ishirini – Tarehe 6 Julai, 2011**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

## D U A

*Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua*

## HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO):**

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), kwa mwaka wa Fedha 2011/2012.

**MHE. ANGELLA JASMI M. KAIRUKI - (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA):**

Taarifa ya Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba Sheria na Utawala kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) kwa mwaka 2010/2011 pamoja na maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka 2011/2012.

**MHE. DKT. CHARLES J. TIZEBA - (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA ARDHI, MALIASI NA MAZINGIRA):**

Taarifa ya Mwenyekiti wa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira Kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) kwa mwaka 2010/2011 Pamoja na Maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka 2011/2012.

**MHE. PAULINE P. GEKUL - MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KUHUSU OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO):**

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani juu ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano) Kuhusu Makadiro ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano) kwa Mwaka wa Fedha, 2011/2012.

**MHE. PAULINE P. GEKUL - MSEMAJI WA MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KUHUSU OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MAZINGIRA):**

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani juu ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira) Kuhusu Makadiro ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira) kwa Mwaka wa Fedha, 2011/2012.

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 185

### Uhitaji wa Maji Safi na Salama Geita

**MHE. JOSEPHINE T. CHAGULLA** aliuliza:-

Ni sera ya Serikali kuwapatia wananchi wote maji safi na salama kuanzia ngazi ya kila mkoa, wilaya, hadi vijijini, lakini mkoa wa Geita pamoja na wilaya zake Nyang'hwale, Bukombe, Chato na Mbogwe, kuna shida kubwa sana ya maji safi na salama.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwapatia wananchi wa Geita na Wilaya zake Maji Safi na salama?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA, (ELIMU)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Josephine Thabita Chagulla, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza mpango wa maji na usafi wa mazingira vijijini, wilaya za Geita na Nyang'hwale, tayari zimepata mkandarasi aitwae *Victoria Drilling Co. Ltd* ambaye amesaini mkataba tarehe 20 Juni, 2011 kwa ajili ya shughuli za uchimbaji wa visima vya maji. Uchimbaji unatarajiwa kuanza mara baada ya kukamilika kwa taratibu za kusaini mkataba wa uchimbaji wa visima 9 katika wilaya ya Nyang'hwale na visima 8 katika wilaya ya Geita. Aidha, ujenzi wa miundombinu ya maji katika vijiji hivyo utafanywa mara baada tu ya shughuli za uchimbaji kukamilika.

Mheshimiwa Spika, katika mji wa Geita upo mpango kabambe wa ujenzi wa mradi mkubwa wa maji unaotekelezwa kwa ushirikiano kati ya kampuni ya kuchimba dhahabu ya Geita *Gold Mine (GGM)* na Halmashauri ya Wilaya ya Geita ikishirikiana na Wizara ya Maji katika mwaka 2011/2012.

Mheshimiwa Spika, kazi zinazotarajiwa kutekelezwa kupitia kampuni hiyo ni:-

(i) Kujenga *pump house*;

(ii) Kujenga *treatment plant;*

(iii) Kufunga *pump* za kusukuma maji na; na

(iv) Kujenga tanki kubwa la kuhifadhi maji pamoja na kulaza bomba itakalopelekea maji hadi kwenye tanki kubwa. Aidha kazi ya utafiti wa athari za kimazingira *(Environment Impact Assessment)* imeshafanyika na utekelezaji wa mradi huo unatarajiwa kuanza mara baada ya kusainiwa kwa mkataba wa makubaliano kati ya kampuni ya Geita *Gold Mine* na Serikali.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa kazi zilizotajwa hapo juu unatarajiwa kukamilika ifikapo Desemba, 2011. Aidha, mradi huu utagharimu jumla ya shilingi bilioni 15.3 ambapo kiasi cha shilingi bilioni 6 kimetengwa na kampuni ya Geita *Gold Mine (GGM*) na kiasi kingine cha shilingi bilioni 9.3 kimeombwa kutoka Serikali Kuu kama maombi maalum *(special request)* katika mchanganuo ufuatao; kisasi cha bilioni 4.5 kiliombwa katika mwaka wa fedha 2010/2011 na kiasi kilichosalia cha shilingi bilioni 4.8 kimeombwa katika mwaka huu wa fedha 2011/2012.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Halmashauri ya Wilaya ya Geita itajenga mtandao wa mabomba ya kusambaza maji kutoka katika matanki ya kuhifadhi maji hadi kwa mtumiaji (*distribution*) na mradi huu unatarajiwa kukamilika ndani ya mwaka wa fedha 2011/2012.

**MHE. JOSEPHINE T. CHAGULLA:** Mheshimiwa Spika, ahsante pamoja na majibu mazuri kabisa ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba kuuliza swali moja la nyongeza kama ifuatavyo.

Tatizo la ukosefu wa maji katika mkoa mpya wa Geita limekuwa likirudisha nyuma maendeleo ya mkoa na taifa pia. Kinamama ambao ndiyo nguvu kazi ya taifa wamekuwa wakitumia muda mwingi na nguvu kwa kutafuta maji tu badala ya shughuli zao za ujenzi wa taifa.

Je, Serikali haioni kuna haja sasa ya kumaliza tatizo hili ili kinamama hawa nao waweze kushirikiki kikamilifu katika ujenzi wa Taifa lao?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimwia Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Thabita kama ifuatavyo.

Ni kweli Serikali inatambua matatizo ambayo kinamama wanapata na sasa hivi ndiyo maana tumeanzisha huo mradi mkubwa wa kuendeleza sekta ya maji katika kila mji na kila wilaya. Kwa hiyo kwa mwaka wa fedha ambao tunao sasa hivi Serikali imetenga shilingi bilioni 3.5 katika mradi unaoitwa *Lake Victoria Commission, Water Facility*, kwa hiyo hii ni miradi ambayo tutaendeleza upatikanaji wa maji katika mji wa Nasio, wa Sengerema na Geita.

Pia baada ya hapo naomba Mheshimiwa kwa sababu umeuliza mipango tu iliyopo naomba unisubiri wakati Waziri wa Maji atakapowasilisha Bajeti yake na ataelezea mipango ambayo ipo kwa ajili ya miji hiyo ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. NYAMBARI CHACHA M. NYANGWINE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kuniona na mimi niweze kuungana na mwuliza swali ili kuuliza swali lingine la nyongeza hasa kuhusiana na wenyeji wa Tarime.

Kwa kweli wilaya ya Tarime ina matatizo makubwa ya maji, tangu enzi za uhuru hadi sasa mimi naamini haijawahi kupata maji safi na salama kwa ajili ya afya ya wakazi wa Tarime. Je, Serikali inatoa msimamo gani kuhusiana na tatizo hilo?

**SPIKA:** Yaani ni yale maji ya *lake* sasa.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Chacha, Mbunge wa Tarime, kama ifuatavyo:-

Katika mji wa Tarime, pia tumekasimu mamlaka ya maji Musoma ili iweze kusimamia uendelezaji na upatikanaji wa maji katika mji ule. Sasa hivi ameshaajiriwa mtaalam mwelekezi ambaye anatathimini kuweza kujua kabisa kiasi gani cha maji kitakidhi na ongezeko la watu lililopo katika wilaya ya Tarime. Kwa hiyo naomba pia Mheshimiwa Chacha utusubiri kuweza kujua mipango kabambe ambayo Serikali imepanga ambayo tutawasilisha kwenye Bajeti ya Wizara ya Maji katika mwaka huu wa Fedha.

**SPIKA:** Wanaotaka kuuliza maswali ya nyongeza wanasimama mara ya kwanza wakisimama baadaye huwezi kupata nafasi.

Na. 186

**Utaratibu wa Ajira za Watumishi wa Halmashauri**

**MHE. MUNDE T. ABDALLAH** aliuliza:-

Utaratibu wa ajira za watumishi katika Halmashauri ilikuwa ikifanywa na Bodi za Halmashauri husika lakini utaratibu wa sasa ajira zote hutolewa na Idara Kuu ya Utumishi Dar es Salaam.

(a) Je, ni utaratibu gani wa uhakika unaotumika kutoa matangazo ya ajira?

(b) Je, Serikali inasaidiaje katika gharama za safari na posho ya kujikimu kwa watu walioitwa kwenye usaili?

**SPIKA:** Namba gani?

**MHE. MUNDE T. ABDALLAH:** Namba 186.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Munde Tambwe lenye, sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Utaratibu wa uhakika wa kutoa matangazo ya ajira unaotumika kwa sasa ni kupitia vyombo vya habari vilivyopo nchini hususan magazeti na tovuti mbalimbali za Serikali.

Kwa kupitia matangazo hayo waajiri na hasa Wakurugenzi wa Halmashauri wanaelekezwa kubandika matangazo hayo kwenye mbao za matangazo zilizopo kwenye maeneo yao.

(b)Serikali haina utaratibu wa kuwarudishia gharama za safari waombaji wa fursa za ajira. Hata sekretarieti ya ajira imeweka utaratibu wa kuwafanyia usaili waombaji kazi katika makao makuu ya mikoa wanakotoka.

Mheshimiwa Spika, kama hatua ya muda mfupi ya kuwapunguzia gharama za waombaji kazi, Sekretarieti ya ajira imefungua ofisi sita za kanda kati mikoa ifuatayo:-

Manyara kwa ajili ya mikoa ya kanda ya Kaskazini, Tabora kwa ajili ya Mikoa ya Kanda ya Kati, Mwanza kwa ajili ya Mikoa ya Kanda ya Ziwa, Morogoro kwa ajili ya Mikoa ya Kanda ya Mashariki na Mbeya kwa ajili ya Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini.

**MHE. MUNDE T. ABDALLAH**: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, naomba nimwulize maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo.

(i) Hivi Mheshimiwa Waziri atakubaliana na mimi kwamba Watanzania wengi hawajui hata maana ya tovuti, hasa vijana wetu waliomaliza shule za kata waliopo kule vijijini, lakini atakubaliana na mimi pia kwamba *TV* hakuna wala magazeti hayafiki kwa wakati?

(ii) Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, Serikali inaona ugumu gani kurudisha ajira hizi kwenye Halmashauri za Manispaa au Halmashauri za wilaya, lakini Serikali pia inaona basi ugumu gani kupeleka ajira hizi angalau kwenye sekretarieti za mikoa kupunguza urasimu, gharama za kwenda kwenye kanda ili vijana wetu hawa waweze kupata ajira za udereva, uhudumu na kuzing'ang'ania wao kwenye Serikali Kuu? Naomba majibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu majibu ya nyongeza ya Mheshimiwa Munde Tambwe Abdallah, kama ifuatavyo.

Kuhusu suala la tovuti, ni kweli kwamba wapo ambao hawafahamu lakini pia katika dunia ya sasa wapo ambao wanafahamu.

Hilo suala la tovuti ni njia moja tu ambayo kama nimeelezea, tumesema tunapitia magazeti, na katika Halmashauri husika, Wakurugenzi wanaagizwa kuweka katika mbao za matangazo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la kung'ang'ania juu, napenda Mheshimiwa mbunge aelewe kwamba kabla hii sekretarieti ya ajira ina mwaka mmoja tu tangu ianze kazi na tuliianzisha baada ya kuona upungufu uliokuwepo kwa ajira hizo hizo ambazo yeye anaziona ni ndogo kwamba zinafanyika katika ngazi za Halmashauri.

Kulikuwa watu wanaajiriana kwa undugu, lakini pia walikuwa wanaajiriwa watu bila sifa lakini kutokana na mashinikizo mbalimbali yaliyokuwepo huko. Na kama nilivyozungumza jana wakati wa Bajeti yangu kwamba tutafungua ofisi za sekretarieti ya ajira kila mkoa kwa ajili ya hizo nafasi ambazo wanaona kwamba tunapata usumbufu.

Kwa hiyo ni lengo letu kuhakikisha kwamba tunashusha kwamba kufungua ofisi lakini siyo kuachia sekretarieti ya mikoa wafanye hiyo kazi, kisheria sasa hivi ni kazi ya sekretarieti ya ajira.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kunipa nafasi niweze kuuliza swali la nyongeza, kwa kuwa Serikali kwenye swali la msingi

imejibu kwamba imefungua ofisi kwenye kanda sita, na kwa kuwa kwa sasa hivi hawarudishi gharama za nauli wala kutoa chakula wala mtu anapolala kule mjini hawamlipi.

Je, Serikali inatambua kwamba wapo vijana wanaolazimika kusafiri mikoa na wanalazimika kufika kwenye eneo la usaili siku moja kabla ili aweze kuwahi *interview* na hana chakula, na hana mahali pa kulala, pengine hata nauli amekopa, kwa hiyo inakuwa ni maisha magumu sana kwake?

Je, Serikali ina mpango gani wa kusaidia kwa kutambua hali ya vijana wa Tanzania, wakati inaandaa kupeleka kwenye mikoa ina utaratibu gani wa kusaidia vijana hawa waweze kufanya *interview* zao vizuri na kurudi makwao wakiwa angalau wanajiweza? Ahsante.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Magdalena Hamis Sakaya, kama ifuatavyo:-

Kama nilivyotangulia kusema kwamba kwa sasa hivi ambapo hatujafungua sekretarieti za mikoa huwa tunawafuata katika mikoa yao. Zile kanda tumezifungua tu kwa maana ya kupokea maombi, na tunachofanya huwa tunataka wale waombaji waonyeshe wanatoka wapi.

Kilichojitokeza ni baadhi ya vijana yeye yuko Kigoma lakini anasema yupo Dar es Salaam na ukiangalia hata tunavyofanya usaili kama ule usaili unahusu uwajiriwa kwa ajili ya Kigoma huwa tunawafuata huko huko ili kuwapunguzia hizo gharama ambazo Mheshimiwa Mbunge ameziona.

**MHE. MICHAEL L. LAIZER:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza; kwa kuwa Wabunge wengi wanaona jambo hili hata wananchi wanaona jambo hili kwamba ni kero, italeta kero kwa wananchi je, Serikali haiwezi kusikiliza kilio cha wananchi pamoja na sisi Wabunge ikabadilisha utaratibu huu kwa sababu italeta matatizo?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA):** Mheshimiwa Spika, nimeelezea kwa kifupi tu kwa nini tumefikia kuanzisha sekretarieti ya ajira, lakini Waheshimiwa Wabunge watakubaliana na mimi kwamba kabla ya kuanzishwa utaratibu huu ambapo tuliachia kila mamlaka ya ajira iajiri kwa wakati wake. Kulikuwa na vijana ambao wao walikuwa wamejiweka kwamba wao kazi yao ni kuomba kazi kila siku, na kuchukua posho ya kujikimu kila siku.

Kwa hiyo ilikuwa ni gharama kubwa sana kwa Halmashauri, wanatangaza kazi watu wanaenda, wanaenda kuripoti wanachukua pesa za kujikimu wanaondoka.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo upungufu ambao tunauona ni mdogo sana ambao naahidi kwamba tutayafanyia kazi, Manufaa ni makubwa sana, na huko kwenye

Halmashauri na hata kwenye Wizara kulikuwa na upungufu mwingi sana mpaka tunafikia hivyo na siyo sisi ambao tunafanya kuwa na sekretarieti ya ajira. Kabla ya kuanzisha tumeenda katika mataifa mbalimbali tumejifundisha wenzetu India wanafanya hivyo na ni nchi kubwa kushinda sisi, Singapore wanafanya hivyo, na Botswana, Namibia wanafanya hivyo hivyo. *(Makofi)*

Kwa hiyo naomba watupe muda tutarekebisha upungufu na tutaendelea kufungua matawi katika maeneo mbalimbali nchini. *(Makofi)*

Na. 187

**Mpango wa Stakabadhi Ghalani**

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU** aliuliza:-

Ingawa mpango wa Stakabadhi ghalani umefanikiwa kwa baadhi ya mazao hasa Korosho.

(a) Je, kuna ulazima mkiubwa kiasi gani wakulima kushiriki mpango huo?

(b) Ikiwa zao la mafuta halipati tija kutokana na mpango huo, kwa nini iwe ni lazima wakulima kushiriki mpango huo ambapo ni kinyume na taratibu za soko huria?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda na Biashara, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Murtaza Mangungu, Mbunge wa Kilwa Kaskazini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo;-

(a)Mheshimiwa Spika, faida za matumizi ya mfumo wa stakabadhi za maghala zimedhihirika wazi kwa waliotumia ikiwa ni pamoja na wakulima kupata bei nzuri zaidi, kushawithi mabenki kutoa fedha zaidi za kununulia mazao, kuongezeka kwa ubora wa mazao na kupunguza gharamza za ununuzi na uuzaji wa mazao na hivyo bei ya mkulima kuongezeka. Aidha, mfumo huu unaruhusu wanunuzi kushindana katika mnada mmoja badala ya kununua mazao kiholela majumbani kwa wakulima bila kuzingatia vipimo halisi au rasmi na ubora unaotakiwa. Kutokana na faida hizo kuna ulazima mkubwa wa wakulima kushiriki mfumo huo.

(b)Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa takwimu zilizopo, wakulima wa zao la Ufuta wamenufaika na mfumo huo ukilinganisha na mfumo wa zamani. Takwimu zinaonyesha kuwa katika msimu wa mwaka 2010/2011, wakulima wa Ufuta wa Mkoa wa Lindi waliuza Ufuta wao kwa bei ya wastani wa shilingi 1,600/= kwa kilo ukilinganisha na bei ya wastani iliyotolewa na wanunuzi binafsi ya shilingi 900/= hadi 1,000/= kwa kilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii kuwaomba Waheshimiwa Wabunge wote tusaidiane kuelimisha wakulima katika maeneo ya manufaa ya Mfumo wa Stakabadhi za Maghala, ili waondokane na *propaganda* za walanguzi wanaotaka kuendelea kuwanyonya wakulima wetu.

**MHE. MURTAZA MANGUNGU:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri Viwanda na Biashara lakini nasikitika kusema kwamba takwimu ambazo amezitoa si sahihi. Hakuna mkulima yeyote ambaye ameweza kulipwa zaidi ya shilingi 1,600/= kama anavyosema. Ninaomba nimuulize maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, nimeipitia vizuri sana Sheria ya Stakabadhi Ghalani, na Sheria hii haijatoa sharti kuwa ni lazima kwa mkulima kushiriki katika Stakabadhi Ghalani, ni kitu ambacho ni *option.* Kwa nini iwe ni lazima wao kushiriki katika hili wakati Serikali haisaidii lolote kwenye kilimo cha Ufuta?

La pili, aniambie kwamba yuko tayari kutangaza sasa hivi kupitia Bunge hili wananchi wa Kilwa waruhusiwe kuuza Ufuta sehemu yoyote wanayotaka kwa sababu ni haki yao na wamelima wenyewe?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Viwanda au Kilimo? *There is nothing to do with* viwanda sasa hii.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, naomba nijibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Murtaza Mangungu, kama ifuatavyo.

Kwanza kwa niaba ya Serikali nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Murtaza kwa jitihada anazozifanya kuwasemea wakulima na ni wajibu wetu sisi wote Wabunge kuendelea kuwasemea wakulima ili tuhakikishe kwamba mwisho wa siku wanapata faida katika kilimo na kupata tija.

Sehemu ya kwanza ya swali lake naomba nimrudishe kwenye Sheria ambayo ilianzisha mfumo wa Stakabadhi za Maghalani.

Sheria Namba 10 ya mwaka 2005 na Kanuni zake zilikamilika mwaka 2006 na Sheria hii imeweka wazi kwamba mfumo wa Stakabadhi za Maghala unaendeshwa kwa hiari na wakulima wanashirikiana katika vikundi vyao, vyama vya ushirika, makampuni makubwa yanaruhusiwa vilevile mkulima mmojammoja mkubwa mwenye *critical mass* za uzalishaji anaruhusiwa kujiunga na mfumo huu ili mradi aweze kutumiza masharti yaliyowekwa. Kama nilivyosema kwenye jibu la masingi, faida inayopatikana kwenye mfumo huu imekuwa kubwa kuliko hasara zake.

Pili, wakulima ambao wameendelea kuuza kupitia wanunuzi binafsi ambao wengi wamekuwa na tabia ya kuwalangua wakulima. Kwanza kama tulivyosema juzi kwa kutumia vipimo visivyo rasmi, vipimo ambavyo kwa kweli havina ubora na

vinawalangua wakulima, na wanunuzi hawa wameendelea kuupinga sana mfumo wa stakabadhi za Maghala. Lakini Serikali inarudia kusema kama tulivyosema mwanzo kwamba mfumo huu ni mzuri kwa wananchi. Mfumo huu unaendelea kuwafaidisha wakulima na mfumo huu unawakomboa wakulima kwa kuweka ushindani wa soko katika eneo moja lenye viwango vilivyokubalika.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi ili niulize swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa, hivi sasa kule Mbozi kuna maeneo mengi ambayo yanalima Mahindi, wananchi kupitia utaratibu ambao si mzuri wanauza Mahindi kwa bei ndogo ambayo naamini wanashawishiwa na hao wanunuzi au walanguzi. Serikali kwa kupitia Bodi ya Mazao Mchanganyiko haioni sasa kuna umuhimu wa kuanzisha pia utaratibu kwa zao la Mahindi iil wananchi waweze kufaidika?

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Zambi.

Mheshimiwa Spika, kwanza nimshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri.

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Godfrey W. Zambi kwamba kuna haja kubwa sasa ya kupanua mfumo wa Stakabadhi Ghalani ili uhusishe mazao ya chakula.

Nchi yetu imekuwa sasa ndiyo Ghala la nchi jirani na hivyo ni muhimu sana tuwe na mfumo rasmi ambao utatumika katika kuuza na kununua mazao ya chakula. Serikali imepanga kuongeza ujenzi wa Maghala ya kuhifadhia chakula katika maeneo makubwa ya uzalishaji ili hii iwe ndiyo msingi wa kuanzisha *Commodity Exchange* katika nchi yetu.

Na. 188

**Soko la Afrika Mashariki**

**MHE. DKT. MARY MACHUCHE MWANJELWA (K.n.y. MHE. BETTY MACHANGU)** aliuliza:-

(a)Je, Serikali imejiandaaje kuwa na elimu ya ujasiriamali na usindikaji wanawake wa Kilimanjaro na Mikoa mingine ya Tanzania ili waweze kumudu ushindani unaotoka nchi nyingine za Afrika Mashariki?

(b)Je, Serikali ina mikakati gani ya kuwapatia wanawake wajasiriamali Mkoani Kilimanjaro mashine za kusindika mazao yao (hata kwa mkopo) ili kuongeza thamanai kwa mazao yao na hatimaye kumudu ushindani katika soko la Afrika Mashariki?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda na Biashara, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Betty Machangu, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo.

(a)Mheshimiwa Spika, Wizara ya Viwanda na Biashara kwa kupitia Taasisi zake mbalimbali ikiwemo Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo *(SIDO),* imekuwa ikitoa mafunzoya ujasiriamali na usindikaji kwa zaidi ya miaka 28 sasa.

Mafunzo hayo ni usindikaji, utengenezaji wa mvinyo na juisi, uhunzi, useremala, ufungashaji wa bidhaa, ubora wa bidhaa, ujuzi wa kuanzisha na kuendesha biashara na ushiriki kwenye maonyesho ya biashara. Katika kipindi cha miaka mitano 2006/2007 hadi 2010/2011 jumla ya wajasiriamali 59,915 wakiwemo wanawake 29,442 walishiriki mafunzo hayo. Aidha, hadi kufikia Aprili, 2011, *SIDO* Kilimanjaro ilikuwa imetoa mafunzo ya aina hii kwa washiriki 973 wakiwemo wanawake 635. Mafunzo haya yamegharamiwa kwa pamoja na washiriki wenyewe, shirika la *SIDO,* Halmashauri za Wilaya na Taasisi zisizo za Kiserikali.

(b)Mheshimiwa Spika, aidha, kupitia Taasisi zake, Wizara ya Viwanda na Biashara imewezesha upatikanaji wa teknolojia 99 kutoka ndani na nje ya nchi. Shirika la *SIDO,* kwa kupitia vituo vyake vilivyopo Arusha, Mbeya, Kilimanjaro *(KIDC),* vimewezesha utengenezaji wa mashine mpya mbalimbali 506 na vipuri 1,622 na kuzisambaza kwa watumiaji wakiwemo wajasiriamali wa Mkoa wa Kilimanjaro. *(Makofi)*

Vilevile, kupitia mfuko wa *NEDP* wajasiriamali wa Mkoa wa Kilimanjaro. Vilevile, kupitia mfuko wa *NEDP (National Entrepreneurship Development Fund)* wanawake wajasiriamali 868 walipata mikopo yenye thamani ya shilingi 423,425,000 kwa madhumuni hayo.

Wizara ya Viwanda na Biashara kwa kupitia Taasisai zake mbalimbali na kwa kushirikiana na wadau wengine itaendelea kutekeleza mipango na mikakati mbalimbali ya kuwaendeleza wajasiriamali wadogo wote nchini wakiwemo wa Mkoa wa Kilimanjaro. *(Makofi)*

**MHE. DKT. MARY MACHUCHE MWANJELWA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niulize swali la nyongeza.

Kwa kuwa, wajasiriamali wengi nchini Tanzania wanaojulikana kwa jina la Mamantilie ni Wanawake, na Wanawake hawa ndiyo wanaosaidia sana ku-*promote* biashara katika viwanda vikubwa kama vile Coca Cola, Pepsi Cola, Sayona, Azam na watumiaji wengi ambao wanakunywa hivi vinywaji wanatokana na viwanda hivi vikubwa. Je, Serikali ina mkakati gani katika kuwasaidia wajasiriamali wa aina hii ili kuweza kuwawezesha ama kuingia nao ubia au makubaliano kuwainua kichumi na kielimu?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali moja la Mheshimiwa Dkt. Mary M. Mwanjelwa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nakubaliana naye kwamba wajasiriamali wengi nchini ni Wanawake, na Serikali inaweka mikakati ambao inaendelezwa ya kuwasaidia kwa kuwapa mitaji kwa kadri inavyowezekana na hasa wanapokuwa katika vikundi ili waweze kujiendeleza.

Katika mfuko wa *National Entrepreneurship Development Fund kama* nilivyosema kwenye jibu la msingi ulioanzishwa mwaka 1994 hadi sasa ukubwa wake umefikia bilioni 4.8 na umepokea maombi yenye thamani ya bilioni 75 na hadi kufikia sasa hivi wajasiriamali 145,000 wameweza kupewa mikopo mbalimbali nchini kote. Hadi sasa hivi mikopo 51,000 ilishawahi kutolewa yenye thamani ya bilioni 26. Hizi ni jitihada za Serikali na tutaendelea kushirikiana na wajasiriamali hawa wadogo kuwaendeleza.

**MHE. CHRISTINA LISSU MUGHWAI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niulize swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa, mahitaji ya kusindika mazao kama yalivyoonyeshwa katika swali la msingi yapo pia katika Mkoa wa Singida. Je, Wizara ya Biashara ina mpango gani wa kuwawezesha wajasiriamali wa Mkoa wa Singida ili waweze kusindika mazao ya Alizeti na Asali na hivyo kuinua kipato chao na kipato cha Mkoa kwa ujumla?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Lissu kama ifuatavyo.

Kwanza, nakubaliana naye kwamba ni muhimu tukaendelea kuwasaidia wajasiriamali na wakulima wadogowadogo hasa katika teknolojia ya kusindika mazao. Katika Mkoa wa Singida tayari *SIDO* wameanzisha kiwanda cha mfano nchi nzima kwa ajili ya Asali. Wakulima na warinaji wa Asali wanapeleka Asali yao kwa pamoja na Asali hiyo inapatiwa *process* inapata thamani na wanaweza wakaiuza kwa pamoja.

Kwa kutazama zao la Alizeti, tayari Serikali kwa kushirikiana na wawekezaji inakamilisha kiwanda chenye thamani ya shilingi bilioni 10 katika Mkoa wa Singida. Kiwanda hiki tunategemea kitakamilika mwaka huu, kitakuwa ni kiwanda kikubwa kuliko vyote nchini kwa kusindika zao la Alizeti na kuliongezea thamani na kuweza kuwasaidia sana wakulima wote wa Mikoa ya Singida, Manyara na Shinyanga. *(Makofi)*

Na. 189

**Kuajiriwa kwa Wahitimu wa Chuo cha Diplomasia Nchini**

**MHE. KIUMBWA MAKAME MBARAKA** aliuliza:-

Chuo cha Diplomasia kilichoko Kurasini Jijijini Dar es Salaam kimeboresha mafunzo yake kwa kozi ya *Diploma in International Relations* kutoka mafunzo ya mwaka mmoja na kuwa miaka miwili.

Je, Serikali imejiandaa vipi kuajiri wahitimu hao?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu waziri! Naomba wanaojibu wakae karibu maana mtamtia wasiwasi Spika atakuwa hajui kama mpo au hampo.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Nje Ushirikiano wa Kimatiafa, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Kimbwa Makame Mbaraka kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, ni kweli chuo cha Diplomasia kilichoko Kurasini Dar es Salaam kimeboresha mafunzo yake ya kozi ya *Diploma in International Relations* kutoka mafunzo ya mwaka mmoja na kuwa miaka miwili. Uboreshaji huo umefanyika ili kukidhi matakwa na viwango vya kusajiliwa na *NACTE.*

Mheshimiwa Spika, wahitimu wa mafunzo haya mara nyingi hutokea kazini na kujiunga na mfunzo haya kwa lengo la kujiendeleza na hivyo kurejea katika ajira zao. Wahitimu wengine huajiriwa na mashirika yasiyo ya Kiserikali na taasisi zingine zinazohitaji watu wenye ujuzi wa masuala ya kimataifa. Aidha, wahitimu wengine huendelea na elimu ya shahada katika vyo vikuu nchini kwa kuwa Cheti cha *Diploma* hiyo sasa inawezesha kujinga na vyuo vikuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Utumishi wa Umma *(Standing Orderf for the Public Service)* toleo la mwaka 2009 kifungu D 4(1) ajira katika Utumishi wa Umma hutegemea kuwepo kwa nafasi husika kwenye Ikama na ambayo imetengewa fedha kwa ajili ya kulipia mshahara.

Kwa upande wa Wizara yangu, waajiriwa kutoka chuo hicho ni wale waliohitimu Stashahada ya Uzamili yaani *Post Graduate Diploma,* kulingana na matakwa ya Muundo wa Utumishi wa Wizara.

**MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi ili niulize swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa, umekiri hapa kwamba wewe katika Idara yako unachukua wenye Shahada ya Uzamili na chuo kile kinatoa *Diploma* tu. Kwa nini kisiongeze mitaala na kutoa mpaka *level* hiyo ya Uzamivu?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali moja la Mheshimiwa Mnyaa kwamba nimeeleza kwamba wanapomaliza *Diploma* hiyo wanapata nafasi ya kujiunga katika vyuo vingine ambapo vyuo vikuu vipo vingine ambavyo vinatoa fani hiyo ya mahusiano ya Kimataifa. Aidha baadaye wakipenda wanaweza kurudi chuoni kwa *Post Graduate Diploma*. Chuo chetu cha Diplomasia au katika vyuo vingine. Kwa hiyo, kuweza ku-*qualify* kujiunga na Wizara yangu au wengine wenye matakwa kama yangu.

Kwa hiyo, hakuna ulazima kwamba chuo chetu kiwe na kiwango hicho wanachokitaka kwa sababu fani hiyo inapatikana katika vyuo vingine.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

Na. 190

**Mapato yatokanayo na KINAPA**

**MHE. FREEMAN A. MBOWE** aliuliza:-

Mlima Kilimanjaro ni chanzo muhimu cha mapato ya Utalii na ajira kwa waongozaji watalii '*potters*' lakini pia mahusiano mema baina ya *KINAPA,* Watalii na wenyeji wa maeneo jirani na hifadhi hiyo.

(a) Je, ni nini mapato ya KINAPA kwa kipindi cha miaka 10 sasa, mwaka hadi mwaka na kiasi gani kinatolewa kama mgao utokanao na mapato hayo kwa Halmashauri ya Wilaya ya Hai na Wilaya nyingine zinazozunguka Mlima Kilimanjaro, mwaka hadi mwaka kwa kipindi cha miaka 10?

(b) Je, kiasi gani halali na haki wanachotakiwa kupewa wafanyakazi hao niliowataja na Serikali ina mpango gani wa kulinda haki?

(c) Je, ni lini Serikali itaweka utaratibu mzuri wa gawio kwa Halmashauri zinazozunguka badala ya utaratibu uliopo wa kutegemea *KINAPA* kupitia ujirani mwema?

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Freeman A. Mbowe, Mbunge wa Hai, lenye sehemu (a), (b) na ( c) kama ifuatavyo:-

(a) Mamlaka ya Hifadhi za Taifa Tanzania *(TANAPA)* kupitia Hifadhi ya *KINAPA* ilikusanya mapato jumla ya Tsh. 180,342,099, 351 katika kipindi cha miaka 10 kuanzia mwaka 2001 hadi mwaka 2010. Mchanganuo wa mapato kwa muda wa miaka 10 umeambatanishwa na Mheshimiwa Mbunge amepatiwa.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia *TANAPA* haina utaratibu wa kutoa mgao kwa Halmashauri za Wilaya zinazozunguka Mlima Kilimanjaro au zinazozunguka hifadhi kwenye maeneo mengine bali hutoa mchango kupitia utaratibu wa Ujirani Mwema kwa ajili ya kusaidia Miradi ya Maendeleo inayoibuliwa na Wananchi wa vijiji vilivyo ndani ya Wilaya zinazozunguka hifadhi ikiwemo mlima Kilimanjaro.

Katika kipindi cha miaka 10 kuanzia 2001 – 2010, *TANAPA* imetoa jumla ya Tsh. 1,409,518,081 katika miradi iliyokamilika, lakini kuna shilingi milioni 428 za miradi inayoendelea na hili nalifafanua kwa sababu Mheshimiwa Mbowe ana jibu, mwaka 2010 tumeonesha ni shilingi milioni 25, kuna nyingine shilingi milioni 424 ambazo ziko kwenye Miradi inayoendelea kama mchango katika kusaidia miradi ya maendeleo ya wananchi. Mchanganuo kuhusu michango kwa muda wa miaka 10 umeambatanishwa na Mheshimiwa Mbunge amepatiwa. Aidha, michango isiyo ya moja kwa moja inayotokana na utalii wa mlima Kilimanjaro inakadiriwa kuzidi Tsh, bilioni 8.8 kwa mwaka ambayo inajumlisha malipo kwa wafanyakazi wanaojishughulisha na utalii (*Tour Operators*), wapagazi (*potters*) pamoja na wapishi. Pia wananchi zaidi ya 28,000 hunufaika kupitia kilimo cha mbogamboga pamoja na zawadi ambazo huuzwa mahotelini na kwenye maeneo mengine wanakofikia wageni.

Faida nyingine ni pamoja na uhifadhi wa vyanzo vya maji yanayotumika majumbani Mjini Moshi na maeneo mengine yakiwemo viwandani kama *(Bonite Bottle Co. Ltd.)* na umwagiliaji katika mashamba ya mpunga na miwa.

(b) Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa kanuni za Sheria ya Utalii, 2009 Kifungu cha 20 (2) jedwali Na. 4 imeelekezwa kuwa viwango stahiki vya malipo ya kwa Wapagazi (*potters*) ni dola za Marekani (US$) 10 kwa siku. Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii alifanya mkutano mwezi Mei, 2008 Mjini Moshi uliowajumuisha wamiliki wa kampuni za biashara za utalii na waongozaji watalii na kuridhia kwa pamoja kuwa malipo kwa ajili ya mwongoza watalii yawe ni dola 20 pamoja na dola 15 kwa mpishi kwa siku. Hivyo ni jukumu la vyama vinavyosimamia na kuendesha biashara ya utalii na kwa kushirikiana na wafanyakazi wenyewe kupitia chama chao cha CHODAWU kuhakikisha kuwa stahili hizo na zingine zilizoanishwa kwenye Sheria ya Kazi na Mahusiano kazini zinalipwa.

(c) Mheshimiwa Spika, utaratibu unaotumiwa na Serikali kwa sasa ni ule ambao umetamkwa na Sheria ya Hifadhi za Taifa ya mwaka 2002 ambao ni wa kuchangia Miradi ya Maendeleo kwa njia ya ujirani mwema *(Support for Community Initiated Projects).* Aidha, Wizara yangu iko tayari kushirikiana na Halmashauri zinazohusika kujadili uwezekano wa kutafuta vyanzo vingine vya mapato katika Halmashauri hizo kupitia biashara ya utalii. Tayari tumeanza mazungumzo na Waheshimiwa Wabunge wa Mkoa wa Kilimanjaro kuona uwezekano wa halmashauri hizo kuwa na tozo zao wenyewe ambazo watakusanya.

**MHE. FREEMAN A. MBOWE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. Namshukuru pia Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake ya msingi, hata hivyo nina

maswali mawili madogo ya nyongeza;(i)Mheshimiwa Spika, kwa sababu sasa ni dhahiri kwamba chanzo cha mapato yatokanayo na utalii kupitia Hifadhi ya Kilimanjaro *(KINAPA)* ni muhimu sana kwa mapato ya utalii katika taifa, na kwa sababu chanzo hiki kinachangia karibu nusu ya mapato yote ya *Tanzania National Parks,* na kwa kuwa ujirani mwema na usalama wa watalii wanapokuwa wanatembelea eneo hili ni jambo la msingi sana na linatakiwa litiliwe nguvu iwezekanavyo.

Katika majibu aliyotoa Mheshimiwa Waziri kwamba sasa Serikali iko katika mazungumzo na Wabunge wetu wa Mkoa wa Kilimanjaro ili kuona ni vipi tunaweza kuoanisha mawazo ya pamoja. Waziri haoni vilevile kwamba kuna umuhimu wa kuweza kuanzisha hii *council tax* ambayo italipwa moja kwa moja na makampuni yanayopandisha watalii mlimani, hususan kodi maalum kwa ajili ya makampuni yasiyo ya kitanzania ambayo yanapandisha wageni mlimani, kwa sababu yapo makampuni ya nje ambayo yanatoka nchi jirani na mengine kutoka Ulaya ambayo yanaleta watalii kupanda mlima moja kwa moja na hayawajibiki kulipa kodi yoyote ya moja kwa moja kwa Serikali Kuu wala Serikali za Mitaa.

Je, haionekani sasa kuna umuhimu wa kuangalia namna ya kuyabana makampuni haya ili yaweze kuchangia katika pato letu la utalii ndani ya Halmashauri za Wilaya na vilevile Serikali Kuu?

(ii)Kwa sababu ni kweli kuna malipo stahiki ambayo wamepangiwa kupata Wapagazi, Wapishi na wale waongozaji watalii katika mlima, lakini bado yamekuwepo malalamiko makubwa sana ya watumishi hawa ambao wanafanya kazi ngumu ya kupanda mlima, kupunjwa na makampuni haya hususani yale ambayo yanatoka nje moja kwa moja na hayawajibiki kwa sheria zetu za ndani.

Je, Waziri anatupa kauli gani ya Serikali ambayo itaongeza mkazo kwa makampuni haya ili kwa kweli Watanzania hawa wanaofanyakazi ngumu sana ya kupanda mlimani na mizigo waweze kupata stahiki zao? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, naomba kwanza nimshukuru sana Mheshimiwa Mbowe kwa mawazo mazuri mengi tu ambayo tumekuwa tukiyapata kutoka kwake pamoja na Wabunge wengine wa Mkoa wa Kilimanjaro kuhusu suala hili.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi ni kweli kwamba ukiangalia mapato ya moja kwa moja yanayotoka *TANAPA* kwenda kwenye jamii au Halmashauri au miradi ya maendeleo ni sh, bilioni 1.4 katika sh bilioni 180 ambayo ni *around percent* moja (1%) ya mapato yote, ndiyo maana tukawa tumekubaliana kwamba kimsingi ni lazima tutafute mkakati mzuri zaidi wa kuhakikisha kwamba Halmashauri hizi zinapata mapato.

Kwa hiyo pendekezo hili la kuanzisha *Council Taxes* pamoja na kodi nyingine kwa wafanyabiashara wa sekta hii kimsingi sisi tunakubaliana nalo, lakini tunahitaji kufanya mazungumzo tu ili kuwa na tahadhari kwa sababu sekta ya utalii ni *delicate*, *sensitive* kwa bei kwani mkiweka bei kubwa inaweza ikafanya wageni wakaona inakuwa *expensive* kuja kutembelea vivutio vyetu hivi.

Kwa hiyo tutazungumza ili tuweze kuangalia kiasi kinachoweza kutozwa kisilete madhara kwa maana ya kupunguza idadia ya wageni wanaotembelea vivutio vyetu.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na swali la pili kwamba usimamizi wa malipo haya ambayo tumekwishakubaliana wengi wa wafanyabiashara wanakuwa wanakaidi na ni kawaida ya wafanyabiashara kwa kweli kwa sababu wangependa kulipa kidogo ili wapate faida. Tayari tumekwishazungumza na wenzetu wa Wizara ya Kazi na waliishaniambia kwamba wameishatuma Makamishina wao kwenda kwenye eneo hilo. Tunategemea kwamba Wizara ya Kazi pamoja na sisi tutashirikiana kwa pamoja ili kuwabana hawa wafanyabiashara kuhakikisha kwamba wanalipa haya malipo maana tuliishakubaliana. Walikuwepo *Potters* na *Tour Operators* tukakubaliana kwamba kiwe kinalipwa kiasi nilichotaja. Kwa hiyo, ni usimamizi tu ambao tutaimarisha. *(Makofi)*

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Spika, naomba nimpongeze kwanza Mheshimiwa Waziri kwa majibu hayo mazuri sana, lakini nilikuwa naomba nimwulize swali moja dogo.

Ninafahamu Mheshimiwa Waziri toka ameingia kwenye Wizara yake amekuwa akikabiliana na kufanyakazi kwa nguvu na kufanya maamuzi mazito sana.

Mheshimiwa Spika, liko tatizo moja dogo lakini ni kubwa. Mheshimiwa Waziri aliishafanya vikao na kuanza kulitatua tatizo la *concession fees* ili kuongeza mapato ya Serikali. Ningeomba kujua Mheshimiwa Waziri amefikia hatua gani ili kuiruhusu *TANAPA* ianze kushughulikia suala la malipo ya *concession fees* kwa *fixed rates* kuliko ilivyo sasa ambapo wawekezaji wanalipa tu bila kufuata utaratibu ambao ni maalum?

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Jenista Mgahama, Mbunge wa Peramiho, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba *TANAPA* waliwahi kufanya mazungumzo na wawekezaji waliojenga mahoteli kwenye *Parks* kwamba kiwango cha malipo na utaratibu wa ulipaji kibadilishwe. Mwaka 2008 – 2009 tulikuwa tunaelekea kwenye mtikisiko wa uchumi, mapendekezo haya yalipoletwa Wizarani, Wizara iliona pengine isingekuwa vizuri kwa wakati huo kwa sababu wangeweza kuyaongeza kwenye bei zao.

Wizara ikasema kwamba suala hilo lisifanyike kwa wakati huo, baada ya mtikisiko wa uchumi kuwa umeisha na mimi mwenyewe nilipokutana na Bodi ya *TANAPA* tarehe 20 Desemba, 2010 niliwambia kwamba sasa waanze kutoza kwa jinsi walivyokubaliana.

Kwa hiyo, kwa sasa hivi Wizara kama Wizara haina tatizo na suala hilo na tuliishawaruhusu kwa maandishi kwamba waendelee kutekeleza makubaliano yao na wadau wao.

Na. 191

**Tuhuma za mauaji ya Watu wawili yaliyofanyika ndani ya Pori la Akiba Selous**

**MHE. SELEMAN S. JAFO** aliuliza:-

Hivi karibuni wakazi wawili wa Tarafa ya Chole Wilayani Kisarawe waliuawa kikatili na Askari wa Wanyamapori kwenye Mbuga ya Hifadhi ya *Selous:-*

(a) Je, ni hatua gani zimechukuliwa dhidi ya askari waliohusika na ukatili huo ambapo baada ya kuwaua waliwachoma moto?

(b) Je, Serikali imeweka utaratibu gani wa kuzuia mauaji zaidi yasiendelee kwa wakazi wa Kisarawe ambao wanapakana na Hifadhi ya Selous?

(c) Je, Serikali ina mpango gani wa kuzisaidia familia hasa watoto walioachwa na hao waliouawa wa kijiji cha Chole na Kirui?

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Seleman S. Jafo, Mbunge wa Kisarawe, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Wizara yangu ilipata taarifa za kuwa wananchi wawili ambao inadaiwa kuwa wameuawa na kikosi cha askari wa wanyamapori ndani ya Pori la Akiba la Selous. Kwa mujibu wa taarifa zilizochapishwa kwenye vyombo vya habari kati ya tarehe 12 na 14, mwezi Februari, mwaka 2011, baada ya kupata taarifa hizo Wizara yangu ilifuatilia suala hilo na kubaini kuwa kwa mujibu wa ratiba ya doria ya kikosi, hakuna kikosi cha askari wa doria kilichofanyakazi katika maeneo hayo na kusababisha mauaji hayo ya wananchi katika kipindi hicho.

Mheshimiwa Spika, natumia fursa hii kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa suala hili limefikishwa katika Jeshi la Polisi Kisarawe na kufunguliwa jalada la kumbukumbu namba KS/IR/144/2011. Uchunguzi unaendelea kufanyika kulingana na taratibu, kanuni na sheria za nchi ili kubaini ukweli kuhusu tatizo hili. Hivyo namwomba Mheshimiwa Mbunge pamoja na Wananchi wa Kisarawe kwa ujumla wawe na subira wakati uchunguzi wa suala hili ukifanyika kupitia vyombo vinavyohusika.

(b) Mheshimiwa Spika, eneo la Kisarawe pamoja na maeneo mengine ya mapori yamekuwa na ongezeko la ujangili na hata ujambazi katika miaka ya karibuni kutokana

na mahitaji ya raslimali zilizohifadhiwa kuongezeka. Wizara yangu itaendelea kufanya kazi na taasisi zingine za ulinzi na usalama kuimarisha usalama wa watu pamoja na maliasili zetu. Hata hivyo, Wizara yangu haiwezi kuwahakikishia usalama wananchi wanaoingia porini usiku bila taarifa. Ni muhimu wananchi wakazingatia utaratibu wa kufanya mawasiliano na uongozi wa Hifadhi ili kupatiwa ulinzi waingiapo Hifadhini kwa shughuli zao halali.

(c) Mheshimiwa Spika, kwa kuwa bado uchunguzi unaendelea, utakapokamilika Serikali itachukua hatua zinazostahili ikiwa ni pamoja na kuwalipa kifuta machozi ndugu na jamaa wa wafiwa kwa mujibu wa taratibu zilizopo.

**MHE. SELEMAN S. JAFO:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa fursa ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwanza nimepata majibu ya Mheshimiwa Waziri, lakini kwa masikitiko yangu ni kwamba u-*seriousness* katika suala hili hauko makini sana hasa kwa wapiga kura wangu wa Jimbo la Kisarawe. Kwa kuwa watu hawa walipigwa risasi, wawili walifariki pale pale na bahati mbaya vichwa vyao vikachukuliwa kwa ajili ya uchunguzi lakini watu hao walichomwa moto, na mmoja wao hadi hivi sasa naendelea kumhudumia katika hospitali ya Muhimbili mpaka hivi sasa yuko ni mlemavu; majibu hayo kwa kweli mimi sijaridhika nayo na inaonesha kwamba Wizara hii haijali wananchi wangu na wapiga kura wangu wa jimbo la Kisarawe. (*Makofi*)

(a ) Je, Serikali iko tayari kufanya *gwaride* la utambuzi kwa ajili ya kugundua hawa askari waliohusika na tatizo hili?

(b) Kwa vile mafuvu mawili yamechukuliwa kwa ajili ya uchunguzi na hivi sasa ni karibu miezi mitano imeishapita?

Je, vichwa hivyo vimewekwa wapi na lini vitarejeshwa kwa ajili ya kufanya mazishi katika jimbo letu la Kisarawe? (*Makofi*)

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII**: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Seleman Jafo, Mbunge wa Kisarawe kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza niseme tu kwamba kwa dhati kabisa Wizara yangu pamoja na viongozi na Serikali yote kwa ujumla tunasikitika kwa jinsi jambo hili lilivyotokea. Lakini, kama nilivyosema kwamba, kwa uchunguzi ambao sisi kama Wizara tumeufanya na maelezo tuliyoyapata ni hayo, ndiyo maana jambo hili likaripotiwa kwenye chombo ambacho kina dhamana ya kusimamia usalama wa wananchi kwa maana ya Jeshi la Polisi. Jeshi la Polisi wanafanyakazi zao kwa mujibu wa taratibu na sheria ambazo zinawaongoza katika ufanyajikazi wao.

Mheshimiwa Spika, katika swali lake la kwanza amezungumzia kuhusu gwaride la utambuzi, kwa upande wetu kama Wizara ambayo kwa kesi hii sisi ni watuhumiwa

hatuna tatizo wala mamlaka yoyote ya kuwaelekeza polisi wafanye kazi namna gani. Kwa hiyo, Polisi wanaruhusiwa kufanya gwaride la utambuzi au kitu kingine chochote ambacho wanaona ni muhimu kifanyike ili kuweza kuwatambua ambao wamehusika.

Mheshimiwa Spika, swali la pili kuhusu vichwa ambavyo vimechukuliwa na lenyewe lina sura hiyo hiyo kwamba vimechukuliwa na chombo ambacho kinafanya uchunguzi kwa maana ya polisi kwa sisi kama Wizara hatuwezi kujua vilichukuliwa vikapelekwa wapi kwa sababu vilichukuliwa na mamlaka nyingine. Lakini kwa sababu Serikali iko hapa tumesikia, nina amini kwamba pengine baadaye kidogo tutaweza kumfahamisha hatua gani zimefikiwa katika uchunguzi wa suala hili.

**MHE. MARTHA J. UMBULLA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi niulize swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa matatizo haya ya tarafa ya Chole kule Kisarawe yanafanana sana na matatizo ya wananchi wanaozunguka Ziwa Manyara, Tarangire na maeneo ya Mamire kule Babati Vijijini, ambapo wananchi wanaendelea kuuawa na Tembo na kuingia kwenye mafarakano makubwa na askari wa Wanyamapori huku tukijua kwamba Serikali iliishawaambia wahame na hata kupewa fidia lakini imeshindwa kuwaelekeza wahamie maeneo gani kwa hiyo wanaendelea kupata matatizo.

Je, ni kwanini Serikali haiwezi kuchukua hatua ya kuwalekeza wananchi wahamie wapi?

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII**: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Martha J. Umbulla. Mbunge wa Viti Maalum, Mkoa wa Manyara, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kumekuwepo na tatizo la mpaka kati ya Hifadhi ya Tarangire pamoja na vijiji vya Ayamango, Gijedabul pamoja na kijiji kingine sikikumbuki vizuri. Tatizo hili limekuwepo kwa muda mrefu kidogo, uongozi wa mkoa ulikuwa na jukumu la kutafuta eneo ambalo wanaweza wakahamishiwa. Kuna shamba la *Galapo Estate* ambalo lilikuwa limetolewa hati kwa watu binafsi, tuliishaanza kufanya mawasiliano na Ofisi ya Rais ambayo ndiyo yenye mamlaka ya kuweza ku-*revoke title* kwa hiyo mchakato wa ku-*revoke title* unaendelea ili eneo hilo liweze kupatikana kwa ajili ya wananchi kuhamishiwa pale.

**MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE:** Mheshimiwa Spika, swali aliloliuliza Mheshimiwa Seleman Jafo pamoja na majibu yaliyotolewa na Mheshimiwa Waziri ni *very serious* hasa linaposikika kwa Watanzania. Kwa kuwa Wizara ya Mambo ya Ndani, Serikali kwa ujumla imo humu ndani na Waziri amesema Wizara ya Maliasili na Utalii wao ni watuhumiwa lakini Wizara ya Mambo ya Ndani ndiyo hasa inayofanya uchunguzi wa jambo hilo.

Je, Wizara ya Mambo ya Ndani wanasema nini juu ya vifo vya watu wale? (*Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, aah Mheshimiwa Naibu wa Uratibu, wewe unajifisha huko, wote mnatakiwa kuwepo hapa ili mjibu maswali yanayotokea hapa. (*Kicheko*)

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani kwanza nikuombe radhi, lakini kuhusu suala hili, kwa kawaida tunafanya uchunguzi kuhusu masuala haya na niseme kwamba hatuwezi tukafanya haraka kusema kwamba huu ndiyo msimamo wa Serikali kwa sababu viko vyombo vingi ambavyo vinahusika katika kupata taarifa. Lakini kubwa ambalo ninaweza nikalihakikishia Bunge lako Tukufu ni kwamba, linafanyiwa kazi na hiyo ni kauli ambayo ninasema na kabla Bunge hili halijaisha tutakuwa tumewapa taarifa kamili kujua tumesimama wapi. (*Makofi*)

Na. 192

**Wanafunzi wanaohitimu Shahada ya Kwanza ya Sheria**

**MHE. MHONGA S. RUHWANYA (K.n.y. FELIX MKOSAMALI**) aliuliza:-

Wanafunzi wanaomaliza shahada ya kwanza ya sheria katika vyuo vikuu nchini ni wengi sasa:-

(a) Je, kwa nini *Center* ya *Law School* ni moja tu nchini?

(b) Je, Serikali imeweka utaratibu gani wa kuwezesha kuwakopesha wanafunzi hao ili waweze kuhudhuria mafunzo hayo, kwani wengi wao walisoma kwa mikopo?

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Felix Mkosamali, Mbunge wa Muhambwe, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Taasisi ya mafunzo ya Uanasheria kwa vitendo Tanzania (Law School of Tanzania) ilianzishwa chini ya sheria ya Bunge Na. 5 ya mwaka 2007 (ambayo sasa ni Sura ya 425 ya Sheria za Tanzania) kwa ajili ya kutoa mafunzo mahsusi ya Uanasheria kwa vitendo kwa wahitimu wa shahada ya kwanza ya sheria ili waweze kuajiriwa katika utumishi wa umma au kufanya kazi kama mawakili wa kujitegemea kwa mujibu wa kifungu cha 12 cha sheria hiyo. Taasisi hii ilianza kuendesha mafunzo yake Machi, 2008 katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kama mkakati wa muda mfupi wakati mipango ya ujenzi wa miundombinu yake ikiendelea.

Ujenzi wa majengo ya taasisi hii umeanza tangu tarehe 18 Novemba, 2010. Ujenzi huu ambao umefadhiliwa na Mradi wa Maboresho ya Sekta ya Sheria (Legal Sector Reform Programme) nchini unajumuisha majengo ya kisasa ya madarasa, maktaba, jengo la utawala, mahakama ya mazoezi, ukumbi wa mgahawa katika awamu ya kwanza na utakamilika mwezi Februari, 2012. Taasisi itakuwa na uwezo kudahili kwa mara moja wanafunzi 1,000 mara baada ya majengo haya kukamilika.

Mheshimiwa Spika, naomba ieleweke kwamba uendeshaji wa mafunzo ya uanasheria kwa vitendo ni wa kipekee na ni tofauti kabisa na uendeshaji wa mafunzo ya shahada ya kwanza ya sheria na kwamba unahitaji miundombinu maalum ya kisasa na pia unahitaji rasilimali watu kubwa na yenye utaalam wa hali ya juu katika kuendesha mafunzo. Hivyo, taasisi itahitaji kwanza kujenga uwezo na kujiimarisha katika maeneo yote ya mafunzo kabla ya vituo *(Centers)* zitakazokidhi viwango hivyo hivyo vya ubora kuanzishwa sehemu zingine mikoani.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali ilianzisha Bodi ya Mikopo kwa Wanafunzi wa Vyuo vya Elimu ya Juu nchini (*Higher Education Students' Loan Board*) wa sheria Na. 9 ya Bunge ya mwaka 2004 ili iweze kuratibu na kutoa mikopo kwa wanafunzi wahitaji *(needy students).*

Kwa mujibu wa sheria hiyo, Wanasheria wanafunzi wanaohudhuria mafunzo ya uanasheria kwa vitendo katika Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo si miongoni mwa wanafunzi wanaostahili kisheria kunufaika na mikopo hiyo, kwa sababu *"Law School of Tanzania'* imeanzishwa mwaka 2007 na sheria ya bodi ya mikopo imeanzishwa mwaka 2004. Juhudi za Wizara ni kuwakopesha wanafunzi hao pale upatikanaji wa fedha unaporuhusu.

(c) Mheshimiwa Spika, hata hivyo, Serikali imekuwa ikitoa fedha kupitia Wizara yangu kwa ajili ya kuwakopesha wanafunzi wa taasisi hii. Mikopo hii inasimamiwa na Bodi ya Uendeshaji ya Taasisi hii. Hadi sasa wanafunzi 1,016 wa Taasisi hii wamekwishapewa mikopo yenye jumla ya shilingi bilioni tatu, milioni mia tatu arobaini na tatu, laki tano na themanini na tano elfu (3,343,585,000.00).

Kwa sasa Serikali inaendelea kutafuta njia bora na ya kudumu ya utoaji mikopo kwa wanafunzi wahitaji wa taasisi hii kwa sababu utaratibu uliopo sasa siyo endelevu.

**MHE. MHONGA S. RUHWANYA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa kuwa Serikali imesema kwamba Sheria ya Bodi ya Mikopo ilitungwa mwaka 2004 kabla ya Sheria ya *Law School* mwaka 2007 ambayo imemtaka kila anayetaka kuwa Wakili lazima apitie *Law School*.

Je, Serikali haioni kwamba kuna haja ya kuileta Sheria ya Bodi ya Mikopo ikarekebishwa ili kuweza ku-*accommodate* watu wa *Law School* kwa sababu wengi wamesomeshwa kwa mikopo hivyo ni wazi hawawezi kujilipia mafunzo ya *Law School*?

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA**: Mheshimiwa Spika, Serikali inachofanya kwa sasa ni kuanza kuhuisha mitaala kwamba baadhi ya vyuo vikuu vinatoa Shahada ya Sheria kwa miaka 4, nyingine kwa miaka 3. Kwa hiyo, hatua ya kwanza ni kuuhisha mitaala na hatua ya pili itakuwa ni kuangalia hiyo Sheria ya Bodi ya Mikopo ili tuweze ku-*accommodate* hao wanafunzi ambao wanachukua *Law School* na ifahamike sasa hvi Mheshimiwa Rais ameunda Tume kuangalia Bodi ya Mikopo na hilo nalo pia tumelipeleka ili tuone kwamba hao wanafunzi pengine wanaweza wakawa-*accommodated* katika hayo mapendekezo mapya ambayo Tume ya Rais imeundwa kuangalia Bodi ya Mikopo.

**SPIKA:** Ahsante kwa sababu ya muda tunaendelea na Mheshimiwa David Ernest Silinde.

Na. 193

**Upatikanaji wa Katiba ya Nchi**

**MHE. DAVID E. SILINDE** aliuliza:-

Serikali ipo katika mchakato wa kuandika Katiba Mpya lakini Katiba iliyopo sasa haipatikani ili Watanzania waweze kuisoma na kutoa michango ya kufaa katika Katiba Mpya inayokusudiwa:-

(a) Je, Serikali inaweza kueleza sababu za uhaba wa upatikanaji wa Katiba ya sasa kwenye maeneo mbalimbali nchini?

(b) Je, Serikali inachukua hatua gani za haraka za kusambaza Katiba hizo za sasa kwa wananchi ili waweze kuzisoma na kujua kasoro zake mapema kwa ajili ya kurekebisha kasoro hizo katika Katiba mpya?

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa David Silinde, Mbunge wa Mbozi Magharibi, napenda kutoa maelezo ya jumla kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbunge atakubaliana nami kuwa wananchi wengi wa Tanzania leo hii wanafahamu umuhimu wa Katiba na Sheria za nchi katika maisha yao ya kila siku kuliko wakati mwingine wowote katika historia ya nchi yetu. Hivyo basi, kwa niaba ya Serikali nawapongeza sana wananchi na nina imani kubwa kuwa watashiriki kikamilifu katika mchakato wa kupata Katiba Mpya.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Ni kweli kuwa kuna uhaba wa nakala za Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 katika sehemu nyingi hapa nchini. Hivi sasa, Serikali ina mpango wa kuongeza maduka ya Serikali ya kuuza nakala za Sheria mbalimbali ikiwepo Katiba. Kwa sasa maduka ya vitabu vya Serikali yapo katika mikoa michache ambayo ni Mwanza, Arusha, Dodoma, Morogoro na Dar es Salaam. Aidha, itakapoanzishwa Tume ya Kuratibu mchakato wa Katiba Mpya, Serikali inakusudia kuchapa nakala nyingi za Katiba na kuzisambaza katika maeneo mbalimbali yakiwemo maduka ya vitabu ya Serikali. Hii itawawezesha wananchi wengi kuielewa na hatimaye kutoa michango mizuri wakati Taifa litakapokuwa katika mchakato wa kuandika Katiba Mpya.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali itajitahidi kwa kadri ya uwezo wake wa kifedha kusogeza huduma kuhusu elimu ya Katiba karibu na kila mwananchi ili kumwezesha kupata nakala ya Katiba ya sasa. Natoa wito kwa taasisi za Serikali na zisizo za Kiserikali kutoa elimu kwa wananchi kuhusu Katiba ikiwa ni pamoja na kununua kwa wingi Katiba hizo na kuwasambazia wananchi.

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Naomba kuuliza maswali madogo mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri amekiri wazi kabisa kwamba nchi yetu ya Tanzania ina uhaba mkubwa wa Katiba. Je, sasa unaweza ukawaeleza Watanzania wawe na uhakika ni lini maana yake tunataka muda kamili sio wakati ukifika. Ni lini sasa na kwa kipindi gani Watanzania wawe na uhakika wa kupata Katiba wa kupata Katiba za kutosha?

Pili, kwa kuwa sasa Waziri Mkuu alishatoa tamko nchini kwamba mchakato wa kuanzisha Katiba Mpya utaanza tarehe 26 Aprili, 2014 siku ambayo tutakuwa tunaazimisha miaka 50 ya Muungano.

Je, ni kwa nini sasa Serikali isifikirie upya kwamba Katiba Mpya tuanze sasa itakapofika tarehe 26 Aprili, 2014 tunapotimiza miaka 50 tuwe tunazindua Katiba Mpya ili iendane na miaka 100 inayofuatia? Ahsante.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA**: Mheshimiwa Spika, suala la kusambaza Katiba limeshaanza. Nafikiri katika sehemu nyingi tu sasa hivi Katiba zimesambazwa na taasisi za Serikali nyingi tumezishawishi zinunue Katiba katika sehemu mbalimbali kuanzia Halmashauri na Halmashauri kule wana vijiji, kata kule kote tumewaomba wasambaze hizo Katiba na mimi Wizara yangu pia ina mkakati huo wa kusambaza Katiba katika sehemu mbalimbali. Kwa hiyo, hilo suala tumeshaanza ndiyo maana umekuta Watanzania wengi sasa hivi wana mwamko wa kusoma Katiba na wanaifahamu Katiba ilivyo.

Suala la pili, mchakato wa Katiba umeshaanza na Muswada tutauwasilisha. Nafikiri nikubaliane tu na Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba mwaka 2014 sisi tumeshajipangia kwamba Katiba mpya ndipo itakapozinduliwa.

Mchakato wake ndio huu tunaoendelea nao sasa hivi na Muswada uko Bungeni. Kwa hiyo uko mikononi mwa Spika na tunaendelea na mchakato kama anasema kwamba tuendelee kuuweka katika kipindi hiki sisi kama Serikali tuko tayari, kama tutauwasilisha mwezi Oktoba sisi tuko tayari. Lakini kikubwa tukubaliane Waheshimiwa Wabunge kwamba mchakato huu uanze mapema iwezekanavyo badala ya ku-*delay* hapa na pale.

Na. 194

**Ujenzi wa Majosho ya Mifugo na Ofisi Katika Jimbo la Kishapu**

**MHE. SULEIMAN M. N. SULEIMANI** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itajenga majosho na Ofisi za kisasa katika maeneo ya Jimbo la Kishapu ili kusaidia wafugaji wa Jimbo hilo kunufaika na mifugo yao kuhudumiwa vizuri?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi naomba kujibu swali la Mheshimiwa Suleiman Masoud Nchambi Suleimani, Mbunge wa Kishapu kama ifuatavyo;-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Mipango ya Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya *(DADPs)* imekuwa ikijenga na kukarabati majosho nchini kuanzia mwaka 2003/2004 kwa njia shirikishi ambapo wafugaji huibua miradi itakayotatua matatizo yanayowakabili na kuiwasilisha Serikalini ili kutengewa fedha za utekelezaji kufuatana na umuhimu.

Kati ya mwaka 2003/2004 na 2009/2010 Serikali kupitia Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu ilikarabatiwa majosho 6 ya Mwamalasa, Mwamashele, Mwadulu, Idukilo, Magalata na Mwasubi kwa gharama ya shilingi 25,326,000/=. Aidha, katika kipindi hicho hicho majosho 3 mapya ya Bulekela, Mwamanota na Mpumbula yalijengwa kwa gharama ya shilingi 44,000,000/=.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2010/2011 Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu iliainisha vipaumbele vichache ambavyo ilivitengea fedha.

Vipaumbele hivyo ni pamoja na kufundisha wafugaji matumizi ya *power tillers,* kupatiwa mashine ya kukamulia mafuta ya alizeti, kununua pikipiki kwa ajili ya maafisa

ugani, ujenzi wa hifadhi ya nafaka na ujenzi wa lambo na haikutenga fedha kwa ajili ya kujenga ofisi ama majosho kutokana na ufinyu wa Bajeti.

Serikali kupitia Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu itatenga fedha kukarabati na kujenga majosho na Ofisi na miundombinu mingine kulingana na upatikanaji wa fedha. *(Makofi)*

**MHE. SULEIMAN M. N. SULEIMAN**: Mheshimiwa Spika, nashukuru. Namshukuru pia Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake. Nina maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo;-

Kwa kuwa wananchi wa Jimbo la Kishapu asilimia 80 ya wananchi hao ni wakulima na wafugaji na Mbunge wao Suleiman Masoud Nchambi Suleiman, akiwa ni mmoja wa wakulima na wafugaji hao.

Kwa kutenga kiasi kidogo cha fedha kwa ajili ya suala zima la ufugaji ni dhahiri kwamba Mheshimiwa Waziri atakubaliana nami kwamba hawaoni umuhimu wa wafugaji wa Jimbo la Kishapu.

Je, Mheshimiwa Naibu Waziri kwa niaba ya Serikali anawaahidi nini wananchi wa Jimbo la Kishapu kwani kutoboresha mazingira ya ufugaji pia kunaleteleza kufifia, kuzembea ama kupotea kabisa kwa bidhaa ambazo zinatembea ardhini kwa maana ya dhahabu zinazotembea mbuzi, ng'ombe, kondoo na kadhalika. Hiyo pia inapelekea kutotimia kwa ahadi ya Mheshimiwa Rais ya soko la mifugo kwa wananchi wa Jimbo la Kishapu na Mkoa wa Shinyanga kwa sababu hata kiwanda cha nyama ambayo ni ahadi ya Mheshimiwa Rais mpaka leo haijakamilika.

Kwa hiyo, mazingira haya ya kutowaandaa wakulima vizuri pia nadhani yanasababisha hata ahadi ile isikamilike kwa sababu hawatakuwa na sehemu nzuri ya kupeleka bidhaa zao?

**SPIKA:** Mheshimiwa usihutubie nataka swali tu.

**MHE. SULEIMAN M. N. SULEIMAN**: Nashukuru sana Mheshimiwa Spika.

**NAIBU WAZIRI MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI**: Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa jinsi anavyofuatilia kwa karibu maendeleo ya wafugaji wa Jimbo lake.

Serikali inaona umuhimu wa mifugo katika nchi nzima na kwa upande tu wa Jimbo lake umuhimu tunauona sana na ndiyo maana katika Bajeti zilizopita 3 jumla ya lita 13,705 za *deep* ya ruzuku zimetolewa kwa ajili ya wafugaji wa eneo hilo kuweza kuogesha. *(Makofi)*

Mbali na hilo miundombinu pia niliyoitaja imekuwa inakazaniwa kuimarishwa na kujengwa kwa sababu Serikali inaona umuhimu wa mifugo na katika jimbo la Kishapu tu kwa mapato ya Halmashauri mifugo imekuwa ikichangia asilimia 3.7 na makusanyo yanapoboreshwa kuna uwezekano wa mifugo kuchangia zaidi ya asilimia 25 ya mapato ya Halmashauri.

Pili, ahadi zilizotolewa na hasa hiyo ya Rais kwa uhakika itatimizwa? Tayari Wizara yangu imekamilisha maandalizi ya Rasimu ya Programu ya Kuendeleza Sekta ya Mifugo. Katika rasimu hiyo mkazo utawekwa katika afya ya mifugo, uboreshaji wa malisho, lakini pia kuboresha miundombinu ya masoko na kiwanda alichokitaja cha *Triple S* itakuwa ni moja kati ya vitu vya kuboreshwa chini ya mkakati huo wa kuimarisha masoko.

**SPIKA:** Mheshimiwa Wabunge muwe mnaangalia muda. Kwa hiyo, maswali yamekwisha na muda tumepita sana.

Tunao wageni katika *gallery* ya Spika. Kwanza leo tutakuwa na Ofisi ya Makamu wa Rais na wapo Maafisa wanaohusika wakiongozwa na Katibu Mkuu Ndugu Sazi Salula. Yupo pamoja na Naibu Katibu Mkuu Ndugu Ngosi Mwihava.

Yupo Mkurugenzi wa Utumishi na Utawala Ndugu Tutubi Deo Magazini. Yuko Mkurugenzi wa Baraza la Hifadhi ya Mazingira (NEMC) Eng. Boniventura Bana. Yupo Mkurugenzi wa Mazingira Dr. Julius Ningu, Yupo Mkurugenzi wa Muungano Ndugu Baraka R. Baraka. Yupo Mkurugenzi wa Sera na Mipango Ndugu Joan Mbuya. Yupo Katibu wa Makamu wa Rais Ndugu Zahoro Haji. Yuko Msaidizi wa Makamu wa Rais Ndugu Jerome Assey. Yupo Msaidizi wa Makamu wa Rais Ndugu Penzi Nyamngumi, Yupo Msaidizi wa Makamu wa Rais Ndugu Seif Msongolo. Hawa ndio wanaokuja kuwasilisha Bajeti yao leo.

Yupo mtoto wa kwanza wa Mheshimiwa Samia Hassan Ndugu Ameir Hafidh Ameir. Leo Waziri ndio anawasilisha hotuba yake.

Tunao wanafunzi 10 wa Shule ya Sekondari ya Bukombe Shinyanga wako wapi hawa wanafunzi. Karibuni sana na poleni na safari. Wapo wanafunzi 45 na walimu 3 wa Shule ya Msingi Chemchem Dodoma naomba wasimame na walimu. Ahsante karibuni sana wanafunzi msome vizuri.

Yupo pia Prof. Kusiluka kutoka Chuo Kikuu Huria yuko na wenzie sijui wako wapi. Huyu hapa Prof. Kusiluka na tunaye barua yao ya Chuo Kikuu Huria nafikiri watakutana na nyie Waheshimiwa Wabunge wakati tutakaokuwa tumepanga, wanakuja kuwaelezeni kuhusu umuhimu wa Chuo Kikuu Huria na kwamba kwa watu *busy* kama nyinyi mnaweza kuwa mnasoma wakati mnaendelea na mambo yenu hapa. Wako wengi humu ndani wamesoma kupitia vyuo hivyo. Kwa hiyo wamekuja wanaongea na wenzetu tuliowateua hapa tuwawakilishe katika Chuo Kikuu Huria.

Kwa hiyo, wakati mwafaka wa kuongea na hawa ndugu tutawapangia na ni vizuri tujifikirie kama mnataka kwenda kusoma huko.

Kuna matangazo ya kazi. Makamu Wenyeviti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini sijui kwa nini wanakutana pamoja. Anaomba niwatangazie Wajumbe hao wa Kamati za Kudumu hizo mbili kwamba leo saa 7.00 mchana kutakuwa na kikao cha Kamati hizo katika ukumbi Na. 231.

Kwa hiyo mtakutana na Chama cha Wanawake Wachimba Madini Tanzania, Tanzania *Women Miners Association* (TAWOMA). Kwa hiyo Kamati ya Katiba na Sheria na Kamati ya Nishati na Madini chumba na. 231 saa 7.00 mnakutana na hao wageni wenu.

Mheshimiwa Abdulkarim Shah, anaomba niwatangazie Waheshimiwa Wabunge kuwa, leo tarehe sita kutakuwa na Kikao cha Wabunge ambao Majimbo yao yanajishughulisha na uvuvi. Ajenda za Kikao zitatolewa hapohapo kwenye kikao. Ninasikia Mheshimiwa Shah ndiyo Mwenyekiti wenu.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji, Mheshimiwa Profesa David Mwakyusa, anaomba Wajumbe wa Kamati yake, wakutane leo saa saba katika Ukumbi Namba 227. Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma za Jamii, Mheshimiwa Dkt. Faustine Ndugulile, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba, leo watakutana saa saba katika Ukumbi wa Pius Msekwa C.

Kwa hiyo, haya ndiyo matangazo ya kazi. Katibu kwa hatua inayofuata.

## KAULI ZA MAWAZIRI

### Hali ya Chakula Nchini

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni Namba 49 (i) na (ii) ya Kanuni za Bunge, Toleo la 2007, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ya kutoa Kauli ya Serikali juu ya Hali ya Chakula Nchini.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2009/10 na mwaka 2010/11, nchi yetu imeshuhudia kuwepo kwa hali ya ukame, inayotokana na mabadiliko ya tabia nchi. Hali hiyo imesababisha maeneo mengi ya nchi kuwa na ukame usiotarajiwa. Mwenendo wa mvua za vuli na za masika kwa ujumla, haukuwa wa kuridhisha. Maeneo mengi ya nchi yanayopata mvua hizo, yalipata mvua za wastani au chini ya wastani na mtawanyiko wa mvua ulikuwa na vipindi virefu vya ukame *(Dry Spells),* ulioathiri ukuaji wa mazao shambani.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla, hali ya upatikanaji wa chakula imeendelea kuwa ya kuridhisha. Pamoja na hali ya chakula kwa ujumla kuwa ya kuridhisha, kuna baadhi ya maeneo yenye upungufu wa chakula kutokana na mvua kutonyesha vizuri katika maeneo yanayopata mvua za vuli na katika baadhi ya maeneo yanayopata mvua za msimu. Hii imechangia kwa kiasi kikubwa, kuwepo kwa upungufu wa chakula katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, tathmini ya awali ya uzalishaji na upatikanaji wa chakula nchini imebaini kuwepo na ziada ya uzalishaji chakula katika Mikoa saba ya Rukwa, Ruvuma, Mbeya, Iringa, Kigoma, Mtwara na Kagera na kumekuwa na Mikoa minane ina utoshelezi ambayo ni Morogoro, Lindi, Tanga, Dodoma, Singida, Tabora, Kilimanjaro na Manyara. Aidha, kuna upungufu katika Mikoa sita ya Mwanza, Shinyanga, Mara, Arusha, Pwani na Dar es Salaam. Aidha, uzalishaji wa chakula nchini hususan nafaka kwa msimu wa kilimo wa 2010/2011 (chakula kinachovunwa sasa), unatarajiwa kufikia tani 6,786,600 wakati mahitaji ni tani 7,200,340 na hivyo kuwa na upungufu Kitaifa wa tani 413,740 za nafaka.

Mheshimiwa Spika, uzalishaji wa mazao ya chakula yasiyo ya nafaka (viazi, muhogo, ndizi, maharagwe na kadhalika), kwa mwaka 2010/2011, unatarajiwa kuwa tani 6,024,217 wakati mahitaji ya Taifa ni tani 4,299,073; hivyo kuwa na ziada ya tani 1,725,143. Kwa ujumla tunayo ziada ya chakula. Pamoja na ziada hiyo, Wananchi walio wengi hutumia zaidi vyakula vya nafaka; hivyo, ni dhahiri kuwa upungufu wa nafaka unaashiria kuwepo kwa upungufu wa chakula nchini. Tathmini ya awali ya upatikanaji wa chakula pia imebainisha kuwepo kwa upungufu wa chakula katika Wilaya 48 zilizo katika mikoa 16. Wilaya hizo zimeoneshwa katika karatasi ambayo mtapewa.

Mheshimiwa Spika, bei ya mazao ya nafaka katika masoko makuu nchini bado ipo juu licha ya kuwa huu ni mwanzo wa mavuno na licha ya juhudi za Serikali za kutoa akiba kutoka kwenye Maghala ya Taifa ili kukabiliana na kupanda kwa bei hizo. Kwa mfano, bei ya mahindi kwa kilo kwa baadhi ya miji ni kama ifuatavyo:-

Musoma ni shilingi 600, Moshi 500, Tanga shilingi 500, Mwanza shilingi 485, Singida shilingi 485, Arusha shilingi 465, Tabora shilingi 450, Dar es Salaam shilingi 450 na Shinyanga shilingi 430. Bei ya wastani ya mahindi ya tarehe 6 Juni, 2011 *(Spot Price)*, kwa kilo ni shilingi 440. Bei ya mchele kwa kilo iliongezeka kutoka shilingi 1,040 mwezi Januari hadi 1,260 mwezi Mei, 2011 wakati bei za mazao mengine hususan maharage nazo zimeendelea kupanda.

Mheshimiwa Spika, hali ya Chakula Duniani na Nchi jirani: Taarifa ya Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa *(FAO)*, iliyotolewa mwezi Mei, 2011 inaonesha kuwa, katika mwaka 2010/2011, uzalishaji wa nafaka duniani unatazamiwa kushuka kwa asilimia 1.2. Kutokana na kushuka huko, takriban nchi 30 duniani zinatazamiwa kukabiliwa na upungufu wa chakula na zitahitaji chakula cha msaada. Nyingi ya nchi hizo zipo katika kundi la nchi maskini zenye kipato kidogo za Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla, mavuno pungufu hasa kwa mazao ya nafaka yanayotazamiwa katika msimu wa 2010/2011, yataathiri hali ya chakula hususan miongoni mwa jamii za wafugaji katika Nchi za Afrika Mashariki. Aidha, baadhi ya nchi jirani hususan Burundi, Somalia, Kenya, Uganda, Congo (DRC), Sudan ya Kusini, Madagascar na Msumbiji, zinatazamiwa kuwa na maeneo yanayokabiliwa na upungufu wa chakula kutokana na sababu mbalimbali hasa ukame na vita vya wenyewe kwa wenyewe.

Mheshimiwa Spika, kutokana na sababu hizo, bei za mazao ya nafaka katika maeneo hayo hususan, Kenya Uganda, Somalia ya Kusini na Sudan ya Kusini, zimeendelea kupanda kuanzia kipindi cha Januari hadi Mei, 2011. Bei za juu zaidi zimeripotiwa katika masoko ya Kampala, Mogadishu, Juba na Nairobi, ambako kwa ujumla bei za sasa za mahindi zimepanda kwa zaidi ya asilimia 120, ikilinganishwa na viwango vya mwezi Aprili, 2011. Kwa mfano, katika Soko la Nairobi, bei ya mahindi imepanda kutoka dola 215 kwa tani au shilingi 323 za Kitanzania kwa kilo mwezi Januari hadi kufikia dola 465 kwa tani au shilingi 744 za Kitanzania kwa kilo mwezi Juni, 2011, sawa na ongezeko la asilimia zaidi ya 130. Kwa upande wa Kenya, tatizo hili limeongezeka kutokana na kuporomoka kwa thamani ya Shilingi ya Kenya na hivyo bei ya mahindi kupanda sana kwa mlaji. Aidha, Serikali ya nchi hiyo imetangaza kushuka kwa uzalishaji wa mahindi kwa magunia milioni 14.8 au tani 1.322 milioni za mahindi. Hali hii ya ongezeko la bei ya mazao ya chakula hususan yale ya nafaka, imechochea ongezeko kubwa la biashara ya mazao ya chakula kutoka nchini kwenda nchi hizo jirani. Biashara hiyo imechochea chakula kingi nchini kupelekwa Kenya, Uganda, Burundi, Sudan Kusini, Somali na Kongo (DRC).

Mheshimiwa Spika, ili kukabiliana na upungufu wa chakula uliojitokeza katika Wilaya 48 nchini, Serikali ama imekwisha chukua au inaendelea kuchukua hatua zifuatazo:-

(i) Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu, inaendelea na usambazaji wa chakula cha msaada wa tani 36,970 zilizoidhinishwa na Serikali kwa walengwa walioathiriwa na upungufu wa chakula katika maeneo mbalimbali nchini. Hadi tarehe 30 Juni, 2011 jumla ya tani 30,301.884 za mahindi zilikuwa zimechukuliwa na Halmashauri husika kutoka *NFRA* na kusambazwa kwa walengwa.

(ii) Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula *(NFRA)* inaendelea na hatua za kuhamisha jumla ya tani 115,000 za akiba ya chakula iliyoko kwenye vituo vyake vilivyoko Sumbawanga, Makambako na Songea kwenda kwenye maghala yaliyo karibu na maeneo yenye upungufu wa chakula ya Dar es Salaam, Dodoma, Shinyanga na Arusha. Hatua hii itaiwezesha Serikali kukabiliana na upungufu wa chakula na mahitaji mengine ya soko kwa haraka zaidi na pia itatoa nafasi ya kuhifadhi nafaka itakayonunuliwa msimu wa ununuzi wa 2011/2012, unaotarajiwa kuanza tarehe 15 Julai, 2011.

(iii) *NFRA* inaendelea na zoezi la uuzaji wa mahindi kiasi cha tani 50,000 zilizotengwa kwa ajili ya kudhibiti upandaji wa bei ya mahindi na unga hususan mijini ili kukidhi dhamira ya Serikali ya kuhakikisha Wananchi wanapata unga kwa bei nafuu. Utaratibu huu unahusisha mikoa 13 ya Dar es salaam, Pwani, Arusha, Dodoma, Kilimanjaro, Singida, Morogoro, Mwanza, Mara, Mtwara, Lindi, Shinyanga, na Tabora.

(iv) Kutokana na bei nzuri sana ya mahindi na mpunga na mazao mengine ya chakula kwa wakulima, wakulima wengi wanauzia mazao yao shambani na upo uwezekano wa kuuza mavuno yote bila kujiwekea akiba. Hivyo, Serikali inawahimiza Wananchi wote katika ngazi ya kaya hususan wakulima, wajiwekee akiba ya chakula cha kutosha kwa ajili ya mahitaji ya kaya zao mpaka msimu ujao.

(v) Serikali inawahimiza Wananchi kutumia aina mbalimbali za chakula ikiwa ni pamoja na muhogo, viazi vitamu, viazi mviringo, ndizi na vyakula vingine ambavyo vinapatikana kwa wingi katika maeneo yetu.

(vi) Serikali imeagiza Mikoa na Halmashauri za Wilaya zenye upungufu wa chakula, kuongeza upatikanaji wa chakula katika maeneo yao kwa kuhamasisha wafanyabiashara wenye uwezo wa kununua chakula kutoka mikoa yenye ziada kwa ajili ya kuuza kwa Wananchi katika maeneo yao yenye upungufu.

(vii) Kuiwezesha Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko katika mwaka 2011/2012, kununua mazao kutoka kwa wakulima wa Mikoa ya Rukwa, Katavi, Iringa, Mbeya, Ruvuma, Kigoma na Morogoro na kuyauza katika mikoa yenye upungufu wa chakula. Manunuzi haya yatatumia fedha zilizotengwa kwenye bajeti ya mwaka 2011/2012 (tani 16,000) na mikopo kupitia Taasisi za Fedha ili kuhakikisha kwamba, ununuzi wa chakula unaongezeka.

(viii) Kuiwezesha *NFRA* kununua tani 200,000 za nafaka kutoka kwa Wakulima wa Mikoa ya Rukwa, Katavi, Iringa, Mbeya na Ruvuma na kuzihifadhi katika maghala yake kwa ajili ya kukabiliana na upungufu wa chakula unaoweza kujitokeza.

Mheshimiwa Spika, pamoja na juhudi za Serikali za kuhakikisha upatikanaji wa chakula nchini, ninapenda kurudia kuwa, hivi sasa kumezuka tabia ya baadhi ya wafanyabiashara kwenda kwa wakulima na kununua mazao yakiwa bado mashambani. Kwa kufanya hivyo, imebainika kuwa, bei wanazopewa wakulima ni za chini mno na hivyo wakulima kutopata stahili ya jasho lao. Serikali inaandaa mpango wa kujenga masoko na maghala ya chakula katika maeneo ya uzalishaji ili kuwawezesha wakulima kutumia utaratibu wa stakabadhi ghalani kwa kuuza mazao yao. Aidha, katika sehemu za mipakani, imedhihirika kuwa, mazao ya chakula na hasa nafaka, yanavushwa kwenda nchi za jirani kwa vibali vya kugushi na nafaka na vyakula vingine vinaondoka nchini kwa kasi inayohatarisha usalama wa chakula nchini.

Mheshimiwa Spika, ili kuepuka hatari ya Taifa kukumbwa na tatizo kubwa la upungufu wa chakula, Serikali imeamua kuchukua hatua za ziada kama ifuatavyo:-

- Kuanzia tarehe 1 Julai, 2011 Serikali imefuta vibali vyote ambavyo vilikwishatolewa kwa maombi ya kusafirisha mazao ya chakula nje ya nchi.

- Kupiga marufuku uuzaji wa mazao yote ya chakula nje ya nchi kwa kipindi cha miezi sita kuanzia tarehe 1 Julai, 2011 hadi tarehe 31 Desemba, 2011.

Mheshimiwa Spika, madhumuni ya hatua hizi ni pamoja na kuipa Serikali, nafasi ya kufuatilia mwenendo mzima wa upatikanaji wa chakula nchini, kwa lengo la kujihakikishia usalama wetu wa chakula katika kipindi hicho na baada ya hapo. Aidha, Serikali inawakaribisha nchi jirani zenye upungufu wa chakula na zinazohitaji kununua chakula nchini, kushauriana na Serikali moja kwa moja ili wauziwe chakula kwa utaratibu wa biashara ya Kimataifa badala ya biashara inayoendelea sasa.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge, ninawashukuru sana kwa kunisikiliza. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, ahsante sana. Tunashukuru kwa taarifa hiyo. Tuliona taarifa isomwe hiyo kwa sababu ya hali halisi ya upungufu wa chakula ndani ya nchi. Sasa tunaendelea; Katibu kwa hatua inayofuata.

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2010/2011
### Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO):** Mheshimiwa Spika baada ya kupokea Taarifa iliyowasilishwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira na ile iliyowasilishwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Kadumu ya Bunge, Katiba Sheria na Utawala kuhusu utekelezaji wa shughuli katika Ofisi ya Makamu wa Rais, ninaomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu sasa likubali kupokea, kujadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha ya Ofisi ya Makamu wa Rais ya Mwaka 2011/2012.

Mheshimiwa Spika, ninaomba nitumie fursa hii, kuwapongeza Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Dkt. Mohamed Gharib Bilal, kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kuchaguliwa kwao kwa ushindi mkubwa ni ishara ya imani ya Wananchi kwa Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninapenda kutoa shukrani za pekee kwa aliyekuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein, kwa uongozi wake thabiti na maelekezo aliyotupa katika kutekeleza majukumu yetu. Aidha, ninampongeza kwa kuchaguliwa kwake kuwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Vilevile ninawapongeza Wananchi wa Zanzibar kwa kuwa na

Serikali ya Umoja wa Kitaifa. Ni nia ya Serikali kuona kuwa kunakuwa na amani katika pande zote mbili za Muungano ili kudumisha Muungano wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia ninapenda kumpongeza Mheshimiwa Mizengo Kayanza Pinda, kwa kuteuliwa tena na kuthibitishwa na Bunge hili Tukufu kuwa Waziri Mkuu. Aidha, ninakupongeza wewe Mheshimiwa Anne Makinda, kwa kuchaguliwa kuwa Spika wa Bunge hili kwa kura nyingi na kutuwakilisha vyema sisi Wabunge Wanawake na Wanawake wa Tanzania nzima. Ninampongeza pia Mheshimiwa Job Y. Ndugai, Naibu Spika, kwa kuchaguliwa kushiriki nafasi hiyo. Vilevile ninawapongeza Wabunge na Madiwani wote, waliopata ridhaa ya Wananchi ya kuongoza kwa kupigiwa kura za kutosha katika Uchaguzi wa Oktoba 2010. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninapenda kutoa shukrani kwa wote walioshiriki kwa namna moja au nyingine, kufanikisha matayarisho ya Bajeti. Kwa namna ya pekee, ninapenda kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala chini ya Mwenyekiti wake, Mheshimiwa Pindi Hazara Chana, Mbunge wa Viti Maalum, Mkoa wa Iringa, pamoja na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira, chini ya Mwenyeketi wake Mheshimiwa James Daudi Lembeli, Mbunge wa Kahama, kwa ushauri, maoni na ushirikiano walioutoa katika kuimarisha utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Makamu wa Rais. Ofisi imezingatia ushauri na mapendekezo yaliyotolewa na Kamati na itazingatia yale yatakayotolewa na Waheshimiwa Wabunge wakati wa kuchangia hoja hii.

Mheshimiwa Spika, ninapenda kuwashukuru Mheshimiwa Pauline Philipo Gekul na Mheshimiwa Susan Anselm Jerome Lyimo; Wasemaji Wakuu wa Kambi ya Upinzani kuhusu Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), kwa ushirikiano na michango yao katika kuimarisha hoja hii. Vilevile, nichukue nafasi hii maalum kumshukuru Mheshimiwa Leticia Mageni Nyerere, aliyekuwa Msemaji wa Kambi ya Upinzani kuhusu masuala ya Mazingira, kwa michango yake mizuri katika kutayarisha hoja hii. Ninapenda pia kutoa shukrani zangu za dhati kwa Waziri mwenzangu, Mheshimiwa Dkt. Terezya Luoga Huvisa, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira), kwa ushirikiano na utendaji wake thabiti na makini katika kutekeleza majukumu ya Ofisi hii.

Mheshimiwa Spika, nitakuwa mchoyo wa fadhila kama sitawashukuru Wafanyakazi wote wa Ofisi ya Makamu wa Rais. Kipekee, ninapenda kumshukuru Katibu Mkuu, Bwana Sazi Bundara Salula, Naibu Katibu Mkuu, Mhandisi Ngosi Charlestino Mwihava, Wakurugenzi, Mkurugenzi Mkuu wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira na Wakuu wa Vitengo, kwa michango yao katika kufanikisha utekelezaji wa shughuli za Ofisi.

Mheshimiwa Spika, ninapenda kutumia fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati kwa Wananchi wa Jimbo langu la Makunduchi, kwa kunipa heshima na dhamana ya kuwa Mbunge wao kwa kipindi hiki. Aidha, kwa niaba ya Mheshimiwa Dkt. Terezya Luoga Huvisa, Waziri wa Nchi katika Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira), ninatoa

shukrani za dhati kwa Taasisi za Elimu ya Juu kwa kumpa heshima na dhamana ya kuwa mwakilishi wao Bungeni.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee na kwa heshima na taadhima, nichukue nafasi hii vilevile kumshukuru Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kutupa dhamana ya kusimamia Masuala ya Mazingira na Muungano katika Ofisi ya Makamu wa Rais. Tunaahidi kushirikiana katika kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi na hivyo, kuiendeleza Nchi yetu kwa Ari zaidi, Nguvu zaidi na Kasi zaidi.

Mheshimiwa Spika, ninapenda kuwashukuru na kuwapongeza Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda, Mbunge, Waziri wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Capt. George Huruma Mkuchika, Mbunge, Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Mustafa Haidi Mkulo ,Mbunge na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Mheshimiwa Hawa Abdulrahman Ghasia, Mbunge, Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Mahusiano na Uratibu, Mheshimiwa Stephen Wasira, Mbunge, kwa hotuba zao ambazo zimefafanua kwa kina utekelezaji wa Sera, Mipango na Mikakati ya Serikali na kutoa mwelekeo wa kazi za Serikali kwa Mwaka wa Fedha wa 2011/12.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha wa 2010/11, Ofisi ya Makamu wa Rais, imeendelea kutekeleza majukumu iliyokabidhiwa kwa kuzingatia Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977, Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, Malengo ya Maendeleo ya Milenia, Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania (MKUKUTA), Sera ya Mazingira ya Mwaka 1997, Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Sura ya 191 na Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi (CCM) ya Mwaka 2010 - 2015.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa niongelee masuala ya Muungano. Katika masuala ya Muungano, Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2010 – 2015, Ibara ya 183, inaelekeza kuwa, ili kuimarisha Muungano, Serikali itajenga mazingira endelevu na kuimarisha fursa za kiuchumi miongoni mwa Wananchi wa kila upande, ili waone na kuamini kwamba, Muungano wa Tanganyika na Zanzibar siyo tu ni ngao madhubuti ya Umoja, Amani na Mshikamano wao, bali pia ni daraja la kuwafikisha katika azma yao ya kuondokana na umaskini na kuharakisha maendeleo yao na Taifa kwa jumla. Aidha, Ofisi imeweza kutekeleza maelekezo ya Ilani ya CCM, Ibara ya 184 kama ifuatavyo:-

(a) Kukamilisha ujenzi wa majengo na Taasisi za Muungano ambazo zimeanzishwa Tanzania Bara na Zanzibar;

(b) Kuimarisha utendaji wa Kamati ya Pamoja ya kutatua changamoto za Muungano kwa kuandaa utaratibu madhubuti wa vikao vya Kamati na utekelezaji wa haraka wa maamuzi yanayofikiwa;

(c) Kuboresha uchangiaji na mgawanyo wa mapato ya Muungano;

(d) Kuzifanyia mapitio na uboreshaji Sheria na Kanuni za Fedha zinazotawala ukusanyaji wa mapato chini ya Mamlaka ya Mapato Tanzania *(TRA)* na Bodi ya Mapato Zanzibar *(ZRB)*, upande wa Tanzania Zanzibar, kwa lengo la kukuza ufanisi katika ukusanyaji wa mapato hayo;

(e) Kuboresha Sheria, Kanuni na taratibu za ajira ya Watumishi katika Taasisi za Muungano ili utumishi huo uwe na sura mwafaka ya ki-Muungano;

(f) Kuimarisha utaratibu wa kuandaa na kutekeleza mikakati na mbinu za pamoja zenye lengo la kuinua uchumi wa pande zote mbili za Muungano; na

(g) Kuendeleza Miradi ya pamoja ya kiuchumi, miundombinu na ya kijamii iliyokwishaanzishwa ikiwemo ya *Tanzania Social Action Fund (TASAF)* na *Marine and Coastal Environment Management Project (MACEMP).*

Mheshimiwa Spika, Ofisi imeanza kutekeleza maelekezo ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2010 kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ukamilishaji wa ujenzi wa majengo ya Taasisi za Muungano zilizoanzishwa Zanzibar unaendelea. Majengo ya Taasisi za Muungano yanayojengwa Zanzibar ni pamoja na Ofisi ya Idara ya Uhamiaji na Makao Makuu ya Mamlaka ya Uvuvi katika Ukanda wa Bahari Kuu - Fumba. Aidha, Serikali inaendelea na ukamilishaji wa awamu ya pili ya ujenzi wa Ofisi ya Makamu wa Rais, Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, ili kuimarisha utendaji wa Kamati ya Pamoja ya kutatua changamoto za Muungano kwa kuandaa utaratibu madhubuti wa Vikao vya Kamati na utekelezaji wa haraka wa maamuzi yanayofikiwa, pande mbili za Muungano zilikubaliana kuwa na utaratibu wa sekta zenye hoja kukutana na kujadiliana na kutoa mapendekezo kwa Kamati. Vikao vya sekta kutoka Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (SMT) na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) katika ngazi za Mawaziri, Makatibu Wakuu na Wataalamu vimefanyika. Vikao hivyo vilifanyika kwa sekta ya fedha tarehe 8 Machi, 2011, 10 Machi, 2011, 24 Machi, 2011 na 5 Aprili, 2011; Wizara za fedha zilijadiliana kuhusu hoja za marekebisho ya Sheria za Kodi, Sheria za Usajili wa Vyombo vya Moto, hisa za SMZ zilizokuwa katika Bodi ya Sarafu ya Afrika Mashariki na faida ya Benki Kuu.

Mheshimiwa Spika, kwa masuala ya nishati, vikao vilifanyika tarehe 7 Machi, 2011 na tarehe 31 Machi, 2011, ambapo sekta zilijadiliana kuhusu ongezeko kubwa la Ankara za Umeme kutoka Shirika la Umeme Tanzania kwenda Shirika la Umeme Zanzibar. Aidha, suala la ajira kwa Watumishi wa Zanzibar katika Taasisi za Muungano lilijadiliwa tarehe 14 Aprili, 2011, 15 Aprili, 2011 na 21 Aprili, 2011 na tarehe 2 Mei, 2011. Aidha, kikao cha masuala ya Jumuiya ya Afrika Mashariki kilifanyika tarehe 21 Aprili, 2011 kujadili Miradi ya Maendeleo inayoombewa ufadhili chini ya Jumuiya ya Afrika Mashariki. Vikao hivi vimechangia kurahisisha utendaji wa Kamati ya Pamoja ya SMT na SMZ ya kushughulikia masuala ya Muungano.

Mheshimiwa Spika, Tume ya Pamoja ya Fedha imekamilisha mchakato wa kitaalamu wa kuchambua na kupendekeza vigezo vya mgawanyo wa mapato na uchangiaji wa gharama za Muungano. Mapendekezo hayo yamewasilishwa rasmi kwa Serikali zote mbili kwa maamuzi.

Mheshimiwa Spika, pande mbili zimekubaliana kufanya uboreshaji wa Sheria na Kanuni za Fedha na majadiliano yanaendelea ili kufikia mwafaka juu ya kuzifanyia mapitio na uboreshaji, Sheria na Kanuni za Fedha zinazotawala ukusanyaji wa mapato chini ya *TRA* na *ZRB* upande wa Tanzania Zanzibar, kwa lengo la kukuza ufanisi katika ukusanyaji wa mapato hayo.

Mheshimiwa Spika, vilevile Kamati ya Makatibu Wakuu wa Sekta za Utumishi wa Umma pande mbili za Muungano, zinaendelea na kazi ya uboreshaji wa Sheria, Kanuni na Taratibu za Ajira ya Watumishi katika Taasisi za Muungano. Kazi hiyo inatarajiwa kukamilika ndani ya mwaka huu na kuwasilishwa kwenye Kamati ya Pamoja ya SMT na SMZ kwa maamuzi.

Mheshimiwa Spika, mikakati na mbinu za pamoja zimeandaliwa ili kuinua uchumi wa pande zote mbili za Muungano. Mikakati ya MKUKUTA na MKUZA imeandaliwa na kutekelezwa na pande zote mbili za Muungano, misaada ya wafadhili isiyo na masharti na mikopo kutoka nje imeendelea kugawanywa kwa pande mbili ili kuinua uchumi. Aidha, Miradi minane ipo katika hatua za kuombewa ufadhili chini ya mwamvuli wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Ofisi itaendelea kuhimiza uandaaji na utekelezaji wa mikakati na mbinu za pamoja ili kunufaisha pande zote mbili kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, Miradi ya Maendeleo imeendelea kutekelezwa na kunufaisha pande zote za Muungano. Mfano wa Miradi ya Maendeleo iliyoandaliwa na kutekelezwa pande zote mbili ni Mradi wa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii *(TASAF)* na Mradi wa Usimamizi wa Mazingira ya Bahari na Ukanda wa Pwani ya Tanzania *(MACEMP).*

Mheshimiwa Spika, mapitio ya utekelezaji wa mpango wa mwaka 2010/11 na malengo ya mwaka 2011/12: Kama inavyofahamika, mwaka huu wa 2011 Muungano wetu umetimiza miaka 47. Katika kipindi hicho, Muungano wetu umekuwa na mafanikio katika maeneo ya kijamii, kiuchumi na kisiasa. Wananchi wanaendelea kunufaika kwa kupata fursa ya kuishi kwa amani na kufanya shughuli za kimaendeleo popote katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Sote ni mashahidi kuwa, Muungano wetu ndiyo nguzo kuu ya umoja na amani.

Mheshimiwa Spika, Katika Mwaka wa Fedha wa 2010/11, Ofisi imeendelea kutekeleza majukumu yake ya msingi ya kufuatilia utekelezaji wa kila siku wa mambo ya Muungano na yasiyo ya Muungano ili kudumisha Muungano na ushirikiano wa Serikali zote mbili. Katika kipindi hicho, Ofisi ilipanga na kutekeleza yafuatayo:-

Kuondoa vikwazo katika utekelezaji wa masuala ya muungano: Katika kujadili na kutafuta ufumbuzi wa changamoto katika utekelezaji wa masuala ya Muungano, Ofisi iliandaa na kufanya vikao viwili vya Sekretarieti ya Kamati ya Pamoja ya SMT na SMZ

vilivyofanyika tarehe 7 Februari, 2011, Zanzibar na tarehe 28 Februari, 2011, Dar es Salaam, kwa ajili ya maandalizi ya Vikao vya Makatibu Wakuu, Mawaziri na Kikao cha Kamati ya Pamoja ya SMT na SMZ. Kikao cha Makatibu Wakuu wa SMT na SMZ kilifanyika tarehe 1 Machi, 2011 Dar es Salaam na kikao cha Mawaziri wa SMT na SMZ kilifanyika tarehe 19 Machi, 2011, Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, katika vikao hivyo, pamoja na mambo mengine, suala la wafanyabiashara wa Zanzibar kutozwa kodi mara mbili lilijadiliwa. Utakumbuka kuwa, Bunge lako Tukufu katika Mwaka wa Fedha wa 2010/11, lilielezwa kwamba, suala hili lilishapatiwa ufumbuzi. Hata hivyo, ninasikitika kusema kwamba, kutokana na sababu za kiutendaji na utaratibu uliokuwepo, suala hili lilionekana kuwa bado ni changamoto. Ili kukabiliana na changamoto hiyo, Mamlaka ya Mapato Tanzania, imetengeneza mfumo mpya *(Import - Export Valuation Database)*, ambao unathaminisha sawa viwango vya kodi kwa bidhaa zinazotoka nje ya nchi kwa Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar. Mfumo huo umeanza kutumika tarehe 25 Februari, 2011. Aidha, Mamlaka ya Mapato Tanzania, imeahidi kufanya ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa mfumo huu.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Pamoja ya SMT na SMZ imeendelea kulifanyia kazi suala la ushirikiano wa Zanzibar na Taasisi za Nje. Katika kipindi hiki, mwongozo wa namna ya kuishirikisha SMZ katika masuala yote ya Kimataifa kuanzia hatua za awali unaandaliwa. Mwongozo huo utazingatia maeneo ya ziara za Viongozi wa Kitaifa; Mikutano ya Kimataifa; nafasi za masomo ya elimu ya juu nje ya nchi; na utafutaji fedha za misaada za kutekeleza Miradi mbalimbali kutoka nje ya nchi. Katika Mwaka wa Fedha wa 2011/12, Ofisi itaendelea kuratibu Vikao vya Kamati ya Pamoja ya SMT na SMZ ya kushughulikia masuala ya Muungano.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha wa 2010/11, Ofisi imeendelea kuratibu gawio la asilimia 4.5 kwa SMZ litokanalo na misaada ya kibajeti ya kila mwaka na hadi kufikia Julai, 2010 SMZ ilipata shilingi bilioni 37.6 kati ya shilingi bilioni 33.5 zilizokadiriwa kwa mwaka 2010/11 ili kuimarisha ushirikiano wa kiuchumi na kijamii. Fedha hizi zilitumika kutekeleza Miradi ya Maendeleo katika Sekta za Kiuchumi na Kijamii Zanzibar kulingana na vipaumbele vya mwaka huo. Aidha, kwa mujibu wa Sheria Na.16 ya Mwaka 2009 ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo, inamtaja Waziri anayeshughulikia masuala ya Muungano kuwa, ndiye mratibu wa Mfuko huu kwa upande wa Zanzibar. Kwa mwaka huo wa fedha, Ofisi ilipokea shilingi bilioni 1.24 kwa ajili ya Majimbo ya Zanzibar. Katika Mwaka wa Fedha wa 2011/12, Ofisi itaendelea kuratibu masuala ya kiuchumi, kijamii na kisheria na mambo yanayohusiana na Katiba katika Muungano kwa faida ya pande mbili za Muungano.

Mheshimiwa Spika, katika jitihada za kutoa elimu kwa umma kuhusu masuala ya Muungano, kwa Mwaka wa Fedha wa 2010/11, Ofisi ilishiriki katika Maonesho ya Nane Nane yaliyofanyika Mjini Dodoma, kuanzia tarehe 1 - 8 Agosti, 2010; na yale ya Wiki ya Utumishi wa Umma kuanzia tarehe 16 - 23 Juni, 2011 Dar es Salaam. Vile vile Ofisi ilichapisha nakala 18,000 za Jarida la Muungano Wetu, Toleo la Pili, nakala 2,850 za Kitabu cha Picha, kinachoonesha matukio mbalimbali ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar kwa kipindi cha 1964 - 2010 na nakala 4,000 za Kalenda ya Mwaka 2011 na kusambazwa kwa wadau. Aidha, Ofisi iliandaa na kurusha vipindi maalum vya runinga

katika Maadhimisho ya Siku ya Mapinduzi Zanzibar yaliyofanyika tarehe 12 Januari, 2011 Zanzibar na Maadhimisho ya Miaka 47 ya Muungano yaliyofanyika tarehe 26 Aprili, 2011, Zanzibar. Aidha, toleo la Taarifa Maalum ya Muungano kwenye Magazeti ya Uhuru, Habari Leo na Zanzibar Leo, lilichapishwa. Vilevile elimu ya Muungano ilitolewa kwa Wananchi wakati wa uzinduzi wa Maadhimisho ya Miaka 50 ya Uhuru wa Tanzania Bara, uliokwenda sanjari na Siku ya Mazingira Duniani, yaliyofanyika Kitaifa Mkoani Ruvuma. Katika Mwaka wa Fedha wa 2011/12, Ofisi itaendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu masuala ya Muungano kupitia redio, runinga, vijarida, makala za magazeti, vipeperushi na maonesho ya kitaifa.

Mheshimiwa Spika, mbali na kushughulikia masuala ya Muungano, Ofisi inaratibu ushirikiano katika masuala yasiyo ya Muungano kisera, kubadilishana utaalamu na wataalamu, ushiriki katika masuala ya kitaifa, kikanda na kimataifa, utafiti na ziara za mafunzo. Katika Mwaka wa Fedha wa 2010/11, Ofisi iliandaa na kusambaza Ratiba ya Vikao kwa Wizara/Sekta zinazohusika. Katika kipindi hicho, vikao vimefanyika katika Sekta za Viwanda, Biashara na Masoko; Katiba na Sheria; Miundombinu na Mawasiliano na Sekta ya Maji, Sekta ya Nishati na Utumishi wa Umma.

Mheshimiwa Spika, katika Sekta ya Viwanda, Biashara na Masoko, masuala yaliyojadiliwa yalihusu ufunguaji wa Ofisi za TANTRADE Zanzibar, suala la ajira, suala la wafanyabiashara kutozwa kodi mara mbili, kuangalia uwezekano wa kuondoa kodi ya ziada ya asilimia mbili inayotozwa kwa bidhaa zinazotoka nje ya nchi na kuimarisha ushirikiano katika suala la vipimo na mizani. Aidha, Wizara za Katiba na Sheria za SMT na SMZ zilijadili masuala ya miundo ya Wizara za Katiba na Sheria za pande mbili za Muungano na namna ya kuiboresha miundo hiyo na utoaji huduma za msaada wa kisheria kwa pande zote mbili. Vilevile sekta zilijadili changamoto zinazojitokeza na namna ya kukabiliana nazo na kuainisha maeneo ya ushirikiano ambayo ni mikataba ya kimataifa, mikutano, mafunzo na Miradi ya pamoja.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Uchukuzi ya SMT na Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano ya SMZ zilijadili masuala ya kiutendaji yakiwemo ya utafutaji na uokoaji wa vyombo vya usafiri majini vinavyohitaji msaada, kulinda mazingira ya bahari, malipo ya gharama za uendeshaji wa Kituo cha Taarifa cha Kitaifa cha kutambua na kufuatilia meli kutoka umbali mrefu *(National Long Range Identification and Tracking of Ships – LRIT Data Centre)*, usalama wa meli zinazosajiliwa chini ya Bendera ya Tanzania na Rejesta ya Zanzibar *(Zanzibar International Register of Shipping TZIRS)*, masuala ya uharamia na ugaidi kwenye vyombo vya usafiri na udhibiti wa ushindani katika boti za abiria.

Mheshimiwa Spika, aidha, Sekta za Maji za SMT na SMZ zilijadiliana na kukubaliana maeneo ya ushirikiano. Maeneo hayo ni pamoja na ushirikiano katika mikutano inayohusu Sekta ya Maji ndani na nje ya nchi, ukusanyaji wa takwimu za maji, mafunzo na mfumo pepe wa kupata taarifa za maji na usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji. Katika Mwaka wa Fedha wa 2011/12, Ofisi itaendelea kuratibu ushirikiano katika masuala yasiyo ya Muungano kwa kuhakikisha kwamba, Sekta, Wizara na Asasi zisizo za Muungano, zinakutana angalau mara nne kwa mwaka.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio yaliyopatikana katika kutekeleza masuala ya Muungano, zimejitokeza changamoto zikiwemo za kuuelimisha umma kuhusu masuala ya Muungano na yasiyo ya Muungano. Aidha, Serikali inatambua kuwa zipo changamoto katika kumaliza vikwazo vinavyokwamisha shughuli za Muungano. Dhamira ya Serikali zetu mbili ni kuondoa vikwazo hivyo kwa kuhakikisha kwamba, vinatatuliwa ipasavyo ili Muungano uendelee kuwa imara.

Mheshimiwa Spika, katika masuala ya Hifadhi ya Mazingira, Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2010-2015, Ibara ya 193 (ukurasa wa 92 - 93), inaelekeza kuwa, Chama kitahakikisha kuwa, kazi iliyoanzwa ya Hifadhi ya Mazingira inakuwa endelevu. Aidha, katika Ibara hiyo, Serikali inaelekezwa kutekeleza mambo yafuatayo:-

(a) Kuimarisha zoezi la kitaifa la kupanda miti hususan miti ya asili kila mwaka katika maeneo yaliyotengwa kwa ajili hiyo. Viongozi wa Vitongoji, Mitaa, Vijiji na Kata watakiwe kuikagua mara kwa mara miti iliyopandwa ili kuhakikisha inakua. Aidha, miti ipandwe katika maeneo ya shule, barabara, zahanati za vijiji, Vituo vya Afya na makazi ya watu. Wakuu wa maeneo hayo wahakikishe lengo la kupanda miti linafanikiwa.

(b) Serikali za Vijiji na Halmashauri za Wilaya na Manispaa zitunge sheria ndogo za Hifadhi ya Misitu.

(c) Kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Hifadhi ya Mazingira katika vyanzo vya maji na kusimamia utekelezaji wa mkakati usafi katika fukwe.

(d) Serikali ichukue hatua ya kuandaa sera na kutunga sheria itakayosimamia matumizi ya nishati mbadala ili kupunguza uharibifu wa mazingira.

(e) Kupunguza gharama ya vifaa vya nishati mbadala ili Wananchi wanaojenga nyumba za kisasa vijijini watumie nishati hiyo badala ya kuni na mkaa wa miti.

(f) Kuhimiza na kuhamasisha ufugaji wa kisasa vijijini ili uwe kichecheo cha hifadhi ya mazingira.

(g) Serikali iimarishe usimamizi wa viwanda na biashara kutochafua mazingira.

(h) Kutekeleza mradi wa vijiji vya mfano vya hifadhi ya mazingira *(eco-village).*

(i) Vipeperushi vyenye mafunzo rahisi ya hifadhi ya mazingira viandaliwe, vichapishwe kwa wingi na vitumike kwenye mafunzo ya elimu yenye manufaa nchini kote.

(j) Kufanya tathmini ya athari za kimazingira katika Miradi ya ujenzi.

Mheshimiwa Spika, Ofisi imeendelea kutekeleza maelekezo ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2010 kama ifuatavyo:-

Kuimarisha zoezi la kitaifa la kupanda miti na miti ya asili kila mwaka katika maeneo yaliyotengwa kwa ajili hiyo. Viongozi wa Vitongoji, Mitaa, Vijiji na Kata, watakiwe kuikagua mara kwa mara miti iliyopandwa ili kuhakikisha inakua. Aidha, miti ipandwe katika maeneo ya shule, barabara, zahanati za kijiji, Vituo vya Afya na makazi ya watu. Wakuu wa maeneo hayo wahakikishe lengo la kupanda miti linafanikiwa.

Mheshimiwa Spika, Ofisi imeendelea kuratibu na kufuatilia utekelezaji wa Kampeni ya upandaji miti hapa nchini. Kwa mujibu wa taarifa ya kipindi cha mwaka 2009/10, jumla ya miti 198,331,913 ilipandwa, ikiwa ni sawa na asilimia 76 ya miche ya miti yote iliyokuwa imelengwa kupandwa. Kati ya miti iliyopandwa, miti iliyoota ni 152,404,333, sawa na asilimia 77. Wilaya 32 katika mikoa 20 zimefanikiwa kuvuka lengo lililoainishwa katika Mkakati wa Kuhifadhi Mazingira ya Ardhi na Vyanzo vya Maji kwa kupanda miti milioni moja na nusu kwa mwaka. Utekelezaji wa kampeni hii unaenda sanjari na tuzo ya Rais ya Hifadhi ya Vyanzo vya Maji, Kupanda na Kutunza Miti. Ili kuelewa mwenendo wa utekelezaji wa kampeni hii pamoja na tuzo ya Rais, Ofisi imeandaa taarifa ya tathmini ya utekelezaji wake. Aidha, katika msimu wa mwaka 2010/11, utekelezaji wa kampeni ya upandaji miti unaendelea katika mikoa yote nchini. Serikali za Vijiji na Halmashauri za Wilaya na Manispaa zitunge sheria ndogo za Hifadhi ya Misitu.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha 2010/11, Ofisi iliandaa mwongozo rahisi wa kuandaa Mipango ya Usimamizi wa Mazingira ya Kisekta na Serikali za Mitaa na ilifanya vikao sita vya kisekta vya kujadili masuala ya uhuishaji wa mazingira katika Sekta na Serikali za Mitaa.

Kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Hifadhi ya Mazingira katika vyanzo vya maji na kusimamia utekelezaji wa mkakati wa usafi katika fukwe.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Mwaka wa Fedha wa 2010/11, Ofisi imefanya tathmini ya utekelezaji wa Mkakati wa Kuhifadhi Mazingira ya Ardhi na Vyanzo Vya Maji kwa kipindi cha miaka minne kuanzia 2006 hadi 2010. Matokeo ya tathmini yanaonesha kuwa, Wananchi wengi waliitikia wito wa kuhifadhi vyanzo vya maji kwa kushiriki katika upandaji miti na kupunguza shughuli za kijamii katika vyanzo vya maji.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, taarifa ya tathmini ilibaini kuwa, bado kuna changamoto kubwa ambazo ni uhaba wa fedha zilizotengwa katika utekelezaji wa Mkakati; kutofanikiwa kwa udhibiti wa matukio ya moto; kutotambuliwa katika mfumo wa utumishi, kada ya Maafisa Mazingira katika Serikali za Mitaa; kutokuwepo kwa kasma ya shughuli za mazingira katika Halmashauri hizo; na kutofanikiwa kwa uondoshaji wa mifuko ya plastiki iliyopigwa marufuku.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2010/11, Serikali kwa kupitia Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira, iliimarisha usimamizi wa viwanda, biashara na migodi ili shughuli zake zisichafue mazingira. Baraza lilifanya ukaguzi wa viwanda, migodi, sehemu za biashara na uzalishaji ili kuhakikisha kuwa, taratibu na kanuni za hifadhi ya mazingira zinafuatwa. Aidha, viwanda na taasisi 20 na migodi minane ilikaguliwa na kupewa amri ya kuboresha mifumo ili kuzingatia hifadhi ya mazingira. Pia ukaguzi wa mazingira ulifanyika katika Kata za Mikocheni na Mivinjeni, Dar es Salaam na kubaini utupaji wa taka ngumu holela kwenye maeneo yasiyo rasmi.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2011/12, mkazo utaelekezwa katika kukuza uwezo wa Serikali za Mitaa katika kusimamia ukusanyaji na utupaji wa taka ngumu na taka miminika na zile za hatari katika maeneo yao. Baraza litaendelea kufuatilia, kupitia na kusimamia utekelezaji wa Mipango ya Usimamizi na Uperembaji wa Mazingira *(Environmental Management and Monitoring Plans)* ili kudhibiti uchafuzi unaoweza kutokea katika viwanda, biashara na migodi.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha wa 2010/11, hatua za awali za utekelezaji wa Mradi wa Vijiji vya Mfano vya Hifadhi ya Mazingira *(eco-village)*, zilianza kwa kufanya tathmini na uchambuzi wa Miradi itakayofadhiliwa kupitia mpango huo. Mradi huu unatarajiwa kutekelezwa katika vijiji hapa nchini. Shughuli zitakazofanyika katika vijiji vitakavyochaguliwa zitahusu hifadhi ya mazingira kwa ujumla; kwa mfano, mipango shirikishi ya matumizi bora ya ardhi, usimamizi shirikishi wa misitu, kilimo na ufugaji endelevu, usimamizi wa matumizi ya maji na elimu ya mazingira mashuleni. Katika kipindi cha mwaka 2011/12, utekelezaji wa Miradi itakayoteuliwa utaanza. Vipeperushi vyenye mafunzo rahisi ya hifadhi ya mazingira viandaliwe, vichapishwe kwa wingi na vitumike kwenye mafunzo ya elimu yenye manufaa nchini kote.

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha kuwa umma unazingatia usimamizi wa mazingira, Ofisi ilitoa elimu ya hifadhi ya mazingira kwa umma, kupitia njia mbalimbali. Kwa mfano, kupitia Maadhimisho na Maonesho ya Siku ya Mazingira Afrika, Siku ya Kupambana na Kuenea kwa Ukame na Jangwa Duniani, Siku ya Mazingira Duniani, Siku ya Wakulima Nanenane na Siku ya Ozoni Duniani. Elimu ilitolewa kwa kutumia machapisho, kwa mfano, vipeperushi, mabango, vitini, fulana na kofia, vikundi vya sanaa, ngonjera na kwaya, kutumia magari ya matangazo, runinga, redio, warsha na makala magazetini. Katika maadhimisho haya, elimu ya mazingira ilitolewa kwa kutumia vipeperushi nakala 10,000, Shajara nakala 1,000, fulana na kofia 20,000; mabango 50, vitini nakala 10,000; vikundi kumi vya sanaa, ngonjera na kwaya mbalimbali; magari ya matangazo na runinga, redio na makala 25; warsha moja na maonesho ya matumizi ya majiko bunifu, nishati mbadala itokanayo na vitofali vya makaa ya mawe *(briquettes)* na makapi ya mazao (Ndizi, Kahawa na Mkonge). Aidha, Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira katika Mwaka wa Fedha wa 2010/11, lilichapisha na kusambaza kwa wadau vipepererushi 20,000 vyenye mafunzo rahisi ya hifadhi ya mazingira; Jarida la Baraza la mwezi Januari – Juni, 2011 nakala 5,000; na nakala 1,000 za kalenda ya mwaka 2011.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha wa 2010/11, Baraza limeendelea kusimamia na kuhakikisha kwamba, Miradi ya Ujenzi inafanyiwa Tathmini ya Athari ya Mazingira (TAM), kwa mujibu wa Sheria ya Mazingira (Sura ya 191). Katika kipindi hicho, Miradi 14 ya Ujenzi na Uendelezaji kwenye Vivutio vya Utalii ilifanyiwa TAM na kupata Hati za TAM *(Environmental Impact Assesment-EIA Certificates).*

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Mwaka wa Fedha wa 2010/11, Ofisi iliendelea kuratibu utekelezaji wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira na Programu yake *(Environmental Management Act - Implementation Support Programme-EMA-ISP).* Katika kipindi hiki, Kanuni za Usimamizi Endelevu wa Ardhi Oevu *(Regulations on Sustainable Management of Protected Wetlands);* na Kanuni za Usimamizi wa Ukanda wa Pwani *(Regulations on Promotion of Integrated Coastal Protected Zone Management)* zimeandaliwa. Vilevile Miongozo miwili inayohusu Uendeshaji wa Mfuko wa Taifa wa Mazingira na Uendeshaji wa Baraza la Rufaa la Mazingira inaandaliwa.

Mheshimiwa Spika, Miongozo miwili rahisi *(Popular version)*, inayohusu uandaaji wa Mipango Kazi ya Mazingira ya Kisekta na Serikali za Mitaa *(Popular version for Sectoral Ministries and Local Government Authorities Environmental Action Plans);* na Matumizi Salama ya Bioteknolojia ya Kisasa *(Popular version for Biosafety Guidelines)* imeandaliwa. Dondoo mbili zinazohusu Kanuni za Matumizi Salama ya Bioteknolojia *(Highlights for Biosafety Regulations);* na Kemikali Zinazomong'onyoa Tabaka la Ozoni *(Highlights for Ozone Depleting Substances Regulations)* zimeandaliwa. Aidha, watumishi tisa wamejengewa uwezo kuhusu Tathmini ya Athari kwa Mazingira (TAM), Tathmini ya Kimkakati ya Mazingira na mbinu zinazotumika katika Majadiliano ya Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, Ofisi imekamilisha tafsiri ya Ripoti ya Hali ya Mazingira kwa Lugha ya Kiswahili. Tafsiri ya Ripoti hii inatoa fursa kwa Wananchi wengi kuielewa na kuitumia katika kutekeleza mikakati na mipango ya hifadhi ya mazingira. Aidha, Ofisi kwa kushirikiana na Serikali ya Denmark, imewezesha Wizara tano kuandaa Mipango kazi ya Mazingira ya Kisekta. Wizara hizo ni Kilimo, Chakula na Ushirika; Maji; Ujenzi; Afya na Ustawi wa Jamii; na Nishati na Madini. Mipango kazi hii itawezesha Wizara hizi kuhuisha mipango yao katika utekelezaji wa shughuli za mazingira.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2011/12, Ofisi itakamilisha Kanuni mbili na Miongozo miwili. Kanuni hizo ni Kanuni za Usimamizi Endelevu wa Ardhi Oevu *(Regulations on Sustainable Management of Protected Wetlands);* na Kanuni za Usimamizi wa Ukanda wa Pwani *(Regulations on Promotion of Integrated Coastal Protected Zone Management).* Miongozo inayohusu Uendeshaji wa Mfuko wa Taifa wa Mazingira na Uendeshaji wa Baraza la Rufaa la Mazingira inayoandaliwa sasa itakamilishwa. Aidha, Ofisi inatarajia kuandaa Kanuni tano na Miongozo minne inayohusu usimamizi wa mazingira.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Mwaka wa Fedha wa 2010/11, Ofisi iliendelea kutekeleza Programu ya Kuhuisha Masuala ya Mazingira kwenye Utekelezaji

wa MKUKUTA I. Shughuli zilizotekelezwa katika kipindi hiki ni kuchapisha na kusambaza aina tatu ya vitabu vinavyohusu: Miradi yenye mafanikio katika juhudi za kuhifadhi mazingira na kupunguza umaskini; Mwongozo wa Kufundishia Uhusiano kati ya Umaskini na Mazingira; na Mwongozo wa Kufundishia Tathmini ya Mazingira Kimkakati. Jumla ya nakala 3,000 za vitabu na nakala 1,000 za Jarida la Umaskini na Mazingira zilichapishwa na kusambazwa kwa wadau ili kukuza uelewa. Aidha, Ofisi ilifuatilia na kutathmini shughuli za Programu kwa sekta na taasisi zinazoshiriki katika kutekeleza Programu ambazo ni pamoja na Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI, Wizara ya Fedha na *NEMC.* Kwa kuwa ufadhili wa Programu hii unafikia ukomo mwezi Desemba, 2011, Serikali ipo katika majadiliano na Washirika wa Maendeleo ili kuendelea na utekelezaji chini ya MKUKUTA II. Katika kipindi cha mwaka 2011/12, Ofisi itaendelea kuratibu uhuishaji wa mabadiliko ya tabianchi katika mipango ya kisekta na kukuza uelewa na uwezo wa kutoa taarifa zinazohusiana na Sheria ya Mazingira kwa Wananchi hasa wale wa vijijini.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Mwaka wa Fedha wa 2010/11, Ofisi imefanya tathmini ya utekelezaji wa Mkakati wa Kuhifadhi Mazingira ya Ardhi na Vyanzo Vya Maji, kwa kipindi cha miaka minne kuanzia mwaka 2006 hadi 2010. Matokeo ya tathmini yanaonesha kuwa, Wananchi wengi waliitikia wito wa kuhifadhi vyanzo vya maji kwa kushiriki katika upandaji miti na kupunguza shughuli za kijamii katika vyanzo vya maji. Hata hivyo, taarifa ya tathmini ilibaini kuwa, bado kuna changamoto kubwa ambazo ni uhaba wa fedha zilizotengwa katika utekelezaji wa Mkakati; kutofanikiwa kwa udhibiti wa matukio ya moto; kutokuwepo kada ya Maafisa Mazingira katika mfumo wa Utumishi wa Serikali Kuu na Serikali za Mitaa na kutokuwepo kwa kasma ya mazingira katika Halmashauri na uondoshaji wa mifuko ya plastiki iliyopigwa marufuku kutofanikiwa kama ilivyotarajiwa.

Mheshimiwa Spika, aidha, katika kipindi cha 2011/12, Ofisi kwa kushirikiana na wadau wengine, itafanya mapitio ya Mkakati ili kurekebisha upungufu uliojitokeza katika hatua za utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha 2010/11, Ofisi imeendelea kuhamasisha na kuelimisha jamii, taasisi na watendaji katika ngazi ya wilaya na mikoa kuhusu utekelezaji wa Tuzo ya Rais ya Kuhifadhi Vyanzo vya Maji, Kupanda na Kutunza Miti. Fomu za ushiriki, Mwongozo wa Tuzo ya Rais na vipeperushi husika vimeendelea kusambazwa kwa Wananchi kupitia Vikao vya Kamati za Mashauriano za Mikoa *(Regional Consultative Committee - RCC)* katika Mikoa ya Tanga, Tabora na Mara pamoja na uhamasishaji uliofanyika kwa njia ya machapisho, maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani na Maonesho ya Nanenane.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Mwaka wa Fedha wa 2011/12, Ofisi itaendelea kuratibu na kufuatilia utekelezaji wa kampeni ya upandaji miti nchini kwa kuhamasisha Wananchi pamoja na kuanza mchakato wa kupata washindi wa Tuzo ya Rais ya Kuhifadhi Vyanzo vya Maji na Kupanda Miti. Aidha, Tuzo hii itatolewa tena kwa washindi wa ngazi mbalimbali na Mheshimiwa Rais wakati wa kilele cha

Maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani, tarehe 5 Juni, 2012. Kwa kuwa mwaka 2010, mikoa 16 tu ilishiriki, ni matarajio yangu kwa mwaka 2012 mikoa yote itashiriki.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Mwaka wa Fedha wa 2010/11, Bunge lako Tukufu liliarifiwa juu ya maandalizi ya uzinduzi wa Mkakati wa Kuhifadhi Mazingira ya Bahari, Ukanda wa Pwani, Maziwa, Mito na Mabwawa sita. Ninaomba kutoa taarifa kwamba, Mkakati huu ulizinduliwa rasmi tarehe 6 Julai, 2010 Wilayani Mafia, Mkoani Pwani. Aidha, nakala 500 za tafsiri rahisi ya Mkakati huu zimechapishwa na kusambazwa kwa wadau ili kuweza kueleweka zaidi kwa jamii yetu.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2011/12, Ofisi itaendelea kuratibu utekelezaji wa Mkakati ikiwa ni pamoja na kuelimisha na kuhamasisha wadau kushiriki kikamilifu katika utekelezaji wa Mkakati huu. Nichukue nafasi hii, kuomba uongozi wa mikoa, uendelee kutupatia fursa ya kushiriki katika Vikao vya Kamati za Mashauriano za Mikoa ili kuendelea kuelimisha watendaji na wadau kuhusu wajibu na majukumu yao katika kutekeleza Mkakati huu.

Mheshimiwa Spika, Ofisi iliendelea kuratibu utekelezaji wa Programu Endelevu ya Hifadhi ya Mazingira ya Bonde la Ziwa Tanganyika, inayohusisha Nchi za Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Burundi, Tanzania na Zambia. Kwa upande wa Tanzania, Miradi mitatu inatekelezwa chini ya Programu hii, ambayo ni Mradi wa Usimamizi wa Bonde *(Catchment Management);* Mradi wa Usimamizi wa Majitaka katika Manispaa ya Kigoma/Ujiji; na Mradi wa Uendelezaji wa Uvuvi na Hifadhi ya Mazingira.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Mwaka wa Fedha wa 2010/11, shughuli zilizotekelezwa ni uongoaji wa maeneo yaliyoharibika sana ambapo miti 26,000 imepandwa katika eneo la Kibirizi na Buronge na miti 141,914 imepandwa katika vijiji sita vya mfano; uandaaji wa vikundi kumi na tisa vya uvuvi shirikishi *(Beach Management Units)* katika vijiji kumi katika Mikoa ya Rukwa na Kigoma ili kuhamasisha uvuvi endelevu; ujenzi wa mialo minne ya kisasa katika Wilaya za Mpanda (1), Nkasi (1) na Kigoma (2); uanzishaji wa vikundi vya jamii vinavyofanya shughuli mbadala za kiuchumi katika vijiji sita vya mfano ambavyo ni Kisumba (Sumbawanga), Korongwe (Nkasi), Karema (Mpanda), Titye (Kasulu), Ilagala (Kigoma Vijijini) na Nyange (Kibondo); kufuatilia utekelezaji wa sheria ndogo za usimamizi wa mazingira na mipango ya matumizi bora ya ardhi katika vijiji vya mfano. Aidha, Kamati za Mazingira kumi zimeanzishwa na zimehamasishwa kuhusu utekelezaji wa mipango ya matumizi bora ya ardhi katika vijiji vya mfano. Vilevile semina mbili kuhusu uanzishwaji na ufuatiliaji wa Miradi, uvuvi endelevu na usimamizi shirikishi wa Ziwa Tanganyika ziliendeshwa kwa Maafisa Mipango, Maendeleo ya Jamii na Uvuvi katika Wilaya za Nkasi, Mpanda, Sumbawanga na Kigoma.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2011/12, Ofisi itaendelea kuratibu shughuli zifuatazo: Hifadhi ya mazingira ya lindimaji katika Bonde; uendelezaji wa uvuvi endelevu; kutoa mafunzo kuhusu usimamizi wa maji taka na taka ngumu; ujenzi wa kilomita 102 za barabara kiwango cha changarawe katika Mikoa ya Kigoma na Rukwa; kujenga vyumba kumi vya madarasa na nyumba mbili za walimu; kujenga wodi

tano za akina mama; nyumba mbili za wahudumu wa afya; zahanati mbili; visima vya maji ishirini; hosteli moja na vyoo matundu ishirini na nne, katika Wilaya za Sumbawanga, Nkasi, Mpanda, Kigoma na Kasulu chini ya Miradi Midogo (*Community Infrastructure);* ujenzi wa ofisi ya doria Buhingu katika Wilaya ya Kigoma na ununuzi wa boti nne za doria na vifaa kwa ajili vituo vya doria na kukarabati Ofisi za Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi - TAFIRI na Uvuvi Kigoma.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2010/11, Ofisi iliendelea kufanya uhamasishaji wa wadau katika Wilaya zinazopakana na Ziwa Nyasa ambazo ni Mbinga, Ludewa, Makete, Njombe na Kyela ili kujenga uelewa wa umuhimu wa Tanzania kushiriki kikamilifu katika Programu ya Hifadhi ya Mazingira ya Bonde la Ziwa Nyasa. Vilevile Wilaya husika ziliendelea kukusanya takwimu na taarifa sahihi zitakazosaidia kukamilisha andiko la Mradi. Aidha, mwezi Januari, 2011 majadiliano kati ya Watendaji wa Wilaya husika kuhusu mapendekezo ya shughuli za kipaumbele zitakazotekelezwa na Tanzania, yalifanyika kwa pamoja na ujumbe wa Benki ya Dunia ambao unaratibu maandalizi ya Mradi.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Mwaka wa Fedha wa 2011/12, shughuli zitakazotekelezwa ni kukamilisha maandalizi ya Programu ya Hifadhi ya Bonde la Ziwa Nyasa kwa ushirikiano na Serikali za Malawi na Msumbiji; na kuelimisha jamii katika Mikoa ya Mbeya, Iringa na Ruvuma kuhusu umuhimu wa kuhifadhi mazingira ya Bonde la Ziwa Nyasa.

Mheshimiwa Spika, Ofisi imeendelea kuratibu Programu ya Ushirikishwaji wa Wananchi katika Usimamizi na Uhifadhi wa Mazingira, inayotekelezwa na Mashirika mbalimbali yasiyokuwa ya Kiserikali chini ya ufadhili wa Shirika la Kimataifa la Maendeleo la Marekani *(USAID).* Mashirika hayo ni pamoja na *World Wide Fund for Nature (WWF); Jane Goodall Institute; AFRICARE;* na *African Wildlife Foundation (AWF).*

Mheshimiwa Spika, katika kipindi hiki, Programu hii kwa kupitia Taasisi ya *Jane Goodall Institute* imeendelea kutekeleza Mradi wa kusaidia Jamii kuhifadhi Mazingira, hususan katika maeneo ya Mfumo-ikolojia wa Gombe na Masito katika Wilaya za Kigoma na Mpanda. Mradi huu unatekelezwa katika eneo la kilomita za mraba 12,047, ambapo asilimia 63 za eneo hilo zimefunikwa na misitu ya miombo na kilomita za mraba 2,200 ni maeneo yaliyohifadhiwa. Mradi huu umetoa mafunzo kuhusu hifadhi ya mazingira, ikiwa ni pamoja na shughuli za kilimo endelevu. Jumla ya vijiji 49 vinatekeleza Mradi huu na jamii katika vijiji hivi imeweza kuongeza kipato chao kutokana na shughuli za kilimo na matumizi endelevu ya rasilimali kwenye maeneo yaliyohifadhiwa.

Mheshimiwa Spika, katika Ukanda wa Kaskazini, *AWF* imeendelea kuhamasisha jamii kuhifadhi mazingira na kuongeza kipato kutokana na matumizi endelevu ya rasilimali kwenye maeneo yaliyohifadhiwa. Katika azma ya kuongeza kipato cha jamii, hususan jamii za wafugaji, machinjio ya kisasa yamejengwa katika eneo la Makuyuni (Ranchi ya Manyara).

Mheshimiwa Spika, Miradi ya Ushirikishwaji Jamii katika Hifadhi ya Mazingira katika Mikoa ya Morogoro, Pwani, Lindi, Ruvuma, Iringa na Tabora, imeendelea kutekelezwa kwa kushirikiana na *WWF*. Miradi hii inasaidia kuwezesha jamii kuandaa sera na mipango yao ya kuhifadhi mazingira na maendeleo endelevu, ambapo eneo lililo chini ya hifadhi ya jamii ni kilomita za mraba 125,000. Aidha, Jumuiya sita katika Maeneo ya Hifadhi za Wanyamapori *(Wildlife Management Areas–WMAs)*, ziliingia mkataba na wawekezaji katika maeneo yao. Hadi sasa jumla ya Jumuiya tisa ambazo ni Nalika, Mbompa, Uwima, Magingo, Mbarang'andu, Juhibu, Jukumu, Mungata na Wami-Mbiki zinanufaika na mapato kutokana na uwindaji wa kitalii, ambapo jumla ya mapato ni Dola za Marekani milioni nne kwa mwaka. Aidha, *USAID* imetoa kiasi cha Dola za Marekani laki tatu na arobaini na nne elfu, sawa na shilingi milioni 576 kwa Ofisi kwa ajili ya kuimarisha shughuli za uratibu na utoaji wa taarifa kuhusu utekelezaji wa Programu hii kwa Serikali, *USAID* na wadau wengine. Mwaka 2011/12, Ofisi itaendelea kuratibu shughuli za Programu hii kwa kuzingatia Mipango na Mikakati iliyowekwa.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha wa 2010/11, Ofisi iliendelea kuratibu mchakato wa utoaji wa Tuzo ya Rais ya Uongozi na Ubora wa Hifadhi ya Mazingira katika Uchimbaji Madini kwa kuandaa Vigezo na Miongozo mipya, ambayo imezingatia upungufu na changamoto zilizojitokeza katika Sekta ya Madini. Tuzo hii ni muhimu katika kuhamasisha uboreshaji wa hifadhi ya mazingira katika shughuli ya uchimbaji wa madini. Aidha, mwaka 2010/11 mchakato wa kumpata mshindi wa Tuzo hii haukufanyika kutokana na ufinyu wa bajeti. Katika mwaka 2011/12, Ofisi itaendelea kuratibu mchakato wa utoaji Tuzo ya Rais ya Uongozi na Ubora wa Hifadhi ya Mazingira katika Uchimbaji Madini.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha wa 2010/11, Ofisi iliendelea kuratibu utekelezaji wa Mkataba wa Umoja wa Mataifa kuhusu Mabadiliko ya Tabianchi, Programu ya Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi iliyoandaliwa mwaka 2007 na pia mipango na mikakati inayohusiana na mabadiliko hayo nchini. Serikali kupitia Mradi wa Kujenga Uwezo wa Nchi katika Kuhimili Athari za Mabadiliko ya Tabianchi unaofadhiliwa na Serikali ya Denmark, iliandaa mafunzo kwa wadau takriban 400 katika kanda nne ambazo ni Kusini (Mtwara, Lindi na Ruvuma); Kaskazini (Arusha, Kilimanjaro, Manyara na Tanga); Ziwa (Mwanza, Mara, Kagera na Shinyanga); na Magharibi (Rukwa, Tabora na Kigoma). Lengo la mafunzo hayo ni kujenga uwezo wa Maafisa wa Halmashauri katika kuandaa na kutekeleza mipango inayojumuisha mikakati ya kuhimili mabadiliko ya tabianchi. Aidha, Ofisi inaandaa Mkakati wa Taifa wa Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi, unaolenga kutoa miongozo juu ya shughuli zote zinazohusiana na mabadiliko ya Tabianchi. Serikali kupitia Mamlaka ya Hali ya Hewa, iliendelea kutathmini mwenendo wa hali ya mabadiliko ya tabianchi *(Climate Change Scenarios)* ili kusaidia katika kutoa taarifa sahihi na kuandaa mipango ya kuhimili athari zitokanazo na mabadiliko ya tabianchi. Mradi huu unatarajiwa kukamilika katika Mwaka wa Fedha wa 2011/12.

Mheshimiwa Spika, mwaka wa jana, Bunge lako Tukufu liliarifiwa kuhusu utekelezaji wa Mpango wa Kupunguza Uzalishaji wa Hewa Ukaa inayotokana na Ukataji

Miti na Uharibifu wa Misitu (MKUHUMI), unaolenga kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi katika Sekta ya Misitu kupitia msaada wa Serikali ya Norway. Mpango huu unalenga pia kubaini njia bora ya kutoa motisha kwa Wananchi na taasisi mbalimbali zinazotunza na kuhifadhi misitu na kuweka mfumo bora na madhubuti wa soko la biashara ya hewa ukaa katika ngazi ya Kitaifa na Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Mwaka wa Fedha wa 2010/11, Ofisi iliendelea na maandalizi ya Mkakati wa Kitaifa wa MKUHUMI. Aidha, utekelezaji wa Miradi ya Majaribio ya MKUHUMI kupitia Asasi Zisizo za Serikali, uliendelea katika Wilaya za Arusha, Kondoa, Kigoma, Kilosa, Kilwa, Rungwe, Muheza, Kisarawe na Shinyanga kwa upande wa Tanzania Bara. Mradi wa majaribio wa MKUHUMI kwa upande wa Zanzibar uliendelea kutekelezwa katika Wilaya za Chakechake, Wete, Mkoani, Micheweni, Kusini Unguja, Kati na Kaskazini B. Aidha, Watanzania 17 wa Shahada ya Uzamifu *(Ph.D)* na 25 wa Shahada ya Uzamili katika Sayansi *(M.Sc)*, wamepata ufadhili kusoma hapa nchini na nje ya nchi ili kujenga uwezo kutekeleza MKUHUMI na kufanya utafiti. Vilevile Ofisi iliendelea kutoa machapisho anuai na kuyasambaza nchini kote. Machapisho haya ni pamoja na Jarida la MKUHUMI (nakala 7,000); vipeperushi vya aina nne kuhusu MKUHUMI (nakala 15,000) na kijitabu kimoja (nakala 5,000).

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha wa 2010/11, Ofisi ilianza utaratibu wa kuanzisha Kituo cha Kitaifa cha Ufuatiliaji wa Uzalishaji wa Hewa Ukaa *(National Carbon Monitoring Centre-NCMC)*, pamoja na Mfuko wa Kitaifa wa MKUHUMI *(National REDD+ Trust Fund-NRTF).* Kituo hiki kitakusanya taarifa kuhusu kiasi cha hewa ukaa kinachopunguzwa kutokana na shughuli za uhifadhi wa misitu na kufuatilia masuala yote yanayohusu upunguzaji wa hewa ukaa. Mfuko pia utasimamia fedha zitokanazo na shughuli za MKUHUMI nchini na kuhakikisha kuwa, Wananchi wanaoshiriki kuhifadhi misitu kwa ajili ya upunguzaji wa hewa ukaa wanapatiwa malipo stahili ili kuwahamasisha kuendelea na juhudi hizo.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha wa 2011/12, Ofisi itaendelea kuratibu utekelezaji wa shughuli za MKUHUMI, ikiwa ni pamoja na kuendelea kujenga uwezo na kukuza uelewa kwa umma, kukamilisha uanzishwaji wa Kituo cha Hewa Ukaa (NCMC) na Mfuko wa MKUHUMI.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Mwaka wa Fedha wa 2010/11, Bunge lako Tukufu liliarifiwa kuwa Tanzania imepata jumla ya Dola za Marekani milioni 2.9, sawa na shilingi bilioni 4.06 kutoka Serikali ya Japan kwa ajili ya kutekeleza Mradi wa Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi *(Africa Adaptation Programme).* Utekelezaji wa Mradi huu umeanza kwa kutoa mafunzo kwa Maafisa Mazingira na Kamati za Mazingira katika Halmashauri za Wilaya ya Mbinga (Ruvuma), Igunga (Tabora) na Misenyi (Kagera), zenye maeneo ya Miradi ya majaribio. Mafunzo haya yanalenga kujenga uwezo katika usimamizi wa Miradi hiyo. Katika kipindi cha mwaka 2011/12, Mradi huu utatekeleza Miradi minne ya majaribio katika Halmashauri za Wilaya ya Igunga (Tabora), Mbinga (Ruvuma), Misenyi (Kagera) na Kaskazini A (Kaskazini Unguja), yenye lengo la kujenga uwezo wa kuhimili athari za mabadiliko ya tabianchi.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Mwaka wa Fedha wa 2011/12, Ofisi itaanza kutekeleza Mradi wa Kuhimili Athari za Mabadiliko ya Tabianchi katika maeneo ya Pwani wenye thamani ya Dola za Marekani milioni 3.1 na ambazo Tanzania imetengewa kutoka Mfuko wa Mazingira wa Dunia. Fedha hizi ni kwa ajili ya kuandaa na kutekeleza Mradi wa kujenga uwezo wa kuhimili athari za mabadiliko ya tabianchi kwa kutekeleza shughuli za upandaji na hifadhi ya misitu ya mikoko katika Wilaya ya Rufiji; ukarabati wa ukuta wa ufukwe wa Pangani; na uchimbaji wa visima virefu vya maji safi katika Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo. Kwa upande wa Zanzibar, maeneo na shughuli zitakazotekelezwa zitaainishwa kulingana na vipaumbele vitakavyowasilishwa na mamlaka husika.

Mheshimiwa Spika, mwaka jana Bunge lako Tukufu liliarifiwa kuwa, Tanzania ni miongoni mwa nchi nne duniani ambazo zitanufaika na msaada wa fedha kutoka Umoja wa Nchi za Ulaya *(European Union – EU),* kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi *(Climate Change Mitigation and Adaptation)* kama ilivyoanishwa katika Mpango wa Jumuiya ya Ulaya wa Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi *(Global Climate Change Alliance - GCCA).* Mradi huu utatekelezwa kwa miezi 72 kwa gharama ya Euro milioni 2.2, sawa na shilingi bilioni 3.8. Katika kipindi cha mwaka 2010/11, hatua za awali za utekelezaji wa Mradi huo zilianza kwa kufanya tathmini na uchambuzi wa Miradi itakayofadhiliwa kupitia mpango huo. Mradi huu unatarajiwa kutekelezwa katika vijiji vitakavyoteuliwa hapa nchini, ambavyo maandiko ya Miradi yake yatakubalika. Katika kipindi cha mwaka 2011/12, utelezaji wa Miradi itakayoteuliwa utaanza. Shughuli zitakazofanyika katika vijiji vitakavyochaguliwa zitahusu hifadhi ya mazingira kwa ujumla, kuhusisha mipango shirikishi ya matumizi bora ya ardhi, usimamizi shirikishi wa misitu, kilimo na ufugaji endelevu, usimamizi wa matumizi ya maji na elimu ya mazingira mashuleni.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Mwaka wa Fedha wa 2010/11, Ofisi imeendelea kuratibu utekelezaji wa Itifaki ya Kyoto, unaolenga katika kupunguza uzalishaji wa hewa ukaa. Ofisi iliendelea kuelimisha na kujenga uwezo wa wadau kwa kuandaa na kutekeleza Miradi ya *Clean Development Mechanism - CDM.* Ofisi kwa kushirikiana na Shirika la Mpango wa Maendeleo la Umoja wa Mataifa *(UNDP),* kupitia Mradi *wa ONE UN JOINT Programme on Environment – JP 11* iliendesha mafunzo Kwa Sekta Binafsi na Taasisi za Serikali kuhusu jinsi ya kuandaa Miradi ya *CDM.* Mafunzo haya yalifanyika Dar es Salaam mwezi Aprili, 2011. Kupitia Mradi huu, wawakilishi wawili kutoka Sekta Binafsi waliwezeshwa kushiriki katika Maonesho ya Kimataifa ya Miradi ya *CDM – CDM Carbon Expo Barcelona,* mwezi Juni, 2011. Aidha, Programu ya Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi ilitafsiriwa kwa Lugha ya Kiswahili rahisi ili kuwawezesha wadau wengi kufahamu na kuelewa mabadiliko ya tabianchi na athari zake.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Mwaka wa Fedha wa 2011/12, shughuli zifuatazo zitatekelezwa: Kuendelea kujenga uwezo wa kutekeleza Programu, kuandaa Mikakati na Miradi mbalimbali inayolenga katika kuhimili mabadiliko ya tabianchi; kuendelea kuratibu utekelezaji wa MKUHUMI na kutoa elimu kwa umma kuhusu athari

za mabadiliko ya tabianchi; kuchambua na kuidhinisha Miradi ya *CDM* yenye manufaa kwa Tanzania; kuandaa mpango wa nchi wa kutekeleza shughuli mwafaka katika kukabili Mabadiliko ya Tabianchi *(Nationally Appropriate Mitigation Actions-NAMAs)*, chini ya makubaliano ya *Cancun (Cancun Agreement)*, unaozitaka nchi zilizoendelea kutoa fedha za kutosha kuziwezesha nchi zinazoendelea kutekeleza shughuli za upunguzaji wa gesijoto kulingana na mazingira ya nchi husika; na kukamilisha maandalizi ya mkakati wa kitaifa wa kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi pamoja na Mpango Kazi wake.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha wa 2010/11, Ofisi imeendelea kuratibu utekelezaji wa Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Kupambana na Kuenea kwa Hali ya Jangwa na Ukame. Ofisi pia imeandaa Taarifa ya Nne ya Kitaifa ya Utekelezaji wa Mpango wa Kitaifa wa Kukabiliana na Uharibifu wa Ardhi na Kuenea kwa Ukame na kuwasilisha kwenye Sekretarieti ya Mkataba. Tathmini iliyofanywa na kutolewa na Sekretarieti ya Mkataba, imeipongeza Tanzania kwa kutekeleza vizuri Mpango Kazi wa Kitaifa wa Kukabiliana na Uharibifu wa Ardhi na Kuenea kwa ukame.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi hiki, Ofisi imefanya tafiti *(studies)* za kuangalia fursa za upatikanaji wa fedha kutoka vyanzo mbalimbali vilivyopo nchini na nje ili kusaidia utekelezaji wa Mkataba huu. Tafiti tatu zinazohusu Thamani ya Kiuchumi ya Ardhi *(Economic Value of Land)* na Mbinu za Masoko na utoaji Motisha kwa Matumizi Endelevu ya Ardhi *(Incentive and Market Based Mechanism for Sustainable Land Management in Tanzania)* zimefanyika. Kwa sasa tafiti mbili kuhusu fursa za fedha zilizopo kwenye Miradi ya Mabadiliko ya Tabianchi katika Usimamizi Endelevu wa Miradi ya Ardhi *(Sustainable Land Mangement and Climate Change Finance in Tanzania)* zimekamilika. Aidha, kwa mwaka 2011/12, Ofisi itakamilisha tafiti moja iliyobaki na kuanza mchakato wa kuhuisha mapendekezo ya tafiti hizi kwenye mipango na Bajeti ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, mwaka wa jana, Bunge lako Tukufu liliarifiwa kuwa, kwa kushirikiana na Sekretarieti ya Mkoa wa Kilimanjaro pamoja na Shirika la Mpango wa Maendeleo la Umoja wa Mataifa *(UNDP)*, Ofisi ilikuwa inakamilisha utambuzi wa maeneo ya kipaumbele yatakayohusishwa katika Mradi wa Maendeleo Endelevu ya Ardhi Mkoani Kilimanjaro *(Sustainable Land Management in the high Land Kilimanjaro)*, chini ya Mpango Maalumu wa Afrika wa Kupambana na Kuenea kwa Hali ya Jangwa na Ukame *(Terra Africa)*. Sekta zilizoainishwa katika Mradi huu ni Kilimo, Nishati na Utunzaji wa Maliasili na Mazingira. Ninapenda kuchuka fursa hii kulifahamisha Bunge lako Tukufu kuwa, Mradi huu umezinduliwa rasmi tarehe 16 Mei, 2011 na malengo yake makuu ni kupunguza uharibifu wa mazingira yanayosababishwa na ukataji miti ovyo kwa ajili ya kuni, mbao na uchomaji mkaa; kuongeza uzalishaji wa mazao ya kilimo; na kuwezesha maisha bora, huduma bora kutokana na mazingira bora na kupata faida zitokanazo na mazingira bora. Aidha, Mradi huu utatekelezwa na Halmashauri za Wilaya chini ya uratibu wa Sekretarieti ya Mkoa. Wadau wengine ni Ofisi ya Makamu wa Rais, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI), Wizara za Kilimo Chakula na Ushirika; Maliasili na Utalii; Nishati na Madini na Taasisi nyingine.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha 2010/11, Ofisi imeendelea kuratibu utekelezaji wa Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Hifadhi ya Bioanuai kwa kufanya shughuli zifuatazo: Kushiriki na kutoa msimamo wa nchi kwenye Mkutano wa Kumi wa Mkataba wa Hifadhi ya Bioanuai uliofanyika Nagoya Japan, Oktoba, 2010. Moja ya matokeo muhimu ya Mkutano huu ni kupitishwa kwa Mpango Mkakati wa Mkataba kwa Mwaka 2011 hadi 2020.

Mheshimiwa Spika, aidha, taarifa ya mkutano huu ikiwa ni pamoja na hatua muhimu zinazotakiwa kuchukuliwa na nchi imeandaliwa na kusambazwa kwa wadau kwa ajili ya utekelezaji. Hatua zinazotakiwa kuchukuliwa ni pamoja na kuhakikisha suala la biofueli linafanyiwa utafiti wa kina kabla ya kutekelezwa na kuandaa sheria, kanuni na mwongozo kwa ajili ya kutekeleza Itifaki ya usimamizi katika upatikanaji na mgawanyo wa haki na usawa wa faida zitokanazo na matumizi ya bioanuai *(Nagoya Protocol on Access to Genetic Resources and the Fair and Equitable Sharing of Benefits Arising from their Utilization).* Katika Mwaka wa Fedha wa 2011/12, Ofisi kwa kushirikiana na Wadau itapitia Mpango Mkakati wa Taifa wa Kuhifadhi Bioanuai.

Mheshimiwa Spika, Itifaki ya Cartagena ipo chini ya Mkataba wa Hifadhi ya Bioanuai na lengo lake ni kusimamia mazingira dhidi ya athari zitokanazo na bioteknolojia ya kisasa. Katika kipindi cha mwaka 2010/11, Ofisi imeendelea kuratibu utekelezaji wa Itifaki ya Cartagena kwa kuratibu uchambuzi wa maombi ya majaribio ya kimaabara ya zao la muhogo, ambalo vinasaba vyake vimefanyiwa mabadiliko ya kijenetiki ili kuhimili magonjwa. Maombi haya yameruhusiwa na utafiti unaendelea katika Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Mikocheni – Dar es Salaam. Maombi mengine ni ya utafiti nje ya maabara kwa zao la mahindi ambalo vinasaba vyake vimefanyiwa mabadiliko ya kijenetiki ili kuhimili ukame, ambayo yanaendelea kufanyiwa tathmini kabla ya kuruhusiwa.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi hiki, Ofisi ilishiriki katika Mkutano wa Tano wa Itifaki ya Cartagena, uliofanyika Jijini Nagoya, Japan, mwezi Oktoba, 2010. Pamoja na mambo mengine, mkutano huo, uliridhia kuanzishwa kwa Itifaki ya Ziada ya Nagoya – Kuala Lumpur, inayohusu uwajibikaji kisheria na fidia kwa athari zinazoweza kutokea katika Mazingira, bioanuai na afya ya binadamu kutokana na matumizi yasiyo salama ya Bioteknolojia ya kisasa *(Nagoya-Kuala Lumpur Supplementary Protocol on Liability and Redress to the Cartagena Protocol on Biosafety).*

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha wa 2010/11, Ofisi imeendesha warsha nne ili kukuza uelewa kwa wadau kuhusu matumizi salama ya bioteknolojia ya kisasa katika kanda nne zifuatazo: Kanda ya Kaskazini (Arusha, Kilimanjaro na Tanga); Kanda ya Nyanda za Juu Kusini (Mbeya, Iringa, Ruvuma na Rukwa); Kanda ya Ziwa (Mwanza, Kagera, Shinyanga na Mara); na Kanda ya Mashariki iliyojumuisha Mikoa ya Dar es Salaam, Morogoro, Pwani na Zanzibar. Vilevile Ofisi imeendesha mafunzo kwa Wasimamizi wa masuala ya matumizi salama ya bioteknolojia ya kisasa wapatao 50 wakiwemo Wajumbe wa Kamati ya Kitaifa ya Matumizi Salama ya Bioteknolojia ya Kisasa, Wizara, Watafiti, Wanahabari na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali. Mafunzo haya

yalijenga uwezo kwa wasimamizi wa matumizi salama ya bioteknolojia ya kisasa katika taratibu za upitiaji wa maombi ya matumizi ya bioteknolojia ya kisasa hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, aidha, Ofisi ilitoa kompyuta sita kwa Wizara na Taasisi za Utafiti ili kujenga uwezo katika upashanaji na ubadilishanaji wa taarifa kuhusu viumbe, mazao au bidhaa ambazo vinasaba vyake vimefanyiwa mabadiliko ya kijenetiki. Wizara na Taasisi hizo ni Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii; Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi; Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Mikocheni *(MARI);* Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia *(COSTECH);* Chuo Kikuu cha Dar es Salaam *(UDSM);* na Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine *(SUA).*

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha wa 2011/12, Ofisi itatekeleza shughuli zifuatazo: Kutoa mafunzo kwa wadau yanayohusu utambuzi, udhibiti, tathmini na masuala ya kisheria kuhusu bidhaa na viumbe ambavyo vimefanyiwa mabadiliko ya kijenetiki; na kuboresha maabara zilizoainishwa kwenye mtandao unaojumuisha vituo kumi vya Tanzania Bara na kituo kimoja cha Zanzibar vya matumizi salama ya bioteknolojia ya kisasa. Vilevile Ofisi itaratibu mchakato wa kuridhia Itifaki ya Ziada ya Nagoya – Kuala Lumpur.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha wa 2010/11, Ofisi ilishiriki katika kufanyia marekebisho Mkataba Mkataba wa Hifadhi, Usimamizi na Uendelezaji wa Mazingira ya Bahari na Pwani ya Magharibi ya Bahari ya Hindi *(Nairobi Convention);* yaliyolenga kujumuisha masuala ya hifadhi ya bioanuai na mabadiliko ya tabianchi. Aidha, Ofisi ilishiriki katika uandaaji wa Itifaki kuhusu udhibiti wa uchafuzi kutokana na shughuli zinazofanyika nchi kavu. Vilevile Ofisi inashiriki katika mchakato wa kuandaa itifaki kuhusu Usimamizi Timilifu wa Ukanda wa Pwani. Katika Mwaka wa Fedha wa 2011/12, Ofisi itaendelea kuratibu utekelezaji wa Mkataba huu.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha 2010/11, Ofisi imeendelea kuratibu utekelezaji wa programu ya Afrika ya Mtandao wa Hali ya Mazingira *(African Environmental Information Network)* chini ya ufadhili wa *UNEP* kupitia *UNDP*. Lengo la programu hii ni kuongeza uwezo wa nchi katika upatikanaji wa taarifa za Mazingira na uandaaji wa ripoti za hali ya Mazingira nchini. Chini ya Programu hii, Taarifa ya Hali ya Mazingira ya Jiji la Dar es Salaam inaandaliwa. Katika mwaka 2011/12, Ofisi itakamilisha taarifa hii ambayo itatumika kama mwongozo wa kuandaa taarifa za hali ya Mazingira ya Majiji/Miji hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, tarehe 5 Juni kila mwaka Tanzania huungana na nchi nyingine duniani kuadhimisha Siku ya Mazingira Duniani. Maadhimisho haya Kimataifa mwaka huu yalifanyika katika Miji ya Mumbai na Delhi nchini India. Kaulimbiu ya Maadhimisho ya mwaka huu Kimataifa ni: “Misitu: Huduma yako ya Asili” *(Forests: Nature at Your Service).* Kaulimbiu hii inahimiza kuwajibika kwa kila mtu katika kuhifadhi na kutunza Mazingira. Kitaifa, kaulimbiu iliyoongoza maadhimisho haya ni “Panda Miti na Kuitunza: Hifadhi Mazingira”. Maudhui ya ujumbe huu Kitaifa ni

kuelimisha na kuhamasisha Wananchi wote juu ya utunzaji na hifadhi ya Mazingira, hususan kupanda miti na kuitunza na kuhifadhi misitu na uoto wa asili.

Mheshimiwa Spika, Kitaifa, maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani yalifanyika Songea, Mkoani Ruvuma. Maadhimisho yalifanyika nchi nzima kuanzia tarehe 1 Juni hadi siku ya kilele tarehe 5 Juni. Shughuli zilizofanyika ni pamoja na upandaji na palizi ya miti, mafunzo kuhusu mazingira kupitia maonesho na mashindano ya nyimbo na ngonjera ili kukuza uelewa juu ya umuhimu wa hifadhi na usafi wa mazingira na ukaguzi wa shughuli za mazingira na kutoa elimu kwa Umma juu ya Hifadhi ya Mazingira kwa kupitia vyombo vya habari. Aidha, maadhimisho ya mwaka huu yalihusisha uzinduzi wa Maadhimisho ya Miaka Hamsini ya Uhuru wa Tanzania Bara.

Mheshimiwa Spika, ninachukua nafasi hii kuwashukuru wale wote walioshiriki katika Maadhimisho haya. Aidha, ninapenda kutoa shukrani zangu za pekee, kwa Uongozi wa Mkoa wa Ruvuma, kwa kukubali kuwa mwenyeji wa Maadhimisho hayo Kitaifa na kwa Wananchi wa Mkoa wa Ruvuma kwa ushiriki wao.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi hiki, Ofisi imeendelea kuratibu shughuli za Mfuko wa Mazingira Duniani *(Global Environment Facility - GEF)* hapa nchini. Mfuko huu unafadhili maeneo sita ya kipaumbele ambayo ni Hifadhi ya Bioanuai; Mabadiliko ya Tabianchi; Hifadhi ya Ardhi; Hifadhi ya Maji ya Kimataifa; Kemikali zinazomong'onyoa Tabaka la Hewa ya Ozoni; na Kemikali Zinazodumu kwa Muda Mrefu katika Mazingira *(Persistent Organic Polutants - POPs).*

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2010/11, jumla ya Miradi midogo 13 yenye thamani ya Dola za Marekani 331,026 imepata ufadhili wa *GEF.* Miradi hiyo inatekelezwa katika Mikoa ya Kilimanjaro, Morogoro, Pwani, Ruvuma na Tanga. Miradi hii inahusisha maeneo yafuatayo:-

Umemenuru, nishati ya biogesi, ufugaji nyuki, upandaji miti, hifadhi ya misitu, kilimo cha umwagiliaji na ukaushaji wa samaki kwa kutumia umemenuru. Ofisi ilifuatilia utekelezaji wa Miradi hiyo ili kuhakikisha inatekelezwa kama ilivyopangwa. Aidha, Ofisi iliandaa kikao cha wadau cha kujadili Miradi ya kipaumbele ya taifa kwa ajili ya ufadhili wa awamu ya tano ya Mfuko *(GEF 5).* Katika Mwaka wa Fedha wa 2011/12, Ofisi itaendelea kutoa elimu kwa wadau na kushauri jinsi ya kuandaa Miradi kwa ajili ya ufadhili wa *GEF.* Aidha, Ofisi itafuatilia utekelezaji wa Miradi iliyopata ufadhili.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2010/11, Ofisi iliendelea kuratibu utekelezaji wa Mkataba wa Kimataifa unaohusu udhibiti wa usafirishaji na utupaji wa taka za sumu baina ya nchi na nchi na Mkataba wa kanda unaozuia uingizaji wa taka za sumu Barani Afrika (Mkataba wa Bamako).

Katika kipindi hiki, Ofisi iliandaa na kusambaza kwa wadau vipeperushi 5,000 vinavyohusu Mikataba hii ili kukuza uelewa kuhusu umuhimu wa Mikataba hii; ilikusanya takwimu za taka-sumu za viwandani katika Mikoa mitatu ya Dar es Salaam,

Tanga na Morogoro, kwa kushirikiana na Baraza la Taifa la Usimamizi na Hifadhi ya Mazingira. Aidha, kampeni ya usafi wa mazingira katika Miji na Majiji nchini ilizinduliwa na Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, tarehe 12 Februari, 2011. Kampeni hii inalenga kuboresha hali ya usafi wa mazingira ya miji na kujenga utamaduni wa kuzingatia usafi wa mazingira miongoni mwa jamii.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2011/12, shughuli zifuatazo zitatekelezwa: Kuratibu utekelezaji wa Mkakati wa Kitaifa wa Usimamizi wa Taka; kuendelea kukusanya takwimu za usimamizi wa taka; kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa kampeni ya usafi wa mazingira katika Miji na Majiji nchini; kuendelea kukuza uelewa wa jamii kuhusu usimamizi wa taka za sumu; na kuandaa ripoti ya utekelezaji wa Mikataba hii nchini.

Mheshimiwa Spika, kuhusu utekelezaji wa Mkataba wa Kemikali zinazomong’onyoa Tabaka la Hewa ya Ozoni Angani *(Mkataba wa Vienna na Itifaki ya Montreal);* katika kipindi cha mwaka 2010/11, Ofisi iliendelea kusimamia Programu ya Kitaifa ya kuondosha matumizi ya kemikali zinazomong’onyoa tabaka la hewa ya Ozoni angani.

Lengo la Programu hii ni kupunguza matumizi ya kemikali zinazoharibu Tabaka la hewa ya Ozoni angani kwa kufuata ratiba iliyowekwa na Mkataba huu na kukuza matumizi ya kemikali mbadala na njia mbadala ambazo ni salama kwa mazingira.

Mheshimiwa Spika, shughuli zilizotekelezwa ni kutoa mafunzo kwa Mafundi Mchundo 210, juu ya njia bora za kuhudumia majokofu na viyoyozi kutoka mikoa yote nchini na kuratibu Maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Ozoni, tarehe 16 Septemba, 2010. Maadhimisho haya yalifanyika katika Chuo cha *VETA*, Jijini Mwanza kwa kuzindua kituo cha kunasa na kusafisha gesi chakavu za majokofu na viyoyozi. Kituo hiki ni miongoni mwa vituo vitano vilivyoanzishwa kwa ufadhili wa Mfuko wa Mkataba wa Montreal katika Vyuo vya VETA vya Chang’ombe, Dar es Salaam, Kigoma, Mbeya na Mwanza na kwa upande wa Tanzania Zanzibar, Kituo cha Umoja wa Mafundi Mchundo kilichopo Mkunazini-Zanzibar. Aidha, warsha mbili za mafunzo kwa wasimamizi 102 wa Sheria ya Mazingira ziliendeshwa Jijini Dar es Salaam na Mwanza kuhusu majukumu ya Wasimamizi wa Sheria katika utekelezaji wa Kanuni za Usimamizi wa Mazingira (Udhibiti wa kemikali Zinazomong’onyoa Tabaka la Hewa ya Ozoni) za mwaka 2007. Vilevile katika kipindi cha mwaka 2010/11, takwimu za uagizaji na matumizi ya kemikali zinazomongong’onyoa tabaka la hewa ya Ozoni zimekusanywa.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha wa 2011/12, Ofisi itaendelea kuratibu utekelezaji wa Mkataba huu na kazi zifuatazo zitafanyika: Kuendesha mafunzo kwa wasimamizi wa sheria kuhusu majukumu yao katika utekelezaji wa Kanuni za Usimamizi wa Mazingira (Udhibiti wa kemikali Zinazomong’onyoa Tabaka la Hewa ya Ozoni) za mwaka 2007; kutoa mafunzo kwa Mafundi Mchundo 200 wa majokofu na viyoyozi kuhusu njia bora za kuhudumia vifaa hivyo na ubadilishaji wa teknolojia za mitambo ya kupozea inayotumia gesi haribifu, kuendeleza utoaji wa elimu kwa wadau na

umma kuhusu umuhimu wa kulinda tabaka la hewa ya Ozoni; kuandaa Mpango wa Kitaifa wa kupunguza/kusitisha matumizi ya kemikali aina ya *Hydro Chloro Fluoro Carbons (HCFCs)* nchini kwa kufuata ratiba iliyowekwa na Mkataba; kuandaa na kuwasilisha taarifa ya mwaka ya utekelezaji wa Mkataba Serikalini na katika Sekretarieti ya Mkataba. Utekelezaji wa Mkataba wa Kudhibiti Kemikali Zinazodumu katika Mazingira kwa muda mrefu (Mkataba wa Stockholm).

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2010/11, Ofisi imeendelea kuratibu utekelezaji wa Mkataba wa Stockholm kwa kuandaa Mwongozo wa Kitaifa wa Udhibiti wa Kemikali aina ya *Polychlorinated Biphenyls (PCBs);* Ofisi imetoa mafunzo kwa mafundi na wahandisi 60 wa Mashirika ya Umeme Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar kuhusu usimamizi wa kemikali aina ya *PCBs* zinazotumika katika mafuta ya kuendesha mitambo na vifaa vya kusambaza umeme nchini. Aidha, mafunzo yametolewa kwa wadau 60 kuhusu matumizi ya teknolojia bora zilizopo na utaratibu bora wa usimamizi wa mazingira ili kupunguza uzalishaji wa kemikali aina ya *Dioxins na Furans.*

Washiriki wa mafunzo haya walitoka Mikoa ya Mwanza, Kagera, Mara, Shinyanga, Kigoma, Arusha, Manyara, Kilimanjaro, Tanga na Dar es Salaam. Mafunzo yalihusisha wawakilishi kutoka Sekretarieti za Mikoa; Vyuo vya *VETA,* Halmashauri za Miji/Majiji na Hospitali za Mikoa, Maofisa mazingira, Waratibu wa Mikoa, Viwanda vidogo na Shirika la Viwango Tanzania. Kwa mwaka 2011/12, Ofisi itaendelea kuratibu Mpango wa Kitaifa wa Utekelezaji wa Mkataba wa Stockholm. Aidha, Ofisi itaendelea kuratibu utekelezaji wa mradi wa kujenga uwezo wa taasisi husika katika kutekeleza Mkataba.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio yaliyopatikana katika kutekeleza masuala ya hifadhi na usimamizi wa mazingira, kumekuwa na changamoto kadhaa zikiwemo, uelewa mdogo wa jamii juu ya masuala ya mazingira, kukosekana takwimu sahihi za masuala ya mazingira kunaleta changamoto katika upangaji wa mipango ya Mazingira. Pamoja na changamoto hizo, Serikali itaendelea kuelimisha umma na kuwajengea uwezo watendaji katika ngazi mbalimbali kuhusu masuala ya mazingira ili nchi yetu iweze kuwa na mazingira safi na salama kwa kizazi cha sasa na vizazi vijavyo.

Mheshimiwa Spika, sasa ni mwaka wa sita tangu Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura ya 191, ianze kutekelezwa. Kati ya wadau muhimu katika usimamizi na utelekelezaji wa Sheria hii ni Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira *(NEMC).*

Katika Mwaka wa Fedha wa 2010/11, Baraza liliendelea kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria kwa kuzingatia Sera ya Mazingira ya Mwaka 1997, Mpango Mkakati wa Baraza *(NEMC Strategic Plan 2010-2014),* Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2005, Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025, nyaraka na mikakati mingine ya kitaifa ya kuhifadhi mazingira na maelekezo ya Viongozi Wakuu wa Kitaifa.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2010/11, Baraza lilifanya ukaguzi wa viwanda, migodi na sehemu za uzalishaji ili kuhakikisha kuwa taratibu na kanuni za

hifadhi ya mazingira zinafuatwa. Shughuli zilizokaguliwa na kupewa amri ya kuboresha mifumo ili kuzingatia hifadhi ya mazingira ni pamoja na: Viwanda 12 vilivyoko Mikocheni (Dar es Salaam); *Lake Oil Petrol Station (Mwanza); Resolute Gold Mine Ltd (Tabora); Mwanza Beverage Company Ltd (Mwanza); Mwatex (Mwanza); Nyakato Steel Industries (Mwanza); MUTEX (Mara); Mara Milk & Musoma Dairy (Mara); Bunda Oil Ltd (Mara); Musoma Fish Processing (Mara), Prime Catch Fish Processing Ltd na Victoria Dairy (Mara); Banana Investment (Arusha); Mbeya Textile Mill* (Mbeya), pamoja na maeneo ya wachimbaji wadogo wa dhahabu Wilayani Chunya na shughuli za viwanda Mkoani Rukwa ikiwemo *Energy Milling Company Ltd, SAAFI Meat Processing, TPM Mining* na *Sunflower Oil Mills.*

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2010/11, Baraza liliendelea kuhimiza uzingatiaji wa Sheria ya Mazingira kwa kutoa mafunzo kuhusu Sheria ya Mazingira kwa maafisa 31 kutoka Halmashari za Wilaya katika Kanda ya Nyanda za Juu Kusini (Mbeya, Iringa, Rukwa na Ruvuma). Aidha, Baraza lilikagua na kutoa ushauri wa kuboresha machinjio ya Ukonga na Vingunguti Dar es Salaam. Vilevile lilikagua makazi katika maeneo ya Kawe, Masaki, Mikocheni na Kijito cha Mlalakuwa (Dar es Salaam), kufuatia malalamiko ya Wananchi kuhusu uchafuzi wa mazingira. Vilevile Baraza lilitoa amri ya kusitisha ulundikaji wa nguzo za Umeme za Kampuni ya *TANESCO* Katika Kata ya Mivinjeni, Manispaa ya Temeke, kutokana na harufu mbaya na uchafuzi wa mazingira. Amri hiyo ilitekelezwa na tatizo hilo limeondoshwa. Aidha, Baraza kupitia ofisi zake za kanda ambazo ni Kanda ya Ziwa (Mwanza), Kanda Kaskazini (Arusha) na Nyanda za Juu Kusini (Mbeya), zilikamilisha ukaguzi ili kutambua shughuli ambazo zitahusika katika tozo ya uchafuzi wa mazingira kuanzia Mwaka wa Fedha wa 2011/12.

Mheshimiwa Spika, Baraza kupitia Kamati ya Ushauri ya Usimamizi wa Kemikali *(Chemicals Management Advisory Commitee - CMAC)*, lilisimamia uteketezaji wa kemikali chakavu kwa Taasisi za Serikali na Binafsi. Kemikali hizo ni za maabara zilizokwisha muda wake, zinazolundikana katika Chuo cha Maendeleo na Usimamizi wa Maji Ubungo, madawa chakavu kwenye ghala la Madawa *(MSD)* na kuelekeza utupaji salama wa mabati na vifaa vya ujenzi aina ya *asbestos* katika Chuo kipya cha Sayansi na Teknolojia cha Nelson Mandela, Arusha. Aidha, Baraza lilitoa ushauri kuzingatia Sheria na utaalamu kuhusu utupaji taka zitokanazo na uyeyushwaji wa madini ya risasi kwa Kiwanda cha Gaia Eco- Solution (T) Ltd, Tegeta, Dar es Salaam. Vilevile Baraza lilitoa mwongozo na vibali kuelekeza ipasavyo ukusanyaji mafuta na vyuma chakavu kwa Makampuni ya *Baga Investment, VJB General Supplies, Nyakato Steel Mills, Ikhomeo Enterprises, Nushipper Enterprises, Enve Company (T) Ltd, Renus Shipping Services, Singilimo Enterprises* na *Millennium Express Co. Ltd* za hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha wa 2011/12, Baraza litaendeleza jitihada za usimamizi wa Sheria ya Mazingira kwa kufanya ukaguzi wa kudumu katika maeneo yenye uchafuzi mkubwa wa mazingira vikiwemo viwanda na migodi. Aidha, Baraza litaendelea kukuza uwezo wa Serikali za Mitaa katika kusimamia ukusanyaji na utupaji wa taka za aina zote. Baraza litaendesha mafunzo kwa Maafisa Mazingira kutoka Serikali za Mitaa katika Kanda ya Mashariki (Pwani, Dar es Salaam na Morogoro) na Kanda ya Kaskazini (Arusha, Manyara, Tanga na Kilimanjaro) ili kukuza uelewa.

Vilevile Baraza linatarajia kuandaa mikakati ya pamoja na wadau wa mazingira ili kuimarisha usimamizi wa hifadhi ya mazingira nchini.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha wa 2010/11, Baraza liliendelea kufuatilia na kuratibu utekelezaji wa hatua zilizochukuliwa kudhibiti uchafuzi uliotokea katika Mgodi wa North Mara.

Baraza liliendelea kufuatilia na kuratibu utekelezaji wa Mpango Kazi wa Serikali uliozishirikisha sekta zote muhimu kuhakikisha kuwa, uchafuzi uliotokea katika Mgodi wa North Mara unadhibitiwa na hautokei tena katika Mgodi wa North Mara na katika migodi mingine nchini.

Mwekezaji wa *North Mara Gold Mine – Barrick,* ametekeleza masharti yote aliyopewa kurejesha mazingira katika hali yake ya awali, ikiwa ni pamoja na kuandaa mpango madhubuti wa kuhifadhi mazingira katika eneo la mgodi.

Jitihada zinazoendelea sasa ni kurejesha mahusiano mazuri kati ya mgodi na Wananchi wanaoishi katika vijiji vinavyozunguka mgodi. Jitihada hizi zinafanyika kwa kushirikisha mgodi wenyewe, Serikali ya Wilaya ya Tarime, na Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira. Aidha, Wizara ya Maji inaendelea kutafuta vyanzo vya maji mbadala na hadi sasa zaidi ya visima saba vimechimbwa na upembuzi yakinifu umekwishakamilika wa kuchimba visima vingine katika maeneo mbalimbali ya vijiji vinavyozunguka mgodi. Aidha, Wizara za Afya na Ustawi wa Jamii na Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, zinaendelea na utafiti wa kubaini hali halisi ya afya ya binadamu na mifugo na njia sahihi za kuboresha hali hizo.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha wa 2010/11, Baraza liliendelea kusimamia utekelezaji wa agizo la Serikali la kupiga marufuku uingizaji, utengenezaji, uuzaji na matumizi ya mifuko laini ya plastiki yenye unene chini ya mikroni thelathini iliyoanza kutumika Julai, 2006. Katika kutekeleza agizo hili, Baraza lilifanya jitihada kuelimisha jamii kupitia vyombo vya habari na kufanya misako ya kushitukiza ya mara kwa mara katika maeneo mbalimbali nchini, ikiwemo Dar es Salaam, Arusha Mwanza na Mbeya ili kubaini wanaovunja amri hii na kuchukua hatua za kisheria.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2010/11, Serikali iliendeleza juhudi za kusimamia agizo lililopiga marufuku matumizi ya mifuko ya plastiki nchini. Hata hivyo, juhudi hizo zimekabiliana na changamoto za mifuko mingi kuingizwa nchini kwa njia za panya. Aidha, Wananchi wengi wameshindwa kutofautisha mifuko iliyopigwa marufuku, ambayo ni ile yenye unene chini ya mikroni 30. Mifuko iliyoruhusiwa ni yenye unene wa mikroni 30 na zaidi. Katika kukabiliana na changamoto hizo, Baraza limekamilisha utafiti utakaowezesha Serikali kuweka mikakati madhubuti ya kudhibiti tatizo la mifuko ya plastiki nchini.

Katika Mwaka wa Fedha wa 2011/12, Serikali kwa kushirikiana na Wadau mbalimbali, itatekeleza ipasavyo mapendekezo na ushauri unaotokana na utafiti huo.

Mheshimiwa Spika, Baraza kwa kupitia Ofisi ya Kanda ya Kaskazini iliyoko Arusha, lilishirikisha Watendaji wa Serikali za Mikoa ya Tanga, Kilimanjaro na Arusha, kuendesha kampeni ya kudhibiti utupaji taka ovyo kutoka katika mabasi ya abiria. Jumla ya mifuko 300 ya kuhifadhia taka ambayo ni salama kwa mazingira ilisambazwa kwa wamiliki wa mabasi na wafanyabiashara wadogo wadogo. Katika zoezi hili, hali ya utupaji taka katika barabara ya Arusha – Mombo – Muheza – Tanga itafanyiwa tathmini kwa kuwahoji abiria na wamiliki wa migahawa pamoja wafanyabiashara wadogo na wakazi wa maeneo hayo. Baraza pia lilifanya kikao na Sekretarieti ya Mkoa wa Tanga ili kuweka mikakati ya kudumisha usafi wa Jiji la Tanga. Zoezi la kusimamia utekelezaji wa kanuni hii litaendelea katika Mwaka wa Fedha wa 2011/12.

Mheshimiwa Spika, Baraza limeendelea kuratibu Programu ya *Africa Stockpiles (ASP)*, ambayo inalenga kukusanya, kusafirisha na kuteketeza viuatilifu chakavu *(obsolete pesticides)*, vilivyolundikana nchini; ikiwa ni pamoja na kuweka mikakati ya udhibiti ili kuhakikisha kuwa, mlundikano wa viuatilifu hautokei tena hapa nchini. Katika Mwaka wa Fedha wa 2010/11, zoezi la kuainisha vituo vitakavyotumika kukusanya shehena ya viuatilifu chakavu *(collection centres)* katika maeneo sita nchini, ambayo ni Arusha, Morogoro, Nzega, Mbeya, Kibiti na Mahonda (Zanzibar) limefanyika. Aidha, zoezi la kuratibu viuatilifu chakavu nchini kote limekamilika na tani 700 zimebainishwa na kuorodheshwa katika maeneo 135 nchini kote.

Pia zoezi la kuchukua sampuli za udongo na kupima viwango vya uchafuzi lilifanyika, ambapo tani 600 za udongo uliochafuliwa na viuatilifu zimegundulika katika maeneo 14 nchini kote. Vilevile tathmini ya athari ya mradi kwa mazingira ilifanyika na taarifa hiyo ya athari kwa mazingira inatumika kama dira katika kusimamia zoezi la uondoshaji viatilifu chakavu nchini.

Mheshimiwa Spika, zoezi hili la kukusanya viuatilifu chakavu limekuwa na mafanikio, kwani baada ya kufanya kampeni ya kuelimisha wadau na Wananchi wa maeneo husika, hususan watu binafsi, taasisi za umma na asasi zisizo za Kiserikali zote zimeitikia wito na kutoa ushirikiano kwa kiwango cha kuridhisha. Aidha, Baraza limeendelea kutekeleza Mkakati wa Kitaifa wa Mawasiliano wa Programu ya *ASP (ASP Communication Strategy for Tanzania)*, unaosaidia katika kuhakikisha kwamba, jamii kwa ujumla inapata ujumbe kuhusu madhara yatokanayo na matumizi mabaya ya viuatilifu na kuelimisha jamii itoe ushirikiano ili kuhakikisha mlundikano wa viuatilifu chakavu hautokei hapa nchini. Katika kutekeleza Mkakati huu, makala ziliandaliwa na kurushwa kupitia *TBC*, *ITV* na *Radio One*. Aidha, ufuatiliaji umeonesha kuongezeka kwa uelewa juu ya Programu hii ya asp hapa nchini. Zoezi hili la kusafisha mazingira kupitia ukusanyaji na usafirishaji wa viuatilifu na uteketezaji wake, linatarajia kukamilika katika Mwaka wa Fedha wa 2011/12.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha wa 2010/11, Miradi ya Maendeleo 467 ya wawekezaji ilisajiliwa kwa ajili ya kufanyiwa Tathmini ya Athari kwa Mazingira (TAM). Jumla ya Miradi 163 imepata Hati za TAM baada ya kukidhi vigezo kwa mujibu wa Kanuni za TAM, Miradi 146 imefanyiwa TAM na ripoti zake kufanyiwa mapitio kwa ajili ya kupata Hati za TAM *(EIA Certificate)* na Miradi 158 inaendelea kufanyiwa kazi

na wawekezaji na haijarejeshwa ili kuendeleza mchakato wa kupatiwa hati. Kati ya Miradi iliyopewa Hati za TAM, 44 ni ya mawasiliano; 16 ya ujenzi na uendelezaji kwenye vivutio vya utalii; 17 ya miundombinu; 7 ya uchimbaji madini; 28 ya nishati; 36 ya viwanda; 12 maji na 3 ya misitu na kilimo.

Mheshimiwa Spika, haya ni mafanikio kwani kumekuwepo na ongezeko la Miradi iliyosajiliwa ili kufanyiwa TAM kutoka 220 mwaka 2009/10 hadi Miradi 467 mwaka 2010/11, sawa na ongezeko la asilimia 112.3. Aidha, Miradi iliyofanyiwa mapitio na kupatiwa Hati imeongezeka kutoka Miradi 89 mwaka 2009/2010, hadi Miradi 163 mwaka 2010/11, sawa na ongezeko la asilimia 83. Ongezeko hili linaonesha kuwa, wawekezaji wengi wamepata mwamko wa kufuata na kutimiza matakwa ya Sheria ya Mazingira, Sura ya 191, ambayo pamoja na mambo mengine, inawataka wawekezaji kutimiza masharti ya TAM kabla na baada ya uwekezaji.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha wa 2010/11, Baraza liliendesha mafunzo yenye lengo la kukuza uelewa wa wadau kuhusu umuhimu na hatua za kuzingatiwa katika masuala ya TAM. Mafunzo ya TAM yalitolewa kwa Wahandisi na Mafundi mchundo 36 kwa Miradi ya ujenzi wa barabara ambayo yalifanyikia Shinyanga. Vilevile wafanyakazi 14 wa asasi isiyo ya Kiserikali *(Envirocare)* walipata mafunzo juu ya Ukaguzi na Ufuatiliaji wa Mazingira *(Environmental Auditing and Monitoring)*, yaliyofanyika Dar es Salaam. Wafanyakazi 14 wa viwanda vya nguo walipata mafunzo juu ya Ukaguzi na Ufuatiliaji wa Mazingira *(Environmental Auditing and Monitoring)*, Mjini Morogoro. Wafanyakazi 10 wa *Envirocare* walipata mafunzo ya usimamizi wa taka zitokanazo na Viwanda; Ukaguzi na Usimamizi wa Mazingira; Tathmini ya Athari ya Mazingira ya Mzunguko wa Bidhaa *(Life Cycle Assessment - LCA)*. Mafunzo kwa Maafisa 50 wakiwemo Maafisa Mazingira na Kikosi cha wawezeshaji wa Wilaya *(District Facilitation Team)* kuhusu Uandaaji wa Mipango ya Usimamizi wa Mazingira kwa Miradi ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo katika Wilaya, yalifanyika Shinyanga. Vilevile mafunzo kuhusu TAM kwa watendaji 100 wa Serikali wakiwemo Wakuu wa Idara, Maafisa Mazingira na Wataalam wa Mradi wa Usimamizi Kamilifu wa Mazingira ya Pwani *(Intergrated Coastal Management – ICM)* kutoka Jiji la Tanga na Wilaya za Mkinga, Muheza na Pangani yalifanyika Tanga.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha wa 2010/11, Baraza lilipokea jumla ya maombi 210 kwa ajili ya usajili wa wataalamu wa TAM na Ukaguzi wa Mazingira *(Environmental Auditors)*. Maombi haya yalifanyiwa tathmini ili kukamilisha usajili rasmi wa wataalamu hawa. Wataalamu 101 wa TAM na 60 wa ukaguzi wa mazingira wamesajiliwa kwenye Gazeti la Serikali la tarehe 1 Aprili, 2011. Pia, maombi ya makampuni 40 yanayotoa utaalamu elekezi wa TAM na ukaguzi wa mazingira yalipokelewa kwa ajili ya usajili. Makampuni 23 yalisajiliwa kufanya TAM na 12 yalisajiliwa kufanya ukaguzi wa mazingira.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha wa 2011/12, Baraza litaendelea kufanya mapitio ya Taarifa za TAM, kusajili Wataalam wa TAM na Ukaguzi wa Mazingira na kukagua Miradi ya Maendeleo, ili kuhakikisha kuwa, inatekeleza matakwa yaliyoainishwa kwenye Hati za TAM na Mipango ya Hifadhi ya Mazingira

*(Environmental Management Plans).* Vilevile Baraza litaendelea kuwajengea uwezo wadau kuhusu masuala ya TAM ili kuhakikisha kuwa, shughuli za maendeleo zinakuwa endelevu.

Mheshimiwa Spika, elimu ya mazingira ni muhimu sana kwa umma ili jamii iweze kushiriki katika kufanya maamuzi sahihi yanayohusu matumizi endelevu ya maliasili na mazingira kwa ujumla. Katika Mwaka wa Fedha wa 2010/11, Baraza liliendelea kutoa elimu ya mazingira kwa umma kwa kuandaa, kuchapisha na kusambaza kwa wadau: vipeperushi 20,000 kuhusu mazingira na kilimo; nakala 2,000 za Jarida la *NEMC* la mwezi Januari – Juni, 2011; na nakala 1,000 za kalenda ya mwaka 2011. Baraza lilishirikiana na wadau kuandaa tovuti ya mazingira inayoitwa *Tanzania Environment Web Portal (www.tanzaniaenvironment.gov).* Vilevile tovuti ya Baraza imeendelea kuboreshwa kwa kuweka taarifa mpya zinazohusu mazingira na anuani mpya ya tovuti ya Baraza ni *www.nemc.or.tz.*

Mheshimiwa Spika, Baraza lilishiriki katika Wiki ya Maadhimisho ya Siku ya Nane Nane mwaka 2010, yaliyofanyika Mkoani Dodoma ili kukuza uelewa kuhusu mahusiano kati ya kilimo na hifadhi ya mazingira. Aidha, jumla ya vipindi 30 kuhusu mada mbalimbali za elimu ya mazingira vilirushwa kupitia Vituo vya *Channel 10, Star TV* na *TBC1*.

Baraza limeshiriki katika Maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani na Uzinduzi wa Maadhimisho ya Miaka 50 ya Uhuru wa Tanzania Bara yaliyofanyika Mkoani Ruvuma. Katika Maadhimisho hayo, Baraza kwa kushirikiana na wadau, walishiriki katika shughuli za kupanda miti, kutembelea shughuli za hifadhi ya mazingira katika Wilaya za Songea Mjini, Songea Vijijini, Namtumbo na Mbinga. Pia, Ofisi za Baraza za Kanda (Arusha, Mbeya na Mwanza), zilishirikiana na wadau katika kuadhimisha Siku ya Mazingira Duniani na Miaka 50 ya Uhuru kwa kushiriki katika shughuli za hifadhi ya mazingira. Aidha, Baraza liliendelea kushirikiana na wadau vikiwemo vikundi vitano vya kijamii katika ngazi ya kijiji, ambavyo vimewezeshwa kufanya shughuli za mazingira kama vile kupanda miche ya miti na shughuli nyingine mbalimbali za mazingira.

Mheshimiwa Spika, pamoja na juhudi zote za kutoa elimu, vitendo vya uchafuzi wa mazingira kama utupaji taka ovyo, utiririshaji wa maji machafu, matumizi na uchomaji mifuko ya plastiki na ukataji miti ovyo, bado ni tatizo kwa baadhi ya maeneo. Ninapenda kutoa wito kwa Wananchi wote, kushiriki kikamilifu katika shughuli za hifadhi ya mazingira kwani suala la hifadhi ya mazingira ni letu sote na matokeo ya uharibifu wa mazingira hayana mipaka.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha wa 2011/12, Baraza litaongeza kasi ya kukusanya taarifa na kutoa elimu ya mazingira kwa umma kuhusu hifadhi ya mazingira kwa kuzingatia haki, wajibu na majukumu ya wadau katika hifadhi ya mazingira na matumizi endelevu ya rasilimali za nchi. Baraza litaendelea kukamilisha na kuboresha mifumo ya mawasiliano kati ya Baraza na wadau, zikiwemo Tovuti ya Baraza,

Tovuti ya Mazingira *(Environment Web Portal)* na kuhamasisha matumizi ya mitandao hii miongoni mwa sekta husika.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha wa 2010/11, Baraza kwa kushirikiana na *Amani Nature Reserve*, lilitekeleza shughuli za Hifadhi Hai *(Biosphere Reserves)* kwa kupitia ufadhili wa Programu ya Umoja wa Mataifa iitwayo *Joint Program 11*. Katika kutekeleza shughuli hizi, warsha ya wadau kuhusu maandalizi ya mipango ya Hifadhi Hai ilifanyika Tanga mwezi Aprili. Warsha hii ilihudhuriwa na wadau kutoka Wilaya tatu za Tanga zinazopakana na Hifadhi Hai ya Usambara Mashariki (Korogwe, Muheza na Mkinga), Mwakilishi toka Hifadhi Hai ya Ziwa Manyara, Wawakilishi wa *NGOs* na Idara mbalimbali za Serikali. Aidha, Baraza liliendesha mafunzo ya siku tatu huko Tanga kuhusu kutengeneza mwongozo kwa ajili ya maandalizi ya mipango ya usimamizi wa Hifadhi Hai. Mafunzo hayo yalihudhuriwa na wadau kutoka Hifadhi Hai za Usambara Mashariki, Ziwa Manyara na Ngorongoro-Serengeti, pamoja na wadau kutoka taasisi mbalimbali za Serikali. Pia, Baraza liliratibu Kikao cha Kamati ya Taifa ya Usimamizi wa Hifadhi Hai *(MAB National Committee)*, kilichofanyika mwezi Machi, Mkoani Tanga.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2010/11, Baraza liliendelea kutekeleza Mkakati wa Usimamizi Kamilifu wa Mazingira ya Pwani kwa kupitia Miradi ya *Marine and Coastal Environment Management Project (MACEMP), Tanzania Coastal Management Partneship (TCMP-SUCCESS), Regional Programme for the Sustainable Management of the Coastal Zones of the Indian Ocean Countires (ReCoMaP)* pamoja na *Aghulus and Somali Current Large Marine Ecosystems (ASCLME).* Baraza pia lilifanya mapitio na ufuatiliaji wa Mipango Kazi ya Wilaya za Mafia, Kilwa na Rufiji ili iweze kulingana na Mwongozo wa Kitaifa wa Uandaaji wa Mipango Kazi. Aidha, Baraza lilitoa ushauri wa kitaalamu kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa katika utekelezaji wa mipango kazi ya Usimamizi Kamilifu wa Mazingira ya Pwani *(ICM Action Plans).* Baraza lilifanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa mipango kazi ya *ICM* katika mamlaka zote 16 za Pwani za Serikali za Mitaa, ambapo mafanikio kulingana na malengo yaliyowekwa ni zaidi ya asilimia sabini.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2010/11, Baraza lilichapisha na kusambaza kwa wadau nakala 1,000 za Mwongozo wa Uandaaji wa Mipango Kazi ya Usimamizi Kamilifu wa Mazingira ya Pwani (nakala za Kiswahili 500 na za Kiingereza 500). Aidha, Baraza liliandaa na kuchapisha nakala 1,000 za Taarifa ya Mazingira ya Pwani *(State of the Coast Report),* ambayo itatumika kuandaa taarifa ya mazingira kitaifa. Vilevile Baraza liliendelea na mchakato wa kufanya mapitio ya Mkakati wa Usimamizi Kamilifu wa Mazingira ya Pwani ili kuhuisha masuala muhimu yaliyoibuka karibuni kama vile mabadiliko ya tabianchi, uvunaji gesi asilia na mafuta katika eneo la pwani na bahari na mengineyo. Pia, vikundi 459 vilivyoko katika Ukanda huo wa Pwani vimewezeshwa kwa mitaji na utaalamu ili kuanzisha shughuli mbalimbali zinazochangia katika kupunguza umaskini na uharibifu wa mazingira ikiwa ni pamoja na ufugaji kuku, nyuki, samaki, kaa, ng'ombe, mbuzi na kilimo cha mwani. Pia, mafunzo kuhusu Tathmini ya Athari kwa Mazingira yalitolewa kwa Watendaji wa Serikali 100 wakiwemo Wakuu wa Idara, Maafisa Mazingira na Wataalam wa *ICM* kutoka Jiji la Tanga, Mkinga,

Muheza na Pangani. Vilevile Baraza liliratibu mchakato wa kupata maoni kwa ajili ya kuboresha rasimu ya Itifaki ya Usimamizi Kamilifu wa Ukanda na Rasilimali za Pwani na Bahari chini ya Mkataba wa Nairobi *(Integrated Coastal Zone Management Protocol to the Nairobi Convention).*

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha wa 2011/12, Baraza litaendelea kuratibu kikamilifu utekelezaji wa mkakati kamilifu wa usimazi wa mazingira ya pwani na bahari kwa kupitia Miradi mbalimbali ya hifadhi ya pwani inayotekelezwa na Baraza.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha wa 2010/11, Baraza liliendelea kuratibu utekelezaji wa Mradi wa Usimamizi wa Hifadhi ya Mazingira ya Bonde la Mto Kihansi *(Lower Kihansi Environmental Management Project - LKEMP).* Katika kipindi hiki, ukaguzi wa mazingira *(Environmental Audit)*, ulifanyika. Aidha, katika juhudi za kupunguza athari za kemikali kwa watu na Mto wa Kihansi, warsha ya siku tatu ilifanyika Mufindi kuhusu matumizi bora na salama ya viuatilifu katika shughuli za kilimo. Ninapenda kutoa taarifa kuwa, ufadhili wa Mradi huu wa *LKEMP* toka Benki ya Dunia, ulifikia kikomo Juni 30, 2011. Hata hivyo, Shirika la Umeme Tanzania kwa kushirikiana na sekta mbalimbali, wataendeleza shughuli zote zilizoanzishwa na Mradi huu chini ya Mpango wa Mazingira wa Mradi wa Kuzalisha Umeme Kihansi *(Lower Kihansi Hydro Power Project - Environmental Management Plan-LKHP-EMP).*

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha wa 2011/12, Baraza litaendelea kutekeleza Ajenda ya Taifa ya Utafiti katika Mazingira *(National Environmental Reasearch Agenda - NERA)* na kuwajengea uwezo Maafisa Mazingira katika ngazi za Mikoa na Wilaya ili waweze kutekeleza Ajenda ya Taifa kuhusu utafiti katika mazingira. Aidha, Baraza litaendelea kufanya tafiti ili kupata taarifa zaidi kuhusu hali na ikologia ya milima nchini.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha wa 2010/11, Baraza liliendelea kudumisha nidhamu na uwajibikaji wa watumishi katika kutoa huduma. Kanuni za utumishi, fedha na manunuzi zilizingatiwa ili kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira. Aidha, katika kuongeza ufanisi kwa watumishi, watumishi 21 wa Baraza wanaendelea na mfunzo ya muda mrefu ndani na nje ya nchi na watumishi tisa walishiriki warsha mbalimbali ndani na nje ya nchi ili kujenga uwezo katika masuala ya utawala na utekelezaji wa Sheria ya Mazingira.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha wa 2010/11, Baraza lilikamilisha ukarabati wa jengo moja na kujenga ukumbi wa mikutano katika kiwanja chake kilichopo Regent Estate, Mikocheni. Baraza limepanga kufungua Ofisi ya Kanda ya Kati Dodoma na tayari kiwanja kimepatikana. Aidha, katika Mwaka wa Fedha wa 2011/12, Baraza litaendelea kuwajengea uwezo wafanyakazi ili kuongeza ufanisi katika utendaji, litajenga uzio. Maandalizi ya michoro kwa ajili ya ujenzi wa jengo la kudumu yameanza na yataendelea katika Mwaka wa Fedha wa 2011/12.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha wa 2010/11, Ofisi ilijaza nafasi zilizokuwa wazi za Msaidizi wa Makamu wa Rais mmoja, Wakurugenzi wawili; mmoja

kwa ajili ya Idara ya Muungano na mwingine kwa ajili ya Idara ya Mazingira, Wakurugenzi Wasaidizi wawili; mmoja kwa ajili ya Idara ya Sera na Mipango na mwingine kwa ajili ya Idara ya Muungano na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Ndani mmoja. Aidha, Watumishi kada mbalimbali 24 wamepewa ajira ya kudumu, 15 wamethibitishwa kazini na 28 wamepandishwa vyeo kwa kuzingatia Miundo ya Utumishi wa Umma.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha wa 2010/11, Ofisi imefanikiwa kuandaa Miundo ya Utumishi miwili mipya ambayo ni Muundo wa Utumishi wa Kada ya Afisa Mazingira na Muundo wa Utumishi wa Kada ya Mhandisi Mazingira. Miundo hii imewasilishwa Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, kwa ajili ya idhini na kusambazwa katika Wizara, Idara na Wakala wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Mwaka wa Fedha wa 2010/11, Ofisi iliendelea kusimamia utendaji kazi kwa misingi ya Utawala Bora. Hii ni pamoja na kuhakikisha kuwa, kila mtumishi anapangiwa kazi za kutosha kulingana na majukumu ya Ofisi. Aidha, Ofisi iliendelea kulinda haki za Watumishi kwa kufanya vikao viwili vya Baraza la Wafanyakazi ambalo lilijadili na kupitisha masuala yanayohusu wafanyakazi na utekelezaji wa shughuli za Ofisi kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia umuhimu wa kuwaongezea watumishi uwezo wa kielimu na utendaji kazi, katika Mwaka wa Fedha wa 2010/11, Ofisi imeweza kugharamia mafunzo ya muda mrefu na mfupi ndani na nje ya nchi kwa watumishi wapatao 23, kuhudhuria mafunzo ya aina mbalimbali kwa kuzingatia majukumu yao kazini. Kati ya hao, saba walihudhuria mafunzo ya muda mrefu, na 16 walihudhuria mafunzo ya muda mfupi.

Mheshimiwa Spika, katika kuboresha mazingira ya kazi na kuongeza ufanisi, Ofisi imeendelea kusimamia ujenzi wa Jengo la Ofisi Awamu ya Pili katika Kiwanja Na.10 kilichopo katika Mtaa wa Luthuli, Dar es Salaam. Ujenzi huu unaendelea vizuri na unategemewa kukamilika mwezi Desemba, 2011. Aidha, ujenzi wa Ofisi na Makazi ya Makamu wa Rais Tunguu - Zanzibar umekamilika na samani zake zinatarajiwa kukamilisha katika Mwaka wa Fedha wa 2011/12.

Mheshimiwa Spika, kwa Mwaka wa Fedha wa 2011/12, Ofisi itaendelea kuratibu, kusimamia na kushughulikia masuala yote ya Watumishi yahusuyo ajira, maslahi, nidhamu, mafunzo, mapambano dhidi ya rushwa na kuhakikisha kuwa, Watumishi wanapata vitendea kazi ili kuongeza ufanisi. Vilevile Ofisi itaendelea kuhamasisha watumishi kupima afya zao kwa hiari hususan Virusi vya UKIMWI.

Mheshimiwa Spika, mafanikio ya Ofisi hii yamechangiwa pia na Wadau wa Maendeleo; ninaomba nitumie nafasi hii kuwashukuru wote waliotusaidia. Ninapenda kuzitaja baadhi ya Nchi na Mashirika ya Kimataifa yafuatayo: Serikali ya Norway, Jamhuri ya Korea ya Kusini, Serikali ya Uholanzi, Serikali ya Marekani, Shirika la Mpango wa Maendeleo la Umoja wa Mataifa *(UNDP)*, Umoja wa Nchi za Ulaya *(EU)*, Shirika la Maendeleo la Marekani *(USAID)*, Shirika la Mpango wa Mazingira la Umoja

wa Mataifa *(UNEP)*, Mfuko wa Mazingira Duniani *(GEF)*, Benki ya Dunia, *International Development Agency (IDA)*, Shirika la Maendeleo la Canada *(CIDA)*, Shirika la Maendeleo la Denmark *(DANIDA)*, *SADC-REEP*, *Wildlife Conservation Society (WCS)*, *World Wildlife Fund (WWF)*, Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa *(FAO)*, *Crop Life International (CLI)*, Benki ya Maendeleo ya Afrika *(AfDB)*, Shirika la Misaada ya Kiufundi la Ujerumani *(GTZ)* na Asasi Zisizo za Kiserikali *(AZISE)*. Aidha, ninapenda nitumie nafasi hii kuwaomba Wadau wa Maendeleo, waendelee kutusaidia katika kipindi kijacho ili tuweze kufanikiwa zaidi katika vita dhidi ya umaskini na juhudi za kuboresha maisha ya kila Mtanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ili Ofisi iweze kutekeleza majukumu na malengo yaliyoelezwa katika Hotuba hii, ninaomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu liidhinishe maombi ya fedha kwa Mwaka wa Fedha wa 2011/12 kama ifutavyo:-

Mheshimiwa Spika, Fungu 26 - Makamu wa Rais: Katika Mwaka wa Fedha wa 2011/12, ninaomba Bunge lako Tukufu liidhinishe Makadirio ya Matumizi ya Makamu wa Rais - Fungu 26, ya shilingi 4,523,675,000 fedha za matumizi ya kawaida. Kiasi hicho kinajumuisha fedha za mishahara ya watumishi shilingi 524,519,000 na fedha za Matumizi Mengineyo shilingi 3,999,156,000.

Mheshimiwa Spika, Fungu 31 - Ofisi ya Makamu wa Rais: Katika Mwaka wa Fedha wa 2011/12, ninaomba Bunge lako Tukufu, liidhinishe makadirio ya matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais - Fungu 31, ya shilingi 52,822,422,000. Kiasi hicho kinajumuisha shilingi 1,323,754,000 mishahara ya watumishi, shilingi 39,088,289,000 fedha za Matumizi Mengineyo na shilingi 12,410,379,000 fedha za Matumizi ya Maendeleo. Aidha, fedha za Maendeleo zinajumuisha fedha za ndani shilingi 6,067,014,000 na fedha za nje shilingi 6,343,365,000.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Hoja hii imeungwa mkono, ninashukuru kwa kusoma kwa haraka, kwa hiyo, tumepata muda mwingine wa kuweza kujadili. *(Makofi)*

**MHE. ANGELLAH JASMINE M. KAIRUKI (K.n.y. MWENYEKITI KAMATI YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA):** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni 99(7) na 114(11), Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2007, ninaomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu, Taarifa ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano), kwa Mwaka wa Fedha wa 2010/2011 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha wa 2011/2012, kwa Fungu 26 – Ofisi Binafsi ya Makamu wa Rais na Fungu 31 – Ofisi ya Makamu wa Rais.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, ninapenda kutumia nafasi hii ya kipekee kabisa, kuwashukuru Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa UWT Mkoa wa Dar es Salaam, pamoja na Wajumbe wa Baraza Kuu la UWT Taifa, kwa kunichagua kwa kura nyingi zilizoniwezesha kuwa Mbunge katika Bunge lako Tukufu. Mwisho, lakini kwa umuhimu mkubwa, ninapenda kuishukuru familia yangu hususan mume wangu, pamoja na watoto wangu wapendwa, Precious na Esther, pamoja na ndugu na jamaa wote ambao wamekuwa wakiniunga mkono katika utekelezaji wa majukumu yangu na ushauri wamekuwa wakinipatia wakati wote.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza majukumu yake, tarehe 31 Mei, 2011, Kamati ilikutana Dar es Salaam, ili kupokea na kuchambua Taarifa ya Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi hiyo kwa Mwaka 2010/2011 na kupitia Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka 2011/2012.

Mheshimiwa Spika, katika Kikao hicho, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan (Mb), Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano, alieleza Majukumu, Dira na Dhima ya Ofisi ya Makamu wa Rais. Vilevile alieleza masuala yaliyotekelezwa kwa Mwaka wa Fedha wa 2010/2011.

Mheshimiwa Spika, wakati wa kuchambua Bajeti ya Ofisi hii kwa mwaka 2010/2011, Kamati ilitoa maoni na ushauri katika maeneo mbalimbali ili kuboresha utendaji kazi wa ofisi hii. Ninapenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, baadhi ya ushauri ulizingatiwa na kufanyiwa kazi kama ifuatavyo:-

Kuongeza juhudi ili ufanisi wa vikao vya Kamati ya pamoja ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar upatikane na Viongozi wahimizwe kuhudhuria vikao hivyo. Kamati ilipewa taarifa kwamba, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano), imeratibu Kikao cha Mawaziri wa Serikali ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Kikao cha Makatibu Wakuu wa Serikali ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Vikao vya Wataalamu. Pia imeratibu utekelezaji wa maagizo ya Vikao vya Kamati ya Pamoja kwa kuitisha vikao kujadili ongezeko la ankara za umeme, masuala ya fedha, usajili wa vyombo vya moto na suala la ajira kwa Watumishi wa Zanzibar katika Taasisi za Muungano. Vikao hivi vimekuwa na mafanikio kwa baadhi ya hoja kupatiwa ufumbuzi.

Mapendekezo ya Tume ya Pamoja ya Fedha ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kufanyiwa kazi na Serikali kwa haraka na umakini mkubwa. Kamati ilitaarifiwa kwamba, mapendekezo ya vigezo vya kufuata katika mgawanyo wa mapato ya Muungano na uchangiaji wa gharama za Muungano yamewasilishwa rasmi kwa Serikali zote mbili, ambazo bado zinafanyiwa kazi na hatimaye maelekezo yatatolewa.

Jitihada zaidi zinahitajika katika kuimarisha utaratibu uliopo wa vikao vya pamoja vya kisekta ili kuendelea kubadilishana uzoefu, ujuzi, utaalamu, sera na mafunzo. Kamati ilipewa taarifa kwamba, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano), imeratibu vikao vya ushirikiano katika masuala yasiyo ya Muungano kati ya Serikali mbili kwa kutoa ratiba

ya vikao vya ushirikiano kwa Wizara na Taasisi zisizo za Muungano kwa lengo la kuhimiza vikao vya pamoja vya kisekta katika maeneo yasiyo ya Muungano.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio yaliyopatikana mfano kuondoa tatizo la wafanyabiashara wa Zanzibar kutozwa kodi mara mbili, kuelimisha umma kuhusu Muungano na kuimarisha ushirikiano wa kiuchumi na kijamii, changamoto mbalimbali wakati wa utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano), ziliainishwa kama ifuatavyo:-

(a) Vikao vya Kamati ya pamoja ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kushughulikia masuala ya Muungano kutofanyika kwa mujibu wa ratiba kutokana na majukumu ya Viongozi wa Juu ambao ni wahusika wakuu katika vikao hivi.

(b) Kasi ndogo ya upatikanaji wa fedha za bajeti kutoka Wizara ya Fedha na Uchumi zinazopatikana zinakuwa ni kidogo na hivyo kusababisha ucheleweshaji wa utekelezaji wa shughuli zilizopangwa.

(c) Uhaba wa vitendea kazi hususan magari kwa ajili ya ufuatiliaji na utekelezaji wa Miradi ya Ofisi na shughuli za kila siku.

(d) Ufinyu wa Bajeti ya Fungu 31 ambalo linahitaji rasilimali fedha nyingi.

Mheshimiwa Spika, ili Muungano uendelee kuimarika na kushamiri siku hadi siku, Kamati inatoa maoni na ushauri ufuatao:-

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuyapatia ufumbuzi malalamiko ya wafanyabiashara wa Zanzibar kutozwa kodi mara mbili na taasisi za kutoza kodi ikiwemo Mamlaka ya Mapato Tanzania *(TRA).*

Kamati ilielezwa na Mheshimiwa Suluhu Hassan, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano) kuwa, kero hiyo kwa sasa haipo tena kwani bidhaa zinazoingizwa nchini na kukamilisha utaratibu wa forodha kupitia kituo chochote rasmi cha forodha na kuhesabiwa zimeingia ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, hazipaswi tena kulipiwa kodi mara mbili.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilielezwa pia kwamba, katika kuhakikisha tatizo hilo halijitokezi tena, Mamlaka ya Mapato Tanzania *(TRA)*, imeelekezwa kuchukua hatua za kisheria au kinidhamu kwa watendaji wake watakaoshindwa kutekeleza maagizo kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Spika, Kamati inazidi kuipongeza Serikali kwa kulipatia ufumbuzi tatizo la mgawanyo wa mapato yanayotokana na misaada kutoka nchi za je, ambapo kwa sasa Zanzibar inapata mapato yake kwa mujibu wa Kanuni na taratibu zilizokubalika na pande zote mbili za Muungano. Aidha, utekelezaji wa Sheria ya Haki za Binadamu

umepatiwa suluhisho kwani kwa hivi sasa Tume ya Haki za Binadamu imeweka ofisi zake Zanzibar na hivyo kuwawezesha Wananchi kuzitumia kuwasilisha malalamiko yao.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali kuendelea na mazungumzo kati ya pande mbili za Muungano ili kupata suluhisho kwa sekta zote zinazoonekana kuwa na matatizo hivyo kuwezesha Muungano wetu kuimarika zaidi.

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu inazidi kushauri kwamba, pamoja na kazi nzuri ambayo imekuwa ikifanywa na Kamati ya Pamoja ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, pamoja na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, katika kufuatilia na kuzipatia ufumbuzi changamoto za Muungano wetu, ni vyema Kamati hiyo ya kushughulikia masuala ya Muungano ikaongezewa wataalamu zaidi katika sekta zote ili waweze kuyachambua kitaalam, kuyaainisha, kuyawasilisha na hatimaye Kamati kuyatolea ufumbuzi matatizo yaliyoko kwenye mfumo wa Muungano wetu.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilibaini kwamba, pamoja na jitihada za Serikali za kujenga makazi na Ofisi kwa ajili ya Makamu wa Rais wa Serikali ya Muungano, bado Ofisi na makazi hayo hazina samani na hivyo kusababisha Mheshimiwa Makamu wa Rais, kufanya kazi katika mazingira magumu anapokuwa Zanzibar. Kamati inaishauri Serikali kutenga fedha kwenye bajeti hii ili samani za majengo hayo ziweze kununuliwa na hivyo kumwezesha Mheshimiwa Makamu wa Rais kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi wakati wote anapokuwa katika eneo lolote la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, Tume ya Pamoja ya Fedha ya Jamhuri ya Muungano, imeundwa kwa mujibu wa Ibara ya 134 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano (Katiba). Majukumu ya Tume yameainishwa katika Ibara ya 133 na 134 ya Katiba. Ibara ya 133 inaelezea jukumu la Tume katika kuamua kiasi kitachochangwa na Serikali zote mbili ili kwenda kwenye Akaunti ya Fedha ya Pamoja kwa ajili ya kugharamia Masuala ya Muungano. Ibara ya 134 inaelezea jukumu la Tume la kuchambua mapato na matumizi ya Muungano, kuchunguza mfumo na uhusiano wa mambo ya fedha ya Jamhuri ya Muungano na kutekeleza majukumu mengine kama yatakavyopangwa na Rais.

Mheshimiwa Spika, Tume ya Pamoja ya Fedha ilianzishwa Mwaka 2003 kwa Sheria inayoitwa Sheria Na. 14 ya Tume ya Pamoja ya Fedha ya Mwaka 1996.

Kwa mujibu wa Sheria hiyo, Kifungu cha 7 na 8, kazi kubwa ya Tume ni ya ushauri na siyo utendaji. Hata hivyo, Tume iko huru katika kutekeleza majukumu yake na haiingiliwi na mtu yeyote. Katika kutekeleza ushauri, imekuwa ikitumia utaalam wake na tafiti mbalimbali pamoja na kutumia washauri waelekezi. Aidha, Tume inawajibika kwa Waziri mwenye dhamana ya Fedha wa Jamhuri ya Muungano, lakini imekuwa ikiwasilisha ushauri wa wake kwa Mawaziri wenye dhamana ya fedha wa pande zote mbili za Muungano. Hata hivyo, kwa kiasi kikubwa inatoa ushauri ambao utekelezaji wake unatokana na uamuzi wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini kuwa, baadhi ya Maagizo ambayo Kamati hii ilitoa kwa Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano ili yafanyiwe kazi, hayakutekelezwa.

Moja ya Maagizo ya Kamati ilikuwa ni Serikali mbili kufanyia kazi kwa haraka mapendekezo ya Tume ya Pamoja ya Fedha ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ambayo yameshafikishwa Serikalini.

Mheshimiwa Spika, Kamati haioni sababu ni kwa nini mapendekezo haya ambayo ni ya Tume iliyowekwa Kikatiba, hayafanyiwi kazi hadi sasa ili kuwepo na vigezo vya kugawana mapato na kuchangia gharama za Muungano, ikiwa ni pamoja na kufunguliwa Akaunti ya Fedha ya Pamoja kwa mujibu wa Ibara ya 133 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, Kamati imepitia vizuri Sheria ya Tume ya Pamoja ya Fedha ya Mwaka 1996, mstari kwa mstari na kwa kutumia uzoefu na utaalam mkubwa wa Wajumbe wa Kamati, ni maoni ya Kamati kuwa sheria hii ina upungufu na hivyo ni vyema iangaliwe upya ikiwezekana iletwe Bungeni ili iweze kuboreshwa.

Mheshimiwa Spika, vilevile Kamati inashauri yafuatayo yatekelezwe:-

Ni vyema Mawaziri wa Fedha wa pande zote mbili za Muungano wakakutana na kushauriana kuhusu hatua zilizofikiwa na pande mbili katika kushughulikia mapendekezo ya Tume. Aidha, Tume ijulishwe hatua zilizofikiwa na pande mbili katika mapendekezo hayo.

Vilevile Bunge lina haki ya kupata taarifa, ni vyema Sheria inayotaka taarifa kupelekwa kwa Mawaziri wa Fedha iboreshwe ili Bunge na Baraza la Wawakilishi vihusishwe kwa kupelekewa uamuzi uliofikiwa na pande mbili kwa ajili ya kuridhiwa. Utaratibu unaotumiwa na Nchi ya India unaweza kufuatwa na Tume hii kwa kupeleka ushauri wao Bungeni au Baraza la Wawakilishi na siyo kwa Mawaziri.

Kwa kuwa nchi yetu sasa ipo kwenye mchakato wa mabadiliko ya Katiba, inashauriwa kero za Muungano ziangaliwe vizuri kwenye Katiba hiyo na Tume itakiwe kutoa maoni yake katika masuala ya uhusiano wa kifedha katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa ajili ya kuyaweka vizuri masuala hayo kwenye Katiba.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaipongeza Ofisi ya Makamu wa Rais kwa jitihada zake za kutoa elimu kwa umma kuhusu masuala ya Muungano na yasiyo ya Muungano. Kamati inaamini kwamba, changamoto na kero zinaweza kuondolewa iwapo Wananchi wataelimishwa na kufahamishwa kuhusu Muungano. Kamati inazidi kusisitiza elimu zaidi itolewe kwa umma kupitia redio, televisheni, magazeti, majarida, vipeperushi, machapisho na hata makongamano mbalimbali. Aidha, Kamati inatoa ushauri kwa Serikali kutoa elimu ya kutosha kwa Wananchi wafahamu umuhimu wa kufuata sheria na kutojichukulia madaraka mikononi ikiwa ni pamoja na kuwa na utayari wa kusikiliza na kutatua migogoro ili kuepusha matukio ya uvunjifu wa amani ambayo yamekuwa yakitokea kwa siku za hivi karibuni.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano), kwa Taarifa yake iliyowasilishwa mbele ya Kamati kuwa, hivi sasa vikao vya pamoja vya kisekta vinafanyika ikiwa ni utekelezaji wa ushauri wa Kamati hii uliotolewa mwaka jana. Vikao hivyo, kama ilivyoelezwa ni pamoja na kikao cha kisekta cha viwanda, biashara na masoko, kilichofanyika tarehe 8 Machi, 2011, Kikao cha Wizara ya Katiba na Sheria na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, kilichofanyika tarehe 31 Januari, 2011, Kikao cha Wizara ya Uchukuzi ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kilichofanyika tarehe 1 Aprili, 2011 na Kikao cha Wataalam wa Wizara ya Maji ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Wizara ya Ardhi, Makazi, Maji na Nishati, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, kilichofanyika tarehe 17 - 18 Mei, 2011.

Mheshimiwa Spika, haya ndiyo maoni na ushauri ambao Kamati yangu iliyatoa iliposhughulikia Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano). Ninapenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kwamba, baada ya ufafanuzi uliotolewa na Ofisi hiyo, hatimaye Kamati yangu iliyapitisha matumizi ya Ofisi hiyo na kuiruhusu yawasilishwe Bungeni kwa hatua zinazofuata.

Mheshimiwa Spika, ninapenda kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa fursa hii muhimu na kuniwezesha kuwasilisha Taarifa hii mbele ya Bunge lako Tukufu. Pia, ninawashukuru Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, (Mb), Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano), Ndugu Sazi Bundala Salula, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Ofisi ya Makamu wa Rais, kwa ushirikiano mkubwa walioutoa wakati Kamati ilipojadili Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano).

Mheshimiwa Spika, kipekee, ninawashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala, kwa kazi nzuri ya kujadili na kuchambua Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano), kwa Mwaka wa Fedha wa 2010/2011. Uzoefu wao wa muda mrefu katika masuala mbalimbali kuhusu Sekta za Sheria, Utawala, Haki za Binadamu na Utawala Bora, umesaidia kufanikisha kazi hii kwa ufanisi. Kwa heshima kubwa, ninaomba kuwatambua kwa majina kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Pindi H. Chana - Mwenyekiti, Mheshimiwa Angellah J. Kairuki – Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Abbas Zuberi Mtemvu, Mheshimiwa John Paulo Lwanji, Mheshimiwa Nimrod Elirehema Mkono, Mheshimiwa Halima J. Mdee, Mheshimiwa Fakharia K. Shomar, Mheshimiwa Zahra A. Hamadi, Mheshimiwa Mussa H. Kombo, Mheshimiwa Felix Francis Mkosamali, Mheshimiwa Gosbert B. Blandes, Mheshimiwa Azza H. Hamad, Mheshimiwa Mustapha B. Akunaay, Mheshimiwa Jaddy S. Jaddy, Mheshimiwa Tundu A. M. Lissu, Mheshimiwa Deogratias A. Ntukamazina na Mheshimiwa Jason S. Rweikiza. Aidha, ninapenda kuwashukuru kwa dhati, Watumishi wa Ofisi ya Bunge, chini ya Uongozi wa Dkt. Thomas D. Kashililah, Katibu wa Bunge, kwa kuiwezesha na kuisaidia Kamati kutekeleza majukumu yake. Kipekee, ninawashukuru Ndugu Charles Mloka - Mkurugenzi wa Kamati za Bunge, Ndugu Peter

Magati na Ndugu Asia Minja, Makatibu wa Kamati hii, kwa kuratibu vyema kazi za Kamati na kuhakikisha kuwa, Taarifa hii inakamilika kwa wakati uliopangwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, sasa ninaomba Bunge lako Tukufu, likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano), kama yalivyowasilishwa na Mtoa Hoja.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. CHARLES J. TIZEBA (K.n.y. MWENYEKITI KAMATI YA ARDHI, MALIASILI NA MAZINGIRA):** Mheshimiwa Spika, ninayo heshima kubwa, kuchukua fursa hii, kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge, Kanuni ya 99(7) na Kanuni ya 114(11), Toleo la Mwaka 2007, kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu, maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira, kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira), kwa Mwaka wa Fedha wa 2010/2011 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha wa 2011/2012 kwa Fungu 31 na kuliomba Bunge lako Tukufu liipokee na kujadili Taarifa hii na hatimaye kuidhinisha maombi ya fedha kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja.

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kumpa pole Mwenyekiti wangu, Mheshimiwa James D. Lembeli, Mbunge wa Kahama, kwa kufiwa na dada yetu mpendwa, Rose D. Lembeli, mapema wiki hii. Mungu, amuweke mahali pema peponi. *Amin.*

Mheshimiwa Spika, moja kati ya majukumu ya Kamati hii ni Kupitia na Kuchambua Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira), pamoja na kuisimamia na kuishauri kuhusu utekelezaji wa majukumu yake. Katika kutekeleza jukumu hili, tarehe 3 Juni, 2011, Kamati ilikutana Jijini Dar es Salaam na kupokea Taarifa ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira) kuhusu Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha wa 2010/2011 na kuchambua Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha wa 2011/2012.

Mheshimiwa Spika, wakati wa kuchambua Bajeti hiyo, Kamati ilipata fursa ya kujadili mambo yafuatayo:-

Utekelezaji wa malengo ya Ofisi kwa Mwaka 2010/2011 na malengo yanayoombewa fedha kwa Mwaka 2011/2012; muhtasari wa mgawanyo wa Fedha za Matumizi ya Kawaida kwa Idara na Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira *(NEMC)*, kwa Mwaka 2010/2011 na 2011/2012; Utekelezaji wa maagizo ya Kamati yaliyotolewa wakati wa kujadili Bajeti ya Mwaka 2010/2011; na changamoto zilizojitokeza wakati wa utekelezaji wa majukumu kwa Mwaka 2010/2011.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa maagizo ya Kamati yaliyotolewa wakati wa majadiliano ya bajeti kwa mwaka 2010/2011, wakati wa kupitia na kuchambua Taarifa ya Utekelezaji wa Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira), kwa Mwaka 2009/2010 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka 2010/2011, Kamati ilitoa ushauri kuhusu

maeneo mbalimbali kwa Ofisi na Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira *(NEMC)*, ikiwa ni pamoja na:-

- Serikali itenge fedha za kutosha katika Bajeti ya 2011/2012 ili kuwezesha ukamilishwaji wa baadhi ya Kanuni za Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya Mwaka 2004;

- Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira *(NEMC)*, lifanye kazi kwa karibu na Watendaji wa Serikali za Mitaa ili kuboresha utunzaji wa mazingira nchini;

- Serikali iongeze idadi ya Watumishi wenye elimu ya usimamizi wa mazingira katika Halmashauri za Miji na Wilaya ili kukabiliana na changamoto za uharibifu wa ardhi, upungufu wa misitu na miti, uchafuzi wa mazingira kama ilivyoanishwa katika Sera ya Taifa ya Mazingira ya Mwaka 1997;

- Serikali iendelee kutoa elimu kwa umma kuhusiana na mabadiliko ya tabianchi ili kujikinga na majanga mbalimbali ikiwa ni pamoja na ukame, mafuriko na maporomoko ya ardhi;

- Mradi wa Kusimamia Hifadhi ya Mabonde ijumuishe mabonde mengine tofauti na ilivyokuwa, ambapo Mradi wa Kuhifadhi Mazingira ulihusisha Bonde la Ziwa Tanganyika na Nyasa tu;

- Serikali iongeze juhudi katika kutoa elimu ya mazingira kuhusu usimamizi shirikishi wa misitu ili kusaidia kutunza mazingira na Wananchi kufaidika na mazao yatokanayo na misitu; na

- Serikali iiongezee Bajeti Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira) ili shughuli za usimamizi na utunzaji wa mazingira ziweze kutekelezwa kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, ninapenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, Serikali imejitahidi kutekeleza na kuzingatia ushauri wa Kamati isipokuwa bado Serikali imeendelea kutoa fedha kidogo ambazo hazitoshelezi mahitaji halisi ya utekelezaji wa shughuli za uhifadhi na usimamizi wa mazingira nchini. Vilevile Kamati haikuridhishwa na jinsi Serikali ilivyotekeleza ushauri wa Kamati kuhusu kuongezwa kwa juhudi zaidi katika kutoa elimu ya mazingira na usimamizi shirikishi wa misitu, hatua ambayo kama ingetekelezwa, ingesaidia Wananchi kutunza mazingira na kufaidika na mazao yatokanayo na misitu. Kamati inaendelea kuisihi Serikali kuzingatia na kuyafanyia kazi maoni yanayotolewa na Kamati ili kuweza kutunza na kuhifadhi mazingira kwa faida ya vizazi vya sasa na vijavyo.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha wa 2010/2011, Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira), ilikadiria kukusanya jumla ya Shilingi 4,100,000 kama Mapato ya Serikali. Hadi kufikia 30 Aprili, 2011, Ofisi ilikuwa imekusanya jumla ya Shilingi 6,542,500, ambazo sehemu kubwa ya fedha hizo zilitokana na mauzo ya nyaraka za

zabuni mbalimbali, ikiwa ni ongezeko la asilimia 60 ya makisio kwa Mwaka wa Fedha wa 2010/2011.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha wa 2010/2011, Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira), iliidhinishiwa Shilingi 41,542,429,000 kwa ajili ya matumizi ya kawaida; kati ya fedha hizo shilingi 1,010,532,533 kwa ajili ya mishahara na shilingi 37,992,652,002 kwa ajili ya matumizi mengineyo. Aidha, kiasi hicho kinajumuisha shilingi 33, 885,999,999 mgao wa fedha za Bajeti kwa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, sawa na asilimia 101 ya makadirio ya shilingi 33,488,173,000 kwa Mwaka wa Fedha wa 2010/2011. Vilevile kiasi hicho kinajumuisha fedha za ruzuku za *NEMC* shilingi 2,142,525,932. Hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2011, Ofisi ilikuwa imepokea jumla ya shilingi 39,003,184,536 kwa ajili matumizi ya kawaida, sawa na asilimia 94 ya bajeti iliyoidhinishwa na Bunge ya shilingi 41,542,429,000.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha wa 2010/2011, ziliidhinishwa jumla ya Shilingi 23,335,154,000 kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli mbalimbali za Maendeleo; kati ya fedha hizo shilingi 6,067,014,000 zilikuwa ni fedha za ndani na Shilingi 23,335,154,000 zilikuwa ni fedha za nje. Hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2011, jumla ya Shilingi 2, 664,259,584 zilipokelewa, kati ya fedha hizo, Shilingi 2,182,259,584 zilikuwa ni fedha za ndani na Shilingi 482,000,000 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Spika, yafuatayo ni mafanikio na changamoto zilizojitokeza wakati wa utekelezaji wa majukumu ya Mwaka wa Fedha wa 2010/2011:-

Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira), imefanikiwa kutekeleza majukumu mengi ikiwa ni pamoja na haya yafuatayo: Kuendelea kufanya ukaguzi ili kuimarisha shughuli za Uzingatiaji na Usimamizi wa Sheria ya Mazingira katika Viwanda mbalimbali nchini; Kuratibu zoezi la kukusanya; kusafisha na kuteketeza mlundikano wa viuatilifu chakavu nchini na kuweka mikakati ya udhibiti ili kuhakikisha kuwa zoezi hilo halidhuru mazingira na watu na kuwa mlundikano wa viuatilifu haujirudii; kuendelea kusajili Wataalam wa Mazingira; kuendelea kutoa elimu ya hifadhi na usimamizi wa mazingira kwa wadau na jamii; kuendelea kufanya Tathmini ya Athari ya Mazingira (TAM) katika Miradi mbalimbali ya Wawekezaji kabla ya Miradi hiyo kusajiliwa; kuendelea kujenga uwezo kwa wataalam na wadau kuhusu Tathmini ya Athari ya Mazingira (TAM); na kuendelea kuratibu shughuli za Mradi wa Hifadhi ya Mazingira ya Bonde la Kihansi.

Mheshimiwa Spika, changamoto pamoja na mafanikio hayo yaliyopatikana, Kamati imebaini ufinyu wa Bajeti ulikwamisha Ofisi kushindwa kutekeleza majukumu yake. Baadhi ya kazi za msingi zilizoshindwa kutekelezwa kutokana na bajeti isiyokidhi mahitaji ni pamoja na:-

Ofisi kushindwa kufanya Uperembaji wa Mkakati wa Hifadhi ya Mazingira ya Ardhi na Vyanzo vya Maji; Ofisi imeshindwa kufuatilia utekelezaji wa Mkakati wa Hifadhi ya Mazingira ya Bahari, Ukanda wa Pwani, Maziwa, Mito na Mabwawa; Ofisi imeshindwa kuandaa Taarifa ya Pili ya Hali ya Mazingira nchini; Ofisi imeshindwa

kufanya mapitio ya Sera ya Taifa ya Mazingira ya Mwaka 1997; na Ofisi imeshindwa kuandaa Kanuni tatu za Hifadhi ya Mazingira.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira), kwa kujiwekea mikakati mbalimbali ya kukabiliana na changamoto hizo; kwa mfano; Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira *(NEMC)*, kwa Mwaka 2011/2012, litaanza utekelezaji wa Mpango wa Tozo *(Charging Scheme).* Pesa zitakazopatikana kutokana na tozo hizo, zitasaidia kutekeleza baadhi ya shughuli ambazo hazikutekelezwa katika Mwaka wa Fedha wa 2010/2011.

Mheshimiwa Spika, katika kuandaa Bajeti ya Mwaka 2011/2012, Kamati imeona kuwa, Ofisi ilizingatia Mwongozo wa Taifa wa Uandaaji wa Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha wa 2011/2012, Mpango Mkakati wa Ofisi wa Mwaka 2010/11-2014/15 *(Medium Term Strategic Plan)*, maelekezo na malengo ya Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania (MKUKUTA II), Dira ya Taifa ya Maendeleo – 2025 na changamoto zilizojitokeza wakati wa utekelezaji wa Bajeti ya Mwaka wa Fedha wa 2010/2011.

Mheshimiwa Spika, fedha zilizotengwa zimegawanywa kulingana na vipaumbele vya majukumu ya Ofisi na Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira *(NEMC).* Hivyo basi, fedha kiasi cha shilingi 52,822,422,000 katika Mwaka wa Fedha wa 2011/2012 zinaombwa kwa ajili kutekeleza shughuli za msingi zifuatazo:-

- Kutekeleza Ajenda ya Taifa ya Utafiti katika Mazingira *(National Enviromental Research Agenda - NERA)* na kuwajengea uwezo Maafisa Mazingira katika ngazi za Mikoa na Wilaya ili waweze kutekeleza Ajenda ya Taifa kuhusu utafiti katika mazingira.

- Kuratibu shughuli za Mradi wa Hifadhi ya Mazingira ya Bonde la Kihansi.

- Kuwezesha Wizara na Taasisi za Serikali kukusanya takwimu juu ya umaskini na mazingira.

- Kuwajengea uwezo Maafisa Mazingira wa Wilaya pamoja na Kamati za Mazingira za Wilaya ili waweze kujua na kutimiza wajibu wao kwa mujibu wa Sheria ya Mazingira.

- Kutafsiri katika Kiswahili Kanuni sita za Sheria ya Mazingira zinazohusu Tathmini ya Mazingira Kimkakati; Ada na Tozo; Kemikali zinazomong‘onyoa Tabaka la Ozoni *(Ozone Depleting Substance- ODS);* Taka za Sumu; Taka Ngumu; na Usimamizi wa Baiotekinolojia ya Kisasa.

- Kuratibu na kuwezesha utekelezaji wa Mwongozo wa Kitaifa wa Utafiti wa Mazingira *(National Enviromental Research Agenda- NERA).*

- Kuimarisha uwezo wa Serikali kuratibu shughuli za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi nchini.

- Kuimarisha uwezo wa Serikali wa kusimamia fedha za Miradi ya kuhimili mabadiliko ya tabianchi.

- Kuandaa na kuratibu utekelezaji wa mkakati wa upashanaji habari juu ya mabadiliko ya tabianchi.

Mheshimiwa Spika, kama ilivyoelezwa kwenye Hotuba ya Mheshimiwa Waziri muda mfupi uliopita, katika Mwaka wa Fedha wa 2011/2012, Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira), inakadiriwa kuwa na matumizi ya shilingi 52,822,422,000; ambapo shilingi 40,412,043,000 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi 12,410,379,000 ni kwa ajili ya maendeleo. Kati ya hizo; shilingi 6,067,014,000 ni fedha za ndani na shilingi 6,343,365,000 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu ilipitia na kujadili kwa kina Makadirio ya Bajeti ya Ofisi hii na kupitia Kifungu kwa Kifungu na kuridhika nayo na sasa ninaliomba Bunge lako Tukufu likubali kujadili na kupitisha maombi hayo, yenye jumla ya shilingi 52,822,422,000 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha wa 2011/2012.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuujadili Mpango na Bajeti hiyo kwa kina, Kamati inatoa maoni na ushauri ufuatao:-

Kamati inaishauri kuwa, ni vyema Serikali ikaachana na dhana ya kutegemea ufadhili kwa Bajeti ya Maendeleo kwani uzoefu umeonesha, fedha nyingi zinazoahidiwa na wafadhili huwa hazitolewi kwa wakati mwafaka na wakati mwingine kutototolewa kabisa au kutolewa kinyume na walivyoahidi na hivyo, kusababisha kushindwa kutekeleza Miradi iliyokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, ni ukweli pia usiopingika kwamba, Serikali yoyote yenye nia ya kuwaletea maendeleo ya kweli Wananchi wake, inapunguza gharama za matumizi ya kawaida na kuweka fedha nyingi kwenye Miradi ya Maendeleo. Hivyo basi, Kamati inatoa ushauri kwa Serikali kuhakikisha kwamba, katika mwaka ujao wa fedha wakati wa upangaji wa bajeti, ipunguze fedha nyingi zinazotumika kwa matumizi ya kawaida na kuipangia Miradi ya Maendeleo fedha za kutosha. Mwaka huu, Ofisi ya Makamu wa Rais Mazingira, imetenga kiasi cha asilimia 33.3 tu kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Kamati inasikitishwa na kupungua kwa bajeti ya ofisi hii, kwani kwa Mwaka wa Fedha wa 2010/2011, ilipangiwa kiasi cha shilingi bilioni 64,877,583,000, pamoja na kushuka kwa thamani ya shilingi yetu na kupanda kwa gharama za maisha.

Bajeti ya Ofisi hii kwa mwaka huu ni shilingi 52,822,422,000, ambayo ni pungufu kwa asilimia 1.2 ya Bajeti ya mwaka uliopita, ingawa Bajeti ya Serikali wakati huo huo imepanda kwa wastani wa asilimia 15.

Upungufu huu unadhihirisha kuwa, ufanisi wa utekelezaji wa majukumu ya ofisi utashuka. Aidha; ni muhimu ikumbukwe kwamba, kiasi hicho kinajumuisha shilingi 30,423,054,500, gawio la asilimia 4.5 ya misaada ya kibajeti ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, suala la mazingira ni mtambuka Kamati inaishauri Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira), iweke utaratibu wa kukutana na Wizara zote mara kwa mara ili kutoa ufafanuzi wa Sera ya Taifa ya Mazingira na namna ambavyo Wizara husika zinaweza kutekeleza Sera hiyo na kupata maelezo ya namna kila Wizara inavyojizatiti katika kuitekeleza hasa namna ambayo imejiandaa kukabiliana na tatizo la mabadiliko ya tabianchi *(Climate Change).*

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Mazingira Namba 20 ya Mwaka 2004, kifungu cha 33, ambacho kinaelekeza kuteuliwa kwa Mratibu katika Wizara za Kisekta, ambaye atateuliwa kutoka miongoni mwa Watumishi wa Wizara husika na ambaye atakuwa mwenye sifa na ujuzi wa kutosha katika masuala ya mazingira.

Mheshimiwa Spika, Kamati imelitafakari jambo hili na inashauri kwamba Afisa Mazingira asiteuliwe miongoni mwa Watendaji wa Wizara bali ateuliwe moja kwa moja na Baraza la Taifa na Usimamizi wa Mazingira na wawajibike moja kwa moja kwa Mkurugenzi Mkuu wa Baraza. Hatua hii itaongeza ufanisi katika kuhakikisha masharti yote ya usimamizi wa mazingira yaliyomo katika sheria zinazosimamiwa na Wizara yanatekelezwa na kuwasilisha taarifa za utekelezaji kwa Mkurugenzi wa Mazingira na Mkurugenzi Mkuu wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira.

Mheshimiwa Spika, kuna taarifa za kugunduliwa kwa madini ya *uranium* katika maeneo mbalimbali nchini na kwamba uchimbaji wa madini hayo huenda ukaanza hivi karibuni. Kwa kuwa madini haya yanahitaji uangalifu mkubwa, usalama wake usipozingatiwa athari zake ni kubwa sana kwa afya za watu, viumbe wengine na mazingira. Kutokana na unyeti wa suala hili, Kamati inashauri kwamba Serikali na Baraza la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira lifanye tathmini ya athari ya mazingira *(environmental impact assessment)* mapema iwezekanavyo bila ushawishi wa wawekezaji ili kubaini madhara ya uharibifu wa mazingira yanayoweza kutokea na kuishauri Serikali hatua muafaka kabla ya kuanza kutekelezwa kwa zoezi hilo.

Kwa mfano, katika tukio la uchafuzi wa mazingira katika mgodi wa *North Mara*, Serikali ingekuwa imechukua jukumu lake la kutathmini hali ya uchafuzi wa mazingira mara kwa mara, madhara yaliyotokea yangeweza kudhibitiwa mapema. Kamati inazidi kusisitiza kwamba maji kutoka Bwawa la Gokona, yasimwagwe kwenye mazingira au kutumika hadi mtambo wa kuyasafisha utakapokuwa umekamilika na idhini kutolewa kwa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira. Kamati pia imeishauri Serikali kwamba ihakikishe fidia zote stahiki zinalipwa kwa wananchi na ahadi zilizotolewa na wenye mgodi kwa jamii wa eneo lile, zote zitekelezwe.

Mheshimiwa Spika, mwisho, napenda kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii ya kuwasilisha taarifa ya Kamati yangu. Aidha, nawashukuru pia Mheshimiwa

Dkt. Terezya Luoga Huvisa -Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira; Ndugu Sayazi Sarura - Katibu Mkuu, Ofisi ya Makamu wa Rais pamoja na wataalam wote wa Ofisi hii na Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira kwa ushirikiano wao, ushauri na utaalam ambao umeiwezesha Kamati kutekeleza makujumu yake ni kuwasilisha taarifa hii leo katika Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, naomba pia niwashukuru Wajumbe wenzangu wa Kamati kwa busara zao hasa kwa kutekeleza kazi za Kamati hii kwa umahiri mkubwa. Ushirikiano wao na kujituma bila kuchoka kwa kupitia na kuchambua mpango wa makadirio ya bajeti inayoombwa na hivyo kufanikisha taarifa hii ambayo kwa niaba yao naiwasilisha katika Bunge lako Tukufu. Naomba niwatambue kwa kuwataja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa James Daudi Lembeli - Mwenyekiti wa Kamati, Mheshimiwa Abdulkarim Hassan Shah - Makamu Mwenyekiti anayetupenda sana. Wajumbe wengine ni Mheshimiwa Zakia Hamdani Meghji, Mheshimiwa Saleh Ahmed Pamba, Mheshimiwa Philemon Kiwelu Ndesamburo, Mheshimiwa Kheri Khatib Ameir, Mheshimiwa Mariam Salum Mfaki, Mheshimiwa Ali Khamis Seif, Mheshimiwa Susan Anslem Lyimo, Mheshimiwa Jaku Hashim Ayoub, Mheshimiwa Mariam Kasembe, Mheshimiwa Sylvestry Koka, Mheshimiwa Josephat Kandege, Mheshimiwa Magdalena Sakaya, Mheshimiwa Benardetha Mushashu, Mheshimiwa Amina Clement, Mheshimiwa Michael Laizer, Mheshimiwa Kaika Saning’o Telele, Mheshimiwa Dkt. Mary Mwanjelwa, Mheshimiwa Lediana Mafuru Mng’ong’o, Mheshimiwa Meshack Opulukwa, Mheshimiwa Mch. Peter Simon Msigwa, Mheshimiwa Mwanakhamis Kassim Said, Mheshimiwa Eng. Hamad Yussuf Masauni, Mheshimiwa Al-Shaymaa Kwegyir, Mheshimiwa Elizabeth Nkunda Batenga, Mheshimiwa Abdalla Haji Ali na mimi mwasilishaji Mheshimiwa Charles Tizeba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii pia kumshukuru Katibu wa Bunge - Dkt. Kashililah, Katibu wa Kamati - Rachel Nyega kwa kuihudumia Kamati ipasavyo na kufanikisha maandalizi ya taarifa hii kwa wakati. Aidha, nawashukuru Watendaji wote wa Ofisi ya Bunge kwa ushirikiano wao mzuri wa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kwa ukamilifu. Napenda pia nitumie nafasi hii kuishukuru familia yangu, wananchi wote wa Jimbo la Buchosa kwa ushirikiano wao mzuri na ni matumaini yangu kwamba tutachapa kazi ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Kamati ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Sasa namwita Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kuhusu Makadirio ya Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira kwa pamoja - Mheshimiwa Pauline Gekul, una dakika 30. *(Makofi)*

**MHE. PAULINE P. GEKUL - MSEMAJI WA KAMBI YA UPINZANI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):** Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii kuwasilisha maoni na mapendekezo ya Kambi ya Upinzani

kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais - Muungano na Mazingira kwa mwaka wa fedha 2011/2012, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, Kanuni ya 99(7) Toleo la mwaka 2007.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, namshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema na upendo, kwa kunijalia uhai na afya njema hata kuweza kusimama hapa kutimiza wajibu huu wa kuwawakilisha wananchi kwa nafasi yangu ya Waziri Kivuli Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano).

Mheshimiwa Spika, pia nakushukuru kwa dhati wewe kwa kunipa wasaa huu kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani ili kufanikisha lengo letu la kukomaza demokrasia ya kweli katika nchi hii na kuchochea maendeleo ya haraka kwa Watanzania wote.

Mheshimiwa Spika, kwa heshima na taadhima kubwa, naushukuru uongozi wetu wote wa Kambi Rasmi ya Upinzani chini ya Mheshimiwa Freeman Aikael Mbowe na Naibu wake Mheshimiwa Kabwe Zuberi Zitto, pamoja na Wabunge wenzangu wote kwa imani yao kwangu na kwa ushirikiano mkubwa wanaonipa katika kutekeleza wajibu wangu wa kibunge na huu wa Uwaziri Kivuli wa Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano). *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho lakini kwa umuhimu mkubwa, shukrani zangu za dhati nazielekeza kwa mume wangu mpendwa Slaa na watoto wetu wapendwa Irene na Inosensia ambao wamenivumilia sana kwa kipindi chote ambacho nimekuwa katika misukosuko ya siasa katika Jimbo la Babati Mkoa wa Manyara na Taifa kwa ujumla.

**SPIKA:** Wanauliza, Slaa nani?

**MHE. PAULINE P. GEKUL - MSEMAJI WA KAMBI YA UPINZANI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):** Mheshimiwa Spika, ni Saltary Slaa. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, mwaka huu utakuwa ni mwaka wa 47 wa Muungano wa Tanganyika na Zanzibar, uliozaa Jamhuri ya Muungano ya Tanzania. Kumekuwa na ukweli ambao miaka yote watawala wamekuwa wakificha ni kwa nini hasa Tanganyika na Zanzibar ziliungana? Je, nchi hizi ziliungana kwa matakwa ya wananchi au yalikuwa ni matakwa ya viongozi wa pande zote mbili?

Mheshimiwa Spika, ukweli wa kwanini tuliungana ulitokana na uwoga wa mataifa ya magharibi juu ya Zanzibar kuwa *CUBA* ya ukanda wa Afrika ya Mashariki, kutokana na ukweli kwamba baada ya Mapinduzi ya Zanzibar mwaka 1964 nchi ya Ujerumani Mashariki ilifungua Ubalozi wake Zanzibar, pamoja na ushirika wa karibu wa Urusi na Uchina wakati huo. Pia kitendo cha majeshi yote ya nchi za Afrika ya Mashariki kuasi wiki tatu tu baada ya mapinduzi ya Zanzibar na kuzimwa kwa msaada wa Jeshi la Maji la Uingereza, nalo likawa ni kigezo cha Muungano.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Karume naye alikuwa na wasiwasi mkubwa na nafasi yake kutoka kwa vijana wasomi waliokuwa viongozi wa Chama cha Umma waliokuwa wakiongozwa na Marehemu Abdulhamani Babu na Kassim Hanga kuwa wangeweza kumpindua kutokana na msimamo wao, jambo lililosababisha kuingia makubaliano na Rais wa Tanganyika peke yao bila kulihusisha Baraza la Mapinduzi.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inasema Muungano huu wenye utata uliingiwa kwa maslahi binafsi ya watawala kwa kushawishiwa na mataifa ya magharibi yaliyokuwa yakihofia sana siasa za mlengo wa kushoto kujikita katika ukanda wa Afrika ya Mashariki.

Mheshimiwa Spika, hata Jamhuri ya Muungano wa Tanzania yenyewe nayo ilizaliwa katika mazingira yaliyogubikwa na utatanishi wa kisheria uliosababishwa na matumizi ya hati ya dharura. Kwani ni ukweli wa kihistoria kwamba *Sheria ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar ya mwaka 1964 (The Union of Tanganyika and Zanzibar Act, 1964)* – iliyotilia nguvu ya kisheria, makubaliano ya Muungano kati ya Jamhuri ya Tanganyika na Jamhuri ya Watu wa Zanzibar ilipitishwa kwa hati ya dharura siku ya Jumamosi ya tarehe 25 Aprili, 1964, ikasainiwa na Rais Nyerere siku hiyo hiyo na kuanza kutumika kesho yake tarehe 26 Aprili, 1964.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ya uharaka huo, Rais wa Zanzibar, Sheikh Abeid Amani Karume, ambaye chini ya Sheria ya Mamlaka ya Kutunga Sheria *(The Legislative Powers Law)* ya tarehe 31 Januari, 1964 ndiye alikuwa na mamlaka ya kutunga sheria za Zanzibar kwa kushauriana na Baraza la Mapinduzi la Zanzibar, hakupata ushauri wowote wa kisheria juu ya makubaliano ya Muungano na kwa hiyo, hakuwahi kutunga sheria ya kuyaridhia makubaliano ya Muungano kama ilivyokuwa inatakiwa chini ya Hati ya Makubaliano ya Muungano. Aidha, kuna ushahidi - kama anavyosema Profesa Issa Shivji katika kitabu chake *Pan-Africanism or Pragmatism? Lessons of the Tanganyika – Zanzibar Union* kwamba wanasheria wa Kiingereza waliokuwa wanamshauri Mwalimu Nyerere ndio waliotunga *Sheria ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar ya mwaka 1964* kwa upande wa Zanzibar na kuichapisha kwenye *Gazeti la Serikali ya Muungano* la tarehe 1 Mei, 1964 chini ya saini ya Muingereza P.R. Ninnes Fifoot aliyekuwa Kaimu Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya Tanganyika wakati huo.

Mheshimiwa Spika, misingi hii legelege ya kisheria, ndiyo imefanya uhalali wa kisheria na kisiasa wa Muungano kuendelea kuhojiwa hata baada ya miaka zaidi ya arobaini tangu kuzaliwa kwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Haiyumkiniki kwamba kama Muungano usingeharakishwa na wananchi na/au vyombo vya uwakilishi vya pande zote mbili wakashirikishwa kikamilifu katika hatua mbalimbali za kuunda Muungano, kelele nyingi ambazo zimesikika tangu miaka ya mwanzo ya themanini kuhusu uhalali wa Muungano zisingekuwa na nguvu.

Mheshimiwa Spika, siyo sheria iliyozaa Jamhuri ya Muungano peke yake iliyopitishwa kimizengwe kwa kutumia hati ya dharura. Katiba yetu ya Nne, yaani Katiba ya Muda ya mwaka 1965 (*The Interim Constitution, 1965*) ambayo iliingiza rasmi mfumo wa chama kimoja na kupiga marufuku vyama vya siasa vya upinzani, iliingizwa na

kupitishwa Bungeni kwa hati ya dharura. Aidha, mabadiliko ya kwanza ya Katiba hiyo yaliyoletwa na Sheria ya mabadiliko ya Katiba ya muda ya mwaka 1965 ambayo iliingiza masuala ya fedha katika orodha ya Mambo ya Muungano, nayo yaliletwa Bungeni kwa siri chini ya hati ya dharura.

Mheshimiwa Spika, ushahidi wa jambo hili uko katika Taarifa Rasmi ya Majadiliano ya Bunge *(Hansard)* ya Mkutano wa Kumi na Saba wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya tarehe 10 Juni, 1965 ambapo aliyekuwa Makamu wa Pili wa Rais anaripotiwa kusema yafuatayo wakati alipowasilisha Muswada wa Sheria hiyo Bungeni: *"Serikali inayo Miswada miwili ya Sheria ambayo ni ya muhimu sana na ambayo Serikali ingependa ipitishwe leo, ili Sheria hizi zianze kutumika kesho. Lakini ningependa kueleza kwamba, hatukupenda kuiweka shughuli hii katika Order Paper kwa sababu Order Paper ya kila siku hutolewa kila siku asubuhi, na mambo yaliyomo katika Miswada hii ni mambo ya siri, kwa hiyo, kama Miswada hii ingeliwekwa katika Order Paper toka asubuhi, siri ingekuwa imetoka mapema mno kabla ya wakati wake. Ndiyo maana ikazuiliwa mpaka sasa hivi." (*uk. 214 - 216). Taarifa Rasmi inaonyesha kwamba Mheshimiwa Kapilima ndiye Mbunge pekee aliyechangia katika mjadala wa Mabadiliko hayo ya Katiba.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Muungano ulipitishwa kiujanja ujanja tu, baada ya mwaka 1964 mgogoro wa kuhusiana na masuala ya fedha ulianza pale Zanzibar walipotaka kuwa na masuala yao peke yao ya fedha bila kutegemea Tanzania, kwani katika hati za Muungano masuala ya fedha hayakuwa kwenye mambo ya Muungano.

Mheshimiwa Spika, jambo kuu la kulitafakari ni dhamira ya kuundwa kwa Muungano wenyewe na kuhusisha na dhamira za sasa za kuendeleza Muungano wetu. Hili ni suala la msingi katika kuamua mwelekeo wa Muungano wetu ikiwemo utatuzi wa kero zilizopo. Mjadala huu ni muhimu sana kwa kipindi cha sasa na hasa wakati huu ambao kizazi kipya cha Watanzania waliozaliwa baada ya Muungano wakiwa wanatafakari kutaka mabadiliko katika mfumo na muundo wa Muungano, kwa kuwa ni vyema kutafakari kama matakwa haya ya sasa nayo ni dhamira ya ndani au ni msukumo kutoka nje.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 6(a) ya Hati/Mkataba wa Muungano inaitaja Serikali ya Tanganyika, hata kifungu cha (8) cha sheria ya Muungano namba 22 ya mwaka 1964, lakini ukiangalia katika hali halisi ya kiutendaji, Serikali ya Tanganyika haionekani popote kama ilivyo kwa Serikali ya Zanzibar. Hapa ndipo panapoibua hoja nyingi zinazozua mgogoro kuhusu Muungano kama ambavyo ilitokea kwa Rais Jumbe mwaka 1984 na hatimaye kushinikizwa na *NEC* ya Chama kujiuzulu.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla, masuala ya Muungano yamegubikwa na usiri. Mathalan nakala halisi ya Muungano ambayo ndiyo inapaswa kuwa mwongozo/msingi imekuwa kitendawili. Huko nyuma iliwahi kusemwa Bungeni kuwa nakala hiyo ipo. Lakini haijulikani kuwa ni nani mwenye mamlaka ya kuweza kuiona nakala hiyo halisi kwani hata Bunge ambalo ni chombo cha wananchi hawajaletewa kuiona nakala hiyo.

Mheshimiwa Spika, kwa upande mwingine, Katiba na Sheria zetu zinakataza wananchi kuvunja Muungano. Hii ikitafakariwa kwa kina, inamaanisha hata kubadili mfumo wa Muungano ulioko na kadhalika. Mathalan, Katiba inawataka viongozi wa kitaifa kula kiapo cha kuulinda Muungano kabla ya kuanza kazi yao, aidha, Sheria ya Vyama vya Siasa inakiondolea sifa ya kusajiliwa chama chochote cha siasa ambacho katiba yake au sera zake ni za kutaka kuvunja Muungano.

Mheshimiwa Spika, katika hali hii, ili kulinda Muungano ni lazima hatua za haraka zikuchuliwe na ama kuhakikisha siri za Muungano zinafichuliwa na Katiba inabadilishwa ili kulinda Muungano. Ukichambua kwa kina, utaona upungufu mkubwa wa Muungano unaotokana na matatizo ya kimaumbile ya toka wakati wa kuundwa kwa Muungano. Hivyo, suluhisho la kudumu ni kuusuka upya Muungano kupitia Katiba mpya. Hii iende sanjari na kuweka misingi madhubuti ya wazi na yenye kutoa majibu.

Mheshimiwa Spika, ili kutoa msukumo mpya wa hatua kuchukuliwa, leo Kambi Rasmi ya Upinzani, tunachukua fursa hii kunukuu mambo machache ambayo yamekuwa yakilalamikiwa sana katika Muungano huu, kubwa likiwa ni kukiukwa au kudharauliwa kwa hati asili ya Muungano wetu *(Articles of the Union 1964)* ambayo ndiyo iliyoasisi Muungano huu.

Mheshimiwa Spika, Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 pamoja na mabadiliko yake mbalimbali haikuzingatia hati ya asili ya Muungano, hivyo kusababisha kuibuka kwa kero za mara kwa mara. Aidha, Serikali zote mbili kwa vipindi mbalimbali zimekwishaunda Tume na Kamati mbalimbali kuchambua na kutafuta muafaka wa kasoro za Muungano, lakini mapendekezo hayo siku zote yamekuwa yakiishia kwenye makabati tu, na fedha za walipa kodi zikizidi kuteketea.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya kero hizo za Muungano, ni hizi zifuatazo:-

(i)Mambo ya Muungano yaliyoongezwa kutoka 11 hadi kufikia 22, kinyume kabisa na hati ya asili ya Muungano. Hali hii imeleta mkanganyiko na malalamiko mengi hususan katika suala la mafuta na gesi.

(ii) Kumezwa kwa Serikali ya Tanganyika katika Serikali ya Jamhuri ya Muungano pia kumesababisha kuibuka kwa malalamiko ya kila upande kuona upande mwingine unanufaika zaidi. Mfano, ni upande wa Zanzibar kuona haunufaiki vya kutosha na Muungano kama unavyonufaika upande wa Tanzania Bara.

(iii) Kumekuwepo utata juu ya mgawanyo wa mapato kati ya Zanzibar na Serikali ya Jamhuri ya Muungano, mathalan, kumekuwa na tatizo la kupata *formula* nzuri ya mgawanyo wa mapato ya Benki Kuu ya Tanzania ambayo Zanzibar ni mdau kwa mujibu wa Katiba.

(iv)Kumekuwa na malalamiko ya siku nyingi kwamba Serikali ya Jamhuri ya Muungano imekuwa ikiikandamiza Zanzibar kwa kuizuia kuingia mikataba ya kimataifa hata pale mikataba hiyo inapokuwa haihusu mambo ya Muungano.

(v) Ofisi ya Makamu wa Rais katika ibara ya 3 (b) ya hati ya asili ya Muungano ilikuwa chini ya Rais wa Zanzibar, lakini kutokana na mabadiliko ya 11 ya Katiba ya mwaka 1994, Rais wa Zanzibar amefanywa kuwa mjumbe wa kawaida wa Baraza la Mawaziri.

Mheshimiwa Spika, wachambuzi wa masuala ya kisheria wamebainisha kuwa mabadiliko ya Katiba ya Zanzibar ya mwaka 2010 yaliyoasisi Serikali ya Umoja wa Kitaifa *(Government of National Unity)* hayajaoana vyema na Katiba ya sasa ya Jamhuri ya Muungano, hivyo kuibua haja ya msingi ya Katiba hiyo ya Zanzibar pamoja na Katiba mpya ya Jamhuri itakayoandikwa kupatanishwa, yaani kuwa *harmonized*.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani haiwezi kubeza mafanikio ya amani iliyopatikana Zanzibar baada ya marekebisho ya kumi ya Katiba ya Zanzibar. Kambi ya Upinzani inaheshimu na kuthamini maamuzi ya wananchi wa Zanzibar ya kuifanyia marekebisho Katiba ya Zanzibar, lakini tunasisitiza kuwa ipo haja kwa marekebisho hayo kupatanishwa na Katiba ya Jamhuri ya Muungano kupitia mchakato wa kuandikwa kwa Katiba mpya ya Jamhuri, kwani maeneo kadhaa ya Katiba hizi mbili hayapatani kama ifuatavyo:-

(a) Wakati Katiba ya sasa ya Jamhuri ya Muungano ya mwaka 1977 Sura ya (4) Ibara ya 102 hadi 107 inaunda Ofisi ya Waziri Kiongozi wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, wadhifa huo tayari umeshaondolewa na marekebisho ya kumi ya Katiba ya Zanzibar ya mwaka 2010;

(b) Wakati Katiba ya sasa ya Jamhuri ya Muungano inaitaja Mahakama ya Rufaa kuwa ni sehemu ya Muungano, chini ya marekebisho ya kumi ya Katiba ya Zanzibar, Mahakama hii haina tena mamlaka ya kushughulikia shauri lolote kutoka Zanzibar;

(c) Mabadiliko ya Ibara ya (1) na ya (2) ya Katiba ya Zanzibar yanakwenda kinyume na Katiba ya Jamhuri ya Muungano ambayo inaitambua Zanzibar kama sehemu ya Muungano;

(d) Mabadiliko hayo pia yamepishana na Ibara ya 98(b) ya Katiba ya sasa ya Jamhuri, ambayo inatoa taratibu za marekebisho ya Katiba kwa mambo ambayo ni ya Muungano; na

(e) Mabadiliko hayo pia yameitangaza Zanzibar kuwa nchi, hivyo kuzidi kuweka haja ya kuandikwa haraka kwa Katiba mpya ya Jamhuri, kwani hii ya sasa inaitambua Zanzibar kama sehemu ya Jamhuri ya Muungano.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Serikali imeridhia na kukubali kuanza mchakato wa kupata Katiba mpya ya Jamhuri ya Muungano, Kambi ya Upinzani inaona kuwa sasa ni muda muafaka kuanza mara moja kushughulikia kero za Muungano ambazo zimepigiwa kelele kwa muda mrefu sana bila hatua zozote stahiki kuchukuliwa.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani tunatoa rai kwa Serikali kufanya mchakato huu kuwa shirikishi zaidi ili kuwapa fursa ya kutosha Watanzania wote kushiriki katika mchakato huu na kuzingatia kikamilifu matakwa ya pande zote mbili kuhusu muundo wa Muungano.

Mheshimiwa Spika, ili mchakato wa Katiba mpya uwe shirikishi zaidi, ni lazima wananchi watoe maoni yao kuhusu muundo wa sasa wa Muungano na wapendekeze aina ya Muungano ambao wanautaka. Katika hili, ni muhimu na ni lazima nafasi ya kutosha itolewe kwa ajili ya kujadili kero zote ambazo zimekuwa zikiibuliwa na pande zote mbili za Muungano na hatimaye tuweze kuwa na Muungano wenye afya badala ya sasa kuwa na Muungano uliojaa manung'uniko ya mara kwa mara na hii inatokana na wananchi kutokushirikishwa katika kuamua juu ya Muungano wao.

Mheshimiwa Spika, katika Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2011/2012 – 2015/2016) uliowasilishwa na Serikali hapa Bungeni, kulikuwa na mapungufu makubwa kwa sababu yapo mambo ambayo kimsingi ni ya Muungano kwa mujibu wa Katiba iliyopo, lakini hayakuingizwa au kuzingatia ni jinsi gani yatatekelezwa kwa upande wa Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, suala la gesi ni la Muungano kwa mujibu wa Katiba iliyopo na kwa kuzingatia hilo, nafasi ya Zanzibar haijazungumziwa katika Mpango huo jambo ambalo litatia shaka kama katika kutekeleza Mpango ule kwa upande wa matumizi ya gesi Zanzibar itaguswa kimaslahi na hata kwenye Mpango wenyewe gesi iliyozungumziwa ni iliyopo upande wa Bara.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani tunaitaka Serikali kuzingatia na kutambua kuwa pale ambapo maslahi ya Zanzibar yanaguswa katika mipango mbalimbali ya Serikali ni vizuri Serikali ikatambua uwepo wa Zanzibar na kueleza nafasi yake katika suala hilo.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali iwe na Mpango madhubuti kabisa wa kuimarisha Muungano na kuhakikisha kuwa kero zote za Muungano zinaondolewa katika muda mfupi na kuachana na utaratibu wa kimazingaombwe wa kuunda Tume kila mara kushughulikia mambo ambayo yanahatarisha Muungano wetu kwa kuwa bado mambo hayo yapo mpaka sasa.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani tunataka suala la mafuta liachwe mikononi mwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar hasa tukizingatia kuwa visiwa hivi vina raslimali ndogo sana za kiuchumi. Masuala ya raslimali nyingine yatajadiliwa ili kuhakikisha kuwa Zanzibar inanufaika na raslimali za Tanzania na vile vile inatoa mchango wake sahihi katika uchumi wa Taifa.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani pia inaitaka Serikali kuweka mikutano maalum kikatiba ya pamoja kati ya Baraza la Wawakilishi na Bunge la Jamhuri ya Muungano ili hatimaye kukaa chini kama ndugu wamoja na kujadili masuala yenye matatizo yanayohusu Muungano. Pia tunashauri kuwa pawepo na kikao cha Pamoja cha

Uongozi ngazi ya Taifa kutoka pande zote za Muungano na kiwe kinafanyika mara mbili kwa mwaka. Hii itasaidia katika kuendelea kujenga udugu wetu ambao umekuwepo kwa muda mrefu sasa.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inataka sasa pawepo na utaratibu wa kuingiza mambo katika orodha ya Muungano na uwe wazi na msingi wake uwe ni pande zote mbili kuridhia wakati wote kabla ya kuingiza au kupunguza kama mambo ya Muungano yanayopaswa kuzingatiwa.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali itekeleze kikamilifu hati ya Muungano ikiwemo kuanzisha Mahakama ya Muungano ya Katiba na hii itasaidia sana kuondoa malalamiko mbalimbali yanayotokana na aina ya Muungano wetu na wakati huo huo hakuna chombo cha kuweza kutatua malalamiko hayo.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inapendekeza kuwa katika mchakato wa Katiba mpya ambao utaanza, ni vizuri Serikali ikazingatia umuhimu wa kuwepo kwa Serikali tatu kwa maana ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Serikali ya Tanganyika. Hii italeta picha halisi ya aina ya Muungano tulionao ili kuufanya uwe endelevu na kuondoa dhana iliyokaa kwa muda mrefu sana ya kero za Muungano.

Mheshimiwa Spika, katika suala la mikataba ya kimataifa ambayo imewekwa kama mambo ya Muungano, Kambi ya Upinzani inatoa rai kwa Serikali kuiruhusu Zanzibar kuingia katika mikataba hiyo kwa mambo yale ambayo sio ya Muungano. Hili litatoa nafasi kwa sehemu hiyo ya Muungano kufanya yale wanayoona yanafaa bila kuathiri mambo ambayo ni ya Muungano. Kuhusu Ofisi za Wizara za Muungano zilizopo Zanzibar, Kambi Upinzani tunashauri kuwa pawepo na utaratibu mzuri wa kuhakikisha kuwa ofisi hizi zinafanya kazi na kuwa na ufanisi wa kutosha. Kwa mfano, jengo la Ofisi ya Bunge lililopo Zanzibar limekuwa mara zote halifanyi kazi muda mwingi na hata Wabunge wawapo Zanzibar wanashindwa kupata huduma katika ofisi hizi.

Mheshimiwa Spika, ni wakati muafaka sasa kwa Serikali na Bunge kufanya maamuzi na kuhakikisha kuwa Ofisi za Bunge Zanzibar zinakuwa zinatumika na hasa wakati Kamati za Bunge zinapokutana Dar es Salaam, ni vyema baadhi ya Kamati zikakutana Zanzibar. *(Makofi)*

Mheshimkiwa Spika, pamekuwepo na sheria mbalimbali ambazo zimekuwa zikitungwa hapa nchini tangu hata kabla ya uhuru na hata baada ya uhuru kama vile sheria za wanyamapori, madini, ardhi na maji zenye lengo la kuhifadhi na kutunza mazingira.

Mheshimiwa Spika, mnamo mwaka 1982 tulitunga Sheria ya Kisekta iliyohusiana na mazingira ila ilikuwa na mapungufu makubwa kwani sheria hii iliwapa mamlaka *NEMC* ya kuishauri Serikali pindi kunapotokea uchafuzi wa mazingira badala ya mamlaka ya kuweza kuchukua hatua ili kukabiliana na hali hiyo. Sheria hii pia haikuwa inawataka *NEMC* kufanya tathmini ya hali ya kimazingira *(Environmental Impact*

*Assesiment)* kabla ya kufanya maamuzi juu ya miradi mbalimbali kupewa kibali cha kuanza kufanya kazi.

Mheshimiwa Spika, sheria hizi zilikuwa haziwalazimishi wachafuzi wa mazingira kuwalipa fidia wananchi wanaoathirika kutokana na shughuli zao kuchafua mazingira, kulipia gharama za kuyarejesha mazingira waliyochafua/haribu katika hali yake ya kawaida na pia hazikuwa na kifungu cha kuchukua tahadhari ya uchafuzi wa mazingira kabla ya mradi kuweza kuanza.

Mheshimiwa Spika, mnamo mwaka 1998 ilipotungwa Sheria ya Madini pamona na kanuni zake, ndiyo kwa mara ya kwanza zikaweka vipengele vya udhibiti wa uchafuzi wa mazingira unaotokana na shughuli za migodi mbalimbali, kwani shughuli za uchimbaji wa madini ndiyo chanzo kikubwa cha uchafuzi wa mazingira ulimwenguni kutokana na ripoti mbalimbali.

Mheshimkiwa Spika, mnamo mwaka 2006 ilitungwa sheria ya misitu ambayo ilikuwa inalenga kudhibiti uchafuzi wa mazingira kwenye maeneo ya misitu mbalimbali hapa nchini mwetu.

Mheshimiwa Spika, mnamo mwaka 2004 ndipo yalifanyika mageuzi makubwa katika sheria zetu na hasa ilipotungwa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira *(Environmental Management Act)* ambayo ilisimamia na kudhibiti uchafuzi wa mazingira hapa nchini. Pamoja na mambo mengine, sheria hii ilitambua rasmi kuwa usafi wa mazingira ni moja ya haki za kimsingi za binadamu na Mahakama mbalimbali hapa nchini katika kuitafsiri sheria hii wametoa tafsiri kuwa mazingira ni moja ya haki za kuishi kwa binadamu.

Mheshimiwa Spika, sheria hii iliweka wazi kuwa miradi mbalimbali haiwezi kupitishwa bila kwanza kufanyiwa tathmini ya kimazingira *(Environmental Impact Assesment)* na kuweza kujua kama mradi huo utaharibu mazingira na kama unahatarisha mazingira, basi haupaswi kupitishwa.

Mheshimiwa Spika, Sheria hii ya Mazingira iliweka bayana kuwa kama mradi wowote utaonekana kuhatarisha mazingira hata kama mradi huo unaendelea na ushahidi wa kisayansi haujapatikana, ni heri mradi huo kusimamishwa kuendelea kuliko uachwe na hatimaye uje ulete madhara kwenye mazingira na hili lilizingatia kanuni ya tahadhari kabla ya janga kufika.

Mheshimiwa Spika, sheria hii iliweka bayana kuwa yeyote atakayechafua mazingira, atapaswa kulipa fidia wale wote walioathirika na uchafuzi huo na pia kulazimika kuyarejesha mazingira husika katika hali yake ya kawaida.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuwepo kwa sheria hii, na sote tunajua kuwa mchafuzi mkubwa wa mazingira ni miradi mikubwa ya kibinafsi na hata ile inayosimamiwa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inataka kupata majibu kutokana na mambo yafuatayo:- Ni kwanini sheria hii haisimamiwi kikamilifu na hasa kutokana na uchafuzi mkubwa wa mazingira unaofanywa na makampuni makubwa ya madini.

(1) Ni lini Serikali itahakikisha kuwa uchanjuaji wa madini kwa kutumia sumu ya *cyanide* kwenye migodi mikubwa kama ilivyo kule *Barrick North Mara* na *Geita Gold Mine* utaachwa ama utatengenezewa utaratibu wa kuhifadhiwa kikamilifu kutokana na madhara ya sumu hii kwa maisha ya binadamu na viumbe mbalimbali kwenye maeneo ya migodi?

(2) Ni lini Serikali itachukua hatua dhidi ya migodi ya dhahabu ambayo kutokana na shughuli zake husababisha *acid mine drainage* ambazo hupelekea uchafuzi mkubwa wa mazingira? na

(3) Ni lini *NEMC* itaanza kuchukua hatua kwa mujibu wa sheria kutokana na uchafuzi unaofanywa na migodi hii na kuacha tabia ya kukanusha kila mara kuwa hakuna madhara hata kama yanaonekana wazi na ili tuweze kuwalinda wananchi pamoja na viumbe ambao wanaendelea kuangamia?

Mheshimiwa Spika, ripoti ya *face the future* ya mwaka 2001 inaonyesha kuwa zaidi ya aina *(species)* 33 za wanyama, 30 za ndege na 326 miti zipo hatarini kutoweka ulimwenguni na hasa kwenye ukanda wa Afrika ya Mashariki kutokana na uchafuzi na uharibifu wa mazingira unaofanyika kwenye ukanda huu.

Mheshimiwa Spika, dalili za kuathirika kwa mazingira kunajidhihirisha kwa mabadiliko ya tabia ya hali ya hewa duniani kama vile ongezeko la hali ya joto duniani, barafu katika milima imepungua au imekwisha kwa mfano Mlima Kilimanjaro kwenye miaka ya 1970 na 1980 ulikuwa umefunikwa na barafu kwa kiasi kikubwa. Kwa sasa barafu imepungua sana. Athari nyingine ni kuibuka kwa magonjwa kama ya ngozi na kansa. Haya yote yanatokana na maendeleo yasiyokuwa endelevu *(non-sustainable development)*. Kupungua kwa kiwango cha mvua katika maeneo mengi na kuongezeka kwa jangwa.

Mheshimiwa Spika, sote tunatambua umuhimu wa kutunza mazingira kwani tunatambua kuwa:-

(i) Mazingira yanaipatia nchi mahitaji yote ya msingi kwa ajili ya kufanikisha masuala ya jamii na uchumi;

(ii) Mazingira ndiyo makazi ya viumbe vyote, mimea na wanyama ambao ndiyo urithi usiokuwa na badala yake;

(iii) Mazingira ni chombo cha kuweka yale yasiyofaa; na

(iv) Mazingira ni msingi ambao ndiyo itakuwa jawabu la kupunguza umaskini unaotukabili.

Mheshimiwa Spika, ni lazima Serikali ya Tanzania itambue hatari ya kupoteza raslimali hiyo kama vile hewa safi, mabaki ya mimea na wanyama wa kale, nyangumi, miti ya asili na wanyama/mimea ambayo iko mbioni kutoweka.

Mheshimiwa Spika, katika kurekebisha hali hiyo, Kambi ya Upinzani inaishauri Serikali ichukue hatua thabiti kwa kutengeneza na kurekebisha Sera, Sheria na Mfumo wa taratibu ili ziendane na masuala ya jamii, uchumi na siasa.

Kambi ya Upinzani inaishauri Serikali kwa kushirikiana na washikadau mbalimbali kuweka mkazo katika kuendeleza, kukuza na kuhamasisha ushirikishwaji wa Jumuiya na watu binafsi katika kuimarisha uhifadhi na uongozi wa mazingira. Pamoja na hayo, kuwepo kampeni za kutambua umuhimu wa mazingira, elimu ya mazingira na kuendeleza ujuzi ambao utasaidia.

Mheshimiwa Spika, tunaishauri Serikali kuzitumia sera za sekta zinazohusiana na misitu, maji, madini, wanyamapori, samaki, kilimo, mifugo na ardhi ambazo zimeweka kipaumbele masuala ya usimamizi na hifadhi za raslimali na mazingira, kukuza ufahamu wa wananchi wa kuelewa uhusiano kati ya mazingira na uhai na kuendeleza ushirikiano wa kimataifa kuhusu ajenda ya mazingira. Ni dhahiri kwamba uhifadhi na usimamizi wa mazingira duniani na kitaifa una nia ya kushinda matatizo yanayotokana na umaskini, maradhi, hali mbaya na duni ya upatikanaji wa chakula, makazi machafu, maji yasiyo salama, upatikananji wa nishati usioridhisha na ukosefu wa ajira.

Mheshimiwa Spika, kuelewa kwa wananchi juu ya faida za kuhifadhi na kusimamia mazingira kutasaidia kwa kiasi kikubwa katika kutekeleza mipango thabiti ya kuondoa na umaskini, kwa sababu umaskini unaendana na matumizi mabaya ya raslimali na uharibifu wa mazingira na hivyo juhudi za kuuondoa umaskini zinahitaji ushirikiano kutoka kwa wananchi wote.

Mheshimiwa Spika, tunapenda kuchukua fursa hii kuzipongeza Halmashauri za Mji wa Moshi na Jiji la Mwanza kwa kuibuka washindi kitaifa katika utunzanji wa Mazingira hapa nchini mwetu. Napenda kulijulisha Bunge lako kuwa Halmashauri hizi zinaongozwa na CHADEMA tangu uchaguzi Mkuu wa mwaka 2010, na hii inaonyesha jinsi ambavyo CHADEMA inaishi na kutembea katika maneno yake na tunaamini kuwa mwaka ujao Halmashauri za CHADEMA zitaongoza halafu ndipo za CCM ziweze kufuatia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika Mji wa Moshi, Halmashauri imeweka utaratibu wa kuhakikisha kuwa kila mwananchi anashiriki kikamilifu katika kutunza mazingira kwani wamejitungia kanuni na kila mmoja anawajibika kutekeleza kikamilifu kanuni hizo na hata akifika mgeni Moshi huwa anaambiwa na madereva *taxi*, daladala na hata pikipiki kuwa anapaswa kuhakikisha kuwa anatumia kikamilifu vyombo vya kuhifadhia taka na

kama hatafanya hivyo, atakumbana na mkono wa sheria na kila mwananchi ni mlinzi wa sheria hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani tunaitaka Serikali iende sasa ikajifunze kwenye Halmashauri hizi ni jinsi gani waliweza kutunga kanuni na kuziwezesha kujulikana kwa kila mwananchi kwenye eneo lao na kila mmoja anazifuatilia kikamilifu ili miji mingine nayo iweze kuiga mifano hii na kuwa safi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Sera ya Taifa ya Mazingira ya mwaka 1997 iliainisha madhumuni muhimu sana ambayo tunatakiwa kuyazingatia sana tunapotumia raslimali zetu hasa tunaporuhusu uwekezaji, na kama tungeyazingatia ingesaidia kuondoa migogoro, manung'uniko na malalamiko yanayojitokeza kwa sasa. Naomba kwa ridhaa yako niyataje:-

(i) Kuhakikisha udumishaji, usalama na matumizi sawa ya raslimali kwa mahitaji ya msingi ya sasa na ya vizazi vijavyo bila kuharibu mazingira au kuhatarisha afya na usalama;

(ii) Kuzuia na kudhibiti uharibifu wa ardhi, maji, mimea na hewa ambayo ndiyo husaidia mfumo wa uhai wetu;

(iii) Kuhifadhi na kuendeleza urithi wetu na ule unaotengenezwa na binadamu, ikiwa ni pamoja na maisha ya viumbe wa aina mbalimbali na vya pekee nchini Tanzania;

(iv) Kurekebisha hali na uzalishaji wa maeneo yaliyoharibiwa pamoja na makazi ya watu mijini na vijijini ili Watanzania wote waweze kuishi katika hali ya usalama, kiafya, kuzalisha bidhaa pamoja na kuishi katika mazingira mazuri yenye kuvutia;

(v) Kung'amua na kufahamu mahusiano muhimu kati ya mazingira na maendeleo na kuhimiza ushirikiano wa mtu binafsi na jamii katika kuhifadhi mazingira; na

(vi) Kuendeleza ushirikiano kimataifa kuhusu ajenda ya mazingira na kupanua ushiriki na mchango wetu kwa pande zote zinazohusika ikiwa zinahusu nchi jirani na mashirika na mipango ya ulimwengu pamoja na utekelezaji wa mikataba mbalimbali ya kiulimwengu.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaona kuwa Serikali hii ina tatizo kubwa la kutokutekeleza sera, sheria na mipango inayopanga yenyewe. Hii inathibitika kwa kutokutekeleza sera hii ya Mazingira.

Mheshimiwa Spika, imeelezwa wazi kabisa kwamba moja ya madhumuni ya Sera hii ya Taifa ni kuzuia na kudhibiti uharibifu wa ardhi, maji, mimea na hewa ambayo

ndiyo husaidia mfumo wa uhai wetu. Lakini ukweli ni kwamba sote tunashuhudia kemikali zenye sumu zikitiririka katika mito ambayo maji yake yanatumiwa na viumbe hai kama binadamu, mifugo, viumbe viishivyo majini na kilimo cha umwagiliaji na hali hii imesababisha vifo na madhara makubwa kiafya kwa wananchi wetu maeneo mbalimbali hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, ripoti ya Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu ya mwaka 2010 imeeleza kuwa takriban watu 24 wanaoishi karibu na mgodi wa dhahabu wa *Barrick North Mara* waliripotiwa kufa mwezi Mei, 2009 kutokana na maji yenye sumu kutoka mgodini kutiririka mto Tigithe ambao unatoa maji ambayo ni uhai wa wakazi na mifugo ya eneo hilo.

Mheshimkiwa Spika, itakumbukwa kwamba Bunge la Tisa liliwahi kuunda Kamati Maalum iliyoongozwa na Naibu Spika ambayo ilifuatilia suala hili na mpaka leo ripoti ile imewekwa kabatini huku wananchi wakiendelea kuangamia kutokana na Serikali kuwalinda wawekezaji wa madini na kusahau kuwa kuna Watanzania ambao wanakufa kutokana na athari za uwepo wa mgodi huu kutokana na sumu mbalimbali za zebaki ambazo hutiririka kwenye mto huo. Kambi ya Upinzani, tunalitaka Bunge kuiweka ripoti iliyotokana na Kamati hii hadharani na ili wananchi waweze kuelewa nini kilichoonekana na kuripotiwa na Kamati hii. Tunalitaka Bunge liweze kuijadili ripoti hiyo ya Kamati ya Mheshimiwa Job Ndugai na hatimaye Serikali iweze kutekeleza maazimio ya Bunge.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira) haichukui hatua kwa wakati kuhusiana na uchafuzi wa Mazingira. Mathalani katika kipindi cha miaka 10 kati ya mwaka 2001 mpaka 2011 Tume imepokea malalamiko yenye maelezo na vielelezo kuhusu uchafuzi wa mazingira katika eneo la Makuburi Kibangu ambako kuna uchafuzi mkubwa wa mazingira unaotokana na shughuli za Kiwanda cha Mkuani *Traders/Azania Wheat Flour Ltd* katika eneo la makazi ya watu na katika eneo la *Mabibo External* ambapo maji taka (ukiwemo uchafu wa vyoo) toka Hosteli za wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Mabibo Hostel yanatiririshwa katika mto na pembeni ya makazi ya watu hivyo kuleta harufu na madhara mengine ya kiafya. Jambo hilo limekumbushwa tena kwa Serikali kupitia barua kwa Ofisi ya Makamu wa Rais Mazingira ya tarehe 7 Februari, 2011 yenye Kumb. OMU/AF/001/2011. Hata hivyo, hakuna hatua zilizochukuliwa na Waziri wa Mazingira wala *NEMC* wala majibu ya barua hiyo kutolewa pamoja na barua kupokelewa.

Mheshimiwa Spika, taarifa zilizopo zinaonyesha kwamba Maafisa wa Jiji na wa Manispaa ya Kinondoni wametembelea eneo hilo na kuthibitisha kuwepo kwa uchafuzi huo. Hata hivyo, hakuna hatua za kisheria zilizochukuliwa badala yake Maafisa wa Manispaa na Jiji la Dar es Salaam wameishia kutoa onyo na kuacha uchafuzi huo wa kimazingira ukiandelea mpaka hivi sasa.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inataka Ofisi ya Makamu wa Rais Mazingira ieleze kama hatua zinashindwa kushughulikia uchafuzi wa Mazingira Dar es

salaam ambapo maofisa wake wengi wapo, itakuwaje katika maeneo ya mbali ya vijijini? Nini kinapelekea ofisi hii kushindwa kulitafutia ufumbuzi wa kudumu suala hili?

Mheshimiwa Spika, athari za kutotekeleza sera hii ya mazingira inayoeleza kudhibiti uharibifu wa ardhi, maji, mimea na hewa, umeathiri maeneo mengi sana. Kuna tatizo la uchafuzi wa hewa unaofanyika kutokana na viwanda mbalimbali hapa nchini kama Kiwanda cha Ngozi pale Kibaha, Kiwanda cha Ngozi maeneo ya Kihonda Morogoro, Kiwanda cha Ngozi Himo, Kilimanjaro na viwanda vingi vya ngozi vilivyopo maeneo mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Spika, ripoti mbalimbali zinaonyesha kuwa viwanda vya nguo ndiyo vinaongoza ulimwenguni katika kuchafua mazingira na ndiyo maana hata hapa nchini mwetu wananchi wa Mbagala karibu na kiwanda cha nguo cha *KTM* wamekuwa wakilalamika sana kuhusiana na madhara wanayoyapata kutokana na uchafuzi wa kiwanda hiki katika Mto Kizinga.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani, tunaitaka Serikali ilieleze Bunge ni kwanini *NEMC* imeshindwa kuchukua hatua katika kiwanda hiki pamoja na uchafuzi mkubwa wa mazingira ambao umekuwa ukifanyika.

Mheshimiwa Spika, utafiti uliofanywa na shirika lisilo la kiserikali la *Face the Future* mwaka 2001, ripoti yake ilionyesha kuwa zaidi ya asilimia 70 ya uchafu unaotokana na viwanda mbalimbali vilivyopo Jijini Dar es Salaam kama vile vya chuma, madawa, uzalishaji n.k. unaelekezwa moja kwa moja kwenye bahari ya Hindi na kuwa chanzo kikuu cha uchafuzi wa bahari hiyo.

Mheshimkiwa Spika, kutokana na ripoti hiyo, inaonyesha kuwa zaidi ya aina 16 *(species)* ya samaki wapo hatarini kutoweka kutokana na uchafuzi huo wa bahari pamoja na uvuvi haramu wa kutumia baruti ambao unaharibu mazalia ya aina hizo za samaki.

Mheshimiwa Spika, malalamiko ya wananchi yapo maeneo mengi yenye viwanda katika nchi hii. Kambi ya Upinzani inashauri matatizo haya yashughulikiwe yanapojitokeza na uwepo ukaguzi wa mara kwa mara ukishirikisha wakazi wa maeneo husika kuhakikisha kuwa hakuna athari kwa wakazi wa maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inashauri Serikali kwa kushirikiana na wawekezaji katika eneo husika kuhakikisha kuwa wanafanya marekebisho katika maeneo husika yaliyoharibika kutokana na shughuli zao za uzalishaji wazifanyazo. Tumewapa misamaha ya kutosha, basi wasaidie wananchi wetu kuyafanya mazingira yao ya kuishi yawe salama kiafya, kuzalisha bidhaa na kuishi katika mazingira mazuri yenye kuvutia.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani tunaitaka Serikali iwadhibiti wawekezaji ambao wameendelea kuchafua mazingira ya nchi hii na kusababisha madhara mbalimbali bila hatua zozote kuchukuliwa.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani tunaitaka Serikali kuhakikisha kuwa yale maeneo yote ambayo yamekuwa yakitumika kama maeneo ya kuhifadhi madawa na sumu mbalimbali zitokanazo na madawa ya kilimo, kama vile Kibaha na Korogwe (*areas for disposal of agricultural poisons*) yanahifadhiwa vizuri ili yasilete madhara kwa wananchi waishio maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, hali ya utunzaji wa miti yetu na misitu ni mbaya sana hapa nchini mwetu na hii inaonyeshwa na taarifa ya *Population, Health, and Environmental Intergration and Cross Sectoral* ya mwaka 2007 ambayo inasema kuwa Tanzania tulipoteza asilimia 14.4 ya misitu kwa kipindi cha mwaka 1983 - 1993 na sababu kubwa ya upotevu huu wa misitu na miti ni kutokana na zaidi ya asilimia 86 ya Watanzania kutegemea miti kama chanzo cha kupata nishati (kuni, mkaa). Ujenzi wetu kwa asilimia 75 ili ukamilike unategemea pia miti na hata dawa za mitishamba huwa zinapatikana mara baada ya miti kuumia.

Mheshimiwa Spika, ukataji miti na uchomaji wa misitu Tanzania umeendelea kwa kiwango kikubwa sana. Maeneo yaliyoathirika kwa kiwango kikubwa ni yaliyoko katika Mikoa ya Dodoma, Singida, Shinyanga, Mwanza, Mara na Tabora. Sababu kubwa za uchomaji huu wa misitu ni kwa ajili ya shughuli za kilimo, kutafuta nishati hasa mkaa na kuni kwa matumizi ya kupikia na upasuaji wa mbao.

Mheshimiwa Spika, ukataji huu wa miti na uchomaji huu wa misitu umesababisha kuzalishwa kwa hewa ya kaboni ambayo kwa kawaida huhifadhiwa kwenye miti kama hewa ya ukaa *($CO_2$)* na hili limepelekea kuharibika kwa leya ya ozoni *(ozone layer).*

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa ripoti ya *Forest Carbon Projects* ya mwaka 2008 inakadiria kuwa asilimia 18 - 20 ya hewa ya kaboni inayozalishwa kwa mwaka duniani inasababishwa na kupungua kwa misitu ya ukanda wa tropiki.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani tunaona kuwa hili ni janga kubwa na inapaswa sasa tuchukue hatua katika kukabiliana na janga hili na hatua hizo ziwe kama ifuatavyo:-

(i) Nishati mbadala itumike na hasa kwa kutumia vyanzo vya upepo, jua na umeme vijijini na hii itasaidia kuokoa miti mingi ambayo hutumika kwa ajili ya nishati na Serikali igharimie uwepo na upatikanaji wa nishati hizo. Hii inatokana na ukweli kuwa ni asilimia 14 tu ya Watanzania ndio wameunganishwa kwenye umeme wa gridi ya Taifa;

(ii) Gharama za vifaa vya ujenzi ipunguzwe, na hii ni kwa vifaa kama sementi ili wananchi waweze kujenga nyumba kwa kutumia tofali badala ya kutumia miti na hii itaokoa asilimia kubwa ya miti ambayo hutumika kwa ajili ya ujenzi;

(iii) Itolewe elimu ya kina katika kupanda miti na kutunza miti iliyopo pamoja na misitu iliyopo kwani hali hii isipochukuliwa hatua za kina, Taifa hili linakwenda

kuangamia, na ukame umekuwa ukiongezeka kwa kasi kubwa sana maeneo mbalimbali hapa nchini mwetu;

(iv) Mitaala ya Shule za Msingi na Sekondari ibadilishwe na iweke msisitizo katika umuhimu wa kupanda miti na kutunza miti. Hili litasaidia katika kizazi kinachokuja kujua umuhimu huu wa miti katika maisha yao na maisha ya vizazi vijavyo;

(v) Watendaji wa Vijiji, Mitaa na Kata kote nchini, moja ya majukumu yao iwe ni kuhakikisha kuwa kila mwananchi anapanda miti na hiki kiwe ni kipimo kimojawapo katika kupima utendaji kazi wa viongozi hawa; na

(vi) Kila Halmashauri zote nchini zitenge fedha kwa ajili ya kununua miche ya miti na kuigawa bure kwa wananchi kila kipindi cha masika kwenye maeneo husika na Watendaji wa Vijiji, Mitaa na Kata wagawe miche hiyo kwa kila kaya na kila mwananchi apande miche hiyo.

Mheshimiwa Spika, ripoti mbalimbali zinaonyesha kuwa kutokana na mmomonyoko wa ardhi *(land degradation)* sasa karibu asilimia 60 ya ardhi yetu imekuwa na tishio la kuwa jangwa na hii ni taarifa ya utafiti iliyofanywa na *Forest Carbon Projects* ya mwaka 2008.

Mheshimiwa Spika, wananchi wengi wameathirika sana na hali hii ya jangwa. Wapo baadhi ya wafugaji waliolazimika kuhama maeneo yao ya awali na kulazimika kwenda kuishi maeneo mengine. Hii imesababisha migogoro baina ya wafugaji na wakulima. Mauaji baana ya wakulima na wafugaji yaliyotokea katika Wilaya ya Kilosa kati ya Wamasai na wenyeji.

Mheshimiwa Spika, mapigano ya Wamasai na Wasukuma katika Kijiji cha Pawaga Wilaya ya Iringa wakigombea bwawa la kunyeshwa mifugo yao. Kuhamia kwa wingi jamii ya wafugaji kimasai na wasukuma katika Tarafa ya Bwakira Wilaya ya Morogoro vijijini. Maeneo mengine katika nchi ni matokeo ya kuenea kwa ukame kunakosababishwa na uharibifu wa ardhi unaosambabishwa na shughuli za kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, katika kukabiliana na hali ya jangwa, Kambi ya Upinzani inaishauri Serikali kutumia wataalamu wake wa kilimo kuwasaidia wakulima kuelekeza jitihada zaidi katika kuwasaidia wakulima hao kutafuta njia mbadala za kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi kwa kuelezea kwa ufasaha uzalishaji wa chakula na kutangaza mbinu bora za kilimo hicho.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inashauri kuwepo pia kwa njia mbalimbali za kuboresha uzalishaji wa mazao kwa kutumia virutubisho mbalimbali kama vile mbolea, matumizi ya matrekta na kuondokana na kilimo cha mazoea cha kuchoma moto na kuhamahama kutoka shamba moja kwenda eneo lingine.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inasisitiza kuwa kuna kila sababu wakulima wa Tanzania kuachana na tabia zao za kilimo kisichozingatia utunzaji wa

mazingira, ili athari za mabadiliko ya tabia nchi zisizidi kuongezeka na kuzidi kuuharibu uchumi wa Taifa hili kwa kuwa sekta nyingine zote zilizopo nchini zinategemea kwa kiasi kikubwa ufanisi wa Sekta ya Kilimo.

Mheshimiwa Spika, njia nyingine bora ya kupunguza ukataji wa misitu ni kuwa na nishati mbadala. Kambi ya Upinzani inaishauri Serikali kuwahakikisha kuwa tunaongeza miradi ya uzalishaji umeme kwa wingi ili usambazwe mpaka maeneo ya vijijni. Usimamizi wa mazingira umekuwa ukipokea misaada mingi ya kifedha na kiutaalam kutoka kwa Jumuiya ya Wahisani na asasi mbalimbali kuliko Sekta nyingine yoyote nchini Tanzania kwa sababu ya umuhimu wake katika uchumi wa nchi.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inasikitika kuwa pamoja na miradi mingi kupata misaada ya washirika hawa wa maendeleo, ufanisi wake bado ni wa chini ukilinganisha na misaada inayotolewa, kwani tunachoshuhudia ni magari ya kifahari yenye majina ya miradi husika na nembo za wafadhili, huku milima ikiteketea kwa moto na kuua viumbe hai, kuteketea misitu na kuharibu vyanzo vya maji.

Mheshimiwa Spika, inasikitisha sana kuwepo kwa miradi mingi ya mazingira na wafadhili wa kutosha lakini mazingira yetu yakiendelea kuathirika kwa kiwango kikubwa. Kambi ya Upinzani inashauri Baraza na Mazingira kufanya kazi kwa karibu na asasi hizi zinazojihusisha na utunzaji wa mazingira ili kuhakikisha kunakuwa na ufanisi wa kiutendaji wa asasi hizi na kusaidia kuyafanya mazingira haya kuwa nyumba salama kwa kizazi kilichopo na kijacho.

Mheshimiwa Spika, nihitimishe kwa kusema kuwa Tanzania imebahatika kuwa na raslimali nyingi ikiwemo misitu, wanyamapori, madini, mito, maziwa na maeneo kinamasi. Raslimali hii ni muhimu kwa utoaji wa huduma kiuchumi na kijamii. Kufifisha raslimali hii ni kuharibu mazingira endelevu ya shughuli za kiuchumi. Ni wajibu wa kila mmoja wetu kuhakikisha kuwa tunakuwa na uzalishaji unaojali mazingira yetu ambao hautaathiri kizazi kijacho.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MHE. TAUHIDA CASSIAN GALOS NYIMBO:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipatia fursa hii ya kuchangia Wizara ya Muungano. Nianze kwa kuwashukuru wananchi wa Tanzania, kukipa ushindi Chama cha Mapinduzi na leo hii Serikali ya Chama cha Mapinduzi, ndiyo inayotawala Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii vilevile kumpongeza Mheshimiwa Kayanza Mizengo Pinda kwa kuteuliwa kwa mara ya pili kuwa Waziri Mkuu. Napenda kuchukua fursa hii kukupongeza wewe mwenyewe binafsi kuwa mwanamke wa kwanza kuongoza Bunge la Tanzania. Sina budi kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, katika suala zima la kuusimamia Muungano ipasavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nathibitisha haya kwa suala zima la Mawaziri waliotoka Zanzibar. Tunashukuru, Rais ameona umuhimu wa Wizara muhimu na nyeti, kuwateuwa Mawaziri kutoka Zanzibar. Kama vijana wa Zanzibar, tuna imani na Mawaziri na Manaibu Mawaziri walioteuliwa kutoka Zanzibar. Uwezo wao unatosha, wana kila sifa na tunawaamini maana tayari wameshaitumikia Zanzibar vyakutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais, amekuwa kigezo na mfano mkubwa katika suala zima la kudumisha Muungano. Mheshimiwa Rais amekuwa mara nyingi anazungumzia suala la Muungano, lakini ukimwona anawiwa na ana hamu ya kuusimamia Muungano katika kazi zote, imefika wakati alitoa kauli akawaambia, nafikiri ilikuwa mwaka 2010 kauli yake mara nyingi akizungumza katika suala zima la Muungano alikuwa akizungumza Mheshimiwa Waziri Mkuu na Mheshimiwa Waziri Kiongozi Zanzibar, nawataka kila siku japo mwisho wa mwezi mkutane kwa ajili ya kutatua kero za Muungano. Kauli hiyo ya Mheshimiwa Rais ilikuwa inatufurahisha sana vijana wa Zanzibar. Maana tulikuwa tuna imani kwamba anaupenda Muungano na anautetea na anaulinda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitazungumza suala moja tu la elimu kwa umma kwenye suala la Muungano. Inahitajika Serikali yetu itoe elimu kwa umma kwa suala zima la Muungano.  Asilimia 55 ya vijana wa Tanzania hawaelewi suala la Muungano, wanauzungumza tu Muungano, Muungano, lakini hawauelewi. Nitarudia kusema kwamba asilimia 60 ya Wabunge, ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni vijana. Haijalishi kwamba anatokea *CCM, CUF,* Viti Maalum, hawauelewi Muungano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naiomba Ofisi yako kwa jitihada za makusudi, utufanyie semina au mafunzo maalum. Kumekuwa na maneno ya kuudhi ndani ya Bunge, mtu anayezungumza suala la Muungano wakati hauelewi Muungano. Nisiende mbali, nitolee mfano kauli ya sasa hivi. Imezungumzwa kwamba Ofisi ya Bunge Zanzibar haifanyi kazi, sio kweli! *Passport* yangu nimeipatia ndani ya Ofisi ya Bunge ya Zanzibar na mwenzangu na yeye naye hivyo hivyo, huduma zote tunazohudumiwa kama Wazanzibari Wabunge, zinahudumiwa ndani ya Ofisi ya Zanzibar. Hili linamaanisha kwamba, haja kubwa ya Bunge hili kulifahamisha suala la Muungano, upo umuhimu huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nasikitika vile vile kuona kwamba anasimama kijana Mbunge, anazungumza kwamba Zanzibar inamezwa na Muungano. Nani kasema Zanzibar inamezwa na Muungano? Kwa kigezo kipi kinachofanya Zanzibar imezwe na Muungano? Muungano ni Muungano, Zanzibar ni Zanzibar. Kwanza ifahamike kwamba Zanzibar kuna Rais na kwa sasa hivi tuna Serikali Shirikishi. Kwa hiyo, Zanzibar kuna Rais, kama hafahamiki, anaitwa Mheshimiwa Dkt. Mohammed Shein na Makamu wake wa Pili Mohamed Seif Ali Iddi na kwa sasa hivi tuna Makamu wa Kwanza anaitwa Mheshimiwa Seif Shariff Hamad. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, iko haja Bunge hili kulifanyia Semina waelewe wanachokizungumza mahali hapa. Tunapata uchungu vijana wa Zanzibar, hususan wa *CCM,* kuona kwamba unabezwa Muungano pasipokuwa na sababu za msingi. Viongozi wetu wamekuwa makini, viongozi wetu wamekuwa wakiutetea Muungano.

Mheshimiwa Spika, hakuna sehemu isiyokuwa na kero. Familia zetu zina kero. Kama kuna wanandoa, wanazijua. Hata bughudha ndogo ndogo ndani ya ndoa zipo. Leo utazungumzaje Muungano uvunjike wakati wewe mwenyewe nyumba yako huimudu vizuri, kero zipo! Kwanza tengeneza familia yako, tengeneza nyumba yako, halafu uanze kuutomasa Muungano wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunawachukia wanaotomasa Muungano, tena wanatuudhi vijana wa Zanzibar, hususan wa Mkoa wa Mjini Magharibi *CCM*, mnatuudhi! Kauli zao hizo wasitarajie kwamba viongozi hao tunawapenda, hatuwapendi ng'o! Tunasema vijana wa Zanzibar, tutaulinda Muungano, tutautetea, tutaupigania kwa njia yoyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nazungumza haya kwa uchungu. Imekuwa kila mara watu wanapozungumza kero za Muungano hawaisaidii Zanzibar, wanachokifanya kana kwamba wanataka sijui niseme kitu gani. Wanataka kudabua Serikali ya Muungano, hawana nia ya kuisadia Zanzibar! Lakini nazungumza vijana wa Zanzibar wanataka kusaidiwa, wanataka kuondolewa kero zilizokuwepo na siyo hivyo vinavyofanyika ndani ya Bunge hili. Hapa kinachotuleta kama Wabunge, iwe kutoka Zanzibar iwe kutoka wapi, tuzungumze kero za wananchi na siyo vinginevyo. Kama tuna malumbano, tusubiri wakati wa kampeni kwenye majukwaa ya kisiasa. Mtu anayetaka kufanya siasa yake, akaandae jukwaa kwenye Jimbo, hapa tuzungumze kero za wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala zima la Muungano kwa upande wa Zanzibar, vijana tunataka tujue hatma yetu inakwendaje? Suala la elimu, kuna watu wanasafirishwa kwenda nje, tunataka tujue Zanzibar inanufaika vipi? Vijana wanaopelekwa kutoka Zanzibar, mwaka mzima takwimu yake ikoje? Haya yanafanyika na nina imani na uongozi kwa sababu ni viongozi wa Chama cha Mapinduzi, lakini yasiwe siri, yawekwe wazi ili tujue kwamba Zanzibar inanufaika vipi kama vijana kwenye suala zima la Muungano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kero za Zanzibar ni nyingi na kila siku watu kutoka Zanzibar bila kujali itikadi zetu za vyama, kero tunazozitaja ni hizo hizo. Ningeomba Serikali ichukue kero kuu ambazo zinatusumbua itatue hili tatizo. Hata familia unapokuwa nyumbani, utatue kero inayomsumbua mtoto, usijaribu kumpa mtoto vitu ambavyo yeye havihitaji. Tunataka suala la bandari, *TRA*, *ZRB*, suala la kodi kutoka Zanzibar kuja Bara zisawazishwe. Nazungumza haya, Serikali naomba isikie, kwa sababu imekuwa kila tunaposimama sasa hivi wamekuwa wenzetu wanatubeza, tunasikia vijineno vidogo vidogo, hao! Bandari! *TRA!* Sijui kitu gani! Wanatubeza! Lakini tunasema hatutachoka kusema haya maneno kwa sababu, ndiyo yanayotukera, na haya ndiyo yaliyotuleta hapa na Muungano hautavunjika.

Mheshimiwa Spika, vijana wa Zanzibar tuko tayari kuupigania Muungano kwa gharama yoyote. Tutakachokuja kukiwasilisha hapa, kero ziondoke. Mheshimiwa Waziri wa Muungano, tunakuomba, tunaujua umakini wako, tunazijua kazi zako, hujaja kujifunza kazi, umekuja kufanya kazi, tunakuomba mama yetu tatua kero za Muungano. Kwa Mwenyezi Mungu, tutakuombea kila leo akupe uwezo, lakini kero za Muungano

ziondoke na unapokwama usisite kuwaambia wenzio kwamba hapa nimekwama, wakusaidie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kweli kabisa nasema kwamba najisikia uchungu, mara nyingi sana wenzetu wamekuwa hawazungumzi vizuri juu ya Zanzibar. Naamini hawana…

*(Hapa kengele ya kwanza iligonga kuashiria muda wa mzungumzaji unakaribia kwisha)*

**MHE. TAUHIDA CASSIAN GALOS NYIMBO:** Mheshimiwa Spika, muda umekwisha?

**SPIKA:** Bado moja.

**MHE. TAUHIDA CASSIAN GALOS NYIMBO:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Mara nyingi tungewaomba wenzetu wasaidie kutatua matatizo yaliyokuwepo ya Muungano na siyo kubeza Muungano. Hapa ninazungumza, uchungu umenishika sana maana, mimi ni mmojawapo ambaye ni faida ya Muungano. Kwa hiyo, leo unapoanza kusema kwamba Muungano uvunjike, sikuelewi. Tunaiomba Serikali, ichukue jitihada za makusudi kutatua kero za Muungano. Ninaamini Rais wetu yuko pamoja na sisi katika kutatua kero za Muungano. Kama kuna watendaji chini wanaotumiwa na watu, wanataka kuivuruga Serikali ya Chama cha Mapinduzi, tusiwastahamilie wala kuwafumbia macho. Kwa nini wasiondoke? Waondoke tu, kwa sababu wao ndiyo wanaosababisha kero za Muungano zisiondoke. Mheshiniwa Rais hili halifumbii macho, kila siku anazungumza wazi, hadharani, kwamba kero za Muungano ziondolewe. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa yote niliyochangia. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Haya, siku nyingine utatulia kabla hujasema. Mheshimiwa Salim. *(Makofi)*

**MHE. MBAROUK SALIM ALI:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, namshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kunijalia kwanza mpaka wasaa huu kuwa bado ninahema. Lakini lingine, namshukuru kwa kunijalia leo hii kuweza kupata nafasi hii ya kuchangia hotuba hii ya bajeti ya Ofisi ya Muungano na Mazingira. Lakini pia nakushukuru wewe Spika kwa kuniteua kuwa mchangiaji wa pili katika nafasi hii ya hotuba hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wazanzibari bado tutaendelea kuzungumzia Muungano. Kama inavyoeleweka kwamba Muungano ni wa pande mbili, Tanzania Bara au Tanganyika na Zanzibar, lakini kuna suala tujiulize, nafikiri tunatakiwa Watanzania sote tujiulize, kwa nini sehemu moja ya Muungano inakuwa inalalamika zaidi kuliko sehemu nyingine? Nafikiri pamoja na kuwa kuna kero kwa pande zote, lakini inaonekana dhahiri kwamba upande mmoja wa Muungano ile dhahama ya kero, ile dhahama ya ukandamizaji, ile dhahama ya unyanyasaji wa Muungano huu nafikiri upande mmoja

imeinamia zaidi. Mimi ninafikiri Serikali ya Muungano, Serikali ya *CCM,* pamoja na kwamba inasema ni sikivu, lakini hili usikivu naona unakuwa ni mgumu. Kwa hiyo, naiomba sana kwamba katika usikivu, basi hii waipe kipaumbele kwa sababu ni kero. Bila kuondoa kero, basi itakuwa hakuna maendeleo hasa kwa upande ule ambao kero zimeinamia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri katika uwasilishaji wake alitaja mambo kadha wa kadha, kwamba yako katika mijadala. Lakini hivi vikao vimeshakuwa vingi sana na utatuzi wa matatizo haya, utatuzi wa kero hizi, bado unaendelea kukaliwa. Mimi ninafikiri tuliungana kwa nia safi, inapotokea kero ndogo ndogo mimi nafikiri hakutakiwi kuwa na michakato mirefu ya kutatua kero ndogo ndogo ya sehemu zilizoungana. Mimi nafikiri hakuna sababu ya kero tuseme ya *TRA* kuchukua miaka 10, kuchukua miaka mitano, kuchukua miaka mitatu, inajadiliwa. Mimi sioni sababu! Kama kuna ukiukwaji wa jambo Fulani, nafikiri ni *matter* ya *session* moja tu, pakatoka maamuzi likatatuliwa. Sasa hili limekuwa kwa kweli ni mchakato unafanywa mrefu sana. Hii nafikiri ni jambo ambalo linafanywa makusudi!

Sasa mimi ninafikiri, jambo hili linahitaji kwa kweli lifanyiwe marekebisho, Watanzania tuwe kitu kimoja, tudumishe Muungano wetu. Hakuna ambaye hataki Muungano. Watu wote wanataka Muungano, huko Zanzibar ndiyo kuzidi, wanataka Muungano, lakini siyo hivi ulivyo. Kwa hiyo, nafikiri kwamba tukae tutatue matatizo, tuondoe kero ambazo wenzetu au sisi upande mmoja zimetuinamia zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa wenzangu waliopita kwa sababu kila mahali sisi tunataja kero za Muungano na hii ni kuonyesha dhahiri kwamba zinatukera sisi zaidi kuliko upande mwingine. Ikija Wizara ya Afya tutataja Muungano, ikija Wizara ya Elimu tutataja Muungao, ikija Maliasili tutataja Muungano na katika Wizara hii ya Muungano wenyewe ndiyo tunazidi kuutaja Muungano. Mimi nafikiri hiyo ionekane kwamba Muungano bado una matatizo. Kwa hiyo, nafikiri tukae pande mbili, matatizo madogo madogo yaweze kufanyiwa kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri atakapokuja kwa sababu mengi yameelezwa ya Muungano, nilitaka nijue hadhi ya Rais wa Zanzibar ki-*protocol* anapotoa katika ardhi ya Tanzania Bara, anakuwa ana hadhi gani? Au *protocol* ya Rais wa Zanzibar wakati ambapo Rais au Makamu wa Rais wa Tanzania au wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hayupo nchini, kwa sababu inavyoonyesha, haonekani kwamba yuko katika *system*. Yuko yuko tu, kama Rais wa Zanzibar. Lakini kama ni Rais au Rais ni sehemu moja ya Muungano, nafikiri anatakiwa aweke mahali ambapo anajulikana kwamba akiwa Rais hayupo wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, akiwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Basi Rais wa Zanzibar anashikilia hiyo nafasi. Lakini haionekani na inatutia hofu kwamba inawezekana pengine hawa viongozi wa juu wote inawezekana ikaja kutokea hawapo akaja akashika nchi Mkurugenzi wa Taasisi badala ya Rais wa Zanzibar. Mimi nafikiri hili Mheshimiwa Waziri uje utuweke wazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, labda nigusie masuala ya mazingira. Tunasema sana kuhusu mazingira na inasemwa sana kuhusu mazingira kwamba tunatunza mazingira, tunapanda miti, lakini mimi nafikiri hatukupiga tathmini nzuri ya upandaji wa miti tunaofanya na uharibifu wa mazingira ambao unafanywa. Je, kama tunapanda miti tunafanya *survival assessment* ya miti ambayo tumeipanda na kuangalia: Je, upandaji wa miti unauzidi uharifibu wa ukataji wa miti au wa mazingira? Sasa hilo nafikiri hatukuweza kuliweka sawa tukahisi kwamba labda pamoja na kwamba kuna sheria na inaonekana kwamba tatizo letu liko kwenye *enforcement* ya sheria, yaani kwa sababu tunapanda lakini tukishapanda hakuna ufuatiliaji, hakuna *monitoring*, hakuna chochote kinachofanyika, kwa hiyo, tunakuwa tumeiweka pale na hatimaye kwa sababu pia ushirikishaji wa watu, ushirikiaji wa jamii ni mdogo, kwa hiyo, inakuwa ile miti iliyopandwa pia utunzaji wake unakuwa haupo, na hatimaye kwa kweli miti ile inaharibika. Kama kweli tunafanya *survival assessment* kwa kila baada ya kipindi labda tungeweza kujua kwamba hii miti iliyopandwa, huu uhifadhi wa mazingira ambao tunaufanya kweli unakidhi haja au haukidhi haja, unalingana na nini?

Tanzania, sasa hivi inavyoonekana tupo katika hali mbaya ya kimazingira na unajua hakuna jambo ambalo halina kiashiria. Kiashiria cha uharibifu wa mazingira ni majanga. Majanga yamekuwa ni mengi, na kila mwaka ambalo linaendana sambamba na mazingira ni majanga ya njaa, majanga ya ukame. Sasa kama kweli tunatunza mazingira. Kama kweli tunahifadhi misitu yetu, kama kweli tunahifadhi mazingira yetu, nafikiri haya majanga yangekuwa yanaonekana kupungua. Lakini kila mwaka tuna ripoti za ukame, njaa, na hiyo nafikiri bado hatujaweza kuliangalia. Sasa mimi nafikiri tuliangalie. Kwa sababu tunaharibu mazingira, sasa kuna majanga mengine yashaashiria kutokea mfano, vipindi vingi vya nyuma tulikuwa tuna uzoefu tuseme wa tetemeko la ardhi katika maeneo ya miinuko, tuseme maeneo ya Kilimanjaro, Arusha, yale maeneo ambayo yana milima na *volcano*. Lakini ni juzi tu wiki kama tatu zilizopita tulisikia kama kumetokea tetemeko Dar es Salaam. Sasa hiyo ni ishara tosha ya kuona kwamba sasa *nature,* maumbile yanataka kutugeuka kwa sababu hatutii zile kanuni, sheria na taratibu za uhifadhi wa mazingira. *(Makofi)*

Sasa nafikiri Mheshimiwa Waziri tunahitaji tujipange ili tuhakikishe kwamba tunakasimu muda, tunakasimu madaraka, tunakasimu nini tunahifadhi mazingira. Tatizo moja kubwa ni kwamba hakuna ushirikishwaji, sisi au Serikali kama Serikali inajipanga kuhifadhi mazingira. Lakini: Je, wananchi, jamii inaelewa hii? Ni kuonyesha kuwa hakuna elimu ya kutosha ya uhifadhi wa mazingira na ndiyo sababu unapopanda mti, anatokea mchungaji, anaung'oa. Anatokea mchungaji analisha ng'ombe, anatokea mkulima anauchoma moto. Sasa hiyo ni kuonyesha kwamba hakuna elimu ya kutosha. Sasa nafikiri Serikali inatakiwa itenge hasa kwa makusudi pesa au kasima nyingi kubwa mno ya elimu ya mazingira kwa jamii. Nafikiri tukifanya hivyo, kwanza inawezekana tumetanguliza jambo mbele kabla ya kufanya lile ambalo linahitajika, nafikiri ilikuwa itangulie elimu kwanza halafu ndiyo tuanze *operation* nyingine. Lakini sasa tatizo tumefanya mengine bila kutoa elimu, sasa hiyo ndiyo inayotupelekea kwamba wengine wanafanya, wengine wanaharibu, sasa hilo nahisi kwamba tunatakiwa tulifanyie marekebisho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hayo machache, nashukuru. *(Makofi)*

**MHE. MESHACK J. OPULUKWA:** Mheshimiwa Spika, asante kwa kunipatia nami nafasi hii siku ya leo ili kuweza kuchangia ofisi ya Rais Makamu wa Rais Muungano, pamoja na Mazingira.

Mheshimiwa Spika, tangu kuanzishwa kwa taifa hili la Tanzania tumekuwa na matatizo mengi sana na hasa kutokana na muungano ambao baba wa taifa Mwalimu Nyerere pamoja na Rais wa Zanzibar wakati ule walipoanzisha kulikuwa na vitu vya msingi ambavyo nadhani vilikuwa vinaacha maswali mengi kuliko majibu. Na ndiyo maana mpaka leo hii suala la Muungano limekuwa ni kero sana kwa Watanzania, hii ni kwa Watanzania walioko Bara, pamoja na Watanzania walioko Kisiwani. Lakini ili kuweza kulimaliza hili na kwa sababu sasa tunaelekea kwenye mchakato wa katiba mpya, ili kuweza kumaliza matatizo ya Muungano yanayoikabili Tanganyika pamoja na Zanzibar ni wakati muafaka sasa wa kuwa na Serikali tatu, badala ya Serikali mbili kama ilivyo sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tutakapokuwa na Serikali tatu, Tanganyika Serikali yake, Zanzibar ikawa na Serikali yake *then* kukawa na Serikali ya Muungano haya yote tunayoyapigia kelele leo, masuala ya mafuta yanayopatikana Zanzibar, masuala ya umeme, *issue* ya *TANESCO*, masuala ya shule zetu, masuala ya kodi, haya yote yatakwisha kwa sababu yatashughulikiwa na nchi husika ama ni nchi ya Tanganyika au ni nchi ya Zanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda pia kuongelea suala la mazingira, mazingira yetu katika nchi yetu yanaharibika sana kwa sababu wananchi hawashirikishwi katika shughuli za maendeleo. Hawashirikishwi katika shughuli za maendeleo ya kiuchumi pamoja na kijamii. Napenda kulieleza hili kwa kutolea mfano, ukichukulia Mkoa wa Shinyanga ni Mkoa wa wafugaji. Lakini pia kuna wakulima wa mazao mbalimbali likiwemo zao la pamba. Sasa unakuta wananchi wao kila siku ni kuletea maelekezo kutoka juu, lakini siyo kutoka chini. Ukiangalia kwa mfano, katika maeneo yetu ya hifadhi za jamii, napenda kutolea mfano hifadhi mojawapo ya jamii iliyoko katika Wilaya ya Meatu, inaitwa hifadhi ya jamii ya Makao. Wananchi wa maeneo haya ni wafugaji, na kwa sababu ni wafugaji lakini unakuta bado Serikali inashindwa kukaa na hawa watu ili kuweza kupanga vizuri matumizi bora ya ardhi ili angalau kuepuka *damage* au mmomonyoko unaoweza kusababishwa na hawa watu kwa kushindwa kuzingatia hali halisi ya utunzaji wa mazingira yao.

Katika eneo hili ninalolizungumzia kwenye pori kwa mfano la hifadhi la Makao, wananchi wanahamishwa bila kushirikishwa. Sasa watakapokuwa wanahamishwa maana yake ni kwamba hawatakuwa na sababu yoyote ya kuweza kuanza kutunza mazingira yale kwa sababu wanajua ardhi siyo ya kwao. Lakini kwa sheria ya vijiji ya mwaka 1999 inayosema kwamba ardhi ni mali ya kijiji. Tunapoongea kijiji, maana yake tunaongea ni wananchi wale wenyewe wanaohusika, sasa wasipohusishwa maana yake ni kwamba hakuna hata mtu atakayediriki aidha kupanda mti, kama kuna mmomonyoko aidha

kuweza kuudhibiti. Kama kuna tatizo lolote kuweza kulifanyia kazi aina yoyote kwa sababu wanajua mali siyo ya kwao bali ni mali ya mtu fulani au ni mali ya Serikali.

Kwa hiyo, kuna haja kubwa ya kupitia hata Wizara ya Ardhi, ikishirikiana na Ofisi ya Makamu wa Rais kuweza kuwasaidia watu wetu ili kuweza kumilikishwa ardhi zao kimila, ili wajue umuhimu wa ardhi zao. Hili limeweza kufanyika katika maeneo machache, lakini basi liweze kuendelea na katika maeneo mengine ili angalau basi watu waweze kuona umuhimu wa kuwa maeneo ambayo wanaweza wakayatunza wakijua kwamba ni mali yao wenyewe.

Mheshimiwa Spika, lakini pia napenda kugusia kipengele kimoja cha *Airports* zetu. Tukiangalia mji wetu wa Dodoma hapa, *Airport* iko mjini, na hii *Airport* kuwa mjini ni kero kubwa kwa wakazi wa mji wa Dodoma ambao ndiyo Mji Mkuu wetu hapa. Tunasema *noise pollution.* Kunapokuwa na ndege zinatua mara kwa mara, hii *pollution* tunayoizungumzia siyo lazima iwe ni moshi, hata ile kero kuwabugudhi watu ambao wanaokuwa wamepumzika, lakini ndege zinapita nalo pia ni tatizo kubwa. Kwa hiyo, hizi *Airports* zetu, kwa mfano *Airport* tuliyonayo hapa ambayo zipo mjini sana iliyoko Musoma iko mjini sana. Basi ingefanyika utaratibu zikaweza kuhamishwa kuweza kusogezwa mbali na maeneo na makazi ya watu ili kuweza kuepukana na masuala ya *noise pollution.*

Mheshimiwa Spika, pia katika upande huo huo wa *Airports*, kuna *Airport* zetu zinajengwa mahali ambapo siyo vizuri zikajengwa. Kuna *Airport* moja inajengwa ndani ya pori la Makao Shinyanga, na hii *Airport* ina ukubwa unaokaribia kilomita tatu urefu. Nilipokwenda pale *TCAA* kuongea na Mkurugenzi Mkuu nikaambiwa hana taarifa ya ujenzi wa *airport* hii.

Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana ya mazingira, basi ni vizuri angalau uweze kufuatilia ujenzi wa *Airport* hii inayojengwa ndani ya hifadhi ya jamii, kule Shinyanga bila kushirikisha *TCAA*. Bila Wizara yako kuwa na taarifa, basi angalau mambo haya yaweze kuangaliwa kwa umakini kwa sababu bila kufanya hivyo, mazingira yetu yatazidi kuharibika kila siku na wa kulaumiwa ni sisi katika siku zijazo, kwa sababu watoto wetu, vijana wetu watatusuta kusema kwamba tuliharibu mazingira, lakini hatukuweza kuangalia wao wanafaidika vipi katika siku zinazokuja.

Napenda pia kuchangia kitu kimoja ambacho Watanzania wengi wamekuwa wakikilamikia. Kuna hii inaitwa *Environment Impact Assessment*, ambayo Ofisi ya Makamu wa Rais inashughulikia suala hili. Imekuwa ni kero kubwa sana kwa wawekezaji. *Environment Impact Assessment* inafanyika inachukua mpaka miaka miwili, mpaka miaka mitatu kuweza kuipata na matokeo yake hawa wawekezaji au mtu anayetaka kufanya shughuli katika eneo fulani anaamua kuanza kufanya shughuli ile hata kabla ya kupatikana kwa *Environment Impact Assessment* kwa sababu imekuwa ni tatizo na imekuwa ni kero kubwa.

Napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Mazingira Ofisi ya Makamu wa Rais, hili ameweza kulishughulikia kwa karibu sana. Hata zile kero ambazo tayari

zilikuwa zimeshaanza kuwakabili wananchi siku za nyuma, zimeanza kupungua angalau kwa sasa *Environment Impact Assessment* inaweza ikaanza kutoka ndani hata ya miezi sita. Siyo kipindi cha nyuma mpaka miaka mitano unafuatilia *Environmental Impact Assessment* kwenye Wizara inayohusika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kusema hayo, nisingependa kuchukua muda mrefu sana. Naomba kuwasilisha. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. RAJABU MBARUK:** Mheshimiwa Spika, ahsante na mimi kwa kunipa nafasi.

**SPIKA:** Sijui hiyo *machine* yako inapiga kelele, unaweza kutafuta nyingine.

**MHE. RAJABU MBARUK:** Mheshimiwa Spika, ahsante na mimi kwa kunipa nafasi niweze kuchangia hotuba hii ya bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira na Muungano. Kwa vile hii ni mara yangu ya kwanza kusimama katika Bunge hili kuchangia hotuba ya bajeti, kwanza nataka nitoe shukrani kwa wananchi na wanachama wa Chama cha Wananchi *CUF* wa Jimbo la Ole, kwa kunipa imani ili kuja kuzungumzia masuala yanayowahusu wao pamoja na Wazanzibari na Watanzania wote. *(Makofi)*

Vilevile nakishukuru Chama changu cha *CUF*, hususan Mwenyekiti wangu wa Kitaifa, Prof. Ibrahim Lipumba - Katibu Mkuu Maalim Seif Shariff Hamad, pamoja na uongozi mzima wa Chama kwa kuamua kwamba mimi kweli naweza kugombea na nikawa ni Mbunge ambaye naweza kuitetea nchi yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile nataka nitoe pongezi kwa timu ya vijana ya Kigoma ambayo mwaka huu imeweza kubeba kombe la Kopa *Coca - Cola*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa nataka niende moja kwa moja katika kuchangia hotuba au kuchangia bajeti hii. Kwanza nianze na suala la mazingira.

Mheshimiwa Spika, sisi sote tumezaliwa na dunia tumeikuta, na dunia tutaiacha na sisi sote tutakufa. Sasa tunapoondoka sisi ina maana kwamba wako wengine watakuja kukaa. Mwenyezi Mungu katujalia neema katuwekea nchi nzuri, sisi kwa bahati mbaya tumeichafua.

Leo tunaanza kuzungumzia suala zima la uhifadhi wa mazingira, mabadiliko ya tabia nchi. Kwa kweli lazima tukubali kwamba umefika wakati kama binadamu wa kawaida, basi tufanye kazi ya kuhifadhi mazingira ili vizazi vyetu vinavyokuja viweze kuishi vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Bara la Afrika ni tajiri sana, utajiri wake siyo wa pesa lakini ni wa muundo ambao Mwenyezi Mungu kaumba. Kuna ardhi nzuri, ina mimea, miti mingi, hali ya hewa ni nzuri lakini tumeingia katika mtihani. Uchafuzi wa mazingira umetuathiri katika Bara la Afrika, sasa hivi kuna wakimbizi karibu milioni 10 hususani kutoka katika Pembe ya Afrika ambao wamezikimbia nchi zao kwa sababu ya njaa, njaa

hii imetokana na uchafuzi wa mazingira, njaa hii imetokana na kukumbwa na janga. Sasa kama Watanzania tuna jukumu la kuwa tayari kukabiliana na hali hii. Unapoona mwenzako ananyolewa na wewe inabidi uanze kutia maji. Tatizo tulilonalo katika nchi yetu athari tunaziona na tumezisikia, hali kama hiyo ya wakimbizi ambayo sasa hivi wametimia takribani milioni 10 si wa kivita hao, bali ni wakimbizi ambao wanatokana na uchafuzi wa mazingira, hali hii inatisha. Serikali yetu bado haijataka kuwa *committed* na suala zima la mazingira.

Mheshimiwa Spika, Waziri kaeleza mengi, katangaza mengi mazuri, Msemaji wa Kambi ya Upinzani kazungumza vizuri, lakini kwa kweli Serikali yetu haijawa *committed* na suala zima la mazingira, hii inadhihirika katika bajeti. La kushangaza ni kwamba hali ya mazingira inazidi kubadilika, hali ya tabia nchi inazidi kutuathiri, mazao yetu yanazidi kupungua, njaa inazidi kutuelemea lakini bajeti yetu kila mwaka inazidi kuteremka. Hii ina maana kwamba Serikali haijawa *committed* katika suala zima la mazingira.

Mheshimiwa Spika, zaidi ya hapo, suala la mazingira ndani ya nchi yetu linaonekana haliko tu katika Ofisi ya Makamu wa Rais liko vilevile katika Wizara ya Kilimo na Mifugo. Sasa ili nisitumie muda mwingi, nataka nitoe ushauri. Namwomba Mheshimiwa Waziri aliangalie suala hili la mabadiliko ya tabianchi, baada ya kuliona kama ni suala la kimazingira tu lakini sasa hivi alione kama ni *National Agenda.* Tutakapolichukua suala hili kama ni *National Agenda* itakuwa kwa kweli tumejipanga vizuri, tusipange katika ulinzi wa kusubiri nchi nyingine kuja kutuvamia au maadui wengine kutuvamia, *no*! Hili suala la mabadiliko ya tabianchi ni hatari kuliko Jeshi la uvamizi. Kwa hiyo, naiomba Serikali ilichukue suala hili kama ni *National Agenda* sasa hivi, isilichukue tu kama ni kitu cha kawaida cha kimazingira. Duniani sasa hivi nchi nyingi zinalichukulia suala hili kama ni *global issue*, hawalichukulii tena kama ni suala la kawaida. Kwa hiyo na sisi Watanzania tufike mahali tukubali kwamba sasa hivi suala hili ni *global issue.*

Mheshimiwa Spika, vilevile namshauri Rais kwamba hii Idara ambayo inashughulikia suala la mazingira katika Wizara ya Kilimo liondolewe na lirudishwe katika Ofisi ya Makamu wa Rais ili waweze kufanya kazi pamoja. Kuna pesa nyingi zimetengwa ambazo ziko karibu milioni mia na zaidi katika Wizara ya Kilimo, kwa nini fedha hizi zisiondolewe zikaletwa katika Wizara ambayo inahusika na suala hili? Mimi nafikiri hizi Wizara mbili ziangalie ili zichanganye nguvu.

Mheshimiwa Spika, pia nakushukuru ulinipatia nafasi mwezi huu wa saba kwenda Nairobi kuhudhuria Mkutano au Kongamano la Wabunge wa Afrika lililozungumzia suala zima la tabianchi pamoja na mazingira. Tulijifunza mengi na tuna ushauri ambao tutaupeleka kwa Waziri lakini kwa sababu ya muda hatuwezi kuyazungumza yote.

Mheshimiwa Spika, pia nataka nizungumzie suala la Muungano, atakayependa apende na atakayechukia achukie na aliyekuwa hataki ndiyo hivyohivyo, Muungano bado ni kero. Kero za Muungano bado hazijatatuliwa, umri wangu ni miaka 47, Muungano una miaka 47, leo nasimama hapa, unasema anayesema mambo ya nini na nini namna gani?

Tunasema tunataka kero za Muungano zitatuliwe, sisi hilo ndiyo tunalozungumza lakini hatuzungumzii kuvunja Muungano wala hakuna Chama ambacho kiko tayari kuvunja Muungano. Sera ya Chama Cha *CUF* ni Serikali tatu, hii tumeizungumzia miaka 18 nyuma kwamba Sera ya Chama cha CUF ni Serikali tatu na bado hatujarudi nyuma na msimamo wetu ni huohuo na tutaendelea kubaki hapohapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nizungumzia suala la Mfuko wa Pamoja, Kamati imesema kwamba Mheshimiwa Waziri hili suala ameshalifanyia kazi. Kwa kweli sisi tulipeleka masuala mengi kwa Waziri Mkuu na Waziri Mkuu aliweza kutupatia jibu linaloonyesha kwamba huu mfuko kweli unakusudiwa kuendelezwa. Lengo letu la kutaka mfuko huu uendelezwe kwanza ni kuifanya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Serikali ya Muungano zinazoongozwa na Chama Tawala, Chama ambacho sasa hivi kimejivua gamba na hata kubadilisha jina sasa hivi wanakiita Chama cha Mungu, hongera! Hilo nawapa hongera, sasa sijui kama ni Mungu huyu tunayemuamini sote au yuko mwingine, *mashalah!* Tunasema kwamba Mfuko huu wa Pamoja tunauhitaji.

Mheshimiwa Spika, nataka nitoe mfano mdogo tu, Rais wa Jamhuri ya Muungano kabla hajawa Rais …

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUKU (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Mheshimiwa Spika, rafiki yangu Mheshimiwa anachangia vizuri sana lakini usajili wa Chama cha Mapinduzi umebaki kuwa Chama cha Mapinduzi, hakijabadilika na kitaendelea kuwa Chama cha Mapinduzi ingawa ni kweli ndicho kinachotawala Zanzibar na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Kwa hiyo, naomba asimfanyie Mungu utani hapa ndani, tafadhali!

**SPIKA:** Mheshimiwa endelea!

**MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, nakataa maelezo yake.

**T A A R I F A**

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Spika, taarifa!

**SPIKA:** Jamani mbona hatujatolea uamuzi, naomba ukae chini. Taarifa moja imetolewa, nikamwambia aendelee na mara nyingi tunapoteza muda, unajua ukiutumia muda wako vizuri huna tatizo. Kwa mfano alichokisema Mheshimiwa Mbunge akisema aah, nimesikia kisha akaendelea hakuna hata tatizo lakini sasa mtataka mueleze mpaka muingie kwenye matatizo bila sababu. Sasa nimemsikia Mheshimiwa Zitto, ni taarifa kuhusu nini?

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbunge aliyetoka kuzungumza hivi sasa tulikuwa naye Kigoma jana wakati Rais anazindua Daraja la Mto

Malagarasi na katika moja ya hotuba ambazo alikuwa anazungumza Waziri wa Ujenzi, Mheshimiwa John P. Magufuli alitamka kwamba Chama cha Mapinduzi ni Chama cha Mungu na ndiyo jambo ambalo Mheshimiwa Mbunge analizungumza. Sasa kwa sababu Mheshimiwa Lukuvi hakuwepo Kigoma hakusikia hiyo, ndiyo maana ametoa taarifa hiyo.

Mheshimiwa Spika, hiyo ndiyo taarifa yangu.

**SPIKA:** Siyo hivyo tu, ndiyo maana nimesema mkiwa hapa mpime mambo mengine yako ndani ya Katiba za Vyama au Nchi, hayo muyaache huko, haya ya kutaniana hapa mimi naona zote hizo ni taarifa.

**MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, ahsante na Mheshimiwa Zitto ahsante kwa kuweka sawa kwa sababu tulikuwa pamoja.

**SPIKA:** Unapoteza muda!

**MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, ahsante na sitaki nipoteze muda.

Kwa hiyo, tumesema kwamba huu Mfuko wa Pamoja, nataka kutoa mfano mdogo, Rais wakati ni Waziri wa Mambo ya Nchi za Nje alikwenda Korea Kusini, alikwenda kama ni *National Figure* ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, akaenda kuomba msaada kwa ajili ya Daraja la Mto Malagarasi, *fine,* lakini sasa fedha zile zimekuja kwa ajili ya Serikali ya Jamhuri au kwa lugha ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano, ilikuwa fedha zile ziingizwe kwanza katika Mfuko wa Pamoja wa Muungano *then* zijadiliwe, mimi nina hakika hakuna Mzanzibar atakayekataa kwamba fedha hizi sawa chukueni endelezeni daraja, lakini zimepita katika *process* ambayo tunahisi haiko sawa.

Mheshimiwa Spika, tunapozungumza suala la Ofisi ya Bunge Zanzibar, Ofisi ya Bunge kweli iko Zanzibar lakini haiko *active* kama ilivyo Ofisi ya Bunge Dar es Salaam au Dodoma. Tunataka na ile kule iwe *active*, Kamati zifanyike kule na ziwe zinafanya kazi zake, hilo ndiyo tunalolizungumza sisi na hilo ndiyo ambalo tunaliomba kila siku. Hili suala la kusema tumekwenda kuchukua *passport* ni sawa, inawezekana lakini tunachosema ni kwamba ile Ofisi tunataka iwe *active*.

Mheshimiwa Spika, kama hiyo haitoshi, tunapozungumzia suala la Ofisi ya Bunge, nataka uangalie katika kitabu ambacho kina majina ya Wabunge, angalia nafasi za kazi zote za Ofisi ya Bunge, ni Mzanzibar mmoja tu ambaye kaajiriwa anafanya kazi katika Bunge, ndiye tunayemuona hatumwoni mwingine. Sasa tunapozungumza hiki kitu tunakuwa tuna hoja kamili, hata sisi tunakuwa tunapungua nguvu. Kwa hiyo, hili tunaliomba hata ndani ya *management* ya Ofisi ya Bunge nalo liangaliwe.

Mheshimiwa Spika, kwa vile muda umekwenda mimi naomba nikomee hapo, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Kuhusu Ofisi Ndogo ya Bunge Zanzibar, Waheshimiwa Wabunge, kila Ofisi inafanya kazi kukiwa na shughuli zinazofanyika. Sasa hivi uamuzi uliotolewa na Serikali ni kwanza Ofisi yetu itasimamia ujenzi wa Ofisi za Wabunge nchi nzima. Sasa zile Ofisi ni lazima zipewe huduma yake. Sasa kama zitapewa huduma yake hata ile *CDCF* pia itakuwa inatokana na Ofisi ile ya Zanzibar. Kwa hiyo, ni lazima kuwe na Maafisa wa kutosha kufanya kazi hizo, wengi zaidi kuliko tulionao sasa na shughuli nyingine zote zitahamia Zanzibar.

Pia tunasema Kamati kama ikilazimika ambayo haichukui Watendaji wengi kutoka Ofisi za Serikali Bara, wengi watakwenda kule lakini kama utachukua Kamati ambayo Maafisa wanaotaka kuhudumia Kamati wanatoka huku wahamie kule hiyo itakuwa gharama sana. Aidha, tunasema Baraza la Wawakilishi kama wana shughuli zao, Ofisi ile pia wanaweza kuitumia, ndiyo tunachokisema na hilo haliko kwa Mawaziri liko kwangu mimi mwenyewe. Kwa hiyo, ndiyo hivyo ninavyokwambia kwamba Ofisi ile itaanza kufanya kazi kwa sababu kuna shughuli nyingi zitahamia sasa kule Zanzibar kwa hiyo, hilo lisikupe shida, tutalibadilisha.

Waheshimiwa Wabunge, nina tangazo moja tu, Katibu wa Wabunge wa CHADEMA, Mheshimiwa John Mnyika anaomba niwatangazie Waheshimiwa Wabunge wa CHADEMA kuwa kesho tarehe 7 saa 4.00 asubuhi kutakuwa na kikao kwenye ukumbi namba 231 jengo la utawala. Ni kesho saa nne asubuhi.

Kwa kuwa sina tangazo linguine, nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa kumi na moja jioni.

*(Saa 6.55 mchana Bunge lilisitishwa mpaka saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

*Mwenyekiti (Mhe. George B. Simbachawene) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na wachangiaji. Kwa jioni hii, tutaanza na Mheshimiwa Suleiman Nassib Omar na baadaye atafuatiwa na Mheshimiwa Ali Khamis Seif na wengine watafuata. Mheshimiwa Suleiman Nassib Omary, kama hayupo basi Mheshimiwa Ali Khamis Seif.

**MHE. ALI KHAMIS SEIF**: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kunijalia kupata nafasi hii ya kuweza kuchangia bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais. Pili, nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mazingira yana uhusiano mkubwa na maisha ya binadamu, kwa hivyo, kuna msisitizo wa pekee wa kuweza kuyahifadhi mazingira haya

ili binadamu pamoja na viumbe wengine tuweze kuishi salama hapa duniani. Nchi inaweza ikaagizia dawa kutoka nchi za nje, inaweza ikaagizia chakula kutoka nchi za nje, lakini nchi haiwezi ikaagizia hali ya hewa safi kutoka nchi za nje. Vilevile nchi haiwezi ikaagizia maji kwa ajili ya kilimo kutoka nchi za nje, kwa hivyo, ili upate hayo hapana budi Watanzania sote kwa ujumla wetu tufanye kila juhudi ili tuweze kuhifadhi mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, chombo ambacho kinahusika na kazi za kila siku za mazingira ni Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (*National Environment Management Council - NEMC)*. Chombo hiki kwa mara ya kwanza kimekuwepo katika nchi yetu mwaka 1983 ikiwa ni utekelezaji wa Agizo la Stockholm; Mji Mkuu wa Sweden lililozitaka Serikali ziweze kuzipa nguvu Taasisi ambazo zinashughulikia mambo ya mazingira. Baraza hilo limekuwepo hapo kutokana na Sheria Na. 19 ya mwaka 1983, lakini Baraza limekuwa na harakati zinazokubalika kuanzia mwaka 2004 ambapo kulitungwa Sheria Na, 20 ya mwaka 2004 na hapo Baraza badala ya kuwa kama wakati ambapo lilikuwa linashauri tu sasa likawa ndiyo wasimamizi wakubwa wa mazingira hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado nina imani kuwa Baraza la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira, lina upungufu mkubwa wa rasilimali watu na pengine hata fedha. Baraza lilianza na wafanyakazi sita (6) mwaka 1983, hivi sasa lina wafanyakazi karibu 150 ambao kati ya hao Wataalam wa Mazingira ni 86. Kwa kweli kwa ukubwa wa nchi yetu hawa ni wafanyakazi wachache mno, kwa hivyo hapo Serikali waone kuwa bado hawajajipanga vizuri katika suala zima la usimamizi wa mazingira. Naelewa kuwa juhudi zimeanzishwa za kuweza kutafuta Waratibu wa Mazingira katika Halmashauri na hivi sasa Halmashauri 132 tayari zimeshapata hawa Waratibu wa Mazingira, lakini hawa hawana lolote katika Halmashauri za Wilaya, kwa sababu hawana kasma, hivyo, ina maana wanakwenda ofisini na kurudi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema Wataalam ni 89, lakini bado Baraza linataka kujitanua, lina Kanda tatu sasa na baadaye liwe na Kanda saba (7). Kwa hiyo, kwa vyovyote Baraza hili kwa sababu kigezo pekee cha kuona utekelezaji wake ni kuona linaleta ufanisi wa mazingira nchini kwetu, bado uwezo wake nahisi ni mdogo na hivyo kuwepo haja ya Serikali kuliwezesha baraza hili kwa rasilimali watu na rasilimali fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiangalia miradi ya maendeleo ya Baraza pamoja na Idara ya Mazingira kwa mwaka 2011/2012 ni miradi tisa (9), ingawaje ndiyo utaratibu uleule wa miradi yetu kwamba inategemea zaidi fedha kutoka nje, lakini kwa kweli itabidi Mheshimiwa Waziri anifahamishe atakapohitimisha hoja yake, kuna miradi ambayo inachukua miaka mingi kuanzishwa, kwa mfano kuna miradi minne (4) ambayo imeanza mwaka 2009/2010, 2010/2011, huikuti katika miradi hii tisa (9). Kuna mradi wa kuwahamasisha wananchi waweze kupanda miti ili kupunguza gesi mkaa (*carbon dioxide*) au kwa ufupi kuna mradi wanaita (MKUHUMI).

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi huu Serikali ya Norway iliisaidia Tanzania dola (US$) milioni 100 na mradi huu ni wa miaka mitano (5). Kwa hiyo, tunaposema ni mradi

wa miaka mitano ina maana mradi huu utamazilika katika mwaka 2013/2014 lakini utashangaa kwa mradi huu katika miradi ile tisa (9) haumo. Sasa sisi kama wafuatiliaji wa shughuli za Kiserikali sijui tutauona wapi katika matumizi yake. Ukichukua wastani wa miaka mitano ina maana kila mwaka ni dola karibu milioni 20. Ugawaji hasa wa miradi utategemea wanavyopanga wao, lakini ukichukua wastani ni dola milioni 20, ina maana hizi ni Tsh. bilioni 30 lakini ukiangalia miradi yote ile Tisa(9) niliyoisema ya Serikali jumla ya fedha ambazo watatumia ni Tsh. bilioni kumi na mbili na milioni mia nne na kitu (12,400,000,000).

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa huu mradi mmoja ambao unaendelea kwa miaka mitano umefikisha Tsh, bilioni 30 kwa hivyo ningependa kuoneshwa hili suala la mradi huu wa MKUHUMI tutalipata wapi katika bajeti hii? Nafahamu umetajwa katika maelezo ya Mheshimiwa Waziri lakini tunapokwenda katika vitabu vya maendeleo, katika randama ya Wizara hii hukuti mradi huu. Kwa hivyo, wapi tutapata mradi huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili kuna mpango wa kuhimili mabadiliko ya tabia nchi. Nchi ya Japan ilitoa Tsh. bilioni 4.6 huu ni mradi wa miaka miwili, mwaka ulioisha wa 2010/2011 na huu tunaokwenda nao wa 2011/2012 hapa vilevile kuna karibu Tsh.bilioni 2.3 kwa mwaka huu ambazo huwezi ukaziona kokote, huzioni katika mpango wa maendeleo katika ile miradi tisa (9) niliyoitaja wala popote, kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri aje atufahamishe hizi fedha tutazipata wapi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kuna mradi wa kuhimili tabianchi ambao *European Union (EU)* wametoa Euro milioni 2.2 ambazo ni sawasawa na Tsh.bilioni 3.8. Huu vilevile ni mradi wa miezi 72 au miaka sita kwa hiyo ina maana ulianza mwaka 2010/2011 kwa hiyo uendelee zaidi.

Mheshimiwa Mweyekiti, mradi wa nne ambao sijaukuta katika Randama na katika Kitabu cha Maendeleo, Vol. IV, ni mradi wa matumizi bora ya ardhi. Mfuko wa Mazingira wa Dunia hapa walitoa dola milioni 26 ambazo ni sawasawa na fedha ya Tanzania Tsh.bilioni 36.5 huu ni mradi wa miaka minne (4) na huu vilevile huukuti mahali popote. Kwa hiyo, karibu shilingi bilioni 41.6 za miradi ambayo imeanza miaka iliyopita na inatakiwa iendelee kwa miaka hii huzikuti popote, badala yake Wizara miradi waliyo nayo yote ni Tsh. Bilioni 12. Kwa hiyo, nataka Mheshimiwa Waziri atakapokuja hapa aweze kutufahamisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, misitu ina uhusiano mkubwa na kuhuisha mazingira. Asilimia 92 ya nishati ya kupikia hapa nchini iwe ni mkaa au kuni, inatokana na suala zima la misitu na ni muda mrefu kwa kweli Wabunge tunasema itafutwe nishati mbadala. Umeme haiwezekani kwa sababu itachukua muda mrefu kwani hivi sasa ni 14% tu tena kwa mgao kwa hiyo hilo si suala la kusema ni nishati mbadala. Vilevile gesi asilia si rahisi kwa wakati huu. Wizara hii katika bajeti zilizopita ilisema kwamba wanajaribu kuona uwezekano kwa kushirikiana na Taasisi binafsi kutafuta nishati mbadala kutokana na makaa ya mawe. Hata bajeti ya mwaka 2010/2011 Wizara ilituambia kuwa kwa kushirikiana na Tume ya Sayansi na Teknolojia *(COSTECH)* wanafanya utafiti juu ya suala zima la utumiaji wa mkaa wa mawe. Kwa ripoti ya mwaka 2010/2011, Wizara

walisema kuwa imeonekana katika makaa ya mawe kuna gesi ya *sulphur dioxide* ambayo ina madhara kwa binadamu, lakini mwaka huu Wizara imenyamaza kimya sijui wamefikia wapi kwa kweli? Matokeo yake tunawatesa sana wananchi, watu wa maliasili wanapomkuta mtu ana gunia moja tu la mkaa wanamtia katika mashaka, wananchi wafanyeje sasa? Haiwezekani maadam hakuna nishati mbadala ambayo ni rahisi na tena itawafikia wengi, halafu leo tuwaadhibu watu ambao wanachoma mkaa na mkaa ndiyo kama tulivyokwishasema ni karibu 92% ya nishati ambayo tunatumia kupikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo ni sehemu moja kuu ya uchumi katika nchi yetu. Kwa mwaka huu wa 2010 asilimia 24.1 ya pato la Taifa imetokana na kilimo, lakini vilevile katika kilimo kuna uharibifu mkubwa wa mazingira. Hapa nchini kuna karibu wakulima wadogowadogo milioni tano ambao wamesambaa nchini nzima, hawa wanatumia mbolea za chumvichumvi na wakati mwingine Maafisa Ugani hawapo, kwa hivyo, kuna maeneo ambayo sasa hivi bila kutumia mbolea basi mazao hayapatikani, hasa katika maeneo ya Nyanda za Juu Kusini, sehemu za Mbeya huko. Sioni mradi wowote ambao wameuweka katika kuhuisha ardhi ile, hivyo nataka kujua Serikali wana mpango gani katika hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ufugaji vilevile unachangia kwa kiasi kikubwa katika uharibifu wa mazingira. Mimi siwalaumu wafugaji kwa kweli, bado nailaumu Serikali kwa sababu Sheria ya Mifugo ilipitishwa na Bunge la Tisa lakini inaweza ikachukua miaka minne au mitano haitumiki kwa sababu haina kanuni, lakini Sheria ya Gharama za Uchaguzi kwa kweli sijui...

*(Hapa kengele ya ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. ALI KHAMIS SEIF**: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante! *(Makofi).*

**MHE. WARIDE BAKARI JABU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na mimi kunipa fursa hii ili niwe mmojawapo wa wachangiaji wa hoja iliyopo mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, napenda kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema aliyenijalia nami kuwa mzima na mwenye afya tele. Pia napenda kumshukuru Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano) kwa uwasilishaji wake mzuri wa hoja yetu hii leo asubuhi, hotuba ambayo ameielezea vizuri na iliyojaa mwelekeo mzuri kwa masuala yetu ya Muungano na Mazingira. Napenda pia kumpongeza Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira) kwa utekelezaji wake mzuri wa kazi. Pia nawashukuru Watendaji wote wa Ofisi ya Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia nichukue fursa hii kuwashukuru wapigakura wangu wa Jimbo la Kiembe Samaki, walioniwezesha kwa kunichagua kwa wingi na pia kukichagua Chama cha Mapinduzi (CCM), kwa hivyo ninawaambia ahsanteni sana na hongera sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi kwa kweli nataka kwanza niuzungumzie Muungano. Nafikiri kumekuwa na kero kubwa au kelele nyingi za watu kuhusiana na kero za Muungano, lakini mimi binafsi napenda kusema kuwa Muungano tunautaka na tunaomba uendelee kuwepo na udumu milele na milele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kinachogomba au kuleta tatizo kidogo katika Muungano ni kutokuwepo uwazi ndani ya Muungano. Kwa kweli tunashukuru Viongozi wetu Wakuu wa Muungano, Waziri Mkuu pamoja na Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar kwa vikao vyao vya Muungano ambavyo wanakaa mara kwa mara, lakini hapa kinachotokea baada ya kukaa, kuzungumza masuala ya ya Muungano watu wengi wanakuwa hawana habari kuhusiana na kitu gani kimezungumzwa au kujadiliwa katika Muungano, hilo ndiyo linakuwa tatizo. Kwa hivyo, tunaomba wale wote ambao wanashughulikia masuala ya Muungano wawe tayari kuwaelimisha au kuwaeleza wananchi ni kitu gani kimezungumzwa, kimejadiliwa katika masuala mazima ya Muungano. Suala la Muungano lipo kwa muda mrefu na tunawashukuru Waasisi wa Muungano huu kwa kweli, sisi Wabunge leo hii tumo humu ndani, tunaringa kwa sababu ya Muungano na bila ya Muungano nafikiri hata tusingekuwepo. Kwa hiyo, tunashukuru kwa kuwepo Muungano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo lingine la Muungano ninaloliona mimi ni vile vitu ambavyo vinazungumzwa kila siku. Kwa mfano, Wazanzibari wanalalamika kuhusiana na *TRA*, tunaambiwa hapa kuwa hili limeshatafutiwa ufumbuzi, lakini *reality* unapokwenda hasa kwa wale wafanyabiashara wadogowadogo wanapofika *Custom* mtu amechukua *TV* moja au baiskeli tena ya *second hand* anaambiwa alipie ushuru, sasa wale kwa kweli ndiyo wanaokuwa wanaumia. Kama tungekuwa tunaelezwa kama tulivyoelezwa leo kwamba haya yanayotokea mtu anayefanya hivyo achukuliwe hatua, kwa kweli kungekuwa hakuna malalamiko katika suala zima la *TRA* au sehemu za Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia kuna sehemu ambayo napenda kuizungumzia nayo ni kuhusiana na Elimu ya Juu. Watu wanapata mikopo ya elimu ya juu, lakini ukiuliza ni Wazanzibari wangapi wanaofaidika na mikopo ya elimu ya juu, hutaelewa au kupata ile *figure* halisi. Pia ni asilimia ngapi tunayopangiwa kama Zanzibar kwa ajili ya Mfuko wa Elimu ya Juu pia tunakuwa hatuelewi. Kwa hiyo, vitu kama hivyo vidogovidogo ndiyo vinavyoleta kero kubwa katika Muungano wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna masuala ya nafasi za nje kama sehemu ya Ubalozi. Tunaomba na sisi zile nafasi ambazo tayari walikuwa wanashikilia Wazanzibari, tuendelee kupewa hizo *posts* kwani naamini Wazanzibari tuna uwezo wa kuiwakilisha Tanzania kama Wazanzibari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi kwa kweli suala la Muungano napenda nilizungumzie hapo kidogo, lakini pia nataka kuzungumzia suala lingine kuhusiana na Mazingira. Masuala ya Mazingira siyo ya Muungano, lakini tunapokuja Kitaifa tunaambiwa ni Tanzania. Hii inatokana na nini? Ukisoma *documents* nyingi zinazoandikwa na hasa sisi wenyewe Watanzania, Zanzibar kwenye suala la Mazingira

tunaishirikisha kidogo sana. Mimi mwenyewe nitatoa mfano, nimepitia programu moja hii inaitwa *NAPA* (*National Adaptation Programme of Action)* hii kwa kweli ukiitazama kwa undani wake au ukiipima huwezi kukuta hata *portion* moja inayosema kitu gani cha mazingira kwa sehemu ya Zanzibar. Kwa kweli inasikitisha na kama ipo naomba Mheshimiwa Waziri atueleze kwa nini katika mipango hii ya Kitaifa Wazanzibar hatushirikishwi. Zanzibar jamani ni Kisiwa, tena Kisiwa tete, tufikirie Wabunge Kisiwa cha Zanzibar kimo katikati ya bahari. Kipo kwa kweli, ni Kisiwa tete kwa masuala yote ya mazingira na masuala hasa ya maafa. Kwa hivyo tusiposhirikishwa katika mipango madhubuti ya kuweza kukabiliana na matatizo ya mazingira duniani itakuwa kwa kweli mnatutenga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hivyo tunaomba sana kama Zanzibar muweze kutuingiza katika mipango hiyo. Nina wasiwsi sasa hivi Tanzania tunatengeneza Mpango Mkakati wa Tabianchi tunaita *Climate Change Strategy.* Sijui kama kwa kweli Wazanzibar tumeshirikishwa katika mpango huo. Namwomba sana Waziri, kama hatujashirikishwa Zanzibar katika kupanga mipango jinsi gani tutakabiliana na tatizo la *climate change* na Zanzibar jamani *is a part of United Republic of Tanzania*, tunaomba na sisi tuwe *included* tuweze kukaa pamoja katika mambo haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi nataka kuongelea suala moja ambalo nafikiria linajitokeza kwa sasa suala jipya la uchafuzi wa mazingira unaotokana na bidhaa chakavu za umeme au *electronic.* Nafikiria Watanzania wengi bado suala hili hatujalipa kipaumbele na hatujalitazama kwa upana wake. Jamani vifaa vya *electronics* bidhaa hizi kwa mfano *TV*, Redio, Majokofu na vitu vinavyofanana na hivyo imekuwa vinaingizwa sana nchini kwetu. Ukiangalia *containers* zinazoingia vitu hivyo ni *second hands* za vifaa hivyo, lakini ni nini. Vifaa hivyo vinatengenezewa *chemicals* za sumu tena sumu kali na sumu hiyo ni mbaya sana kwenye athari ya binadamu lakini pia katika mazingira yetu. Wenzetu sasa hivi duniani wanafanya nini? Takribani nchi nyingi duniani sasa hivi wana mkakati kabambe wa kukabiliana na tatizo hili la uchafuzi wa mazingira kwa kutumia vyombo vya *electronics.* Leo nilikuwa nasikiliza kwa makini hapa hotuba ya Mheshimiwa Waziri sikuona mkakati gani kama Watanzania tuliouweka wa kukabiliana na tatizo hili la uchafuzi wa mazingira kwa kutumia hizi bidhaa zetu za umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi kwa kweli leo sikutaka kuchangia mengi, *point* zangu ni hizo chache zaidi ya hayo nasema naunga mkono hoja kwa asilimia mia ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waride Jabu, sasa nitamwita Mheshimiwa Regina Mtema na baadaye Mheshimiwa Sylvester Mabumba ajiandae na baadaye Mheshimiwa Halima Mdee.

**MHE. REGIA E. MTEMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi lakini kwenye karatasi yako pameandikwa Regia Mtema na sio Regina Mtema.

**MWENYEKITI:** Sawasawa Mheshimiwa, ni Regia Mtema.

**MHE. REGIA E. MTEMA**: *Yes!*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kupata nafasi ya kuchangia bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira pamoja na Muungano kwa kipindi hiki cha mwaka 2011/2012. Awali ya yote, nipende kuendelea kuwashukuru wananchi wa Kilombero kwa kuwa wanaendelea kuniunga mkono harakati ninazozifanya ndani na nje ya Bunge, nawashukuru sana. Vilevile nichukue fursa hii kuomba radhi baadhi ya maeneo ya Wilaya hiyo ya Kilombero ambayo mpaka hivi leo sijafika kufanya ziara ya shukrani baada ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka jana. Natambua kwamba ni wajibu wangu kufika kwa ajili ya kutoa shukrani kwa kuwa mlikuwa pamoja nami, lakini ninawaahidi nitafika. Nimejitahidi nimeshafika Kata 11 zimebaki Kata 12, katika Kata 23 za Wilaya ya Kilombero. Kwa hivyo, ndugu zangu wa Kata za Idete, Mofu, Mngeta, Mchombe, Chita, Uchindile, Mlimba, Tanganyika Masagati pamoja na Sanje, nawaahidi kwamba nitafika huko kwa ajili ya kuwashukuru. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba sasa niingie kwenye kuchangia hoja iliyoko mezani. Mimi nitajikita kwenye eneo moja tu la mazingira sitazungumzia chochote kuhusu Muungano kwa sababu sifahamu kwa undani kuhusu Muungano. Niungane na Mjumbe aliyepita kutoka Chama cha Mapinduzi amesema wazi kwamba suala la Muungano Watanzania wengi hatulifahamu vizuri nami ni mmojawapo, silifahamu vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mazingira sote tunatambua kwamba ni suala mtambuka na hivyo karibu sekta zote au Idara zote tunapozungumzia mazingira na yenyewe maeneo hayo yanaguswa kwa kuwa ni suala ambalo haliepukiki kwenye kila eneo tunapojadili mambo ya mazingira. Ninayo mambo kadhaa ya kujadili au ya kuchangia kuhusu hotuba yetu ili Serikali iyachukue na kuyafanyia kazi kwa lengo la kuboresha Taifa letu la Tanzania. La kwanza nitazungumzia uchafuzi wa mazingira unaofanywa na Makampuni makubwa kwenye sekta ya madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimependa kuzungumzia suala hili kwa kuwa mimi ni Waziri Kivuli wa Kazi na Ajira na hapa nitawalenga wafanyakazi. Sote tunatambua watafiti mbalimbali wamefanya tafiti zao, sote tumeshasikia taarifa na ripoti ambazo zimetolewa na Kituo cha Haki za Binadamu ambazo zimezungumzia kwa undani kuhusiana na uchafuzi wa mazingira ambao unafanywa na Makampuni makubwa ya madini kama vile Barrick pamoja na *Geita Gold Mine.* Sote tunatambua kabisa kwamba Makampuni haya yanatumia sumu ya *cyanide* ambayo wafanyakazi wengi wanaathirika na sumu hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi karibuni nilizungumza na watafiti wa Kituo cha *Legal and Human Rights Centre* wameeleza kabisa walikuwa kule kwenye haya Makampuni mawili niliyoyazungumza, wafanyakazi wengi wa Makampuni haya wameathirika na sumu hii. Wengi hivi leo wana matatizo ya viuno, wana matatizo ya migongo, wana matatizo makubwa ya kiafya ambayo inatokana na sumu hii ya *cyanide* inawakuta wanapokuwa maeneo ya kazini. Makampuni haya wala hawayajali malalamiko ya wafanyakazi hawa na ukienda kwenye kiwanda hiki cha *Geita Gold Mine*

hawa wafanyakazi wadogowadogo wakijua kabisa kwamba kule ndani kuna hii hewa, kuna hii sumu lakini wanalazimishwa kula chakula wakiwa maeneo hayo, hawaruhusiwi kwenda kula chakula nje ya maeneo wakati wenyewe Wazungu, wafanyakazi wakubwa hawali kwenye maeneo hayo kwa kuwa wanajua kabisa kile chakula kinakuwa *contaminated.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *NEMC* ina taarifa, Wizara husika ina taarifa lakini bado Serikali yetu imekaa kimya kwa kuwa matatizo haya hayajaanza kusemwa leo wala sio ya jana ni ya kipindi kirefu, umefika wakati sasa Serikali ichukue hatua. Serikali tuache urasimu, watu wanaangamia, watu wanakufa kwa sumu, tunakwenda polepole, tumekaa kimya wakati Watanzania wenzetu ambao wanafanya kazi nzito wamejitolea kule, Serikali hatuchukui hatua zinazotakiwa kuchukuliwa. Tunapokwenda ni pabaya. Hawa ni Watanzania wenzetu wana haki kabisa ya kusikilizwa, wamepata madhara na ripoti hizohizo za wenzetu Kituo hiki cha Haki za Binadamu zinaonyesha kwamba hawa waajiri wa Makampuni haya wanapoona wafanyakazi hawa wameugua maana huwa wana kanuni ya kwenda kuwapima wakishaona wameshaanza kuathirika wanawapa likizo za ugonjwa halafu baadaye wanapunguzwa kazini. Hiki ni kinyume na haki za binadamu. Ni *toucher* ya kisaikolojia kwa wafanyakazi, hawa wameathirika wakiwa kazini wanapewa likizo ya kuumwa halafu wanapunguzwa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lazima sasa Serikali ichukue hatua angalau basi kwa mara moja itoe tamko, iwajibike, ifanye kazi ya kutosha ili wafanyakazi hawa wapate haki zao. Kuna wengine wamepoteza maisha, tunaomba Serikali iifanyie kazi ya kutosha Makampuni haya, sheria ichukue mkondo wake, tumeshaambiwa kwamba hizi ni sumu lazima Serikali au *NEMC* pamoja na Wizara husika isimamie sheria zilizopo ili waajiri hawa watimize wajibu wao wafuate sheria kadri zinavyozungumzwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ningependa kuzungumza ni suala zima la uchafuzi wa maji. Imekuwa ni aibu karibu kila mwaka tunasikia taarifa Jiji la Dar es Salaam linapata magonjwa ya kipindupindu (*water born disease*) ni aibu kwa Taifa la Tanzania. Jiji kama Dar es Salaam, Jiji kubwa ambalo linatambulika duniani kote eti limekuwa likiongoza kwa kupata ugonjwa wa kipindupindu, ni aibu. Lazima Serikali iwajibike, *NEMC* ifanye kazi yake vizuri, Wizara ya Mazingira ifanye kazi yake vizuri kwa kushirikiana na Halmashauri husika ili hii aibu ya Taifa letu la Tanzania, Jiji kubwa kama Dar es Salaam eti wananchi wake kupata ugonjwa kipindupindu ni lazima tutoke huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda vilevile kuzungumzia Wilaya yangu ya Kilombero. Hivi karibuni na bahati nzuri Waziri husika wa Mazingira yuko hapa na ameshapata habari katika Kata ya Mgeta kuna kiwanda pale cha KPL (*Kilombero Plantation Limited)* walinyunyuzia dawa kwa kutumia helikopta matokeo yake wakawa wameunguza mazao mengi ya wananchi wanaoishi maeneo hayo tangu Desemba, 2010 mpaka hivi leo wananchi hawa hawajalipwa chochote, hawajui watakula nini wana njaa. Wizara imepewa habari, barua mbalimbali zimeandikwa, vikao mbalimbali vimekaa, lakini inashangaza huu ni mwezi wa Juni na tumeshaingia mwezi Julai sasa Serikali bado haijafanyia kazi. Jamani Serikali ya Tanzania tujitahidi kubadilika angalau kidogo.

Mazao yao yameharibiwa, watu wamejitosa tumesema kwamba walime, wajitume wajiletee maendeleo, Kampuni imeenda imeharibu mazao yao mwezi wa sita sasa wananchi hawajapata haki yao, Serikali imekaa kimya, mnaendelea kutoa porojo, tunafanyia kazi, tuko kwenye mchakato, ifike wakati tufanye kwa vitendo sasa, tumechoka tunataka wananchi hawa wapate haki zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo napenda kulizungumza ni suala zima la uhifadhi wa mazingira v/s maisha ya wananchi. Wilayani kwetu Kilombero tumebahatika tuna Milima ya Udzungwa na TANAPA pale. Inasikitisha miti, wanyama wamekuwa ni bora kuliko Watanzania. Wanyama pamoja na miti pamoja na msitu ule inaonekana ina thamani kuliko maisha ya wakazi wanaoishi maeneo hayo. Leo hii wananchi wanaozungukwa na milima hii ya Udzungwa pale Kilombero wanazuiwa kuokota kuni, wanaambiwa kwamba mkiokota kuni mtaharibu mazingira. Wakati sote tunatambua kabisa wakazi wa Wilaya ya Kilombero zaidi ya asilimia 99 wanategemea kuni kama chanzo chao cha nishati. Habari za gesi hawazitambui, habari za umeme ni kizungumkuti, mtawakatazaje kuokota kuni? Leo hii wanakatazwa wananchi wataishije, watapataje nishati ya moto, watakula nini, ni lazima Serikali iangalie. Ni kweli tunatambua kuhifadhi mazingira ni muhimu lakini lazima tuendane na vipaumbele. Tunatambua kabisa tunahifadhi mazingira haya kwa ajili ya haohao wananchi lakini inapokuja suala la muhimu ambayo…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI**: Sijakusikia kama umeunga mkono hoja au? (*Kicheko)*

**MHE. REGIA E. MTEMA:** Duh! Kuunga mkono hoja itakuwa ngumu, nakushukuru Mheshimiwa Mwenyekiti.

**MWENYEKITI**: Ahsante. Basi anayefuatia sasa ni Mheshimiwa Sylvester Mabumba na Mheshimiwa Aliko Kibona naye ajiandae.

**MHE. SYLVESTER M. MABUMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii nami niweze kutoa mchango wangu katika hoja inayoendelea mbele yetu.

Awali ya yote, napenda kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya njema na kuniwezesha kusimama katika Bunge lako Tukufu. Pia niwapongeze Waheshimiwa Mawaziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais kwa mawasilisho mazuri ya hotuba zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, napenda sasa nielekeze michango yangu katika masuala ya Muungano. Nazipongeza sana Serikali zetu zote mbili kwa kuenzi Muungano wetu toka ulipoasisiwa mwaka 1964 hadi leo hii ukiwa imara na pia haujaweza kuyumbishwa na maadui wa ndani na nje. Muungano wetu wa nchi mbili yaani Tanzania Bara na Zanzibar umeweza kuwawezesha wananchi wa pande mbili kuwa na uhuru wa kuweza kuishi sehemu yoyote ndani ya Muungano wetu na pia

kuweza kufanya biashara yoyote ile halali ili kuweza kuboresha maisha yao na pia kuweza kukuza uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fursa hii inayotolewa na Muungano wetu nawaomba sana Watanzania wenzangu kuhakikisha kwamba tunatumia ipasavyo fursa hizi. Tusingekuwa tumeungana ingelikuwa taabu sana wananchi wa pande mbili kwenda sehemu moja katika Muungano wetu. Leo hii wananchi wa Tanzania Zanzibar wana uhuru wa kufanya biashara Tanzania Bara, wanafahamu kabisa Tanzania Bara ikiwa ni nchi yenye kuwa na idadi kubwa ya watu basi ina soko la uhakika. Wafanyabiashara nafasi hii nawasisitiza waitumie ipasavyo kwa ajili ya kuimarisha uchumi wao, kuimarisha uchumi wetu ndio jambo la msingi na kipaumbele ili tuweze kama wananchi kuchangia maendeleo ya nchi kupitia ulipaji wa kodi, Serikali yetu iweze kutoa huduma kwa watu wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia nizungumzie juu ya muundo wa Serikali mbili ambao nchi yetu imeridhia, Muundo huu umetuwezesha sisi kuweza kuwa wamoja toka mwaka 1964. Kwa sababu hata kile ambacho kinaitwa ni changamoto tumeweza kukaa kwa mapenzi makubwa kujadili kwa makini na kwa maelewano na kuweza kutafutia ufumbuzi wa hizi changamoto ambazo zimeainishwa na Waheshimiwa Mawaziri katika hotuba zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nishauri wachangiaji waliopita wakati wa asubuhi wengine walikuja na mawazo kwamba pengine ni wakati muafaka wa kuwa na Muungano wa Serikali tatu. Shirikisho la Serikali tatu haliwezi kusadia nchi yetu kwa sababu katika historia hatujaona mahali ambapo Muungano wa namna hii umeweza kufanikiwa. Mfano mzuri, Shirikisho la Yugoslavia limesambaratika, Shirikisho la Czechoslovakia limesambaratika pia, Shirikisho la Muungano wa Wasovieti nalo limesambaratika na hata hapa Afrika kulikuwa na Muungano kule Gambia na Senegal ilikuwa inaitwa nchi ya Senegambia nayo haikuweza kudumu ilisambaratika baada ya muda mfupi sana. Kwa vile muundo huu wa Serikali mbili ndiyo muafaka katika mazingira ya nchi yetu, kwanza hata uendeshaji wake inakuwa ni rahisi. Tunapotaka Shirikisho la Serikali tatu maana yake tunataka kuongeza gharama ambazo si za lazima na si za msingi na haziwezi kusaidia nchi yetu kuweza kuhudumia wananchi wetu. Kwa sababu tutaanza kuhangaikia kero za Shirikisho tutapoteza *focus* yetu. *Focus* yetu ni kuhakikisha kwamba wananchi wetu wanahudumiwa ipasavyo ili wapige hatua za kimaendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia nizungumzie kuhusu Zanzibar kama ni mshirika kwenye Muungano. Ndani ya Muungano wetu Zanzibar imepiga hatua kubwa sana za kiuchumi na kijamii. Katika sehemu ya kiuchumi leo hii kila mmoja atakubaliana na mimi kwamba Zanzibar ina miundombinu ya kisasa kabisa, barabara zake zote ni za kisasa. Zanzibar leo hii haina barabara ya vumbi, zote ni za lami. Haya ni matunda ndani ya Muungano wenye Serikali mbili. Zanzibar pia ina bandari nzuri za kisasa Unguja na Pemba pamoja na kwamba Zanzibar ina idadi ndogo ya watu milioni moja na laki mbili Zanzibar ina Vyuo Vikuu vitatu. Haya ni mafanikio makubwa ndani ya Muungano wetu. Mbali ya Vyuo Vikuu hivyo vitatu, Zanzibar ina taasisi za elimu ya juu tatu kama Chuo

cha Uongozi wa Fedha kule Chwaka, ina Chuo cha Afya kule Mbweni na ina Chuo cha Sayansi na Teknolojia cha Karume. Sasa ukiangalia baada ya muda mfupi jamii ya Wazanzibari itakuwa na jamii ya wasomi na wataalam.

Mheshimiwa Mwenyekiti haya yote ni mafanikio ndani ya muundo huu wa Serikali mbili. Kwa hiyo, naomba sana, Serikali zetu ziendelee kuelimisha wananchi wetu juu ya uzuri wa muundo huu hata itakapofika wakati wa mchakato wa kuandika Katiba mpya. Wananchi wetu tuwaongoze kufahamu faida na hasara za kuwa na Shirikisho la Serikali tatu, haitaweza kutusaidia. Wakati tutakapofika naomba sana Serikali zetu zitoe elimu ya kutosha juu ya uzuri wa muundo huu wa Serikali mbili. Kwa upande wa kijamii tunafahamu jamii ya Kimataifa, imeweka Malengo ya Milenia ambayo yanahitaji ifikapo mwaka 2015 watoto wote wenye umri wa kwenda shule wawe wameandikishwa, Zanzibar ilishapindukia hapo. Usajili wa watoto ni zaidi ya asilimia mia moja na tano, haya ni mafanikio. Lakini hata katika huduma za afya zinapatikana chini ya kilomita tatu kuna vituo vya afya ambavyo vinatoa huduma nzuri na vina wataalam, kinachotakiwa ni kuhakikisha wataalam hawa tunawaenzi kwa kuwapatia maslahi ya kutosha yaani mishahara yao, mazingira ya kazi yawe ni mazuri kwao ili wasije wakakimbilia nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile suala la umeme Zanzibar karibu wananchi zaidi ya asilimia 90 wanapata huduma ya umeme. Sasa Zanzibar ni mfano mzuri sana wa kuigwa katika mafanikio ambayo yamepatikana ndani ya Muungano wetu. Kwa hiyo, napongeza sana Serikali zetu mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Serikali hizi zinaendeshwa na wanadamu, changamoto haziwezi kukosekana, nashauri Serikali zetu mbili kwamba changamoto hizi ambazo zinatatiza maendeleo ya wananchi wetu basi kwa udugu Serikali zetu zikae kupitia Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais Zanzibar kuweza kujadili na maamuzi yanapotolewa basi vyombo vinavyohusika na utekelezaji viweze kutekeleza maamuzi ya vikao hivyo. Mfano wananchi na wafanyabiashara wanaotoka Zanzibar wanaotozwa kodi mara mbili hii ni changamoto ambayo tunahitaji kupatiwa ufumbuzi ili wafanyabiashara wetu waondokane na changamoto hiyo ambayo inasumbua. Lakini vile vile ajira katika taasisi za Muungano mfano Wizara ya Fedha na Uchumi ya Tanzania Bara ukiondoa Naibu Waziri katika ngazi ya utendaji nadhani kuna umuhimu wa kuwa na watalaam Wazanzibari ambao pia ni haki yao kupata ajira katika Wizara hii kwa ajili ya kuangalia maslahi zaidi ya Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia hata katika Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia ukiondosha Waziri nafikiri kuna umuhimu wa kuwa na watendaji wa kutoka Zanzibar na pia katika Balozi zetu tuangalie uwiano mzuri ambao wataalam kutoka Zanzibar waweze kupata ili kuweza kuwakilisha vizuri nchi yetu nchi za nje na kwa sababu msisitizo wa sasa ni kwamba tunahitaji Mabalozi wetu waweze ku-*advocate* zaidi masuala ya kiuchumi namna gani nchi yetu itaweza kunufaika kiuchumi. Wanapokuwa katika Balozi waweze ku-*attract* misaada zaidi kwa nchi yetu ili wananchi wetu waweze kusonga mbele na kuweza kuboresha ustawi wa maisha yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna kero moja ambayo haijazungumzwa sana lakini pia inasumbua. Naomba Wizara ya Mambo ya Ndani, kupitia Ofisi ya Makamu wa Rais izungumzie pia usumbufu huu unaopatikana kwamba ukiwa na leseni ya udereva wa gari, ukija Tanzania Bara haikubaliki. Vilevile ukiwa na leseni ya udereva kutoka Bara kule Zanzibar haikubaliki. Lakini utashangaa kwamba Polisi hawa wanakwenda Chuo kimoja cha *CCP* kule Moshi. Sasa kama wanakwenda sehemu moja na hawa ndiyo wanakufanyia *trial* kwa nini leo leseni hizi zisikubalike? Naomba leseni hizi zitambulike ili kuwaondolea usumbufu usiokuwa wa lazima wananchi wetu. Sisi ni wamoja na sisi ni ndugu. Leo hii nimesimama hapa nina asili ya Tanzania Bara lakini nawakilisha wananchi wa Jimbo la Dole ambao wamenipatia mamlaka ya kuweza kuwawakilisha kama Mbunge wao. Haya ni moja ya matunda ya Muungano wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii ukifika Kariakoo utakuta nyumba nyingi nzuri ni za wananchi wenye asili ya Zanzibar, ni matunda ya Muungano. Naomba Muungano wetu udumu na utadumu zaidi chini ya Chama cha Mapinduzi. Chama cha Mapinduzi kiendelee kutawala ili tuweze kufaidi haya yote. Hata hii *CDF* tunayopata…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. SYLVESTER M. MABUMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MHE. ALIKO N. KIBONA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili nipate kuchangia hotuba au mjadala uliopo mbele yetu siku ya leo. Napenda nichukue nafasi hii kushukuru Mawaziri wanaohusika, Waziri wa mambo ya Muungano na Waziri katika masuala ya Mazingira. Nawapa pongezi kwa kazi nzuri ambayo inaendelea kufanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya pongezi au shukrani zangu hizo nizungumzie moja kwa moja suala la mazingira. Mazingira ni kila kitu, ukiona kitu chochote ujue kimesababishwa. Kimesababishwa ama na wewe mwenyewe au yupo aliyekisababisha. Sisi wanadamu tuna uwezo wa kusababisha baadhi ya vitu. Hapa tulipo Bungeni yupo mtu aliyebuni, akafikiria, akapanga jinsi tulivyokaa, viti vilivyokaa na meza. Baadaye akafikiria akaona ni vema kila mmoja akikaa aweze kuzunguka kadiri anavyotaka, ilisababishwa. Vipo vitu ambavyo sisi wanadamu hatuwezi kusababisha kwa mfano, viumbe baharini na nchi kavu. Hivyo, vilisababishwa na Mwenyezi Mungu. Mwenyezi Mungu alimkabidhi kazi ya kwanza katika maandiko matakatifu ni kutunza mazingira. Alimuumba Adam akamweka kwenye bustani ya Eden akampa agizo akasema lima na kutunza bustani. Leo sisi tumekiuka agizo lile na kwa vyovyote tuliumbwa duniani kuendeleza uumbaji wa Mungu, tuupambe upambike uwe mahali salama pa kuishi viumbe vyake, sisi wenyewe na viumbe vilivyo hai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mazingira yetu yameharibiwa kwa sababu mbalimbali, kwa sababu ya ongezeko la watu. Kwa sababu ya shughuli za kibinadamu kama kilimo, viwanda, ujenzi wa makazi karibu na vyanzo vya maji na kwenye maliasili. Lakini

nilikuwa najiuliza na bado naamini kwamba tatizo lipo kwenye usimamizi wa Sheria zetu. Ukipita sehemu mbalimbali zile sehemu ambazo hapo zamani zilikuwa zimeachwa kwa ajili ya vyanzo vya maji sasa hivi zinalimwa mazao mbalimbali na mamlaka zilizokabidhiwa majukumu ya kuangalia mazingira na utawala kwa ujumla hakuna hatua zinazochukuliwa. Hapo kuna tatizo, tatizo la maadili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije kwenye zoezi la kupanda miti. Kabla sijawa Mbunge namkumbuka Mzee mmoja alikuwepo Bungeni nikiwa naangalia vipindi vya Bunge, bahati mbaya sasa hivi ni marehemu alikuwa anatoka Jimbo moja kule Kagera alikuwa anaitwa Fares Kabuye, Mungu amuweke mahali pema peponi. Siku ya kuchangia hotuba iliyohusiana na suala la mazingira nilimsikia akimwonya Waziri anayehusika na mambo ya mazingira wakati ule akiwa Mheshimiwa Mark Mwandosya. Alimwonya akisema: "Mwandosya tusidanganyane hapa kwamba tusikate miti. Miti iliyoumbwa na Mwenyezi Mungu, miti ya asili tutaachaje kukata?" Akasema "leo hii tukisema hapa Dodoma maaskari wakae upande ule na huku na huko hakuna gunia la mkaa kuingia hapa Dodoma, Mbunge gani atakaa hapa Dodoma? Akaendelea kusema Serikali ipande miti." Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeendelea kuishi huko bila kuwa Mbunge mpaka leo naingia Bungeni sijui sehemu zingine kule kwangu sijaona Serikali ikipanda miti kwa maana ya kuwa *serious* katika jambo hili. Miti iliyopandwa na Serikali kwa kawaida haiharibiwi, haikatwi hovyo. Sasa Serikali inasema tupande miti, nikipanda miti ikikua si ninakata na kuuza? Nadhani kwamba wahusika waliangalie wachukue maelezo haya machache waende wakakae wayapanue Serikali ipande miti na mimi kule kwangu Jimbo la Ileje kuna maeneo ya ukanda wa juu ambayo yanakuwa na mvua kwa miezi minane.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri anayehusika baada ya kipindi hiki au kesho asubuhi nitamwona mnipe hela nikaipe Halmashauri tufunike milima ile kwa miti. Hiyo itakuwa miti ya Serikali na haitaharibiwa. Lakini hii ya kusema pandeni miti, pandeni miti, nachelea kusema tunadanganyana. Lakini naomba iandikwe hivyo hivyo tunadanganyana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumze kidogo kuhusu Baraza la Usimamizi wa Mazingira. Hii ni ofisi, ni watu wachache na hawawezi kuangalia matatizo yanayotukabili kuhusiana na uharibifu wa mazingira. Nafikiri Baraza hili liende mpaka vijijini, lianze kwenye vitongoji liende kwenye Vijiji, kwenye Kata, kwenye Wilaya na hatimaye kwenye Mikoa. Kwa uzoefu wangu mara kadhaa shughuli zao zinaishia Wilayani, lakini Wilayani hakuna wapandaji wa mimi. Wananchi wengi wapo vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nashauri Baraza kuanzia sasa, nendeni Makanisani kama ni zile semina wahusisheni Maimamu na Wachungaji. Wale watu wanaheshimika, wanakubalika na watatusaidia katika utunzaji wa mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sipendi kuchukua muda mwingi kwa ajili ya wenzangu, naomba niseme kidogo sana kuhusu Muungano. Naona watu wameongea kwa ukali na kwa uchungu kana kwamba kuna jambo ambalo limembana mguu kwenye

kidole. Wanasema ukikanyagwa sema nimekanyagwa, lakini sidhani kwamba Zanzibar au Tanzania Bara kuna yeyote ambaye amekanyagwa na kuna haja ya kulalamika kiasi hicho. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, dada zangu wameolewa huko, kutoka kule Ileje na mmoja wa Wabunge wenzangu kutoka Zanzibar ni shemeji yangu, wapo dada zangu wengi kule Zanzibar, wapo ndugu zetu akina Mwakanjuki kutoka Mbeya wako Zanzibar, leo nikienda Zanzibar siyo mgeni, tuuenzi Muungano wetu, tuulee Muungano wetu. Matatizo hayawezi kukosekana, tumuunge mkono Rais Jakaya Mrisho Kikwete kwa juhudi ambazo amezianzisha na anazoziendeleza katika awamu hii hatujasikia chokochoko kubwa za Muungano na kule Zanzibar Mungu amejalia kumetulia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Aliko Kibona kwa mchango mzuri, sasa nitamwita Mheshimiwa Sadifa Juma Khamis na baadaye Mheshimiwa Kombo Khamis Kombo na Mheshimiwa Nasib Suleiman Omar wajiandae.

**MHE. SADIFA JUMA KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti ahsante sana kwa kunipatia nafasi ili nami niweze kutoa mchango wangu katika Wizara hii ya Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu *Subhanah Wataala*, muumba wa mbingu na ardhi na kila kilichomo ndani yake, lakini pili nichukue nafasi hii tena kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha mimi binafsi kufika Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ni mara yangu ya kwanza kuchangia hapa, nichukue nafasi hii kuwashukuru wananchi wangu wa Jimbo la Donge, Jimbo dume, dume la mbegu iliyopandwa na CCM. Baada ya hapo niwashukuru na niwapongeze wananchi wangu kwa kutumia haki yao ya msingi ya kidemokrasia na ya kisheria Kifungu namba 14 cha Katiba ya Chama cha Mapinduzi lakini pia kule Zanzibar kifungu namba 68 cha Katiba ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, kuweza kutumia haki yao ya msingi kunichagua mimi kuwa Mbunge wa Bunge hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inaonekana kwamba wamenionesha imani yao kubwa kwangu, nasema hivyo kwa sababu sikuwa na uwezo wa aina yoyote kuweza kufika hapa, siri ya Ubunge huu, mimi nilikuwa nakuna nazi na kukanda unga kule majumbani ndiyo maana akinamama wakanichagua. Kwa hiyo, nimefarijika sana leo kuwa Mbunge wa Jimbo la Donge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakuwa mwizi wa fadhila kama sikumpongeza Spika, kwa kuchaguliwa kuwa Spika mwanamke pekee ndani ya Bunge hili katika historia yetu ya Tanzania, lakini vile vile nichukue nafasi hii tena kumpongeza Makamu wa Rais Dokta Mohamed Gharib Bilal na Mheshimiwa Kikwete kwa kuchaguliwa kwa kishindo ushindi usiokuwa na shaka ndani yake kuongoza Taifa hili. Vile vile niwapongeze

Mawaziri kwa kuchaguliwa kwao kuwa Mawaziri lakini na Wabunge wenzangu kwa kuchaguliwa kuwa Wabunge wa Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mara nyingine nawapongeza Waasisi wa Muungano, Hayati Abeid Amani Karume na Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, kwa kuona umuhimu kwamba imefikia wakati kwa wakati ule kwamba Tanganyika na Zanzibar ni lazima waungane, ni kweli hata mimi naunga mkono zoezi hili, kwamba ilifikia wakati ni lazima waunganishe nchi zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, toka Tanganyika na Zanzibar ziungane kuitwa Tanzania kumekuwa na faida nyingi katika Muungano kwa mfano, suala la umoja na mshikamano wa Taifa letu, ni ukweli usiopingika kusema kwamba kama sikupitia huu Muungano wetu basi umoja na mshikamano wa Taifa letu usingepatikana, lakini suala lingine pia kumekuwa na *sustainable peace and security* ndani ya Taifa letu. Ni ukweli usiopingika kusema kwamba kwa wakati ule ilikuwa lazima tufikie wakati tuungane.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania toka imeungana kumekuwepo na uhakika wa usalama wetu, kwa mfano, kupitia Wizara ya Ulinzi, bahati nzuri mimi nimetokea Zanzibar, najaribu kusema kwamba kupitia Wizara hii ya Ulinzi Zanzibar kumekuwa na uhakika wa *peace and security* kwa upande wetu sisi Zanzibar. Kama tungeachiwa sisi wenyewe tu ukweli ni kwamba Zanzibar kungekuwa na amani lakini siyo kama hii iliyopo sasa. Mifano hai ipo kuanzia miaka ya 2000, 2005 mpaka hapa tulipofikia sasa. Kwa hiyo, nasema kwamba faida zipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini suala lingine ni demokrasia, kuwepo kwa Muungano huu kumesaidia kukua kwa demokrasia, nazungumza hivyo kwa mfano, kihistoria Zanzibar haijawahi kuwa na Mbunge hata siku moja mwenye umri mdogo kama wangu kutokea Jimboni, ndiyo mimi peke yangu nimepata Ubunge kupitia Jimbo, Zanzibar, nilijifunza kwa Mheshimiwa Zitto Kabwe, nina miaka 29, hata nilipokuwa nagombea kule Wazee walisema hivi wewe kweli utaweza kutuwakilisha Bungeni kweli na wengine wakasema asipewe kwa sababu ni mdogo. Lakini sasa kutokana na kile ninachokizungumzia kwamba watu wamesoma kutokana na Muungano huu, kwa upande mwingine watu wamesoma wapo huku akina Mheshimiwa Zuberi Zitto Kabwe ambao sasa hivi wameshakuwa watu wazima tena, lakini tumefaidika kwa kiasi fulani. Zipo changamoto ndogo ndogo ambazo ni lazima tuzizungumzie, kuna faida nyingi sana kijamii, za kielimu, kisiasa na kiuchumi na nyingine nyingi lakini changamoto zipo pia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, ukiangalia katika sekta ya elimu, Wazanzibar wengi tumefaidika kwa Muungano wetu, tumepata wasomi wengi sana nikiwepo hata mimi mwenyewe Sadifa maana nimesomeshwa kwa kupitia Bodi za Mikopo, yupo Mheshimiwa Sungura hapa ambaye na yeye amesomeshwa kwa Bodi ya Mikopo lakini leo hapa anapinga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kusema kwamba Muungano huu umetusaidia, lakini katika sekta hii ya elimu kwa mfano, kuna Bodi ya Mikopo, basi ile Bodi ya

Mikopo tuangalie na uwiano maana nadhani ukiangalia uwakilishi kutoka Zanzibar ndani ya Bodi ya Mikopo haupo pale, nadhani hii ni changamoto na inapaswa kufanyiwa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni suala la elimu ya juu hapo hapo pamoja na kufaidika huko, lakini inapotokea Wazanzibari nao kupatiwa nafasi kwenda kusoma nje ya nchi basi na wao wapatiwe, tunajua kwamba wanapewa nafasi lakini iendelee kwa ari zaidi, nguvu zaidi na kasi zaidi ili tuweze kupata uwakilishi mwingi kutoka kwa Wazanzibari. Vile vile suala la kupatikana kwa vitabu, kama kwa wenzetu huku vitabu vinapatikana na Zanzibar kule wapatiwe, kwa hiyo hii nasema ni changamoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni *School of Law*, huku wenzetu Tanzania Bara wameshaweka *School of Law* nadhani imefikia wakati na kule Zanzibar tuweke *Law School*, tunapata shida sana, naomba niseme kwamba hii ni changamoto ifikie wakati na sisi tuwekewe *School of Law*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna hoja Waheshimiwa walipokuwa wanachangia asubuhi walizungumzia Serikali tatu, kwa mfano, wengine walisema kwamba *solution* ya tatizo la Muungano tuweke Serikali tatu, mimi nasema *running away from the problems is not solution to solve them, I accept, we have to solve the problem by diplomatic means*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuweka Serikali tatu siyo *solution* kwa tatizo hili, wewe umesoma Sheria, bahati nzuri na mimi nimesoma sheria, sisi wasomi wa sheria tunasema, kitu kinacho-*matter* katika mambo kama haya ni *good faith*, kama kutakosekana *good faith, good will, nothing can be done*, hata tukiweka Serikali mia moja, lakini kama tukiwa hatuna nia njema, katu hatutaweza kufanya lolote. Kitu cha msingi ni kuwa na nia njema. Tukiweka kwa mfano, Serikali tatu kutakuwa na Marais watatu, Marais watatu hawa watakuwa na Mawaziri wao, Waheshimiwa Wabunge hapa walisema tupunguze gharama, tupunguze matumizi mabaya ya fedha, tukiwaweka Marais watatu, tukiwaweka na Mawaziri wao tutakuwa na *great burden*. Mawaziri watataka magari mazuri, Mawaziri watataka kusafiri kwenda nje ya nchi wakati hapa Wabunge wanalalamika kwamba, Rais tumpunguzie safari za kwenda nje ya nchi, sasa itakuwa ni mzigo mkubwa. Watataka kwenda kustadi kule, *how the world is*. Sasa tukisema kwamba tuongeze Serikali tatu, nasema *is nothing*. Tuangalie njia muafaka namna gani ambavyo Taifa letu tutalifikisha pale ambapo tunapahitaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado naendelea kuzungumzia suala lingine la changamoto, hapa Wazanzibari huwa wanalalamika kuhusiana na suala la wafanyabiashara kutozwa kodi mara mbili, hii ni changamoto naomba Serikali iangalie ni namna gani ambavyo tutatatua kero zetu hizi *by diplomatic means*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo muhimu na ya msingi ni kuhakikisha kwamba Wazanzibari baada ya kukaa na kujadiliana basi tufikie mahali…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge muda wako umekwisha.

**MHE. SADIFA JUMA KHAMIS:** Muda umekwisha, Loh! Mheshimiwa Mwenyekiti bado sijamaliza kuchangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sadifa Juma Khamis ahsante sana kwa mchango mzuri, sasa nitamwita Mheshimiwa Kombo Khamis Kombo na baadaye Mheshimiwa Nasib Suleiman Omar ajiandae.

**MHE. KOMBO KHAMIS KOMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kupata nafasi ya kuchangia hotuba hii ya Waziri anayeshughulikia masuala ya Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitabu hiki ni kizuri sana, kitu cha kwanza kilichonifurahisha ni picha za Waasisi wa Muungano wetu wa Tanganyika na Zanzibar, kwa nini nikasema kwamba kimenifurahisha kwa kuona picha hizi za waasisi wa Muungano wetu, waasisi wa Muungano wetu walipouasisi Muungano huu walikubaliana kwamba endapo Rais wa Jamhuri atatoka sehemu moja ya Jamhuri basi Makamu wa Rais wa Jamhuri atoke sehemu nyingine ya Jamhuri. Makubaliano haya kutoenziwa ni kwenda kinyume na *articles of union*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini jambo la pili, niseme kwamba Rais wa Zanzibar, kuondolewa kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano ni kuinyima fursa ya msingi Zanzibar. Leo Kamishna wa Jeshi la Polisi aliyepo Zanzibar kama hataki kutii amri ya Rais wa Zanzibar basi ana haki ya kufanya hivyo kwa sababu Rais wa Zanzibar si Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano. Kwa hivyo, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ina haki na wajibu wa kuangalia maslahi ya upande wa pili wa Muungano (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme kwamba wanaosema kwamba Serikali tatu hazina maana ni mtazamo wao, lakini Serikali tatu zina maana na wanaosema kwamba Shirikisho halina maana basi hatuna haja ya kujiunga na Jumuiya ya Afrika Mashariki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado naendelea kusema kwamba suala la kusema kuwa viongozi wa juu kama ilivyosema Kamati kwamba, hawana fursa ya kukutana kutatua masuala ya Muungano kwa sababu eti wana kazi ngumu na za msingi wanazozifanya, kwa nini basi hawaoni kwamba suala la Muungano ni suala gumu la kulifuatilia na kuweza kulipatia ufumbuzi. Leo unasema eti hakuna magari ya kuweza kukutana wakafanya shughuli hii, kama hakuna fedha ya kukutana wakaweza kujadili suala hili na kulipatia ufumbuzi, Serikali ya Jamhuri ya Muungano bado haijawa *serious* katika kujadili kero zinazohusiana na Muungano wa Tanganyika na Zanzibar! (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndani ya Bunge hili yalijitokeza maneno kwamba Zanzibar wameteuliwa watu kuja Dar es Salaam kujadili ile rasimu ambayo ilikuwa inataka kuzungumzia masuala ya mabadiliko ya Katiba. Mheshimiwa Sanya, akasimama, nashukuru Waziri Mkuu, aliona hisia za Wazanzibari pale akanyanyuka akasema kwamba, suala hili ni lazima liende Zanzibar. Matokeo yake tuliyaona. Kwa hiyo, niseme kwamba Muungano imara utajengeka endapo pande mbili za Jamhuri…

**TAARIFA**

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni ya 68(8), nataka kumpa taarifa Mheshimiwa Mbunge, anayeongea anasema kuna uvunjaji wa *Articles of Union* kwa sababu zilisema kwamba anapotoka Rais wa Muungano Makamu wa Rais, awe ni Rais wa Zanzibar. Lakini nataka kumpa taarifa, nataka kumuonesha busara iliyotumika kwa Serikali iliamua kufanya hivyo, hivi ninapokuwa Rais sasa wa Muungano, anatoka Zanzibar, Rais wa Zanzibar atakuwa nani, kama tungekwenda na mfumo ule zamani na imetokea hapa tumekuwa na Rais wa Tanzania anatoka Zanzibar, Mheshimiwa Ali Hassan Mwinyi, lakini Rais wa Zanzibar alikuwepo. Kwa hiyo, ina maana kama tungekuwa hatujabadilisha Katiba ingekuwa ni *crisis* kubwa kama nchi. Kwa hiyo, naomba hilo nalo alifahamu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kombo unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. KOMBO KHAMIS KOMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza sikubaliani na taarifa yake.

**MWENYEKITI:** Endelea.

**MHE. KOMBO KHAMIS KOMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, leo nawashukuru sana ndugu zangu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuunga mkono Sera ya Chama cha Wananchi (*CUF)* kwa madai ya uundaji wa Serikali Tatu. Nasema kwamba uundaji wa Serikali Tatu ya Zanzibar, Tanganyika na Shirikisho Dogo la Jamhuri ya Muungano ndio suluhu pekee ya matatizo ya Muungano. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivyo kwamba siyo lazima Tanganyika itoe karibu Wabunge 250 au Zanzibar itoe Wabunge 50 kuja katika Bunge hili, Baraza la Wawakilishi lina uwezo wa kuteua wajumbe hata 10 na Tanganyika ikateua wajumbe 10 tukaunda Shirikisho la Jamhuri ya Muungano. Kukawa na Bunge la Tanganyika, kukawa na Bunge la Zanzibar. Lakini suala hili nadhani litajadiliwa rasmi katika mchakato wa mabadiliko ya Katiba ijayo. Nina hakika Wazanzibar wataunga mkono Mfumo wa Serikali Tatu na hilo nina uhakika pia kwamba Watanganyika wataunga mkono kuwepo kwa mfumo wa Serikali Tatu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la biashara niseme kwamba sheria ya *double taxation* aliyoisema Mheshimiwa Waziri, bado haijafutwa na bado inatumika na kama imefutwa basi Waziri atakapokuja kutoa ufafanuzi basi tutaomba atueleze ni lini, tarehe gani ilifutwa na lini imeanza kuwa haitumiki sheria ile. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni suala la mazingira. Nadhani Mheshimiwa Waziri, kajitahidi kulieleza ingawaje baadhi ya wachangiaji wamesema kwamba halikuelezwa lakini limo kwenye ukurasa wa 52 hadi 78. Lakini na mimi niseme kwamba si Watanzania wengi ambao wameanza kufikiwa na nishati ya umeme. Kwa hiyo, suala la utumiaji wa miti kwa Watanzania ni suala la lazima. Wala mazingira hayataharibiwa na Mtanzania wa kijijini ambaye anaokota kuni ambazo tayari zimekwishaanguka. Tuangalie vyombo ambavyo vinaharibu mazingira. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, makampuni yanayoharibu mazingira yanajulikana lakini Serikali naona haiko *alert* katika kulifuatilia hili. Takataka za sumu zinazoenezwa na Makampuni hayo yanajulikana lakini hafuatiliwi. Lakini vile vile mazingira tusiangalie juu tu, tuangalie na kwenye bahari kama alivyosema Mheshimiwa Waziri. Kipindi cha mwaka juzi walikufa samaki wengi sana katika Bahari ya Hindi. Nina uhakika kwamba samaki wale hawakufa tu ila ni miongoni mwa takataka za sumu zinamwagwa na Mataifa mengine. (*Makofi*)

Hivyo basi, naiomba Serikali ya Jamhuri ya Muungano, isitoe kipaumbele katika suala la kuangalia maandamano tu, iangalie pia na suala la uharibifu wa mazingira katika maeneo yetu mbalimbali nchini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo machache, nakaa kitako na siungi mkono hoja mpaka Waziri atakaponipa maelezo ambayo yataweza kunitosheleza. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Kombo Khamis Kombo. Hii hoja inasumbua, sisi wengine tuliozaliwa baada ya Muungano tunapata tabu kweli. Maana ukiniambia turudi kwenye Tanganyika, nashindwa kuelewa maana sielewi hata Tanganyika maana yake nini. Sasa sijui, lakini Watanzania wataaamua. Tuendelee.

**MHE. SULEIMAN NASSIB OMAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza tumshukuru Mwenyezi Mungu sana kwa neema zake nyingi alizotupa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii adimu. Tatu, naomba kumpongeza Mheshimiwa Spika kwa kuchaguliwa Spika wa kwanza mwanamke katika Bunge la Jamhuri ya Muungano. Nne, naomba pia kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, kwa kuwasilisha hotuba yake vizuri. Mwisho kabisa, naomba kuwashukuru wapiga kura wangu wa Jimbo la Mfenesini kwa kunichagua kwa kura nyingi. Nawashukuru sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitajikita zaidi katika masuala ya Muungano. Ningependa kwanza kuelezea hii Tanzania imetokana na nini. Sote tunajua kwamba Tanzania imetokana na Muungano wa Zanzibar na Tanganyika. Kabla ya Muungano Zanzibar ilikuwa na bendera yake yenyewe, ilikuwa na Rais wake mwenyewe, ilikuwa na Mahakama yake yenyewe, ilikuwa na wimbo wake wa Taifa. Kadhalika Tanzania Bara, pia ilikuwa na Rais wake, Wimbo wa Taifa, Bendera, Mahakama na kadhalika. Kwa

hiyo, baada ya kuungana nchi hizi zikafanya nchi moja. Kwa hiyo, misingi hii ni muhimu sana kuijua kwa sababu popote panapokuwa na matatizo ndio hapo tutarejea katika misingi hii na kuweza kuyatatua. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nitaanza na faida za Muungano, kuna faida nyingi za Muungano, lakini faida kubwa kuliko zote ni kwamba wananchi wa Tanzania wana uhuru wa kwenda kila mahali, wananchi wa Zanzibar wako Mikoa yote ya Tanzania wanafanya kazi, wanafanya biashara, wanavua, wanafanya kila kitu bila ya kubugudhiwa. Hali kadhalika wananchi kutoka Tanzania Bara, wako Zanzibar wanafanya kazi zao, hawanyanyaswi, hawabugudhiwi. Hili ni jambo kubwa sana kwa sababu bila suala hili kuwepo Wazanzibari wengi wasingekuwa bara na wao kwa kweli kiwango kikubwa sisi ndio tunafaidika kwa sababu tunanyonya mali nyingi huku, tunafanya biashara na sisi kwa kweli ndio tumefaidika zaidi na Muungano huu. Kwa hiyo, lazima tuuthamini Muungano, lazima tuutetee Muungano kwa nguvu zote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika moja ya kero ambazo zinazungumzwa hapa ni suala la mgao wa fedha wa Benki Kuu, tunaambiwa kwamba Benki Kuu mgao wa fedha wa Zanzibar ni asilimia 4.5, kama nilivyosema mwanzo tuangalie namna gani hii Benki Kuu ilianza. Benki Kuu ilianza baada ya kuvunjika *East African Community*. Kule kulikuwa na *Currency Board* ya *East Africa* ambayo Zanzibar ilikuwa na sehemu yake ya fedha, mchango wake na Tanzania vile vile ilikuwa na mchango wake. Kwa hiyo, mchango wa Zanzibar na mchango wa Tanzania Bara ndio uliofanya Benki Kuu hivi sasa. Sasa tunashangaa kwamba Zanzibar ipate asilimia 4.5 kwani jamani si *simple arithmetic* kwamba watu wanapochanganya biashara *ratio* yake unapata. Kwa hiyo, Zanzibar lazima ipate sehemu yake iliyowekwa katika Benki Kuu.  (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni kama kero na halionekani kama kero kwa sababu ni suala rahisi mno. Wengi wetu hawalielewi. Lakini nafikiri nyaraka zipo zenye kueleza hili na turejeeni katika nyaraka na tukishafika katika nyaraka tutaweza kuliona na nafikiri mgao huu wa Zanzibar watapata haki yao kama inavyostahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nitakwenda kuchangia katika kunyanyaswa wafanyabiashara wa Zanzibar Bandarini Dar es Salaam. Mara ya mwisho Mheshimiwa Rais alipotembelea Bandari ya Dar es Salaam, alielezwa suala hili na wafanyabiashara wa watu wa *Clearing and Forwarding Agent* ambao wanashughulikia mali za Zanzibar pale. Mheshimiwa Rais akaagiza kwamba suala hili liondoke mara moja. Hili ni agizo la Mheshimiwa Rais, mpaka sasa halijatekelezwa kwa nini? Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, ametuambia kwamba suala la ushuru mara mbili limeshaondolewa isipokuwa watendaji bado hawajachukua hatua, inashangaza sana hawa watendaji wako vipi hawawezi kupokea amri ya Serikali mara moja kutekeleza suala hili? Ina maana kwamba hawa watendaji ni *arrogant* hawataki kufuata amri. Naomba Serikali iwachukulie hatua mara moja, hawa waondolewe, watafutwe wale ambao watapewa agizo na Serikali na watatekeleza mara moja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine hapo hapo tuliangalia mambo ya *registration* ya magari kama alivyosema Waziri asubuhi kwamba magari ya Zanzibar yanapokuwa na

namba za Zanzibar, yakifika hapa yanafukuzwa mbio na watu wa *TRA* na wanakamatwa na kutiwa ndani. Ingawa sheria ipo hapa inayosema kwamba namba zile zinaweza zikatembelea katika Jamhuri ya Muungano Bara. Hilo watu wa *TRA* hawajalitekeleza na wanafanya makusudi kwa sababu kama alivyotuambia Waziri hilo agizo limeshatolewa. (*Makofi*)

Kwa hiyo, naomba Waziri hapa atakapokuja na nafikiri Wazanzibar wengi hapa wanaelewa kwamba, moja miongoni mwa mambo yanayowavunja moyo Wazanzibari katika Muungano ni suala la wafanyabiashara kunyanyaswa bandarini. Wakifika pale mizigo yao inazuiliwa kwanza, mizigo inaibiwa pale. Hakuna mtu asiyejua suala hili. Mpaka leo bado mna Kamati, Kamati gani mnataka ifanye hili? Hamna haja ya Kamati, ni suala la moja kwa moja kukaa na kuondoa kama alivyoagiza Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, ni suala la Ofisi ya Makamu wa Rais ambayo iko Zanzibar. Tumeambiwa hapa ofisi hii bado haijapata *furniture*, inashangaza! Kwa hiyo, kule Mheshimiwa Makamu wa Rais, akienda Zanzibar anakaa wapi, akae chini? Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri, atakapokuja hapa ningemwomba vile vile atoe ufafanuzi juu ya suala hili la *furniture* za Mheshimiwa Makamu wa Rais, Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni mtu ambaye nina-*support* Muungano sana kwa asilimia mia moja na naunga mkono lakini hizi kero za Muungano lazima zipewe kipaumbele, zitatuliwe haraka ili Muungano wetu uwe mzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja. Ahsante. (*Makofi*)

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja hii iliyo mbele yetu kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais ikihusisha Wizara mbili nyeti sana. Wizara ya Muungano na Wizara ya Mazingira. Kwa kweli Wizara hizi zinahusu mambo ambayo ni tata na tete na yataendelea kuwa hivyo kwa kipindi kirefu sana cha mbele kwa Taifa letu. Yanayohitaji mjadala mpana wa tulipotoka kama Taifa, hapa tulipo na tunataka kwenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajadili kuhusu Muungano wakati huu ambapo tumekwishakubaliana kama Taifa kwamba Taifa linahitaji Katiba mpya. Lakini pamoja na mambo yetu ya ndani kama Taifa ni wakati vile vile ambapo jamii ya nje nayo inatazama ama ni kwa heri au kwa shari kuhusu yote yanayoendelea kama ilivyokuwa mwaka 1964 wakati wa Muungano wetu. Katika mazingira haya kwa sisi ambao hatukuwepo mwaka 1964 kati ya mambo ambayo waliotutangulia na ambao wako kwenye mamlaka wangetusaidia sana kwenye mjadala unaoendelea. Ni kukubali kuweka wazi baadhi ya taarifa za msingi kuhusiana tulipotoka mpaka hapa tulipo kama Taifa. (*Makofi*)

Naelewa kwamba mataifa ya nje ama ni kwa heri ama ni kwa shari yamekwishaanza kutoa hadharani vile vitu wanavyoviita *Classified National Secrets* ambazo zilikuwa zina *Top Secret* huko nyuma lakini wameanza kuzitoa. Kwa mfano, Shirika la Kijasusi la Marekani *(CIA)* limekwishatoa kwenye mitandao yao taarifa

ambazo miaka 25 iliyopita zilikuwa ni siri kwa Shirika la Kijasusi la Marekani na kwa Serikali ya Marekani zikieleza Balozi wao na watu wao walivyoshiriki kwa namna moja au nyingine wakati wa heka heka za kuingia kwa Muungano wetu.

Kwa kiasi taarifa hizi hazileti picha nzuri kwa Taifa letu, zinaleta picha kwamba Muungano huu ulikuwa ni zao la vita baridi. Vita baridi hii na ukoloni mambo leo, haujaisha tunavyozungumza hivi sasa. Kwa hiyo, tutasaidiwa sisi wakati tunapoingia kwenye mjadala wa Katiba kama wazee wetu watafungua makabati ya baadhi ya siri zetu tukaelewa kwa undani dhamira ya waasisi wa Taifa hili walipokuwa wakiingia kwenye Muungano. Itatusaidia hata kuamua ni Muungano wa namna gani tuwe nao. *(Makofi)*

Mimi ni mmoja wa waumini wa shirikisho, bahati nzuri niko kwenye Chama ambacho toka kiasisiwe kinaamini kwenye uwepo wa Serikali Tatu. Lakini bado kuna masuala mazito sana kama Taifa. Tunahitaji tujiulize ya ndani na ya nje, tunajadili kuhusu Afrika Mashariki, tumeanza Soko la Pamoja, tunakwenda mbele zaidi. Tunafikiri kuhusu Shirikisho la Afrika Mashariki, kama unafikiri kuhusu Shirikisho la Afrika Mashariki nafasi ya Tanzania katika Shirikisho hilo Tanzania yenye Muungano wa Tanganyika na Zanzibar ni nini katika Shirikisho? Ndio maana nasema haya ni masuala tete na tata sana yanayohitaji kuaminiana na kujadiliana kuanzia hatua za awali sana.

Lakini nasikitika sioni moja kwa moja dhamira ya kufungua mlango huu wa majadiliano wakati wa mchakato huu wa Katiba unaoendelea. Nimesikitishwa sana na kauli ambayo imetolewa hapa Bungeni wakati wa kujibu swali lililoulizwa kuhusiana na Katiba kuhusiana na mchakato wa Katiba ulipofikia. Wizara inayohusika imeeleza hapa Bungeni suala ambalo Mkutano uliopita wa Bunge tulikuwa na mvutano sana kuhusiana na mchakato wa Katiba, Wizara imesema kwamba Muswada wa Katiba ule ambao Bunge lililopita tulielezwa utaletwa kwenye Bunge hili, Wizara haina hakika kama utaletwa kwenye Bunge hili na katika Mkutano huu wa sasa ama utaletwa kwenye mkutano ujao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara inasema kwa Watanzania kwamba Muswada upo kwa Spika, kwa hiyo, mwenye maamuzi kuhusu Muswada uletwe lini kwa utaratibu gani ni Spika. Wizara inasema kwamba Serikali imejipangia nikitumia kauli ya jana kwamba uzinduzi wa Katiba Mpya utakuwa tarehe 26 Aprili, 2014. Serikali inajipangia suala ambalo lilipaswa kupangwa na ama Bunge kupitia sheria itakayotungwa ya mchakato wa Katiba ama ipangwe na chombo kitakachoundwa na hiyo sheria kitakachosimamia mchakato wa Katiba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kilichonisikitisha zaidi na hili ningependa kupata kauli ya Serikali kwenye majumuisho ya mjadala huu wa Muungano naamini Bunge lililopita Wabunge kwenye Kamati na wananchi mitaani waliukataa Muswada ule wa Katiba. Nilichoelewa mimi nilitarajia na Zanzibar nao wakaukataa ule Muswada wa Katiba, nilitarajia kwa *spirit* na mjadala tete kama huu wa Muungano Muswada ungeenda kuandikwa upya kwa lugha ya Kiswahili uletwe Muswada upya kwa kuwahusisha wadau huko, Wazanzibar wangehusishwa, Wabara wangehusishwa, Muswada ungeletwa upya. Kauli ya Serikali kwamba Muswada bado upo kwa Spika, Muswada upo kwa Bunge

unaonyesha kwamba bado Muswada ni ule ule kitakacholetwa ni marekebisho tu *(Schedule of Amendment).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi sitaki kuamini hivyo kwa sababu tukikosea kwenye kutengeneza Sheria ya Mchakato wa Katiba tunakwenda kutengeneza kero nyingine, siyo kwenye utawala tu wa maeneo mengine bali pia kwenye mjadala mzima wa Muungano. Kwa sababu italetwa *Schedule of Amendment* iwe imebadilika lugha imekuwa kwa Kiswahili ama kwa lugha nyingine, lakini kama pande zote za wananchi ikiwemo pande zote mbili za Muungano hazijaridhika na mchakato unavyokwenda siyo tu wa kuandika Katiba yenyewe wa Sheria yenyewe itakayosimamia huo mchakato, tunaanza kutengeneza nyufa kuanzia kwenye hatua za awali sana za kuandika historia mpya ya Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini kama kweli Serikali ina dhamira ya kushughulikia kero za Muungano kwa miaka mingi ijayo na kuunda Muundo wa Taifa ambao tunakubaliana kama Watanzania hili ndio Taifa tunalolitaka naamini Serikali itatoa kauli rasmi kabisa, si ya majibu, si ya maswali ya nyongeza kauli rasmi kabisa kuhusiana na hatma ya Muswada ambao tuliahidiwa hapa Bungeni kwamba ungeletwa kwenye Bunge hili ukiwa kwenye lugha ya Kiswahili baada ya kupata maoni ya wadau mbalimbali na Kamati zikazunguka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini si hivyo tu suala la kupanga lini Katiba izinduliwe na ikamilike kwa muda gani siyo la Serikali kwa sababu sisi wengine hatukubaliani kwamba mchakato wa Katiba uende mpaka mwaka 2014 hatukubaliani, tunaamini kabisa inawezekana kabisa mpaka mwaka 2013 tukawa na Katiba Mpya inawezekana kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ili tubishane mpaka mwisho tukubaliane kwamba muda unaowezekana ni huu, ni lazima mjadala huu uje kwenye chombo chenye uwakilisha wa wananchi, uje Bungeni tuweze kujadiliana kwa undani wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nijielekeze kwenye vitabu hivi ambavyo ndio kazi kubwa ambayo iko mbele yetu ya kujadili na kupitisha Bajeti. Nianze na Kitabu hiki cha Maendeleo ukurasa wa 36 na 37 Ofisi ya Makamu wa Rais, kuna mambo ambayo ningeomba kupata ufafanuzi kutoka kwa Serikali ili tujenge msingi wa kuikubali ama kuikataa Bajeti iliyoko mbele yetu. Kwenye kifungu cha 1001 kuna Kasma ya Ujenzi wa Ofisi ya Makamu wa Rais ambayo mwaka uliopita wa fedha ilitengewa shilingi bilioni 3.7 na mwaka huu imetengewa shilingi bilioni 3.4. *(Makofi)*

Ningependa kupata ufafanuzi kwa sababu mimi ninavyoelewa sera ya Serikali hii ambayo tulielezwa na Waziri Mkuu hapa wakati anahitimisha hoja ni kwamba ni kuhamia Dodoma. Sasa sielewi kama tunahamia Dodoma hizi shilingi bilioni 3.4 za ujenzi wa Ofisi ya Makamu wa Rais, Dar es Salaam ni za Ofisi ya Makamu wa Rais wa Serikali ipi?

Mimi ningeshauri kwa kweli kwa sababu ukienda ukurasa unaofuata ambao ndio una miradi sasa ya maendeleo ya ofisi hii muhimu sana inayogusa mazingira, inayogusa na Muungano. Kuna miradi miwili muhimu sana, kuna huu mradi uliopo kwenye kasma elfu na mia tatu wa *climate change adaptation* na mradi huu wa kasma hii nyingine ya hapa chini ya *EMA Implementation Support* yaani *Environmental Management Act Implementation Support*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii miradi miwili ni miradi muhimu sana kwa Taifa letu leo na siku zijazo. Nimesema kwamba mazingira yetu yana changamoto za ndani na nje. Kama kuna hatari kwa Taifa letu kwa sisi wengine tulio vijana tutakuwepo, tutaishuhudia ni Taifa letu kuelekea kuwa jangwa. Kuna sababu za nje kwa sababu ya uchafuzi wa mazingira ya Mataifa ya nje, lakini kuna sababu za ndani vilevile kwa hiyo, mabadiliko ya tabia nchi na mabadiliko ya tabia zetu za kimaisha, za kiutamaduni, kurekebisha hali, kukabiliana na hali hiyo, ni jambo la lazima sana. *(Makofi)*

Mradi wa *climate change adaptation* kwa fedha ndani kumetengewa shilingi milioni 92 peke yake. Wakati ujenzi wa Ofisi ya Makamu wa Rais Dar es Salaam ambaye naamini sasa hivi ana ofisi umetengewa shilingi bilioni 3.4. Vipaumbele kama Taifa viko wapi? *(Makofi)*

Kuna mradi huu ambao ndio unasimamia Sheria ya Mazingira na mimi hapa niseme kwamba katika hili kama hakutakuwa na ufafanuzi wa kina, nitaomba kuondoa shilingi kwa kweli. Huu mradi wa usimamizi wa sheria ya mazingira ambao ndio roho pamoja na udhaifu wa sheria yetu ya mazingira ya mwaka 2004 lakini walau imeweka adhabu kwa wakosaji ikiwemo adhabu ya mkosaji anayechafua mazingira kulipia na kulipa fidia siyo fidia, kulipia gharama za kuchafua mazingira, hiyo *principle* ya *polluter pay*.

Sasa hii sheria ambayo ndani yake ina nadharia nzuri sana, maana tatizo la Taifa letu zaidi ni usimamizi wa sheria kuliko sheria zenyewe. Sheria iliyopewa mtandao mzima kwamba kuwe na vyombo ukiondoa Baraza la Usimamizi wa Mazingira kuwe na chombo kwenye ngazi ya Mkoa kuwe na Kamati kwenye ngazi ya Wilaya, Kamati kwenye ngazi ya Kata, kuna Kamati ya Mazingira kwa mujibu wa Sheria mpaka kwenye ngazi ya kijiji hata mtaa ambazo zina mamlaka mpaka kuchunguza ambapo kama fedha zingewekezwa kwenye kuhakikisha hii sheria inasimamiwa, tusingekuwa na malalamiko mengi sana katika uchafuzi wa mazingira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi niseme mwanzoni hili linanigusa sana kwa sababu wananchi walionituma kuwawakilisha hapa…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kumalizika muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Kengele ya ngapi?

**MWENYEKITI:** Ya pili.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mnyika kwa mchango wako mzuri. Lakini kwa kuwa tunapenda mambo wakati mwingine unatumia muda wako vizuri zaidi, inatusaidia. *(Makofi)*

**MHE. SELEMANI S. JAFO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda kukushukuru wewe kwa kunipa fursa hii japo na mimi niongee na Bunge hili pamoja na Watanzania wote wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Kikubwa zaidi napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, mpaka jioni hii nikiwa na nguvu japo katika majonzi ya swali langu la asubuhi lililojibiwa lakini sasa hivi nina nguvu ya kutosha kwa ajili ya kuongea na Watanzania wenzangu na Serikali yangu na wananchi wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza sisi wote tumeumbwa, lakini katika kuumbwa kwetu mara nyingi huwa tunaongozwa na vitabu vya dini. Lakini vitabu vya dini mara nyingi vina sifa kuu tatu, kwanza katika vitabu vya dini vitukufu utakutana na kitu kinaitwa historia. Utakutana na jambo visa na utakutana na sayansi. Vitu hivi vyote ni mwelekeo kwetu sisi viumbe, ni kwa ajili ya kuweza kujifunza na kuweka mustakabali wa maisha yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Bunge hili naomba kwanza niwakumbushe Wabunge wenzangu na niwakumbushe Watanzania wote wale mashahidi waliohudhuria Bunge la Tisa na sisi tuliokuwa tunaangalia katika Bunge la Tisa likiwa linazinduliwa katika vyombo vya habari kama *television* tulimshuhudia Mheshimiwa Rais akizindua Bunge lile na akitoa *speech* nzito sana. Katika *speech* ile ya Bunge la Tisa aliainisha mambo mbalimbali ikiwemo mojawapo ya kushughulikia mikataba yote mibovu na kushughulikia suala zima la mustakabali wa nchi ya Tanzania. *(Makofi)*

Ikiwa hiyo haitoshi akazungumzia suala zima la mpasuko wa kisiasa katika eneo la Zanzibar. Ndio maana nimesema vitu vingine tujifunze kutokana na historia. Tukisema mpasuko wa kisiasa kule Zanzibar kipindi kile tunazungumzia suala zima la Muungano wetu. Napenda ndugu zangu Wabunge na Watanzania ndio neno hili huwa napenda kulirejea sana kwamba tukumbuke wapi tumetoka na hivi sasa tuko wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika suala zima la Muungano Mheshimiwa Rais alisema tutajitahidi kwa ajili ya kushughulikia mpasuko wa kisiasa kule Zanzibar. Sote sisi ni mashahidi hali ya Zanzibar hakuna mtu anayetakiwa kufundishwa katika hiyo. Tulikuwa tukiona jinsi gani unyanyasaji wa raia ulivyokuwa ukitokea kule. Hivi sasa Tanzania Zanzibar imekuwa ni historia kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, historia hiyo ambayo tumeiweka Tanzania na Watanzania tunatakiwa kila sababu ya kujivunia na katika hili tuna kila sababu ya kumshukuru sana na kumpongeza Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika mustakabali wa Muungano. Vilevile ningependa kukishukuru Chama cha *CUF*

ambacho kwa ushupavu wake na ukomavu wake kwa kweli tumezalisha Serikali ya Umoja kule Zanzibar, hili ni jambo la kujivunia sana kwa Tanzania yetu hii. Ndugu zangu haya ni mambo ya kujivunia.

Katika mustakabali tunapozungumzia Muungano wetu leo hii mimi ningependa nukta yangu ya kwanza kuizungumzia katika suala zima la mafanikio makubwa tuliyoyapata kule Zanzibar nikimuangalia Mheshimiwa Mnyaa pale anapendeza kabisa, hana wasiwasi na nchi yake. Haya ni matunda ya Serikali ya Umoja. Katika haya napenda kumshukuru sana Profesa Lipumba, Maalim Seif na viongozi wetu wa Chama cha Mapinduzi kuhakikisha kwamba Zanzibar sasa hivi imekuwa ni sehemu ya mfano siyo kwa Afrika isipokuwa dunia nzima. *(Makofi)*

Ndugu zangu hili jambo ni jambo la kujivunia. Lakini ndugu zangu nini tunajifunza? Sasa hivi tupo katika mchakato mkubwa sana katika suala zima la Katiba, mimi ningependa kuwasihi sana Watanzania tutumie nafasi hii vizuri sana kwa ajili ya kuitengeneza Katiba yetu ilikuwa vizuri zaidi. Tusitumie nafasi hiyo vibaya tukapotosha maana nzima ya mustakabali ambao Rais wetu alihutubia katika kuingia katika mwaka mpya, tutakuwa tumetenda kosa. Tutumie hekima kubwa sana na busara zetu kuhakikisha kwamba tunajipanga vizuri na Tanzania inapata Katiba yake ambayo kila Mtanzania atajivunia na watu wa nje waweze kuiga kutoka kwetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mjadala tunaojadili hapa tunagusa maeneo mbalimbali na suala zima la mazingira. Ningependa kujielekeza katika sehemu nzima mazingira. Naomba kujielekeza katika suala la uchumi na mazingira, tukizungumzia mazingira napenda ku-*site* sehemu chache sana kwa mfano Jiji la Dar es Salaam.

Mheshimiwa Waziri wa Mazingira, tuna changamoto kubwa sana katika Jiji la Dar es Salaam na maeneo mengine mbalimbali katika nchi yetu ya Tanzania. Athari ya mazingira inasababisha mpaka uchumi hauendi vizuri kwa watu wa kipato cha chini. Watu wanaonitazama kutoka Dar es Salaam wao ni mashahidi, wanaoishi maeneo ya Mabibo pale katika mabwawa ya maji machafu, wafanyabiashara wadogo wanaouza vyakula vyao hata biashara zao haziendi vizuri kwa ajili ya maeneo yale siyo salama. Watu wanaokaa maeneo ya Spenko kule Vingunguti wanajua hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali yao ni mbaya sana kwa ajili ya uchafu wa mazingira. Lakini watu wa Pugu Kinyamwezi na pale *Kigogo Fresh* wanajua kuna sehemu kubwa ya utupaji wa takataka kule. Wananchi wale hata maisha yao yamekuwa tatizo kubwa kweli kweli, biashara zinazunguka mazingira yale kwa kweli haziendi vizuri. Kwa kweli naomba kuwasemea wananchi wa Dar es Salaam ndugu zangu, ninaamini wafanyabiashara wale wanaoishi kando kando ya maeneo yale hata biashara haziendi vizuri. Hii ni changamoto kwa Taifa. Naomba tujipange vizuri jinsi gani tutatatua matatizo haya.

Ndugu zangu ukija kuangalia hata suala zima la magari taka yanayozunguka katika miji yetu, mimi nashangaa hata hawa watu wanaopewa *tender* za magari taka ambayo yanatumia matrekta ambayo yanakufa njiani kwa nini wanafanya hivi? Baada ya

kuondoa takataka unakwenda kuchafua sasa mazingira ya Jiji. Hili ndugu zangu haiwezekani, naomba tusimamie hili kwa moyo wote tukijua kwamba huu ni mustakabali wa nchi yetu. *(Makofi)*

Katika suala zima la mazingira naomba nizungumzie athari za mazingira katika maeneo mbalimbali na katika jimbo langu. Ndugu zangu Watanzania mnaelewa wakazi wengi wa nchi yetu wanaishi Jijini Dar es Salaam, lakini asilimia karibuni 80 ya wakazi wote wa Dar es Salaam wanatumia mkaa. Aidha, mtu kama anafanyakazi ofisini, ama anafanyakazi kama mama ntilie au mtu wa kawaida lazima atatumia mkaa. Lakini mkaa ule ukiangalia kwa wakazi wengi zaidi ya mamilioni kutoka Jiji la Dar es Salaam mkaa ule kwa asilimia kubwa unatoka katika Jimbo la Kisarawe. Sasa wenzetu katika maeneo ya madini wanaomba kitu kinaitwa mrabaha, inawezekana na mimi leo Waziri wa Mazingira na Waziri wa Fedha akaangalia ni jinsi gani Kisarawe tutaifidia kwa watu wote wanaoishi Dar es Salaam mikaa yao wanayoitumia kutoka Kisarawe na mazingira ya Kisarawe yanazidi kuporomoka. Jinsi gani tutaiangalia Kisarawe kwa jicho la huruma? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, siku zote nazungumza shida ya maji katika Jimbo la Kisarawe, lakini ukiangalia hata kiwango cha mvua takwimu zinatueleza kipindi cha nyuma Wilaya ya Kisarawe na maeneo ya Mkoa wa Pwani yalikuwa yanapata milimita za mvua zipatazo 1,500 watalaam wetu wa takwimu za mvua sasa hivi imeshuka mpaka 780. Hii inatuonyesha tumeingiza jangwa katika maeneo yetu. Hili inatakiwa tujipange vizuri ndugu zangu ni jinsi gani kwa sababu suala la mazingira ni suala mtambuka, jinsi gani kama nchi tunajipanga vizuri hata katika kutumia nishati mbadala, suala zima la uhamasishaji wa matumizi ya gesi. Ndio maana nimesema mazingira ni suala zima la mtambuka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndugu zangu kama Watanzania tunataka tujipange vizuri katika mustabali wa suala zima la mazingira. Maana naizungumzia Kisarawe, lakini Tanzania hivi sasa imeathirika katika suala zima la mazingira. Kiwango cha mvua kitashuka, ukame utaongezeka, mifugo itakosa hata sehemu ya kunywa maji. Tutachimba visima virefu na tutachimba malambo, hatimaye hata malambo tunayoyachimba mvua itakuwa haipatikani kujaza hayo malambo. Kwa hiyo, tuna kila sababu ya kujipanga vizuri na katika hili sisi kama Serikali, sisi kama Wabunge na sisi kama wananchi, inabidi tutumie nguvu zote zinazowezekana na tuweze kuyahimiza mashirika mbalimbali yaweze kutusaidia katika hali na mali. *(Makofi)*

Kwa kweli mimi kwa upande wangu ndiyo maana nikisimama kwenye jimbo langu kuna watu lazima niwasifu ni kwa sababu wanatusaidia katika ile *Public Private Partnership (PPP).* Siku zote huwa sikosi kuwashukuru. Kwa mfano watu wa *Care International*. Katika jimbo langu wanasaidia sana katika suala zima la upandaji wa miti kupitia mradi wao wa *MISAKA.* Kwa kweli mashirika haya ni lazima tuyaenzi na lazima tuhakikisha kwamba mashirika haya yanasaidia sehemu mbalimbali katika Tanzania yetu hii.

Vile vile ningelipenda niwashukuru ndugu wa *Plan International* kupitia mradi wao wa *CLTS* ambao wamesaidia suala zima la watu kutojisaidia hovyo hovyo, ambalo

tunaona kwamba athari yake baadaye inaweza ikasababisha mambo ya *typhoid*. Mradi ule umesaidia kuwaelimisha watu kwa kiwango kikubwa sana, watu wanatumia vyoo, watu hivi sasa karibuni kila kaya ina vyoo, ina maana hata uchafuzi wa mazingira unapungua kwa kiwango kikubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni changamoto na sisi kama Watanzania lazima tujipange kwa pamoja, lakini inawezekana tufike muda sasa tufanye *competition*. Kwa nini tuna Wakurugenzi katika Manispaa mbalimbali, Wakurugenzi wa Miji, lakini miji kwa nini inaendelea kuwa michafu. Inabidi ikiwezekana tuweke kigezo kwamba mazingira vile vile tuhakikishe kwamba tunaimarisha kwa watu kwamba tunafanya *performance appraisal* kwa utunzaji wa mazingira. Haiwezekani kama Jiji la Dar es Salaam linakuwa chafu au miji mingine. Ina maana kwamba lazima tuongeze katika suala zima na kukaza nati vizuri mazingira yetu yawe mazuri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi napenda kutumia muda wangu mfupi kiasi hicho ningependa kukushukuru sana na kuwashukuru sana wananchi wangu wa Kisarawe kwa kunipa nguvu na kuniombea kila siku kuwa hapa. Ahsante sana naomba kuunga mkono hoja hii iliyoko mbele yetu. *(Makofi)*

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Taarifa Mheshimiwa Mwenyekiti.

**MWENYEKITI:** Taarifa.

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Mwenyekikti, naomba kutoa taarifa kwa ajili ya kumbukumbu katika kikao chako, wakati anazungumza Mheshimiwa Mnyika alizungumza kwamba ali-*site* kwenye kitabu cha Maendeleo kifungu 1001 aka-*site* kwenye kifungu kidogo 6389 ambacho alisema na aka-*site* pia kwenye kifungu cha 5301 akafananisha kwamba Serikali haichukulii umuhimu mambo ya mazingira akasema kwamba suala la ujenzi wa Ofisi ya Makamu wa Rais imewekewa shilingi bilioni tatu lakini suala la mazingira *climate change adoption project* imewekewa shilingi milioni 92 tu. Lakini ukienda kwenye jumla yake ni shilingi bilioni moja laki tano na themanini na saba.

Pia ukitazama kwenye hizi *vote,* hii *vote 1001 Administration and General* jumla yake kwenye kifungu hiki ni shilingi bilioni nne na milioni 900. Lakini kwenye mazingira kifungu 5001 na vifungu vyake vidogo vyote jumla yake ni shilingi bilioni 7, milioni 5,379. Kwa hiyo, nilitaka niweke kumbukumbu kwamba siyo kama Serikali haichukulii umuhimu. Ni hela nyingi zimewekwa kwa ajili ya mazingira. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mnyika mbona unasimama. Mimi sijakupa nafasi bwana. *(Makofi)*

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesimama ili unipe nafasi. Kuna aina mbili za kuomba nafasi ya kusema au ya kusimama. Nimesimama unipe nafasi Mwenyekiti. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge, Mheshimiwa Vita Kawawa amesema taarifa. Akishatoa taarifa mimi nitakuhoji kama hiyo taarifa unaipokea au unaikataa. Sasa labda nikuhoji unaipokea taarifa ya Mheshimiwa Vita Kawawa au unaikataa?

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Naikataa anapotosha maelezo yangu. Naomba niseme tu kwamba…

**MWENYEKITI:** Basi ukishasema unaikataa na kwa kuwa huendelei kusema, basi haijaharibu *Hansard* yako inaendelea kuwa vile vile. Basi tuendelee na msemaji anayefuatia Mheshimiwa Mgimwa.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Basi *okay!*

**MWENYEKITI:** Labda nifafanue tu kwamba hapa ni kwa sababu Serikali itapata fursa pia ya kulisemea jambo hili katika michango ya Wabunge wote. Kwa hiyo, kutakuwa na fursa nzuri ya ufafanuzi wa kutosha, lakini kwa maana Mheshimiwa Vita Kawawa lile limetosha tu kwamba haujaipokea na basi hakuna maelezo zaidi, maana yake siyo mjadala.

**MHE. WILLIAM A. MGIMWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa naomba kuchukua nafasi hii kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii tena niweze kuchangia. *(Makofi)*

Pili nimshukuru Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, kwa hotuba nzuri ambayo kwa kusema kweli ina kina kikubwa katika mwelekeo wa Bajeti nzima na ya tatu, niwashukuru wananchi wangu wa Jimbo la Kalenga kwa kuendelea kunivumilia wakati mimi nawawakilisha hapa Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo nina mambo manne ambayo napenda kuchangia kwenye hotuba hii. Jambo la kwanza ni mapato ya Muungano. Wenzetu kutoka Zanzibar wamekuwa kwa sababu, nafikiri wanayo sababu nzuri. Wamekuwa wakihoji kwamba kuna kero ambapo mojawapo ni suala la mapato ya Muungano. Ni vizuri kutazama kwa undani kabisa ili kushughulikia matatizo. *(Makofi)*

Ninavyotazama mimi Ibara ya 184 ya Ilani ya Chama cha Mapinduzi maana yake ndicho kinachoongoza Serikali hii pamoja na mambo mengine ile ibara ndogo, *section c* imeagiza Wizara iliyo katika Ofisi ya Makamu wa Rais ishughulikie kuboresha uchangiaji na mgawanyo wa mapato ya Muungano. Sasa upande mwingine kuboresha kigezo cha mgawano wa *budget support* ambayo inakuja kwa ajili ya ku-*support both sides of the country.* Pendekezo langu kwa sababu wenzetu wamekuwa wakihoji kwamba upande huo wao hawaridhiki. Ni ushauri, pamoja na kwamba Waziri ameshaeleza kwamba suala hili limeshashughulikiwa na Kamati zimeshawakilisha bado mchakato wa mwisho wa maamuzi. *(Makofi)*

Kwa kuwa hatuna taarifa za maamuzi. Pendekezo langu ni kwamba kwa kuwa ile *4.5 percent* ilikuwa *calculated from a certain base* ambayo ni *criteria* zilizotumika na *criteria* zile inawezekana zilikuwa nzuri kwa wakati ule zikawa *criteria* ile ikibadilika inaweza ikakidhi hali halisi iliyopo sasa. Kwa hiyo, hekima iliyopo ni kutazama upya zile *criteria* zilizotumika ku-*calculate* na kufikia kwenye 4.5% kama ndiyo *ratio* ambayo Zanzibar inastahili. Kwa hiyo, ni vizuri kutazama zile *criteria* zilizojenga ile *base* ya ku-*generate* ile *percentage.* Kwa hiyo, *from that angle* wanaweza wakajenga hoja au kwa pamoja tukasaidia na kutazama kama bado *justification* ya ile *base* au wenzetu wana hoja nzuri itazamwe kwa utaratibu wa ku-*change* mwelekeo wa hali ambayo wanaiona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ni suala la sheria na kanuni za fedha. Ibara hiyo hiyo ya 193 ya Ilani ya uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi, narudia tena kwa sababu ndiyo inayoongoza Serikali hii, *section d* kwa Wizara ambayo imo ndani ya Ofisi ya Makamu wa Rais, imeagiza watengeneze *harmonization* ya Sheria hizi pamoja na sera yaani ili Sheria na Kanuni za fedha zinazotumika Zanzibar na huku Tanzania Bara ziwe *harmonized* kwa ajili ya kuboresha ufanisi wa makusanyo ya fedha. Taarifa tuliyopewa na Mheshimiwa Waziri ni kwamba *harmonization* ya Sheria hizo na Kanuni imefikiwa mahali pazuri, lakini bado wanaendelea. Lakini kwa kuwa matatizo hayo ya malalamiko bado yanaendelea. Nashauri Wizara iharakishe *harmonization* ili matatizo ya kuingiza *imports through Zanzibar visa-vis imports* zinazopitia Dar es Salaam yasiendelee kulalamikiwa kwa sababu malalamiko yanapunguza *efficiency* na ufanisi wa makusanyo ya mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la tatu ni suala la ushauri. Mheshimiwa Waziri alipokuwa anawasilisha hoja ya Muungano nilitarajia kwamba *from the point of Ministry* tungepata mwelekeo wa changamoto wanazozipata wenzetu *rather than* kupata changamoto kutoka kwa wachangiaji. Tungepata changamoto *from the Ministry* yaani kupata changamoto ambazo wanazipata za Muungano *from the point of the government.* Tunapata picha *from the side of the coin* kuangalia namna gani changamoto Serikali inavyoziona za Muungano *visa-vis* changamoto zinazowasilishwa hapa Bungeni. *(Makofi)*

Napendekeza pamoja na changamoto ya kero zinazowasilishwa Bungeni na Waheshimiwa Wabunge kutoka pande zote hasa wale wanaotoka Zanzibar, itakuwa vizuri basi na Serikali kuandaa changamoto inazoziona yenyewe ili tushiriki kuzi-*debate* ili kuchangia na ku-*iron out* malalamiko anmbayo yanafikishwa hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala langu la mwisho ambalo ningependa kuchangia linahusu mazingira. Wizara hii ambayo Ofisi ya Makamu wa Rais imejikita vizuri katika kuboresha mazingira na kusimamia, kwa kusema kweli imefanya kazi vizuri na imeeleza kwa undani kabisa. Lakini nafikiri tuwe wa wazi zaidi. Tunashughulika sana kuboresha mazingira katika nchi hii. Lakini tuchukue maamuzi ambayo kweli baadaye yataboresha mazingira lakini yatawapa nyenzo mbadala wahusika ambao wanaharibu mazingira. Ukitazama jambo kubwa kabisa ambalo ni tatizo, ni tatizo la kukosa mbadala wa *energy* yaani mbadala wa nishati. Nchi nzima imekuwa karibu *deforestated* yaani ni kama imekatwa miti na ile miti kwa sababu inachukua muda mrefu kuota, wananchi kwa

ujumla walio vijijini wana haki ya kukata kuni, wapate moto au wana haki ya kuwa na mkaa ili maisha yao yaendelee.

Serikali na sisi viongozi tuna wajibu wa kusaidia kuona kwamba miti haikatwi kwa ku-*provide energy* ambayo ni mbadala. Utakumbuka kwamba Kamati yetu ya Fedha na Uchumi tulipendekeza kwamba wakati tunabadilisha ile *excise duty* kupandisha kutoka shilingi 52 kwenda shilingi 400 *per litre* kwa mafuta ya taa tuliomba au tulipendekeza nyongeza ile isaidie kwa ajili ya *rural electrification*. Hawa ndiyo watu ambao wanaumia kwa mbadala wa *energy* ambao tukipandisha gharama ya mafuta waweze kupata umeme kama mbadala. Kwa kufanya hivyo tutakuwa tume-*solve* tatizo la kukata miti nchi nzima kwa sababu tutakuwa tumewapelekea umeme. Suala hili tuliliwakilisha, kwa mapendekezo yangu wakati nachangia hoja hii ya Makamu wa Rais mwelekeo ule wa pendekezo likichukuliwa *serious* na Serikali *environmental deforestation* kwa kweli itapungua sana kwa sababu wananchi kwa ujumla hawatakuwa na sababu ya kukata misitu kwa sababu tutakuwa tumewapelekea umeme ambao ni mbadala wa ku-*provide energy* kwao.

Tusipofanya hivyo tutabakia na *dilemma* ya ku-*provide alternative energ*y kijijini. Tutaleta Sheria, tutaleta Kanuni na tutaleta Sera. Sera *will never be effective* kama hatuwatengenezea mazingira ya wao kuwa na *energy* mbadala na *energy* mbadala ni *rural electrification* ndiyo ninanyoiona *is a critical solution.* Tufanye maamuzi ambayo yanawezekanika. Lakini tusichelewe kwa kuweka sera ambazo zitachukua muda mrefu kabla hazijageuka matendo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawasilisha hili kama kumbukumbu kwa sababu ibara ambayo imesisitiza kwamba mazingira ni muhimu katika Ofisi ya Makamu wa Rais na imewapa maelekezo lakini bila kuchukua hatua za mwelekeo wa namna hii nafikiri tutakuwa bado hatujafanya maamuzi ambayo yataleta mabadiliko kwa ajili ya ku-*provide energy* kwenye *rural sector.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo nichukue tena nafasi hii kukushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii. Namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa kupitia kwake na kwa Waziri mwenzake na wananchi wa Jimbo langu la Kalenga kama nilivyosema kwanza kwa kunivumilia nikiwa hapa Bungeni nikiwawakilisha katika mambo haya. Naunga hoja mkono na nasema ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mgimwa, lakini pamoja na kufikisha huo umeme vijijini na bei pia ungeisemea nayo ishuke kidogo ili mtu wa kijijini aweze ku-*afford. (Makofi)*

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kupata nafasi hii ya kuzungumzia hizi hotuba mbili muhimu. Masuala ya Muungano na masuala ya Mazingira ni masuala muhimu sana kwetu. Suala la Muungano linahusu moja kwa moja uhai wetu kama Taifa na uhai wetu kama Watanzania kama nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mazingira linahusu uhai wetu kama binadamu kuendelea kuwepo kwetu katika hii sayari inayoitwa dunia. Kwa hiyo, masuala muhimu sana na kwa sababu ya umuhimu huo leo napendekeza nizungumzie jambo la kwanza la uhai wetu kama Taifa yaani Muungano wetu. Halafu masuala ya mazingira yanayohusu uhai wetu kama binadamu nitayazungumzia katika mchango wa maandishi ambao nauandaa tangu juzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano kuna sehemu ambayo inazungumzia haja ya kuelimisha umma kuhusu Muungano. Masuala au shughuli ambazo zinazungumziwa katika sehemu hiyo ni mambo ambayo yamefanyika katika sehemu ya kuelimisha umma na kwa maoni yangu hiyo inayoitwa elimu kwa umma na imeelekezwa zaidi katika kuyaelezea matukio muhimu katika miaka 47 ya Muungano wetu kama Taifa, kitu gani kilitokea tarehe 26 Aprili, 1964. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, matukio makuu kitu ambacho hakielezwi na kitu ambacho hakijaelezwa kwa miaka 47 ya uhai wetu kama Taifa, ni mambo gani yaliyotokea nyuma ya pazia ambayo yalitufanya tuungane kwanza na pili ambayo yametokea nyuma ya pazia katika miaka 47 ya uhai wetu kama Taifa. Napendekeza kwa muda huu mfupi nilionao niyagusie haya ambayo huwa hayasemwi ili tuweze kuwaelimisha watu wetu kuhusu hasa kitu gani kimekuwa kinatokea kuhusiana na Muungano wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna anayeweza kubisha, kama anaweza na ajitokeze. Hakuna anayeweza kubisha kwamba Muungano wetu ulizaliwa katika mazingira ya siri kubwa, Muungano wetu ulizaliwa katika mazingira ya kuficha wananchi na Muungano wetu ulizaliwa katika mazingira hata ya kuficha vyombo vya uwakilishi vya wananchi vilivyokuwepo wakati huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wasomi wa historia ya Muungano na vitabu vingi vimeandikwa na vinaendelea kuandikwa juu ya Muungano huu. Wameonesha bila shaka yoyote kwamba Muungano kati ya Tanganyika na Zanzibar siku 100 baada ya Mapinduzi ya Zanzibar, ulizaliwa kwa sababu ya shinikizo kubwa kwa upande mmoja la mgongano wa vita baridi kati ya Wamarekani na Warusi, kwa upande wa pili ulizaliwa kutokana na tishio ili kudhibiti tishio la siasa za msimamo mkali zilizozaliwa na Mapinduzi ya Zanzibar na zilizokuwa zinatishia Serikali zilizokuwa na mrengo wa kati au mrengo wa kulia za nchi za Afrika Mashariki ikiwemo Serikali ya Tanganyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kulikuwa na haja ya kudhibiti, kwa upande wa Zanzibar, kudhibiti waliokuwa na msimamo mkali na walioshiriki katika Mapinduzi, Chama cha Umma cha akina Abrahaman Mohamed Babu, akina marehemu Kassim Hanga, Abdullah Twala, Mdungu Ussi na wengineo. Hayo ndio yalikuwa mazingira yaliyozaa Muungano wetu; si kwa sababu tulikuwa na mapenzi makubwa kiasi hicho, ni kwa sababu ya ku-*deal* na hili tishio la Mapinduzi ya Zanzibar kwa siasa za Afrika Mashariki na kwa siasa za Mataifa makubwa, Warusi na Wamarekani. Ndio sababu kubwa ya usiri huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mzee Aboud Jumbe Mwinyi, aliyekuwa Rais wa Zanzibar baada ya Marehemu Karume kuuwawa, aliandika kitabu mwaka 1994 kinaitwa *30 Turbulent Years, The Union between Tanganyika and Zanzibar 30 Turbulent Years* na Mzee Aboud Jumbe Mwinyi anasema kwamba mwezi mmoja baada ya Mapinduzi ya Zanzibar, Mwalimu Nyerere (Mwenyezi Mungu amrehemu) alianza kumshinikiza Mzee Karume kuhusu Muungano. Kumshinikiza, ndio maneno ya Aboud Jumbe, sio ya kwangu na kuna ushahidi mkubwa kwamba hati ya Muungano iliyosainiwa tarehe 22 Aprili, 1964 na Mwalimu Nyerere na Marehemu Mzee Karume, ilisainiwa bila Sheikh Karume kupata baraka za Baraza la Mapinduzi la Zanzibar kwa sababu Baraza la Mapinduzi lilikuwa linapinga Muungano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, na Profesa Shivji, ameeleza katika kitabu chake, *Pan Africanism or Pragmatism? The License of Tanganyika Zanzibar Union* kwamba pamoja na kwamba hati ya Muungano ilihitaji iridhiwe kwa kutungiwa sheria na sehemu mbili zote za Muungano, haikuridhiwa kwa sheria iliyotungwa na Rais wa Zanzibar, kwa ushauri wa Baraza la Mapinduzi kama ilivyokuwa inatakiwa, bali kisheria ilitungwa na mtu anayeitwa Nines Fifoot, aliyekuwa *Acting Solicitor General* wa Tanganyika, inayosema kwamba Zanzibar walipitisha sheria ya kuridhia Muungano. Sheria yenyewe haipo katika rekodi zetu mpaka leo! Kwa hiyo, Zanzibar hawakuridhia Muungano kwa ushahidi ambao upo hapa, angalau umetolewa mpaka sasa hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, upande wa Tanganyika ilipelekwa sheria, Bunge halikuwa kwenye Kikao wakati huo, lakini Bunge liliitishwa kwenye kikao cha dharura, tarehe 25 Aprili, siku tatu baada ya *Article of the Union* kusainiwa, Bunge likaitwa, likakalishwa Karimjee, likaletewa Muswada wa Sheria ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar kwa Hati ya Dharura, ikapitishwa muda ule ule, wajumbe watatu wamechangia, kesho yake terehe 26 Aprili Muungano ukazaliwa! Uharaka wote huu, usiri wote huu, ulitokana na yale mazingira niliyoyasema; mazingira ya vita baridi, mazingira ya tishio la Mapinduzi ya Zanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tuna miaka 47 katika Hati ya Muungano, *Article of Union,* kulikuwa na mambo 11 tu yaliyokubaliwa kuwa ndio sehemu ya Muungano, kuwa hayo ndio Muungano wenyewe na ukiangalia Katiba yetu leo, ukisoma ya kwanza mpaka ya 11, hayo ndio yaliyokubaliwa kati ya Nyerere na Karume mwaka 1964. Kuanzia 12 mpaka 22, ni mambo yaliyoingizwa baada ya tarehe 26 Aprili, 1964, yaliingizwaje? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *item* ya 12 inahusu mambo ya fedha na kuna mgogoro mkubwa juu ya pesa hapa! Tunapunjwa, tunapunjwa, tunapunjwa! Ni kwa sababu tarehe 10 Juni, 1965 kwa kutumia Hati ya Dharura, Bunge lilipelekewa Sheria ya Mabadiliko ya Katiba ya Muda iliyoingiza mambo ya fedha katika orodha ya mambo ya Muungano. Soma *Hansard* ya terehe 10 Juni, 1965 kilikuwa Kikao cha 17 cha Bunge, aliyekuwa Makamu wa Pili wa Rais anasema; "Tunaleta Muswada huu kwa siri, haupo kwenye *Order Paper* kwa sababu, haya masuala hatukutaka, tungeyachapisha kwenye *Order Paper* siri ingefichuka!"*(Makofi)*

Kwa hiyo, mambo ya fedha yaliingizwa kwenye mambo ya Muungano kwa siri, hayakuwepo kwenye *Order Paper* na haya ni maneno ya Marehemu Kawawa, Mwenyezi Mungu amrehemu, si mimi, sio ya kwangu! Na mambo mengine yote ya Muungano, 12 mpaka 22, yameingizwa bila kuwashirikisha Wazanzibari. Ndio maana ya kero za miaka yote hii! Miaka yote hii tukitaka kuingiza mambo, kwa miaka mingi ya Karume, hakuwa anajali sheria! Hakuwa ana-*care* wasomi wanataka nini! Nyerere, akitaka anachomeka Hati ya Dharura, yanapita! Ndio maana ya kero zote hizi. *(Makofi)*

Sasa kwa muda mdogo nilionao naomba nipendekeze kwamba ili tuwe na Muungano wa kweli wa wananchi wa nchi hizi mbili lazima kwanza maswali haya yafuatayo yaulizwe na kujibiwa; swali kwanza ni je, wananchi wa Bara na wananchi wa Visiwani, wanataka Muungano? Halijawahi kuulizwa hilo! Halikuulizwa mwaka 1964, halikuulizwa kwa miaka 47 mpaka leo. *(Makofi)*

Jambo la pili, swali la pili linalohitaji kuulizwa na kujibiwa ni je, ni Muungano wa aina gani tunaoutaka? Halijawahi kuulizwa tangu mwaka 1964, halijaulizwa kwa miaka 47 ya mpaka leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hayo maswali mawili yakishajibiwa basi tukae tutengeneze Katiba ya Muungano; tupate kwa mara ya kwanza, tupate ridhaa ya wananchi wetu. Kusiwe na mtu atakayesema huu ni Muungano wa Nyerere na Karume, kwa sasa hivi kuna ushahidi mkubwa wa ukweli wa tuhuma hizo. Kusiwe na mtu atakayetutuhumu kwamba tumeingiza mambo kinyemela nyemela, Muungano huu unahitaji ridhaa ya wananchi na ridhaa hiyo kwa maoni yangu, haitatokana na Serikali hii. Utaratibu wa kuipata ridhaa hiyo ni lazima, kama nilivyosema, lazima tuanze kwa kuuliza swali la msingi kabisa, tunataka kuendelea nao au la! Kama tunataka, ni namna gani tunaendelea mbele kwa miaka 50 ijayo? Hayo ndio masuala ya kimsingi tunayohitaji kuyauliza; na hayaulizwi kwa sababu watu wana hofu, ukihoji Muungano unaonekana kama unataka kumtukana Nyerere! Hapana, huu Muungano ni wetu wote. Mazuri yake ni yetu wote. Mabaya yake ni yetu wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili tuuimarishe kwa maoni yangu, unahitaji ujadiliwe bila woga. Si mambo matakatifu, si mambo ya Musa yaliyofanyika mwaka 1964, ni mambo ya Kaisari na kwa sababu ni mambo ya Kaisari, tuna haki na tunawajibu wa kuyahoji yaliyofanyika wakati ule, kuhoji yaliyofanyika miaka 47 na kuhoji ambayo yanafanyika leo na kesho ili tuwe na *a more perfect union.* Ili tuwe na Muungano ambao utakidhi haja za pande zote mbili. Wote ni ndugu tumeungana, lakini hata ndoa huwa zinavunjika. Sasa hii ndoa ili iwe imara zaidi tunahitaji ukweli, hatuhitaji *propaganda.* Tumechoka na *propaganda,* tumechoka na picha za tarehe 26 Aprili, tunahitaji mafaili yafunguliwe tuone hivi kitu gani hasa kilitokea? Kassim Hanga, yuko wapi? Abdullah Twala, yuko wapi? Mdungi Ussi, yuko wapi? Walikwenda wapi? Mapinduzi ya Zanzibar, Mapinduzi matakatifu, sawa sawa! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. *(Makofi)*

**MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru na mimi kunipa hizi dakika za mwisho niseme chochote kuhusu Muungano. Tumeshazungumza mambo mengi na muda mrefu, leo ni miaka 47 ya Muungano, lakini ndio hivyo! Tutafika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kuanza kuzungumza, nina swali naulizwa na mwanangu mdogo tangu akiwa mdogo. Leo nitaomba na mimi ninashindwa kumjibu! Leo nitaliomba Bunge hili, Waziri akija hapa akifanya majumuisho labda aweze kutujibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabla ya hapo Mheshimiwa Tundu Lissu, ameyaeleza kwa undani wa kisheria, mimi sitakwenda huko, katika asilimia kubwa naungana nae mkono lakini kwa upande mwingine pia katika mfumo wa Muungano, kama makosa tumefanya, ninamshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano, kwa kuleta haya mabadiliko ya Katiba ambayo ndio mategemeo ya Wazanzibari wengi sasa hivi na ndio mategemeo ya Watanganyika, lakini kwa jina la siku hizi wanapenda sana kuita Tanzania Bara, tunadhani tutaweza kufanya marekebisho ya matatizo haya yote yaliyotokezea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali ninaloulizwa na mtoto wangu tangu mdogo ana miaka sita, saba, mimi nalishindwa kujibu! Ananiuliza baba, hivi kila siku za Sherehe za Muungano, tunamuona Mwalimu Nyerere amekamata vibuyu viwili anachanganya udongo! Mbona Karume hayupo? Ni yeye peke yake anayechanganya! Muungano gani baba huu anachanganya mtu mmoja? *(Makofi)*

Swali hilo mimi nimeshindwa kujibu na ikifika tarehe ya Muungano jamani angalieni, ni Mwalimu peke yake anachanganya ule udongo, mwenzake hayupo ambapo sasa hayo ndio yale ambayo ameyasema Mheshimiwa Tundu Lissu, ndio unaweza ukajipata, dah! Kumbe ilikuwa ni hivi! Naomba Mheshimiwa Waziri, akija hapa atufafanulie kwa nini ilikuwa ni mtu mmoja anachanganya na huu ni Muungano wa pande mbili? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nijikite katika shughuli yenyewe ya Muungano; jambo la kwanza, nimeisoma vizuri hotuba ya Mheshimiwa Waziri, jambo la kwanza ambalo ninaliomba ni kwamba suala la akaunti ya pamoja ni suala ambalo linatia utata na nikubaliane na yule ndugu yangu Mheshimiwa Sadifa, Mbunge wa Donge, aliyesema kwamba mambo haya yanahitaji *political will*, dhamira ya kikweli. Ikiwa leo kama ripoti imetoka Agosti, 2006 mpaka leo akaunti ya pamoja imeshindikana! Na leo Zanzibar inabakia katika masuala ya mikopo, madeni na dhamana! Hawana nafasi isipokuwa wapitie *SMT* kwa Sheria Namba 30 iliyoanzishwa mwaka 1974 ikarekebishwa 2004. Kwamba, Zanzibar haina uwezo wa kukopa au dhamana au misaada, isipokuwa wapitie *SMT* Zanzibar, hili ni udhalilishaji, ndipo hapo tunaposema haya matatizo ya Muungano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tena inaambiwa kwamba ikitaka kufanya hivyo lazima ikubali Jamhuri ya Muungano na Jamhuri ya Muungano ikikataa ndio basi! Ni sawasawa

na lile swali *OIC* ilipoambiwa huko hatutaki, basi! Kwa sababu ya Wizara ya mambo ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Kimataifa! Sisi hatuna ushirikiano wa Kimataifa kule. Kwa maana hiyo, ikiwa tokea mwaka 2006 mpaka leo, Mheshimiwa Waziri naomba ukifika hapa utueleze je, hii lugha tunayopenda kuitumia siku hizi, mchakato utamalizika lini ili akaunti hii iwepo? Hilo la kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili, tukija kuhusu hili la Muungano, kuna Waasisi Wanasheria waliobobea. Kama ni mfumo huu wa Serikali mbili, ukweli wa mambo tumetumia Watanzania wastaarabu, tumetumia neno ambalo mambo makubwa yanafanyika kama jambo jepesi! Hiki kitu cha kusema kero za Muungano! Tumetafuta lugha ambayo ita-*simplify* mambo! Lakini ukweli ni matatizo ya Katiba iliyopo ya Jamhuri ya Muungano kuhusu mambo ya Muungano. *(Makofi)*

Kwa hivyo, zile kero zitaorodheshwa sijui arobaini na ngapi na mpaka leo zimetatuliwa tatu tu miaka 47! Kuna watu siku hizi wanaitwa washauri waelekezi, lakini kama mshauri mwelekezi mkuu nchi hii, Tume ya Marehemu Jaji Francis Nyalali, Tume ya Jaji Robert Kisanga, Tume zote hizi zilizozunguka dunia nzima zikafanya mashauri! Leo tunawakumbuka akina Marehemu Borafia, akina Marehemu Salum Juma Othman, Mwenyezi Mungu awalaze pema na yeye Marehemu Nyalali, Mwenyezi Mungu amlaze mahali pema, wametufanyia makubwa, wakatupa mfumo ni huu ili yaondoke haya tunayoyaita kero, mfumo ni wa Serikali tatu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hao ndio wasomi wa Tanzania hii. Hapo hatuzungumzii *CUF,* hatuzungumzii CCM, hatuzungumzii CHADEMA, hatuzungumzii *NCCR;* wazee walioaminika wakabobea kisheria, wakachukuliwa kumi upande wa Zanzibar, wakachukuliwa kumi huku na hizo Tume nyingine, wakaja na mfumo huu! Huu ndio mfumo ambao utaondosha matatizo. Ni mategemeo yetu Watanzania, najua Bara wanakereka yapo mambo yanayowakera kuhusu Muungano, Wazanzibar yapo mambo yanayowakera kuhusu Muungano, haya yote mfumo ni wa Serikali tatu, walivyoshauri. Lah, ikiwa washauri waelekezi hawa hatuwaamini lazima tuje tushauriwe na wazungu, hilo tena itakuwa suala lingine, ni ugonjwa mkubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukurasa wa saba wa hii hotuba ya Mheshimiwa Waziri, kuna mambo saba, pia ameyazungumza hapa; hayo ya kuzifanyia mapitio, uboreshaji wa Sheria za Kanuni za Fedha, kuboresha Sheria na Kanuni za Utaratibu za Ajira, kuimarisha utaratibu wa kuandaa na kutekeleza mikakati na miundombinu, kuendeleza miradi ya pamoja! Haya mambo, tumeyazungumza miaka 47! Naomba Mheshimiwa Waziri, ukija hapa utuambie hayo maboreshaji yatakamilika mwezi gani? Pawe na *time frame.* Wakuelezwa lugha hii hii kila siku ndio tunasema ile *political will* haipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya Zanzibar kiuchumi, ipo, hali sio nzuri; Serikali ya Jamhuri ya Muungano ni afadhali japo nayo bado. Pana tatizo moja hapa, nataka Mheshimiwa Waziri akija pia atufafanulie; leo Zanzibar wameshapitisha Bajeti, shilingi ya Tanzania inadondoka siku hadi siku na huku imeshapitishwa Bajeti ya Serikali! Je, shilingi itakapoendelea kudondoka, *difference* ile wenzetu hasara watakayoipata, Jamhuri ya Muungano itafidia kiasi gani?*(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri, uje utueleze, Ofisi ya Makamu wa Rais, inayoshughulikia Muungano, uje utueleze itafidiwa kiasi gani kuziba lile pengo ikiwa wenzetu watakuwa *affected* na Bajeti na mtindo huu wa mfumuko wa udondokaji wa shilingi ambayo *control* ipo huku upande wa Jamhuri ya Muungano? Zanzibar, hawana udhibiti wowote! Kwa maana hiyo, shilingi hii ikiachiliwa kudondoka, ina maana tutakuwa *affected* upande ule, na hapo ndio tunahitaji lazima pawe na *compensation*, pawe na kitu na Mheshimiwa utufafanulie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ipo siku niliwahi kuuliza maswali ya papo kwa papo, swali kwa Waziri Mkuu. Kwa kuwafafanulia wale wengine tu kwamba wakati Wazanzibari wanapolalamika ni kwamba Muungano unatakiwa uwe na sura ambazo ni za *balanced…*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kumalizika muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mnyaa.

Waheshimiwa Wabunge, huyo ndiye aliyekuwa mchangiaji wetu wa mwisho kwa siku ya leo. Haya yote tunayoyazungumza juu ya Muungano, jibu lake ni Katiba mpya. Sasa kwa hiyo, jitihada ya kila mmoja wetu ya kuwezesha huo utaratibu wa Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwamba lazima tuwe na Katiba mpya, ukikubalika na sote kwa pamoja, mimi ninaamini yote haya yanakwisha wakati ule. *(Makofi)*

Kwa hiyo, niwapongeze sana kwa michango mizuri, tutaendelea tena siku ya Ijumaa. Kesho ni siku ya…, mimi siiti ya mapumziko maana ni siku ya kushiriki katika Sherehe za Sabasaba na Wabunge hatuji Bungeni kwa sababu tunaenda kushiriki Sherehe za Sabasaba maeneo mbalimbali. Kwa hivyo, kesho hatutakuwa na shughuli ya Bunge, hadi siku ya Ijumaa saa tatu asubuhi. *(Makofi)*

Basi nichukue nafasi hii kuahirisha Bunge hadi Siku ya Ijumaa, saa tatu asubuhi.

*(Saa 1.43 usiku Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Ijumaa,*
*Tarehe 8 Julai, 2011 saa tatu asubuhi)*